

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA ISHIRINI**

**Kikao cha Ishirini na Nane – Tarehe 12 Julai, 2010**

*(Mkutano ulanza Saa Tatuhu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka 2010/2011.

Taarifa ya Mwaka ya Mamlaka ya Elimu Tanzania kwa Mwaka 2008/2009 [*The Annual Report of Tanzania Education Authority for the Year 2008/2009*].

**MHE. OMARI SHABANI KWAANGW' - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

**MHE. NURU AWADH BAFADHIL K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2008/2009 [*The Annual Report and Audited Accounts of the Local Authorities Pensions Fund (LAPF) for the Year 2008/2009*].

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):**

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 201

**Migogoro Katika Shule Za Sekondari za Kata – Mwibara**

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI (K.n.y. MHE. CHARLES M. KAJEGE)** aliuliza:-

Kwa kuwa, mojawapo ya vyanzo vya migogoro katika Shule za Sekondari za Kata katika Jimbo la Mwibara ni Bodi za Shule hizo:-

- (a) Je, Serikali inatambua hilo?
- (b) Je, ni sifa/vigezo gani vinatumika kuwachagua Wajumbe wa Bodi hizo?
- (c) Je, Serikali imefanya juhudhi gani za kumaliza hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swalii la Mheshimiwa Kajege, ninakuomba kwa unyenyekevu mkubwa uniruhusu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, nimpungeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, ambaye Mkutano Mkuu umempitisha kwa kishindo na ninataka nimthibitishie kwamba wananchi wa Siha wapo na yeye na wataendelea kumpa ushirikiano. Kwa kipekee, pia nimpungeze Mheshimiwa Makamu wa Rais Dr. Shein, kwa kupitishwa na Halmashauri ya Kuu ya Taifa kuwa mgombea wa Serikali ya Mapinduzi, Zanzibar pamoja na Dr. Bilal kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo yote nakushukuru sana kwa kunipa ruksa hiyo. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Charles Muguta Kajege Mbunge wa Mwibara, lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba kutoa ufanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mwibara lina Shule za Sekondari za Kata 8 na shule moja ni ya binafsi. Shule hizo ni hizi zifuatazo; Bulamba, Chitengule, Chisorya,

Kwiramba, Muranda, Mwigundu, Nansimo na Nyeruma. Shule zote 8 katika Kata ya Jimbo la Mwibara zina Bodi ambazo zimeundwa kisheria kwa kuzingatia sheria ya elimu namba 25 ya mwaka 1978 kama ilivyorekebishwa na sheria namba 10 ya mwaka 1995.

Kwa kuzingatia sheria hiyo, Bodi za shule zimepewa majukumu ya kusimamia uongozi na uendeshaji wa mipango yote ya maendeleo ya shule, kusimamia nidhamu kwa walimu na wanafunzi na kusimamia matumizi ya fedha za shule.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa kulikuwa na migogoro katika shule mbili za Sekondari za Kata katika Jimbo la Mwibara, ambayo ni migogoro katika shule za Sekondari za Nyeruma na Muranda. Mgogoro wa shule za Sekondari Nyeruma ulikuwa ni kati ya Bodi ya Shule na Mkuu wa Shule.

Chanzo cha Mgogoro huu ni Mkuu wa Shule kutoshirikisha Bodi ya Shule katika uendeleshaji wa shule, kutothamini michango yao ya mawazo na kutokusoma mapato na matumizi ya michango kutoka kwa wazazi. Mgogoro wa shule ya Sekondari ya Muranda ulikuwa kati ya uongozi wa shule na baadhi ya viongozi wa Kata ya Namhula, baada ya kutokea mgomo wa wanafunzi tarehe 19 mpaka terehe 20 Februari, 2009 uliosababishwa na mwanafunzi mmoja kuja na silaha (panga) shulenii na kutishia kuwajeruhi walimu wa shule hiyo, kinyume na taratibu za shule, hasa baada ya shule kuwafukuza wanafunzi 14 waliobainika kuchochea mgomo wa wanafunzi wa tarehe 19 mpaka tarehe 20 Februari, 2009.

(b) Mheshimiwa Spika, sifa au vigezo vinavyohitajika katika kuteua wajumbe wa Bodi za shule ni hizi zifuatazo:-

(i) Mjumbe wa Bodi ya Shule asiwe kwenye Bodi za shule zaidi ya tatu.

(ii) Mjumbe asitoke nje ya mkoa.

(iii) Mjumbe asiwe na majukumu mengi ya kitaifa.

(iv) Wajumbe wanaopendekezwa watoke kwenye maeneo mbali mbali kama Taasisi za Kidini na Jumuiya zisizo za Serikali.

(v) Wadau wa Elimu wanaoendelea na kazi zao Serikalini. Mfano, Wakaguzi wa Shule, Walimu, Maafisa elimu, walimu waliostaafu, wanaruhusiwa pia.

(c) Mheshimiwa Spika, juhudii zilizochukuliwa katika kutatua mgogoro wa Shule ya Sekondari Nyeruma, ni uongozi wa Halmashauri ya Wilaya kwenda shulenii Nyeruma, kukutana na wajumbe wa Bodi ya Shule, Walimu, Wazazi na kusikiliza pande zote.

Mapendekezo yaliyofikiwa ni kumhamisha Mkuu wa Shule, kupisha Ukaguzi wa vitabu vyta fedha katika shule hiyo. Aidha, hatua zilizochukuliwa kutatua mgogoro wa shule ya Sekondari Muranda, ni kuwafukuza wanafunzi baada ya kukiuka taratibu za

shule, kurejesha hali ya utulivu shulen, kuagiza uongozi wa shule kuitisha Kikao cha Bodi ya shule na kumhamisha Mkuu wa Shule na kupeleka Mkuu wa Shule mwingine.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri, ameelezea sifa na vigezo vya hawa wajumbe wa Bodi wa Shule za Sekondari. Kwa kuwa, matatizo yaliyojitokeza Mwibara, yanafanana na shule nyingi za sekondari hapa nchini na kwamba baadhi ya Wajumbe wa Bodi, wanatoka maeneo ambayo ni mbali na zilipo shule na hivyo kuchochea mfumuko wa gharama za kuwashudumia wanapokuja kwenye mkutano wa Bodi.

Je, ni kwa nini Serikali isingeona umuhimu wa kuainisha zaidi vigezo vya Wajumbe wa Bodi watokane na maeneo ambayo wananchi au wana jamii waweze kushiriki katika kuwachagua ili waweze kuteuliwa kwenye hizi Bodi, badala ya kumwachia Mwalimu Mkuu, kuteua watu ambao yeze anadhani wanafaa kufanyanao kazi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, labda kwanza nieleze kwamba ilikuwaje, halafu na sasa ikoje.

Mheshimiwa Spika, zamani aliyekuwa anawateuwa wajumbe wa Bodi, alikuwa ni Waziri mwenye dhamana, yaani maana yeke ni kwamba Profesa Maghembe ndiye angekuwa anawateuwa, lakini sasa alichofanya amekasimu madaraka yale yakawa yanapitia kwa ma-*REO*. Wale Wakuu wa Shule walioko pale walichoagizwa ni kwamba wahakikishe, na hapa nimeisoma, kwamba wale wanaowateuwa na wale wanaowapendekeza ambao hatimaye watapelekwa mpaka kwa Mheshimiwa Waziri, wawe ni watu wanaotoka katika maeneo yale na ni watu ambao wanaweza wakapatikana. Mheshimiwa Spika, sasa msisitizo ambao anauweka hapa, mimi ninauona. Kwa sababu ukisema wajumbe wa Bodi kama ni wa Manyara wakatoka Mtwara, ukawaleta pale ukaanza kuwasafirisha kuwapeleka pale ni kazi ngumu. Lakini nafikiri ninachowezu kukiona hapa ni kwamba Mheshimiwa Mbunge, ana pointi kubwa na anachosema ni kwamba tuhakikishe kwamba wanatoka katika Mkoa uleule. Lakini hata kama wanatoka katika Mkoa uleule anachositisiza yeze ni kwamba watoke pale karibu na shule ili waweze kuisaidia shule. Mimi ninalichukua hili na ninajua kwamba tutafanya mawasiliano na Mheshimiwa Waziri wa Elimu, ili tuweze kuona kwamba hilo linafanyika kama anavyoshauri.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, sasa hivi kuna wingi wa shule hizi za Sekondari hasa kwenye maeneo ya Kata. Na kwa kuwa, mara nyingi uteuzi kama anavyooleza, utaratibu wa kuchukua watu wanaotoka maeneo yaliyo karibu na wanaopatikana katika Mkoa huo uko sahihi, lakini liko tatizo moja kubwa juu

ya uelewa wa wajibu wao katika kufanya shughuli katika Bodi hizo. Na mara nyingi wanaonekana kuburuzwa na walimu kwa sababu hawaelewii wajibu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inawaelimisha ili kuondoa hiyo tofauti iliyopo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Killimbah, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, labda hili nalo nilisemee. Ni kwamba kwanza kabisa ushauri unaotolewa hapa, ukimpleka mtu anayeingia katika Bodi ya Shule, *minimum qualification* walao awe amemaliza *Form IV*.

Ukifanya hivyo inakusaidia sana uelewa, kwa sababu hata kama utapeleka watu wa pale ni lazima uwe na watu ambao wataelewa watakapoeleweshwa.

Lakini mara kwa mara, kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na *TAMISEMI*, tumekuwa tunatoa Semina kwa ajili ya wajumbe hawa ili waweze kuongeza uelewa wao. Kwa hiyo, hili analolisema Mheshimiwa Killimbah, tunakubaliana na yeze na tutafanya hivyo. Lakini suala la *qualification* hapa kwa wajumbe, nalo ni muhimu pia. (*Makofi*)

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Kata nyingi sasa hivi zina Sekondari na zote zimeshafikia *Form IV*. Na kwa kuwa, wanafunzi wanapoanza *Form I*, huwa wanaambiwa wapeleke meza na viti. Je, vile viti vingine huwa vimeenda wapi?

**SPIKA:** Amechomekea tu, lakini labda Mheshimiwa Waziri wa Elimu; maana hili sasa limekuwa mahususi mno. (*Makofi/Kicheko*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nijibu swalii la nyongeza. Lakini pia napenda nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri ambayo ameyatoa katika masali ya awali yaliyoulizwa juu ya suala hili. Katika shule hizi za Sekondari tunapozianza, zinakuw na matatizo mengi. Na moja ya matatizo hayo ni kuwa na viti vya kutosha kwa ajili ya wanafunzi kukalia wakati wanapojifunza na jukumu hili limewekwa chini ya wazazi.

Lakini ninataka kuwaondolea hofu Waheshimiwa Wabunge, kwamba kuanzia Julai 2010, tunaanza kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari Awamu ya Pili na tutatumia takribani shilingi bilioni 150 kwa ajili ya kujenga uwezo na kujenga miundombinu ya shule. Kwa hiyo, shule zina nafasi ya kupanga na kujua ni kipi zitanunua zenyewe na ni kipi wananchi watashiriki. Ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 202

#### **Kuhamisha Kituo cha Polisi Kibiti**

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA** aliuliza:-

Kituo cha Polisi cha Kibiti ni Kituo pekee katika jimbo la Kibiti, lakini kimejengwa katika Hifadhi ya barabara (*Road Reserve*) ya Kibiti – Lindi na kimechakaa sana:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani kukihamisha kituo hicho na kukijenga katika kiwanja kipyä kibiti?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia askari wa Kituo hicho vifaa vya kufanya kazi ikiwemo gari na pikipiki?

(c) Je, Kituo hicho kitarajie kupata kitu gani katika mwaka huu wa fedha 2010/2011?

**NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swalí la Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mbunge wa Kibiti, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba jengo la Kituo cha Polisi Kibiti, ambalo linamiliwi na Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, liko kwenye hifadhi ya barabara (*Road Reserve*). Kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Kituo kipyä pamoja na nyumba za askari, kimeshapatikana.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inao mpango wa kuvipatia Vituo vyote vya Polisi kikiwemo Kituo cha Kibiti, vitendea kazi hasa magari na pikipiki. Kwa sasa Kituo hicho kina pikipiki mbili lakini hakina gari. Hata hivyo kinahudumiwa na gari la *OCD* ambalo pia huhudumia vituo vya Utete, Ikwiriri, Mloka na Muhoro.

(c) Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha 2010/2011 Kituo cha Kibiti, kitapatiwa pikipiki nyingine moja kwa ajili ya kuimarisha ulinzi.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri. Nilikuwa na swalí moja la nyongeza. Kwa kuwa, Serikali imekiri kwamba Kituo hiki cha Kibiti kipo kwenye *Road Reserve*. Na kwa kuwa, wananchi wengi waliokuwa kwenye *Road Reserve* tayari wameshahamishwa na majengo yao yamevunjwa, limebakia jengo la Serikali peke yake. Je, ni lini sasa ujenzi wa Kituo hiki kipyä utanza?

**NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swalí la nyongeza la Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge, atakumbuka kwamba mimi na yeye tulikwenda kwake na nilikwenda katika Kituo hiki nilikiona mimi mwenyewe na tumefanya mazungumzo pale na Viongozi wa askari pale.

Sasa ni kweli hii tumeiona na ni kituo peke yake ambacho kimebaki na kama nilivyomjibu katika jibu langu la msingi ni kwamba mahali pa kujenga kituo pamepatikana na hivi sasa tupo katika mazungumzo. Kama unavyojuua tunajitahidi kuona Halmashauri zinahusika vipi katika mchango wa aina fulani. Hii ndio ambayo tunafanya. Kwa hiyo itakuwa ni vigumu sana mimi kukutamkia kwamba ni lini hasa hii shughuli itaanza.

Lakini kuna moja, mimi mwenyewe nimefika katika eneo hilo tukiwa pamoja na Mheshimiwa Mbunge. Pili, bado tuna mazungumzo na wadau wengine ambao wanahusika.

Kwa hiyo, yote hiyo ni kukuonesha kwamba tupo katika mtiririko wa utekelezaji wa kuhamisha kituo hiki, na hii ninataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na niwahakikishie wananchi wako kwamba hili tunalifanyia kazi na litafanyika. (*Makofi*)

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, tatizo la vifaa vya kutendea kazi katika Vituo vya Polisi lililoko Kibiti ni sawasawa na tatizo lililoko katika Wilaya ya Bukombe.

Kwa kuwa, katika Bajeti mara kadhaa Serikali imeahidi kuwapatia gari wilaya ya Bukombe, ambapo Bajeti iliyopita hawakupata na sasa hivi hatujapata na matukio ni mengi katika Wilaya yetu.

Serikali inawambia nini wananchi wa Bukombe, hasa ambao askari wake hawana gari la kufanya kazi katika operesheni zao na shughuli za kila siku?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mbunge wa Bukombe, kama ifuatavyo.

naomba nichukue nafasi hii nikupe pole, nilishakupa pole kwa mambo yaliyokukuta, lakini jambo la pili nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na kupitia kwake niwahakikishie wananchi wa Bukombe kwamba kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, hapa wakati akiwasilisha Makadirio ya fedha ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, wilaya ya Bukombe itapata gari mpya na hiyo gari ni matumaini yetu kwamba katika mwezi huu wa saba ikijakufika mwisho wa mwezi wa saba mtakuwa mmepata gari mpya. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge ningekuomba uvute subira katika wiki hii chache zilizobaki utapata gari yako.

Na. 203

#### **Mawasiliano ya Simu za Mkononi**

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE** aliuliza:-

Kwa kuwa, mawasiliano ya simu za mkononi katika vijiji vya kandokando ya ziwa Nyasa, vya mikoa ya Mbeya na Iringa hayajawahi kuwepo tangu huduma hiyo ianzishwe nchini:-

Je, ni lini Serikali itahimiza kampuni za simu za mkononi kuwekeza katika vijiji vya Ikombe (Kyela), Lumbila, Nsele, Makonde, Lifuma, Nsisi na Lupingu Wilayani Ludewa?

### **WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swal la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo ya awali ya ufanuzi kama ifuatavyo:

Serikali inatambua umuhimu wa kuwepo huduma ya mawasiliano ya simu katika maeneo mbalimbali nchini kwetu ikiwa ni pamoja na maeneo ya vijiji na maeneo yenye shughuli nyingi za kibiashara kama alivyotaja Mheshimiwa Mbunge. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, huduma za mawasiliano zenye ubora na uhakika, hurahisha mawasiliano ya kibiashara ikiwa ni pamoja na utafutaji wa masoko, utafutaji wa bidhaa na mazao pamoja na usafirishaji. Kwa hali hiyo ni dhahiri kwamba, mawasiliano ni chachu ya maendeleo ya sekta ya biashara.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa napenda kujibu swal la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *VODACOM* tayari imefanya tathimini ya kibiashara katika maeneo ya Manda, Nindi na Matema na kubaini kuwa ni maeneo yanayofaa kuwekewa mitambo ya Mawasiliano.

Mchakato wa kuyawezesha maeneo hayo utakapokamilika utawezesha kupatikana kwa mawasiliano pia katika vijiji vya Makonde, Lumbila, Lupingu, na Ikombe katika maeneo ya Kyela na Wilaya ya Ludewa. Hata hivyo, juhudzi za kurekebisha mitambo mipya ambayo tayari imeshajengwa katika maeneo ya Namswea, Lituhi, Ilumgu, Lugalawa, milo na Mlangali tayari zimeshaanza ili kuwawezesha wananchi wengi wa mwambao wa ziwa Nyasa waweze kupata mawasiliano.

Mtandao wa *TTCL Mobile* unapatikana katika eneo la Ikombe, Lumbila, na Nsele kuititia mnara wao uliopo Kyela. Maeneo mengine yaliyobaki (Makonde, Lifuma, Nsisi na Lupingu) bado hayajapata huduma hii. Hata hivyo, *TTCL* inaendelea kuyaweka maeneo husika katika mipango yake.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya simu ya *TIGO, ZAIN* na *ZANTEL* zimewewa vijiji vya Ikombe (Kyela), Lumbila, Nsele, Makonde, Lifuma, Nsisi na Lupingu wilayani Ludewa katika mipango yake ya kufanya tathimini ya kibiashara katika mwaka wa 2010/2011.

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Spika, asante sana naomba kuuliza swal moja la nyongeza. Kwa kuwa maeneo mengi aliyojataja Mheshimiwa

Waziri amekiri kwamba hayana mtandao wa mawasiliano ya aina yoyote yakiwemo yale maeneo ambayo yako katika Mkoa wa Mbeya na yale ambayo yako Mkoa wa Iringa, kando kando ya ziwa Nyasa. Na kwa kuwa maeneo hayo yapo karibu sana na Malawi na yanapokea mitandao ambayo inafanya kazi nchini Malawi.

Je, Waziri yuko tayari kuzungumza au kuyasababishia mazungumzo makampuni ya simu ya Tanzania aliyoyataja na yale ambayo ni ya Malawi yakakaa pamoja na kuruhusu uwezekano wa wananchi hao kuweza kupata mawasiliano ya uhakika. Je, anaweza kufanya hilo?

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, Mawasiliano tunayoyapata sasa hivi ni yale yanayotumia *satellite*, *satellite* ni kwamba mawasiliano hayo yanatumia mawimbi na Waheshimiwa Wabunge wote mnafahamu mawimbi hayana mpaka na tatizo hili halipo mahali pamoja tu haliko Kyela, mipakani kote kuna tatizo kama hili. Lakini *TCRA* tayari inazungumza na nchi jirani ili waweze kurekebisha tatizo ili kusudi kusikuweko na *cross border transmission* ipungue lakini haiwezi kutoka kabisa moja kwa moja na kuna teknoloji ambayo inatumika kwa sasa hivi ambayo kuieleza hapa itachukua muda mrefu ambayo inatumia kama wanaita *cross border colors* ambayo inasaidia ikifika mpakani basi yale mawasiliano yasivuke kwenda kwingine.

Hili ni jibu ambalo kwa kweli ni la muda mfupi lakini kwa uhakika zaidi kwa kuwa Serikali imeshaanza kujenga mkongo wa mawasiliano wa Taifa ambao hautatumia *microwave* ambao hautatumia satellite basi tatizo hili kwa sehemu kubwa itakamilika. Na kama tulivyoeleza huko nyuma Serikali imedhamiria kufika mwisho mwa mwaka wa fedha huu kwamba mkongo wa mawasiliano ya taifa utakuwa umefika makao makuu ya mikoa yote utakuwa umefika makao makuu ya wilaya zote hivyo itapunguza sana tatizo hili la maingiliano ya mawasiliano.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana naomba niulize swalii moja dogo la nyongeza kabla ya hapo nimfahamishe Mheshimiwa Waziri kwamba niujuavyo mimi mawimbi ya mtandao haya hayapigi kona na minara ambayo Waziri unasema inarekebishiwa ya Milo, Lugalawa, Mlangali hayawezi mawimbi yakashuka kule chini Makonde haiwezekani lakini baada ya hapo, nilikuandikia barua kwamba watu wa *VODACOM* waliniahidi kwamba kuna mitandao minara mitatu ambayo wangeweza kugawa moja kwako Kilolo, Makete, na Ludewa, nilitegemea huo wa Ludewa tungeweza kuweka ya mwambao kwa mfano Lupingu. Sasa Mheshimiwa Waziri hili limefikia wapi?

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kweli napenda kukiri kwamba aliniandikia barua na tulizungumza juu ya tatizo la mawasiliano wilayani Ludewa na hasa kufikia kule ziwani, nilichukua hatua nikazungumza na watu wa *VODACOM* na wao wameahidi katika mwaka huu wa fedha watakamilisha na kuhakikisha kwamba mawasiliano yanafika katika wilaya ya Ludewa.

## Nyumba Bora kwa Wanajeshi - Tabora

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA (K.n.y. MHE. AZIZA S. ALLY)** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika nchi yetu wapo wanajeshi ambao wanaishi kwenye nyumba za jeshi na nyumba hizo hazina ubora wowote.

Je, Serikali inajiendaaje kuwasaidia wanajeshi wa Tabora kupata nyumba bora?

**SPIKA:** Inaonekana Manaibu Mawaziri wanashughuli maalum sijui wapi kila swali linajibu na Waziri ukiacha lile la Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo la nyumba za kuishi kwa wanajeshi katika kambi mbalimbali nchini. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ina mipango ya kutenga fedha zaidi za maendeleo kwa kazi hizo za ukarabati na ujenzi wa nyumba za askari makambini. Mwaka wa fedha 2008/2009 zilitengwa Tsh.5 bilioni ambazo zimetumika katika ukarabati na ujenzi wa mabweni ya askari.

Katika Bajeti ya mwaka 2009/2010, Wizara ya Ulinzi na JKT ilitenga jumla ya Tsh. 33.5 bilioni, katika hizo JWTZ ilitengewa Tsh. 20 bilioni na JKT Tsh.13.5 bilioni. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara ya ulinzi imetenga Tshs. 18,454,334,000 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba mpya na kukarabati zilizopo katika makambi mbalimbali ya JWTZ ambapo JKT imetengewa Tsh.12,649,883,000.

Kambi ya Milambo - Tabora, ipo katika mpango wa kufanyiwa ukarabati na ujenzi wa makazi mapya ya wanajeshi.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza pamoja na majibu ya kuridhisha ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize kama ifuatavyo.

Kwa kuwa kambi ya wanajeshi wa Tabora Milambo, ni ya miaka mingi kabla ya uhuru na kwa kuwa jeshi hilo kambi hiyo ilianzishwa pamoja na Lugalo. Je, Serikali haioni umuhimu wa kutoa kipaumbele kwa jeshi hilo kambi hilo ili waweze kukarabati angalau miundombinu kutokana na hali mbaya ilivyo sasa hairidhishi. Je, Serikali inasema nini kwa hili?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana sana na Mheshimiwa Mcemba, kwamba hali ya makazi na miundombinu katika kambi hii ya Milambo ambayo mimi mwenyewe nimeitembelea hairidhishi hata kidogo. Na ndiyo maana nimesema katika jibu langu la msingi kwamba tuna mpango kabambe ya kuhakikisha kwamba makambi yote ya zamani yanakarabatiwa majengo yake na ikiwezekana tunajenga majengo mapya. Nakubaliana naye kwamba kipaumbi kitatolewa Milambo kwa sababu nakiri kwamba hali ya pale sio nzuri kabisa.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWAKO:** Mheshimiwa Spika, hsante mimi naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri swali dogo la nyongeza kwa sababu maeneo ya mpakani kwenye mipaka yetu na Kongo, Burundi na Rwanda, kumekuwa na vituo vya wanajeshi kwa maana ya *detach*, katika maeneo ya Manyovu, Muyama, Kitanga na Kijage, na wanajeshi hawa kwa kweli wanaishi katika nyumba duni sana kabisa kabisa na inaonekana vituo hivi ni kama vya muda tu. Sasa kwa sababu maeneo ya majirani zetu ni maeneo tete kwa muda mrefu na bila shaka kwa muda mrefu ujao. Je, ni kwanini Wizara ya Ulinzi sasa haifanyi hizi *detach* kuwa vituo kamili vya ulinzi?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, viteule ni utaratibu wa jeshi kwamba katika kila kambi ambayo iko maeneo ya mipakani kuwe na viteule vyake ambavyo vinahusika na na kufanya doria katika mipaka yetu. Kwa kawaida viteule haviwezi kuwa ni makazi ya kudumu kwa sababu vinakuwepo pale tu ambapo mahitaji yanakuwepo.

Lakini nakubaliana naye kwamba hali ya viteule hivyo kwa maana ya miundombinu bado sio nzuri na ndiyo maana nimesema Serikali inajitahidi sana katika miaka mitatu iliyopita tumekuwa tunapata nyongeza ya Bajeti kila mwaka ili kuboresha hali katika makambi pamoja na viteule anavyovizungumzia Mheshimiwa Mbunge katika mipaka yote na si Kigoma peke yake. (*Makofi*)

Na. 205

#### **Faida ya Kujiunga na Soko la Pamoja la Afrika Mashariki.**

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI** aliuliza:-

Je, Tanzani itanufaika kiasi gani kwa kuridhia Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana kwa makofi hayo na nimeelewa maana yake. (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mbunge wa Ole, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu, liliridhia Itifaki ya Soko la pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki mwezi Aprili, 2010 kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Tanzania inataraji kunufaika katika maeneo yafuatayo kwa kuridhia Itifaki hiyo:-

(i) Kuongezeka kwa soko la bidhaa, Mitaji, huduma na ajira, na vile vile kutoa fursa zaidi za uwekezaji pamoja na ushirikiano katika Nyanja za kiuchumi na kijamii.

(ii) Uhuru wa raia wa Tanzania kuingia na kutoka katika nchi nyingine mwanachama kwa madhumuni ya kufanya shughuli za kiuchumi na hivyo kupunguza umaskini.

(iii) Kufaidika na soko la watu takribani milioni 130. Hii itaongeza mauzo ya Tanzania ikiwemo bidhaa za kilimo na hivyo kupelekea wakulima wetu kuongeza kipato chao na tija katika mazao ya kilimo.

(iv) Tanzania itaweza kubuni sera na kuweka mikakati madhubuti kwa kushirikiana na nchi wanachama itakayowezesha kukua kwa uchumi na kuondoa umaskini.

(v) Uhusiano baina ya Tanzania na Nchi Wanachama utaimarika na kujenga umoja wa kikanda wenye nguvu na sauti kubwa zaidi katika nyanja za kimataifa. (*Makofii*)

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza, kwa kuwa kuna ushauri kwamba Serikali iandae mazingira sahihi na mikakati madhubuti ya kitaifa ambayo itawawezesha Watanzania kunufaika na itifaki ya soko la pamoja. Je, Serikali imejipanga vipi katika kutekeleza ushauri huo?

Kwa kuwa kuna malalamiko kwamba wananchi wa baadhi ya nchi uanachama wa jumuiya ya Afrika Mashariki wameshanunua ardhi ya Tanzania hasa kwenye maeneo ya mipakani mwa nchi. Je, Serikali inasemaje kuhusu malalamiko hayo?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu Mkakati. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuitia Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki inaratibu mkakati wa kitaifa wa kujitayarisha kuingiza nchi katika soko la pamoja. Sasa hivi mkakati huo uko katika hatua za mwisho ili kuhakikisha kwamba Watanzania wote wanashiriki kikamilifu katika soko la pamoja na kuleta maslahi kwa nchi yetu.

Pili, kuhusu ununuvi wa ardhi. Sheria za ardhi zipo, wale ambao wanajinunulia ardhi kiholela Sheria zitafuata mkondo wake na ufanuzi umetoka katika suala zima la Umoja wa Soko la Pamoja kwamba suala la ardhi linaabakia chini ya Sheria na sera za nchi Wanachama. Hivyo basi, utaratibu wa Sheria zilizopo ndiyo utaongoza utaratibu mzima wa umiliki wa ardhi nchini mwetu. Kwa wale wote ambao wamenunua ardhi

kinyemela ni vema wakazirudisha ardhi hizo kwa wahusika vinginevyo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao. (*Makofii*)

Na. 206

### **Utekelezaji wa Mradi w maji wa Umwagiliaji wa Misizwe**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Utekelezaji wa mradi wa umwagiliaji wa Misozwe umekuwa ukikwama kwa kucheleweshewa fedha za ujenzi zinazopitia Halmashauri ya Wilaya, kuharibika kwa mitambo ya ujenzi pamoja na kuondoka mara kwa mara kwa Watendaji katika eneo la ujenzi.

Je, Serikali inachukua hatua gani kurekebisha mapungufu hayo ili mradi ukamilike haraka?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, naomba nitoe maelezo mafupi kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inajenga Bwawa la Misozwe ambalo litakuwa na uwezo wa kuhifadhi maji yatakayotumika kwa umwagiliji wa hekta 100 katika skimu ya umwagiliaji wa Misozwe. Bwawa hili litawanufaisha wananchi wapatao 3,456 kutoka katika kijiji cha Misozwe na vijiji vya jirani vya Kwatango na Kicheba.

Ujenzi wa bwawa hili ulianza mwezi Januari, 2009 kwa kutekelezwa na Mkandarasi ambaye ni Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa (*Drilling and Dam Construction Agency (DDCA)*) ambaye anasimamiwa na Mhandisi wa Umwagiliaji wa Kanda ya Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, wakati wa uchimbaji wa eneo la tuta la Bwawa ilibainika kuwepo kwa mwamba mkubwa uliozuia kufikia kina cha msingi wa tuta.

Kwa ajili ya usalama wa Bwawa (*Dame Safety*) Wizara yangu ililazimika kufanya uchunguzi wa kina wa mwamba uliopo kabla ya kuendelea na ujenzi na wakati wa uchunguzi tulilazimika kusitisha kwa muda kazi ya ujenzi wa tuta.

Aidha, uduni wa vifaa vya ujenzi ambavyo Mkandarasi (*DDCA*) alikuwa navyo ulichangia kuchelewesha maendeleo ya kazi hiyo kwa sababu wakati alipoanza ujenzi alilazimika kutumia mitambo ya kukodi ambayo nayo haikuwa imara sana.

Hali hii sasa imerekebisha na sasa Mkandarasi anaendelea na kazi. Hatua ya jenzi iliyofikiwa ni asilimia 50 ambayo inajumuisha kukamilika kwa uchimbaji wa utoro

wa maji (*Spillway*) wakati kazi ya upasuaji wa mwamba na kuzuia mmomonyoko wa udongo zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda sasa kujibu swal la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua zifuatazo za kurekebisha kasoro zilizojitokeza ili kuharakisha kazi ya ujenzi inakamilika haraka iwezekamavyo.

Wizara yangu imeipatia *DDCA* mitambo mipya ikiwemo *Bull Dozer, D8* moja na kijiko kimoja (*Excavator*) ambazo ni zana za msingi katika ujenzi wa tuta. Vifaa hivyo pamoja na vingine muhimu vimepelekwa kwenye eneo la ujenzi.

Wizara imetenga shiilngi milioni 700 kwa ajili ya kukamilisha Bwawa la Misozwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa usimaizi wa kazi unaboreshwu, nimemwagiza Mhandisi wa Umwagiliaji wa Kanda ya Kilimanjaro kupeleka Watalaam Wasimamizi wa kazi ambao watakuwapo katika sehemu ya kazi mpaka kazi itakapokamilika katika mwaka huu 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, gharama za ujenzi wa mradi wa umwagiliaji wa Misozwe, zinachangiwa na fedha kutoka Mfukowa Tafa wa Kukendeleza Kilimo cha Umwagiliaji (*NIDF*) na Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji ngazi ya Wilaya (*DIDF*). Fedha za *NIDF* zinatumwa kupitia Ofisi ya Mhandisiwa Umwagiliaji Kanda ya Kilimanjaro na fedha hizi zimeanza kutumika kumlipa Mkandarasi kwa sehemu ya kazi alizokamilisha. Aidha, katika mwaka 2008/2009, Serikali iliipatia Halmashauri ya Wilaya ya Muheza shilingi milioni 100 kutoka Mfuko wa *DIDF* kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya Umwagiliaji katika Skimu ya Misozwe.

Mheshimiwa Spika, ninayo taarifa kwamba Mheshimiwa Mntangi, amekuwa anafanya jitihada za kuhakikisha kwamba kazi ya ujenzi wa Bwawa hazisimami ikiwa ni pamoja na kutoa nyumba yake mwenyewe bila malipo ili Wataalam waitumie wanapokuwa katika eneo la kazi. Kipekee nampongeza sana kwa moyo huu wa uzalendo na ninamwomba yeche binafsi na wananchi wa Misozwe kuwa subira kidogo wakati Wizara yangu inachukua hatua za kukamilisha Bwawa la Misozwe.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya. Lakini vilevile kwa jibu hili ambalo limetolewa kisayansi. Nawashukuru sana na ninapokea pongezi walizonipa.

Hata hivyo, kwa mtizamo wa mbele naomba kuuliza swal moja tu dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri nyingi ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Muheza haina watalaan wa kutosha wa umwagiliaji, na ninafahamu baada ya ujenzi wa hilo Bwawa itafuatia kazi ya ujenzi wa skimu yenyewe pamoja na kujenga vitalu.

Je, Wizara itatusaidia kama nilivyoomba kuweka andiko tayari ili kusaidia ujenzi wa hizo hekta 100 maandalizi ya skimu na vitalu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, kama ifuatavyo.

Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi tumerekebisha kasoro zilizojitokeza hapo nyuma kwa maana hiyo basi nimemwagiza Mhandisi wa Umwagiliaji ili ahakikishe kwamba Wataalam wanapatikana kwa wakati watakuwepo pale kuhakikisha wanasimamia kazi ile. Hata sasa hivi ninavyozungumza taratibu zinafanywa ili kuhakikisha kwamba zana zile nilizozitaja ikiwa ni pamoja na vifaa vyote vya kujengea vinapelekwa kwenye saiti. Naomba nimhakikishie kwamba Wataalam watakuwepo na vifaa vitakuwepo mpaka Bwawa likamilike.

**SPIKA:** Kabla sijawapa wengine kuuliza maswali ya nyongeza, naomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali anisikilize nimepokea malalamiko kadhaa na hata leo mawili hapa kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba baadhi ya shughuli wanazofanya kutekeleza ahadi kule Majimboni wanavamiwa tena na TAKUKURU.

Sasa Bunge hili uhai wake bado sasa hali hii inakuwaje yaani unamkamata Mbunge aliahidi kupeleka Cherehani kwa kikundi cha Wanawake anapeleka Cherehani zinakamatwa. Sasa ninaomba Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali atusaidie ili tuweze kutulia kule katika Majimbo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Kaboyonga swali la nyongeza halafu Mheshimiwa Said Amour Arfi.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Hali ya Muheza katika mradi wa umwagiliaji inafanana kwa kiasi fulani na miradi inayoendelezwa pale Tabora Mjini hususani tuna mradi katika kijiji cha Inala wa hekta 400. Ninapenda Mheshimiwa Waziri anieleze mpaka sasa Serikali imefikia wapi katika ombi letu la kupata msaada wa Serikali katika umwagiliaji katika eneo la Inala katika Manispaa ya Tabora.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, mradi huu wa Inala mimi nafurahi kwamba binafsi nilipata fursa ya kuupitia na kuuona na hatua tuliyokwishaifikia ni kwamba nimekwishamwagiza

Mhandisi wa Umwagiliaji wa Kanda ile aukagua na aufanyie tathmini na kazi sasa zinazoendelea ni kuandaa tu gharama za kuuendeleza mradi ule.

Halafu kuutafutia fedha na kwa kuwa fedha zake na kwa kuwa fedha zake ni nyingi kidogo basi zitaombewa katika mfuko huo wa *District Irrigation Development Fund* na ninataka nimhakikishie kwamba fedha zinatafutwa na nina hakika zitapatikana. (*Makofî*)

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, miradi mingi ya umwagiliaji inachelewa kutokana na kuwa na ofisi chache za kanda. Serikali ina mpango gani sasa wa kuteremsha wataalam katika ngazi ya mkoala ili kufanya miradi hii ikaenda haraka zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali zuri sana na Mheshimiwa Said Amour Arfi kama ifuatavyo:-

Ni kweli katika ngazi ya Halmashauri tunao upungufu mkubwa na siyo ngazi ya Halmashauri tu, hata katika ngazi nyingine tuna upungufu. Sisi tunahitaji wataalam angalau 700 lakini tulionao ni kama 166 kama kumbukumbu zangu ziko sahihi. Kwa hiyo, bado tuna upungufu mkubwa.

Lakini hatua ambayo tunaifanya kwa sababu hatuwezi kusubiri tunachukua hatua nyingi sasa hivi. Kwanza tunaendelea kuzihamasisha Halmashauri ziendelee kuweka Bajeti zao na kwa ajili ya kuajiri wataalam katika ngazi ile ya Halmashauri. Lakini wakati huo huo tunataka kuchukua wataalam ambao wako katika kanda na wengine ambao wako katika Makao Makuu kwenda kuendelea kusaidia kazi katika ngazi ya Halmashauri wakati Serikali inajienda kuajiri wataalam wengine.

Mheshimiwa Spika, kazi ya wataalam ni kazi kubwa kidogo pia inahitaji mambo ya ufundishaji wengine bado wanafundishwa katika vyuo. Kwa hiyo, lazima tuendelee kuvumiliana wakati tunasubiri kuwatafuta wataalam hao.

Na. 207

#### **Mfuko wa *Stimulus Package***

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA** aliuliza:-

Kutokana na kushuka kwa uchumi kutokana na mtikisiko wa uchumi duniani Serikali ilitenga kiasi cha shilingi trilioni 1.7 ili kunusuru kampuni binafsi na vyama vya ushirika vilivyoshindwa kujidesha kibiashara kutokana na mdororo wa kiuchumi.

- (a) Je, ni kampuni na vyama vya ushirika vingapi kwa majina idadi yamepata/vimepata kiasi gani katika mfuko huo wa *Stimulus Package*?
- (b) Je, ni kiasi gani kimetumika na kiasi kimebakia katika mfuko huu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, kabla ya kujibu swal la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) naomba kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, licha ya kwamba Mheshimiwa Mhonga amefanya masahihisho lakini napenda na mimi nitoe maelezo ya awali.

Napenda kulikumbusha Bunge lako Tukufu kuwa mpango wa kunusuru uchumi kutokana na athari za msukosuko wa kifedha duniani ulikadiriwa kugharimu kiasi cha shilingi trilioni 1.7 tu na siyo shilingi trilioni 3.6 kama alivyonukuu Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya.

Aidha, mpango huu haukuwa kwa ajili ya kunusuru kampuni binafsi ya vyama vya ushirika vilivyoshindwa kuijidesha kibashara kutokana na msukosuko wa kiuchumi pekee bali ulikuwa ni pamoja na kuziba pengo la mapato, fedha za kigeni na kunusuru ajira.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swal la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Spika, mchanganuo uliofanywa unaonyesha kuwa Makampuni na vyama vya Ushirika 99 vimetegemewa kunufaika na Mpango wa Kunusuru Uchumi. Uthibitisho na usahihi wa kiasi kilichotolewa kwa kila kampuni au chama cha ushirika utajulikana baada ya ukaguzi wa mahesabu kukamilika.

Hata hivyo, ni muhimu kuzingatia kuwa Kanuni za kibenki haziruhusu kutoa taarifa za mteja mmoja mmoja kwa umma hivyo namwomba Mheshimiwa Mbunge baada ya kukamilika kwa ukaguzi akubali kupokea idadi ya Kampuni na Vyama vya Ushirika vilivyonufaika pamoja na jumla ya fedha badala ya mteja mmoja mmoja.

(b) Mheshimiwa Spika, katika ujumla wake mpango mzima wa Taifa wa kunusuru uchumi hadi mwishowa mwezi Machi 2010, umetumia jumla ya shilingi trilioni 1.2. Utekelezaji wa mpango wa kunusuru uchumi unaendelea vizuri. Ni vigumu kwa kiasi kidogo cha fedha kilichotengwa kuweza kukidhi athari zote zilizotokana na msukosuko wa kiuchumi.

Hata hivyo, ni ukweli usiopingika kuwa mpango huu umesaidia kwa kiasi kikubwa kunusuru uchumi wetu na athari ya msukosuko wa kiuchumi.

**SPIKA:** Kabla sijaruhusu swal la nyongeza nilikuwa naona Mheshimiwa Waziri wa Kazi pamoja na kuwa viti hivi vinazunguka amekigeuza kabisa kwamba ananipa mgongo Spika. Kwa hiyo, nilikuwa naona muangalie hilo natakiwa niweze kuwaona Waheshimiwa Wabunge, huwezi kugeuka kabisa maongezi yakakolea sasa ukawa umempa Spika mgongo. (*Makofi*)

Lakini la pili ningewomba sasa arudi kwenye kiti chake kwa sababu amekalia kiti cha Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mhonga swal la nyongeza tafadhal!

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swal moja la nyongeza.

Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri kwamba pesa hizo hazikuwa kwa ajili ya makampuni binafsi na Vyama vya Ushirika pekee na kutoa maelezo ya ziada kwamba ni kwa ajili ya kuziba pengo na fedha za kigeni na kunusuru ajira.

Lakini mpaka sasa tayari zimetumika trilioni 1.2 na amesema kwamba vyama ambavyo vilitegemewa kujitokeza vilikuwa kama 99 maana yake ni kwamba havijitokeza ama vimejitokeza kidogo.

Je, Serikali ina agenda gani na fedha zilizobakia kwa nini isitolewe Elimu ya kutosha ili Vyama vingi vya Ushirika viweze kujitokeza kunufaika na mpango huo?

Swali la pili, Serikali haijaeleza kikomo cha matumizi ya mfuko huo yaani haijaeleza *period* yake itakuwaje. Je, hii siyo *EPA* ya pili?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu .....

**S PIKA:** Mheshimiwa Waziri, hii ni mara ya pili sasa unaniita Naibu Spika. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, samahani!

Mheshimiwa Spika, unajua nimefurahi sana ulivyomwondoa Mheshimiwa Kapuya kwenye kile kiti. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, samahani sana!

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, taarifa yangu nimeeleza mpaka mwezi Machi na hapa sasa hivi tupo Julai, ninachotaka kumwambia Mheshimiwa Mhonga ni kwamba tutakapokuja ku-up date tunaweza tukaona kwamba hizo fedha zilizokuwa hazijatoka mwezi Machi mpaka sasa ni kiasi gani zimeshatoka.

Kwa hiyo, namwomba avute subira kwa sababu bado zilikuwa zinaendelea kutoka baada ya kukamilisha hesabu za makampuni mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili aliuliza kwamba hatujatoa muda wa kutumia fedha hizi. Ninachotaka kumweleza Mheshimiwa Mbunge ni kwamba makampuni yaliyoomba ni 99 na hayo makampuni siyo kwamba umeeleza kwamba wewe umepata hasara na wewe umepata hasara na Serikali inakupa pesa tu, hapana! Yanafanyiwa mchanganuo, zinatazamwa risiti zake, akaunti zake, tunakwenda moja kwa moja, tuna cross check kule ambapo alipeleka mauzo vilevile kama kweli ile bei ndiyo bei iliyo kwenye ile risiti, kwa kweli yanafanyika mambo mengi tu.

Nataka nimhakikishie kwamba tukishamaliza mchakato wa haya makampuni 99 tutajua kwamba sasa muda wa hizi fedha kutumia umeshakwisha na hatutakuwa tena na muda mwingine. Sisi fedha tumezitoa lakini la msingi zaidi tunaangalia haya makampuni 99 tumalize hesabu tuweze kuwapatia hizo fedha.

**SPIKA:** Tunafidia muda wa matangazo yaliyokuwapo asubuhi ya kuwasilisha Hati. Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, swali la nyongeza.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu hili swali alisema kwamba, kuna makampuni yanafanyakazi zake binafsi kwa hiyo taarifa haziwezi kutolewa.

Je, anafahamu katika Sheria ya *Immunities and Privileges Act* ya Bunge na kwa kuwa fedha hizi zimetolewa na Serikali, ni fedha ya Serikali na ni za Umma, Wabunge wana haki ya kupata taarifa ya kila mmoja ambaye amepata fedha hizo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, sasa hivi sijakosea. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hamad Rashid, kaka yangu kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, hayo aliyoyaeleza ni sahihi kabisa lakini nilichokisema ni kwamba, taratibu za kibenki haziruhusu kutoa taarifa kwa mteja mmoja mmoja kwa

Umma. Nikiitoa hapa maana yake nimetoa kwa Umma. Lakini kwa Mheshimiwa Mbunge tunaweza tukampatia baada ya mahesabu kukamilika. (*Makofi*)

Na. 208

### **Mkoa Unaongoza kwa Umasikini Tanzania**

**MHE.MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Tanzania ina mpango wa Sera ya MKUKUTA; na kwa kuwa, Tanzania ina Mikoa Ishirini na Sita (26):-

- (a) Je, ni Mkoa gani unaongoza kwa umasikini nchini?
- (b) Je, ni Wilaya gani inafaa ipewe changamoto zaidi kwa sababu ya Umasikini wake?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleima Mussa, Mbunge wa Jimbo la Mfenesini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, utafiti wa kaya (*HBS*) uliofanyika mwaka 2000/2001 na ule wa afya uliofanyika mwaka 2005, ulionesha kuwa Mkoa wa Singida ndiyo unaongoza kwa Umasikini.

Kwa kuwa, utafiti mwingine wa kaya uliofanyikamwaka 2006/2007 haukutoa takwimu za Umasikini Ki-mkoa, kuna uwezekano mkubwa wa takwimu hizo kuwa zimepitwa na wakati. Vigezo vya msingi viliviyotumika katika kupima Umasikini ni pamoa na:-

- (i) Upatikanaji wa mahitaji wa msingi kama vile chakula, mavazi, malazi na usafiri;
- (ii) Kiwango cha uandikishaji wa watoto; wenye umri wa kujiunga na elimu ya msingi;
- (iii) Kiwango cha vifo vya watoto walio chini ya miaka 5;
- (iv) Kiwango cha kujua kusoma na kuandika;
- (v) Kiwango cha vifo vya mama wajawazito; na

(vi) Upatikanaji wa maji safi na salama.

Mkoa wa Singida ulikuwa na idadi kubwa ya watu (55%) ambao walikuwa hawapati mahitaji ya msingi.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia tafiti hizo hizo, Wilaya ya Bunda kwa upande wa Tanzania Bara ambayo ilikuwa na 68% ya watu ambao hawakuwa wakipata mahitaji ya msingi na Wilaya ya Micheweni kwa upande wa Zanzibar ambayo ilikuwa na 74%.

Cha msingi ni kuimarisha huduma za Kijamii pamoja na kutoa elimu zaidi ili wazee waweze kuona umuhimu wa wa elimu kwa watoto wao.

Aidha, kuna haja kubwa ya kubuni njia bora ambazo zitawasaidia vijana na akina mama zaidi kupata ajira. Fursa za kiuchumi zilizopo katika maeneo hayo kama vile uvuvi na ufugaji zitumike ipasavyo kwa lengo la kuinua maisha ya wananchi wa maeneo hayo. (*Makofî*)

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru pia kwa majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa.

Kwa kuwa, tafiti nyingi zimeonesha kwamba, mionganini mwa watu masikini wanawake ni masikini zaidi, na vilevile utafiti uliofanywa na Benki Kuu katika Mji wa Songea ulionesha kwamba, mfumo wa VIKOBA unasaidia katika kuondoa Umasikini;

Je, Serikali ipo tayari sasa kuorodhesha Wilaya zote ambazo zina Umasikini zaidi kwa wanawake ili iweze kuanzisha Mfumo wa VICOBRA kwa lengo la kuwasaidia kuondokana na Umasikini wa kipato? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Devota Likokola kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa Devota kwamba, utafiti unaofuata wa HBS utatoa vigezo vingine ili kuweza kuona kwamba, ni Wilaya gani ambazo zina Umasikini zaidi, na kwa kiwango gani kwa wanawake na wanaume.

Lakini vilevile nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa upande wetu Serikali tumeona umuhimu wa kuwa na VIKOBA katika maeneo yetu.

Lakini kama hilo halitoshi, Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM), tunayokwenda kuinadi tumeeleza umuhimu wa kuanzisha VIKOBA katika maeneo mbalimbali. (*Makofi*)

Na. 209

### **Kuliwezesha Shirika la Ndege – ATCL**

**MHE. LUCAS L. SELELII** aiuliza:-

Kwa kuwa Shirika la Ndege (*ATCL*) linakabiliwa na madeni na uhaba wa Ndege illi liweze kukidhi mahitaji ya usafiri ndani na nje ya nchi.

- (a) Je, kuna mpango mkakati gani wa kulifanya shirika liwe na ufanisi wa manufaa?
- (b) Je, ni fedha kiasi gani zimetengwa kuwezesha *ATCL* ishindane kimataifa?

### **NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwani niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ua Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mbunge wa Nzega, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mpango mkakati wa Serikali wa kuifanya Kampuni ya Ndege ya Tanzania (*ATCL*) ijiendeshe kwa ufanisi ni kuishirikisha sekta binafsi.

Katika jitihada za kuishirikisha sekta binafsi kuendeleza kampuni ya *ATCL*, mwaka 2007 Serikali ilimpata Mwekezaji kutoka Jamhuri ya Watu wa China ambaye alikubali kuendeleza kampuni hiyo kwa kununua asilimia 49 ya hisa za Serikali ndani ya Kampuni.

Baada ya mazungumzo ya awali na Serikali kukamilika, mwekezaji huyo kwa pamoja na *ATCL* waliandaa mpango wa muda mrefu wa Kampuni (*ATCL Strategic Plan*) ambao ulihitaji Dola milioni 507.7 kutekelezwa.

Kama hatua ya awali ya utekelezaji wa mpango huo, Mwekezaji alitoa dola milioni 21.27 ambazo pamoja na matumizi mengine, zilinunuliwa ndege mbili aina *Dash 8 – Q300* zinazotumiwa na *ATCL* kwa sasa. Matarajio ya Wizara na Serikali kwa ujumla ilikuwa kwamba kufikia wakati huu, *ATCL* ingekuwa inaendeshwa kwa pamoja kati ya Serikali na Mwekezaji huyo.

Kwa kuwa mazungumzo na mwekezaji huyo yamechukwa muda mrefu kukamilika, Serikali imeanza mikakati ya kuwasiliana na wawekezaji wengine ambao wameonyesha nia ya kuwekeza kwenye kampuni endapo mazungumzo na mwekezaji huyo yatashindwa kufikiwa muafaka.

(b)Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Serikali ilitenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya uendeshaji wa ATCL. Hata hivyo, kutokana na mahitaji mbalimbali ya kampuni, Serikali imekuwa ikitoa fedha nje ya Bajeti yake kwa ajili ya matumizi ya kampuni na hadi tarehe 30 Aprili, 2010, Serikali ilikuwa imetoea shilingi bilioni 14.89 nje ya Bajeti kwa matumizi ya kampuni.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mwekezaji huyu alitoa karibu nusu ya pesa zote ambazo zililitajika kuifufua *Air Tanzania*; na kwa kuwa, mwekezaji huyu huyu amejenga hata jengo la VIP, taarifa ambazo ninazo ni Serikali wenyewe ndiyo wanazunguka zunguka katika kukamilisha mazungumzo na mwekezaji huyu ambaye ameonesha nia ya kufanya vizuri zaidi;

Je, Serikali haoni kwamba yenyewe ndiyo inachelewesha mpango na si mwekezaji ambaye yuko tayari?

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani wa kuharakisha ukuaji wa utalii, lakini bila Shirika la ndege utalii hauwezi kukua?

Je, Serikali haoni kuwa itajipoteza mapato yake yenyewe kwa kukosa shirika la ndege la uhakika? (*Makofit*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ua Miundombinu, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelili, Mbunge wa Nzega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hili la kwanza ya kwamba Serikali ndiyo inachelewesha mchakato huu wa mazungumzo na mwekezaji huyu, nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, sisi sahihi kwa sababu jitihada zote za Serikali katika kuhakikisha kwamba, mazungumzo haya yanakamila zimekuwa zikifanyika kwa jitihada za hali ya juu sana, isipokuwa tu kwamba kumekuwa na mawasiliano hafifu kipindi fulani kutokana na kutokuwa na mawasiliano ya karibu sana na mwekezaji huyu, na ndiyo maana tumesema kwamba hatujakata tamaa bado, tutaendelea kufuutilia mazungumzo haya mpaka yaweze kukamilika. Lakini wakati huo huo tunaendelea kuwasiliana na wawekezaji wengine ambao wameonesha nia ya kuinusuru ATCL. Kwa hiyo, nia na madhumuni ya Serikali ni kuhakikisha kwamba ATCL inafufuka na kufanyakazi ili iweze kuwashudumia wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalii la pili kwamba, utalii unapotea kutokana na kukosekana kwa shirika la ndege, Tanzania. Mimi ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kabisa ya kwamba bila kuwa na shirika la ndege la uhakika la wananchi, shughuli za utalii zinaweza zikaathirika. Ndiyo maana sasa hivi jitihada hizi zote zinazofanywa na Serikali ni kuhakikisha kwamba, tunakuwa na shirika la ndege lenye uhakika ili kuweza kuwavutia watalii.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, swali la msingi ni kuhusu madeni ya ATCL, na kwa kuwa, madeni hayo yamesababishwa na wataalam kuitia Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu kwa kukodi ndege aina ya *Air Bus* ambayo walijua fika kwamba, ndege hii ingekwenda katika matengenezo baada ya muda wa miezi michache;

Je, Serikali imewachukulia hatua gani wale waliolisababishia shirika hili kupata hasara? (*Makofifi*)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nuru Bafadhili, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli baada ya kubadilika mwelekeo wa uendeshaji wa Shirika la ATCL, Serikali iligundua kwamba, ukodishaji wake wa ndege ya *Air Bus* 320 haukuwa wa tija kwa maana hiyo ni kwamba, Serikali imechukua hatua ya kusitisha mkataba huo kwa sababu hauendani tena na mpango ambao tunaenda nao.

Katika kusitisha mpango huo pia tunaangalia yejote yule ambaye alienda kinyume wakati wa kukodi ndege hiyo, hatusemi hapa kwa uhakika kwamba, kuna watu ambao waliisababishia hasara nchi, ila ni kwamba mpango umebadilika, mwekezaji ambaye alikuwa anatarajiwa kuingia, alivuta miguu kuingia katika mktaba wa kuiendedha ndege hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini nichukue fursa hii rasmi kusema kwamba, sasa hivi tumerudi katika maelewano mazuri na mwekezaji, na Serikali iko katika mchakato wa kuunda upya Shirika la Ndege ndani ya mwaka huu wa kalenda, 2010 tunatarajia kwamba kazi hiyo tuwe tumeimaliza. (*Makofifi*)

Na. 210

### **Usambazaji wa Umeme Vijijini**

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA** aliuliza:-

Kwa kuwa ni dhamira ya Serikali kusambaza umeme kwenye vijiji vyote vya hapa nchini chini ya mpango wa *Rural Electrification Programme* ikiwa ni hatua ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005.

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake hiyo ya kutandaza nyaya za umeme kwenye nguzo zilizokwisha chimbiwa na wananchi kati ya mji mdogo wa Mkwajuni na Kijiji cha Galula kilichoko umbali wa kilomita 20 tu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda, Mbunge wa Songwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa umeme kati ya Mji Mdogo wa Mkwajuni na Kijiji cha Galula unahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo kV 33 kutoka Mkwajuni kwenda Galula kupitia Vijiji vya Iseke, Mbala na Kanga, umbali wa kilomita 22 na ufungaji wa *tansfoma* nne zenye jumla ya ukubwa wa *kVA* 200. Umeme huo utatokea Mkwajuni ambapo utaungwa kwenye njia ya umeme kutoka Chunya ya msongo wa *kV* 33. Mradi huo unatarajia kugharimu shilingi 1,860,000,000 na kiasi cha wateja 140 wanatarajia kufaidika na mradi huu.

Mheshimiwa Spika, mradi wa umeme wa vijiji hivi ulianza kutekelezwa tangu mwaka 2003 na mpaka sasa kazi zilizokwishafanyika ni kufyeka na kusafisha njia ya umeme na kuchimbia nguzo umbali wa kilomita sita.

Kazi ya kumalizia kuchimbia nguzo umbali uliobaki ilishindikana baada ya nguzo zaidi ya 70 zilizokuwa eneo la ujenzi (*site*) kuchomwa moto na watu wasiojulikana.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TANESCO* inatafuta fedha zingine kwa ajili ya kukamilisha mradi huo. Naomba nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wa karibu wa mradi huu na ninamhakikishia kwamba Serikali itafanya kila jitihada ili wananchi wa maeneo haya wafikiwe na huduma ya umeme kama ilivyokusudiwa hapo awali.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa, mradi huu umechukua sasa hivi miaka 7 kabla haujatekelezwa vyovoyote vile mbali na kufyeka majani na kuchomwa nguzo.

- (a) Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuwaambia wananchi wa Songwe ni lini sasa huu mradi utatekelezeka?
- (b) Kwa kuwa, kumbukumbu zenu katika Wilaya ya Chunya ni kwamba mradi huu unakwenda sambamba na miradi ya Mlimanjiwa na Lupa miradi ambayo tayari imeshaanza kushughulikiwa. Je, ndio kusema kwamba huu mradi hivi sasa hautashughulikiwa kama kumbukumbu zetu zinavyoonesha?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Sigonda kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli mradi umechelewa lakini kama nilivyosema kwenye majibu ya msingi tatizo la kuchelewa mradi lilitokana na ile *disruption* iliyotokea ya kuchomwa moto zile nguzo. Kwa hiyo, kama kulikuwa na mpango wowote ambao

ulikuwa umeshapelekwa pale na nguzo zimeshapelekwa *site* zimechomwa moto, nguzo 70 ni kipande kikubwa cha ule mradi.

Kwa hiyo, kama nilivyosema kwenye majibu ya msingi huu mradi kwa sababu maeneo yote ya pale Chunya yanapelekewa umeme pamoja na yale maeneo ya Mheshimiwa Mwambalaswa, ninaamini kama nilivyosema kwamba tutatafuta fedha ili mradi huu utekelezwe.

Mheshimiwa Spika, kwa hili pia naomba nisisitize kwamba wananchi nao wana mchango wao pamoja na utawala wa pale kusimamia miundombinu itakayowekwa pale. Sasa kama mtu amekwenda amechoma moto nguzo 70 ametuletea hasara sisi wote na ucheleweshaji wa mradi huo.

Kwa hiyo, naomba kama ilivyo kwenye watu wanaoiba mafuta kwenye *transfoma* tuweke mkazo ule ule tuweke ili sisi sote kwa pamoja tushirikiane kulinda hii miundombinu kwa sababu hasara yake ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, hili la pili ni kweli pana mradi pale wa Mlima Njiwa na Mradi wa Lupa ambao uko kwenye miradi ambayo imetengewa fedha kwa ajili ya kuunganisha vijijini umeme unaotoka kwenye *grid*. Kwa hiyo, pale maeneo ya kwake pana mradi ule wa Makongorosi, Lupa na Tingatinga nadhani, halafu kwa Mbozi pana Mlima Njiwa.

Kwa hiyo, ni kweli kwamba kuna miradi hiyo inaendelea na jumla yote hii pamoja na ule Rungwa imetengewa shilingi bilioni 4.3. Sasa kwa kuzingatia kwamba miradi yote jumla imetengewa shilingi bilioni 99 ule ukomo wa fedha umetuzuia kwenda kukamilisha hilo na ndio maana nikasema pesa ikipatikana na mradi huu utatumbukizwa kwa sababu pale pale karibu ipo miradi inayotekelzwa na inasubiri kuunganishwa. (*Makofit*)

**MHE. RADHAMANI A. MANENO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Nina swalii dogo tu la kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na majibu yake mazuri kwenye swalii la msingi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *TANESCO* ilianza utaratibu wa kupeleka umeme katika Kijiji cha Kiwangwa ambacho umeme umetoka pale Msata lakini tangu walipoanza utaratibu wa kwenda kupima kwa ajili ya kupeleka umeme kwenye kijiji hicho ikiwa ni pamoja na umeme kutoka Kimange kwenda Mbewewe mpaka sasa jitihada hiszo naona haziendi vile ambavyo nilivyokuwa nimetarajia.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari sasa kunihakikishia katika miezi hii michache iliyobaki kuhakikisha wananchi wale wanapata huduma hii ya umeme ikiwa ni pamoja na kuwasambazia huduma hii ya umeme ambayo walikuwa wanaitarajia kwa muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli huu mradi Mheshimiwa Maneno amekuja ameufuatilia na kutoka pale Kiwangwa kutokea Msata nadhani pana kama kilomita 15 hivi, lakini kimsingi mradi huu wa umeme ni mradi muhimu kwa sababu pale pana uzalishaji mkubwa sana wa matunda. Kwa hiyo tumehimiza *TANESCO* wamalize mradi huu lakini ucheleweshaji kidogo umetokea kwa sababu pana utekelezaji wa maeneo ya Magindu kule kwa Dr. Msabaha ambao pia umechelewa chelewa kidogo.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie tu kwamba tumeshakabana na Meneja wa *TANESCO* wa Mkoa wa Pwani na tumemuhimiza kwamba mradi huu wa Kiwangwa pamoja na ule wa Magindu ambao tayari umeshaanza utekelezaji ipate kukamilika haraka iwezekanavyo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita. Kama ilivyo ada sasa ni wakati wa kusoma matangazo na tunaanza na wageni wetu. Leo hii wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundis Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, ni hawa wafuataao.

Kwanza ni mkewe Waziri anaitwa Bibi Kudra Maghembe, asimame aah yule pale, ahsante sana. Karibu sana pamoja na watoto wao ambao ni Bi. Namcheja, Bi. Namvumo. Majina ya Kipare haya sijui Namcheja ni nini na hii Namvumo ni nini, lakini nadhani yana maana fulani. (*Makofi*)

Karibuni sana familia ya Mheshimiwa Waziri tunafurahi kila mara ambapo familia zinapoungana mkono na Waheshimiwa Mawaziri wetu ambao wanafanya kazi ngumu sana katika nchi yetu. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo pia Watendaji Wakuu wa Wizara kama ifuatavyo. Kwanza ni Prof. Hamisi Dihenga, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis, yule pale. Bwana Selestine Gesimba, Naibu Katibu Mkuu, Bwana Aminiel Mrutu, Kaimu Kamishna wa Elimu, Bwana Edmund Kinwasi, Mkurugenzi Utawala na Rasilimali Watu, Bibi Marystella Wassena, Mkurugenzi Ukaguzi wa Shule, Prof. Wilbard Abeli, Mkurugenzi Elimu ya Juu, Mheshimiwa Suleiman Mwinyi, Mkurugenzi Mafunzo ya Ufundis, Bwana Martin Mwanukuzi, Kaimu Mkurugenzi Sera na Mipango na Bwana Charles Philemon, Kaimu Mkurugenzi Elimu ya Sekondari.

Wapo pia Watendaji Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis kama ifuatavyo. Prof. Mayunga Nkunya, Mkurugenzi Mtendaji Tume ya Vyuo Vikuu (*TCU*), yule pale, Dr. Joyce Ndalichako, Katibu Mtendaji Baraza la Mitihani Tanzania, ahsante sana, Dr. Ally Mcharazo Mkurugenzi Bodi ya Huduma za Maktaba, ahsante sana. Bibi Rosemary Lulabuka, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Elimu Tanzania (*TEA*), ahsante sana.

Bwana George Nyatega, Mkurugenzi Mtendaji Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, ahsante. Dr. Paul Mushi, Mkurugenzi Taasisi ya Elimu Tanzania (*TIE*), Bwana Zebadia Moshi, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis (*VETA*), ahsante

sana na Bwana Joffer Magira wa Baraza la Elimu ya Ufundu (*NACTE*), ahsante sana. Pamoja nao wapo Wakurugenzi Wasaidizi na Maafisa Waandamizi ningeomba kwa pamoja msimame ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuwatambua, wale ambao sikuwajata. Ahsante.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Waziri John Chilligati, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao ni Makatibu wa Siasa na Uenezi na Makada wa CCM jumla yao ni 30. Naomba pale walipo wasimame wale Makada wa CCM Waenezi, wale pale ahsante sana, karibu sana. Tunafurahi kuwaona. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Waziri wetu wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Mheshimiwa Bernard Membe ambao ni Watanzania walio nje ya nchi na ambao ni Viongozi wa Matawi mbalimbali ya Chama cha Mapinduzi nje ya nchi. Kwanza Mwenyekiti wa Tawi la CCM Uingereza Maina Owino hawapo kumbe. Basi naona hakuna maana kuwasoma waliosalia nadhani au wako kwenye *basement* sijui, ahsante sana. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni kama ifuatavyo. Bwana Sheikh Shughuli, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Buguruni, yule pale ye ye mwenyewe nadhani si Sheikh ila ye ye ni Bwanasheikh, mambo hayo!!! na Bwana Tamim Omar Tamim, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Tandale. Karibu sana Waheshimiwa tumefurahi kuwaona hapa. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Savelina Mwijage ni kama ifuatavyo. Mheshimiwa Honespholi Akenyanya, Diwani wa CUF kutoka Bukoba, Mheshimiwa Diwani Zainabu Marijani CUF Bukoba, yule pale, karibu sana, Ndugu Ziada Athuman, Mwenyekiti wa Wanawake CUF kule Kagera, yule pale ahsante sana. (*Makofi*)

Ndugu Alex Livinga, Kiongozi wa Vijana CUF Bukoba akifuatana na Yazidi Sabiti naye Umoja wa Vijana CUF kule Bukoba. Karibuni sana ndugu zetu. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa George Malima Lubeleje ambao ni Wakufunzi 20 kutoka Chuo cha Ualimu Mpwapwa, wale wa Chuo cha Ualimu Mpwapwa naomba wasimame tafadhali. Ahsanteni sana. Tunawahitaji sana mipango hii ya Sekondari za Kata na kadhalika basi walimu tunakuhitajini sana sana. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Devota Likokola, ambao ni kama ifuatavyo. Ndugu Zita Maliyaga, Katibu wa UWT Mkoa wa Ruvuma, Ndugu Monica Ntili, Katibu wa UWT Tunduru na Ndugu Maimuna Matendeu, Katibu wa UWT Namtumbo. Yule pale. Bi Chiku Kassim, Katibu wa UWT Mbanga, Bi. Rukia Mkindu, Katibu wa UWT Songea Vijijini, yule pale na Bi Tabia Awadhi, Katibu wa UWT lakini sasa haikumalizia ni wapi nadhani ni mojawapo ya Wilaya hizo. Karibuni sana kutoka Ruvuma.

Wageni wa Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini kama ifuatavyo. Ndugu Wilson Mtatuu, Mwenyekiti wa CCM, Babati Mjini yule pale. Karibu sana Mwenyekiti, Bwana Reginald Sanka, Katibu Mwenezi wa CCM, Babati Mjini,

ahsante sana. Bi. Fatma Hassan, Katibu wa UWT, Babati Mjini, Bwana Peter Mchuno, Mwenyekiti wa Vijana wa Wilaya ya Babati Mjini na Ndugu Kassim Issa, Katibu Msaidizi wa CCM, Babati Mjini. Ehee mwenzetu amejikusanya wapiga kura hawa.

Wageni wa Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, ni kama ifuatavyo. Prof. Robert Orr kutoka *California State Christian University*, aah yule pale Profesa. *Welcome, you have come all the way from United States, we are happy that we have these relationships person to person, institution to institutions that make quite a difference in this world. Welcome and feel at home please.*

Prof. Edward Nasioki ambaye naye anatoka *California State Christian University*. Aaah huyu Mmasai ameendelea kweli huyu, anaishi California. Bwana Gidion Nassani ambaye ni *Managing Director* wa NDC, naona hayupo ambaye amefuatana na Ndugu A. Mwakibolwa na Ndugu Msaburi, sijui ni Msaburi au Massaburi. Pamoja na hayo wapo familia ya Mheshimiwa Mzindakaya ambao ni Christopher Mzindakaya na Vailet Mzindakaya. Ahsante sana. (*Makofi*)

Bado wanaendelea Paul Mzindakaya, Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana, Mkoa wa Rukwa, David Mzindakaya, Jackline Mzindakaya, Frank Mzindakaya, Ehee !!! Mwenyezi Mungu amemjalia huyu mwenzetu maana yake si haba. (*Makofi*)

Wengine ni Mary Zumba, Lt. Zeno Nkoswe, Mwalimu Peter Mtuka, huyu atakuwa ni mzee sana ni Mwalimu wa Dr. Mzindakaya alipokuwa *Middle School*. Looch !!!! Mzee Mtuka uko wapi? (*Makofi*)

Aah Ahsante sana baba. Ahsante kwa kazi iliyotukuka kweli kweli. Maana yake Dr. Mzindakaya nadhani *Middle School* itakuwa ni miaka ya 1950 hivi. Kwa hiyo, laah!!!. Helman Mwaisawa na Mwalimu Eva Ntwenya, ahsanteni sana.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Andrew Chenge na Mheshimiwa John Cheyo ambao ni Waheshimiwa Madiwani waliotumwa na Baraza la Madiwani la Bariadi kufuatilia mafao yao. (*Kicheko/Makofi*)

Wanafuatilia mafao ya Wabunge au wanafuatilia mafao yao sijui, mafao nadhani ya Madiwani. Mheshimiwa Shiwa Danhi, Diwani ya Kata ya Satiwi *UDP*, wako wapi Waheshimiwa Diwani ooho!!! yule pale, yule pale na Mheshimiwa Juma Siyangereja Bupilipili, Diwani wa Kata ya Mwaubingi CCM.

Nadhani wamekaa pamoja pale basi Wabunge wenu watawasaidia kuweza kupata hayo mafao mnayoyafuata. Lakini inawezekana haya mafao yamechelewa kule Dar es

Salaam, kwa hiyo bado mna safari nyingine tena. Sidhani kama hapa kuna Hazina ya kuweza kuwalipa. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri Aggrey Mwanri, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ambao ni Ndugu Michiyuki Shimoda ili naona jina la Kijapan hili, aah ndiyo, *you are welcome Mr. Shimoda, welcome to the house we always welcome visitors from the development partner's groups, coming into the house. Thank's very much.* Junsuke Suzuki, Mjapan, mwingine huyo *equally welcome*, Phaniel Kyombo, Mwalimu wa Dini lakini pia muelimishaji wa masuala ya kijamii na Simon Mollel. (*Makofi*)

Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM kutoka Wilaya ya Siha yule pale, karibuni sana, karibuni sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Mtutura ambaye ni Bwana Ramadhani Mtutura Kaudagaa maarufu kule Tunduru kama Kaudagaa ni mdogo wake Mheshimiwa Mbunge. Bwana Kaudagaa uko wapi? Haya ahsante. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Pindi Chana ni wawakilishi wa Jumuiya ya UWT kutoka Mkoa mpya wa Njombe ambao ni Merry Mng'ong'o, Jane Ngenzi, Sina Mtandika, Consolata Msembele na Tumaini Mtewa, majina haya naona yanakosewa Tumaini Mdogo na Augusta Mtemi.

Wapo pia wanafunzi 30 na walimu 2 kutoka Shule ya Msingi Nkuhungu, wale vijana wa Nkuhungu Shule ya Msingi. Aah wale pale, karibuni sana, karibuni sana nyinyi ni wenyeji hapa Dodoma au angalau mnasomea hapa tunafurahi sana mnajibidisha kuja kuona shughuli za Bunge na tunawashukuru pia walimu kwa kuchukua hatua hiyo.

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Maida Ahmad Abdallah ambaye ni binti yake anaitwa Shuweika Mohamed Ali. Bi. Shuweika pale ulipo. Ahsante sana.

Sasa Idara yetu ya Elimu kwa Umma ina wageni wafuatao ambao ni wawakilishi wa viongozi wa wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu hapa nchini *TAHILSO* kama ifuatavyo Bwana Julius Twiulumba, Mwenyekiti wa *Senate* ambaye anatoka Chuo cha *KCMC*. Yule pale wako upande huu.

Bwana Prosper Ng'oro, Katibu wa *TAHLISO* kule Ruaha *University*, Bi Shamila Ismail, Katibu Msaidizi *TAHILSO* ni wa Zanzibar yule pale, karibu sana, Ndugu Doto Miteko, Kamishna kutoka Kanda ya Ziwa.

Bi. Salma Hassan Kamishna kutoka Zanzibar yule pale, Bwana Amani Nduije, Kamishna kutoka Iyuko, sijui ndiyo Iringa hii au, Ndugu Ali Sichonge, Kamishna Kanda ya Kati, Ndugu Zafarani Yusuph, Rais Mstaafu *CDTI* Arusha. Yule pale na Moses Rapson Mwakilishi kutoka Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Dar es Salaam, yule pale. (*Makofî*)

Huo ndio mwisho wa mgeni wetu, kuna mgeni mwingine. Ohoo 1!! Mheshimiwa Dr. Mzindakaya katika ile familia kumbe pia amekuja mkewe ambaye ni Mrs. Theresia Mzindakaya, yule pale, karibu sana, karibu sana. Hapa nimeandikiwa kwamba nimesahau kuwatambulisha Wakuu wa Vyuo Vikuu, sio nimesahau hawakuandikwa tu. (*Makofî*)

Tuseme aliyeleta tangazo ndio amesahau. Naomba Wakuu wetu wa Vyuo Vikuu tafadhalini msimame pale mlipo aah ndio loo!!! Watu muhimu kweli kweli hawa.

Basi Sekretariat mnapoandika matangazo mhakikishe kwamba watu wote mnawajumuisha kwenye karatasi ya tangazo, viongozi muhimu kama hawa ndiyo wa kutanguliza.

Matangazo ya kazi zetu. Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, amenitaka nitangaze kwamba Mkutano wao wa Kamati ya Fedha na Uchumi ni saa 7.00 mchana Ukumbi Na. 231. Kamati ya Fedha na Uchumi saa 7.00 mchana leo Ukumbi Na. 231.

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, anatangaza kuwa kutakuwa na Kikao saa saba mchana, Ukumbi wa Msekwa B.

Waheshimiwa Wabunge leo mchana saa saba na nusu kutakuwa na hafla ya Mahafali fupi ya kutunukiwa Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Shahada ya

Heshima ya Uzamivu. *Honorary Doctorate Degree*, itakayotolewa *California State Christian University*. Kwa hiyo, tunaombwa wale wote ambao tunafurahi kumuunga mkono tunaombwa tuwepo pale Ukumbi wa Pius Msekwa saa saba kamili. Ni sherehe fupi na ni ya Kimahafali lakini imepangwa kwa hadhi inayostahili. Ni vizuri tuwepo pale kwa sababu mwenzetu huyu ni Mbunge ambaye amekaa muda mrefu kuliko Mbunge mwingine katika Bunge hili na anatuonesha mfano, ana Kiwanda kizuri cha Nyama, anaendelea kusoma na anaendelea kutambuliwa katika Vyuo Vikuu nya mbali. Kwa hiyo, nadhani atafurahi tukimuunga mkono. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wafuatao wanatakiwa kwa haraka sana wapeleke picha (*Passport Size*) kwa Afisa Itifaki Bwana Berege. Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mheshimiwa Christine Ishengoma, Mheshimiwa Mchungaji Getrude Rwakatare, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Oscar Mukasa, Mheshimiwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali na Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene.

Tafadhalini niliowataja au wasaidizi wenu au kwa vyovvye vile, kijana wetu Herman Berege, Afisa Itifaki atakuwa pale Jengo la Utawala *Ground Floor* mumpati picha kwa mambo muhimu ambayo yanahitaji utambulisho uwepo. Huo ndiyo mwisho wa matangazo ila niseme tu wale wanaopenda sana kuondoka ondoka wiki hii ni muhimu sana, Rais atakuja kulihutubia Bunge saa kumi jioni tarehe 16. Natoa taarifa ya awali kwa sababu wengine wanakuwa mara hawapo, siku hiyo ya Ijumaa. Siku hiyo hatutakuwa na shughuli yoyote ya Bunge ila tuwepo tu Rais ataaingia saa kumi kamili kama ilivyo taratibu katika kuja kuliaga Bunge. Kwa hiyo tuwepo. Lakini zipo sababu ndogo ndogo nyingine na muhimu, wale wasiokuwepo wanaweza kudhani kwamba zile barua walizopata labda ndiyo mwisho kuna barua nyingine tena sasa usipokuwepo unawenza ukahangaika bure, kumbe Mheshimiwa Waziri wa Fedha ana mambo mazuri ameyaandaa.

Waheshimiwa Wabunge sasa namwita Mheshimiwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali kuhusu hizi vurugu zinazoendelea huko Majimboni. Badala ya kukamata mafisadi wa kweli unaanza kukamata Wabunge, sasa sijui ndiyo ukweli wenywewe. (*Makofi/Kicheko*)

### **Ufafanuzi Kuhusu Vurugu Majimboni**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ingawa mimi si Mwanachama wa Chama cha Mapinduzi, napenda kukipongeza Chama cha Mapinduzi kwa kufanya mambo mazuri, mambo mazuri sana. Kwanza kumpendekeza Rais aliyeniteua kuwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali, kuchaguliwa kuwa mgombea na pia kwa uteuzi kwa mtu makini kwa nafasi ya Mgombea Mwenza na vilevile mtu makini katika nafasi ya Urais wa Zanzibar. Nawatakia kheri sana Wanachama wa Chama cha Mapinduzi na wananchi wa Tanzania tukamilishe suala hili la uchaguzi kwa amani na utulivu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa ufanuzi kuhusu jambo ambalo nimewahi kulitoa ufanuzi. Lakini mara hii naomba kurejea kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sehemu ya Pili ambayo ina malengo muhimu na misingi ya mwelekeo wa shughuli za Serikali. Haya ni mambo ambayo tunaweza kubishana lakini hatuwezi kupingana. Ni wajibu wa viongozi wa aina zote kuhakikisha kwamba nchi yetu inatawaliwa kwa mujibu wa Sheria na kwamba Sheria za nchi zinalindwa na kutekelezwa na kuhakikisha kwamba aina zote za dhuluma, vitisho, ubaguzi, rushwa, uonevu au upendeleo zinaondolewa nchini. Anayebisha hiyo anyoshe mkono na kwamba nchi inatawalia kwa kufuata misingi ya Demokrasia na Ujamaa (*Social Justice*).

Mheshimiwa Spika, nimewahi kusikia malalamiko ya usumbufu wanaoupata Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili la Tisa wanapotoa *vikorombwezo* vya maendeleo katika Majimbo yao. Nilitoa ufanuzi kwamba Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili wataendelea kuwa Wabunge mpaka pale Bunge litakapovunjwa kwa ajili ya kuwezesha Uchaguzi Mkuu wa kawaida kufanyika na haya si maneno yangu lakini ni maneno ambayo yako kwenye Katiba Ibara ya 65 (2). Ibara hiyo inazungumzia maisha ya Bunge na inasema kwamba: “Kwa madhumuni ya Katiba hii maneno ‘Maisha ya Bunge’ maana yake ni ule muda wote unaoanzia tarehe ambapo Bunge jipya limeitishwa kukutana kwa mara ya kwanza baada ya Uchaguzi Mkuu na kwisha tarehe ya kuvunjwa kwa Bunge kwa ajili ya kuwezesha Uchaguzi Mkuu mwingine wa kawaida kufanyika”. Kifungu hicho kinasomeka na kifungu kingine cha Ibara ya Katiba ya 90 (3) kwamba: “Muda wa Maisha ya Bunge ukimalizika Bunge litahesabiwa kuwa limevunjwa”. Huo ndiyo mwelekeo wa Katiba. Kwa hiyo, Katiba inajibu maswali ambayo Waheshimiwa Wabunge baada ya wewe Mheshimiwa Spika kunitaka nieleze nimepata maswali mengi kwenye vikaratas. Hilo la kusema hili Bunge linakwisha lini? Bunge litakwisha pale ambapo litavunjwa Kisheria wala si tarehe 16. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nimepata swalí lingine kwamba Wabunge wanaporudi Majimboni tarehe 17 mwezi wa saba je, dhambi kupokelewa na wananchi wake kwamba amemaliza kazi waliyomtuma. Nini masharti ya kuzingatia, huyu ni mtu mzuri anataka ushauri wa kisheria wa bure. Jibu ni kwamba ni ruksa. Ila tarehe ya kumaliza kazi sio tarehe 17 mwezi wa saba ni baada ya hapo na kutakuwa na tangazo la Serikali kwa mujibu wa Sheria ambalo linahitimisha umri wa Bunge. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hadi wakati huo Wabunge wanayo haki na dhamana ya kusukuma ahadi za vyama vyao kwa wapiga kura. Katika ujenzi wa shule, hasa ndugu zangu kwa ajili ya mabweni ya wasichana, barabara, huduma za kijamii, kwa mfano, wale wenzetu wenyewe ulemavu, kutoa baiskeli za kuwasaidia na cherehani. Lakini katika kufanya hivyo; naomba mzingatie hii lakini na hapa afadhali niwe peke yangu. Ninaviomba vyombo vinavyohusika hasa TAKUKURU tekelezeni Sheria kama ilivyo kama vyerehani hivyo vitatolewa kwa watu binafsi wahojini wanaovitoa vyerehani hivyo na Waheshimiwa Wabunge ukiulizwa swalí naomba ujibu. Kama mtu anakuja na anafikiria kwamba hivi vitu ni vya rushwa tafadhali jibu. Usipojibu hata mimi ninayo Mamlaka kwenye hiyo Sheria ya kukushughulikia. Hivyo vitu mnavyovitoa kwa watu binafsi vinatia mashaka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba Waheshimiwa Wabunge msome kwa makini Sheria ya Gharama za Uchaguzi haswa Ibara ya 21(1) (a). Naomba sana msome hiyo Sheria na usihofu kuuliza maswali. Nitaisoma kwa Kiingereza kwa sababu ninayo hapa. Haya ni mambo yanayozuiwa. Yaani *prohibited practices*. Tiliyazungumza sana wakati wa kutunga Sheria hii. Kuna kitu kinaitwa *Unfair Conduct* (Tabia isiyofaa).

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Magufuli anamsumbuu Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Nadhani amesikia.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, during the nomination process wakati wa hatua ya uteuzi. *Election campaign*, wakati wa kampeni (or in election) wakati wa uchaguzi an act of prohibited practice shall be committed by; jambo linalozuiwa kutokutekelezwa na mtu:

“(a) Every person who, before or during the campaign period, directly or indirectly, by any other person on his behalf, gives, lends or agrees to give or to lend, or offers, promises, or promises to procure or to endeavor to procure, any money or valuable consideration to or for any voter or to or for any person on behalf of any voter or to or for any other person, in order to induce any voter to vote or to refrain from voting, or corruptly does any such act, on account of such voter having voted or refrained from voting at any nomination process or election.”

Mheshimiwa Spika, sasa hatuwezi kuzungumza mambo ya jumla na hatuwezi kulaumu watu wote. Hizi kesi za vyerehani au chochote zinazotolewa na Waheshimiwa Wabunge wa sasa zinatofautiana. Kuna wengine wanafanya kwa kuvunja kifungu, kwamba nia yake yeye ni kutoa cherehani ile kum-induce mtu yule aje akuchague na kwenye kura za maoni na nini anasema mtu wa CHADEMA pale. Kwa hiyo, someni vizuri hii Sheria, Sheria hii iko wazi huna kitu cha kuogopa, ukiulizwa swali jibu kwa sababu hata hapa ukisimama pale kwenye ukumbi unapita, kijana wa usalama anakuuliza unafanya nini hapo? Huwezi kusema, wewe hujui mimi ni Mbunge. Hapana, hilo si jibu. Tutakushughulikia tu. Kwa hiyo, toeni majibu mazuri, Capt. Komba sifahamu nia ya swali lako hili kupeperushwa bendera, je, ni halali hadi Bunge kuvunjwa. Kupeperusha bendera ya nini? Hiyo Mheshimiwa Spika atalisemea lakini nafikiri mpaka Bunge likivunjwa unapokwenda kwenye uchaguzi kwenye kampeni usiende na bendera yako. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nadhani nimejaribu kueleza kwa ufasaha na kwa mujibu wa Kiswahili ambacho kilichelewa sana kufika kwetu lakini nadhani ni Kiswahili fasaha. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Cheyo, Kanuni?

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Kanuni 68 (7).

**SPIKA:** Endelea.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, katika wiki hii tutatunga Sheria ambayo inamruhusu Waziri anayehusika na Serikali za Mitaa kuvunja Baraza lote la Madiwani siku saba kabla ya siku ambayo imetajwa na Mheshimiwa Rais kwamba Bunge limevunjwa. Sasa Sheria yenewe hatujaipitisha, ndiyo kwanza Muswada umeletwa, siku ya kuvunjwa Bunge haijatajwa. Ni vipi basi Mabaraza yote ya Madiwani yamevunjwa nchi nzima? Naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Hapo, Mheshimiwa hudai Mwongozo, umeuliza swalii na hilo linapaswa kujibiwa na Serikali. Kwa hiyo, mtajibiwa wakati unaostahili. Wamesikia, watakujibu.

Waheshimiwa Wabunge, ni mawili nataka kusema, fununu nilizonazo kwa sababu nakaa kaa kidogo na wakubwa, Bunge linaelekea kuvunjwa tarehe 1 Agosti. Nilitaka mjue hivyo tu, tarehe 1 Agosti. Kwa tafsiri sasa ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu ni kwamba kama umechelewa chelewa kutimiza ahadi, wakati wako ni mwezi huu wa Julai kuweza kutimiza ahadi. (*Makofi/Kicheko*)

Lakini, hapo hapo nitahadharishe vyombo mbalimbali, Waheshimiwa Wabunge wana *CDCF*, kuna Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo na Fedha zimetolewa mwezi uliopita na nyininge zimefika mwezi huu. Ninachoomba kwenye hili la *CDCF* na pia kwenye yale mengine aliyosema Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, jamani tuwe wawazi tu. Hii ya cherehani za usiku, hivi wewe unafikiri TAKUKURU atakuachaje kama unafikisha ka-*pick up* usiku, hakuna hata watu wanaohudhuria, hakuna risala, hakuna... (*Makofi/Kicheko*)

Kwa hiyo, Mbunge aliye makini, atasababisha risala iandaliwe, atasababisha wawepo wananchi na vyote vitatolewa hadharani na viongozi mbalimbali wakiwepo, basi hiyo ndiyo dawa! (*Makofi/Kicheko*)

Jambo lingine tu, nashangaa sana Waheshimiwa Wabunge wote mliongea na kadhalika, hakuna hata mmoja aliyenipongeza kwa kuzawadiwa shilingi 500,000/= na *Radio Clouds* kwa sababu mimi ni mmoja wa viongozi au pengine ni peke yangu tu ambaye mwezi uliopita kabla mashindano ya Woza South Africa (Kombe la Dunia), nilitabiri kwamba Hispania itakuwa Bingwa. Kwa hiyo, leo asubuhi nimetangazwa mshindi na hivi punde nakwenda kuchukua mshiko wa laki tano! (*Kicheko/Makofi*)

Kutokana na hafla hiyo, ingawa ni ndogo, lakini si haba, namwomba Mheshimiwa Job Ndugai, aje andeleze shughuli wakati nakwenda kushughulikia mambo ya Jimbo! (*Kicheko/Makofi*)

*Hapa Mwenyekiti (Mheshimiwa Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011 - Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı**

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu; baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, likubali kuitisha makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı kwa mwaka 2010/11.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana kuwa mgombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Chama cha Mapinduzi katika uchaguzi wa mwezi Oktoba mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nimpongeze sana Mheshimiwa Dr. Mohamed Ghalib Bilal kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza wa Chama cha Mapinduzi. Naomba pia nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuteuliwa kuwa mgombea urais wa Zanzibar wa Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchaguzi wa Oktoba, 2010 CCM imewaletea Watanzania viongozi hodari na wachapakazi wa hali ya juu watakaoivusha Tanzania kutoka nchi inayoendelea kuelekea Taifa la uchumi wa kati. Naungana na Wabunge na Watanzania wote kuwatachia viongozi wetu ushindi wa kishindo mwezi Oktoba, 2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, napenda kuungana na wenzangu kuzipa pole familia za marehemu Mheshimiwa Rashidi Mfaume Kawawa, Waziri Mkuu wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Muasisi wa CCM na Mheshimiwa Sigifrid Seleman Ng'itu, Mbunge wa Ruangwa waliotangulia mbele ya haki katika mwaka wa fedha wa 2009/10. Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani zangu za dhati kwa Naibu Mawaziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı, Mheshimiwa Gaudentia Mugosi Kabaka na Mheshimiwa Mwantumu Bakari Mahiza, Wabunge wa Viti Maalum kwa ushirikiano, uaminifu na uchapakazi walionionesha katika Wizara hii. Aidha, napenda kumshukuru

Katibu Mkoo wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii, Profesa Hamisi Omari Dihenga, Naibu Katibu Mkoo Ndugu Selestine Muhochi Gesimba, pamoja na Kamishna wa Elimu Mwalimu Aminiel Stephano Mrutu, Wakurugenzi wa Idara, Viongozi wa Vyuo Vikuu, Mashirika na Mabaraza Chini ya Wizara, Viongozi katika ngazi mbalimbali, Maprofesa, Walimu, Wahadhiri na Wafanyakazi wote kwa ushirikiano walionipa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara na katika maandalizi ya bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutoa shukrani na pongezi kwa Mwenyekiti Profesa Mayunga Nkunya na Wajumbe wa Baraza la Ushauri la Elimu la Taifa kwa ushauri wao mzuri. Aidha, napenda kuwashukuru Viongozi wa Vyama vyaa Wafanyakazi na Vyama vyaa Wanataluma kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Mwanga kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2005. Ripoti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya yetu inaonyesha utekelezaji wa hali ya juu uliofikia takriban asilimia 95. Hivyo, nawaomba wana-CCM na wananchi wa Mwanga waendelee kuniunga mkono katika kura za maoni zilizo mbele yetu ili tuendelee kuiletea Wilaya yetu maendeleo ya Kimbunga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani zangu za dhati kwa mke wangu mpenzi Kudra Maghembe na watoto wangu Ngwali Maghembe, Dr. Mwanamkuu Maghembe na Mcheja na Namvuma Maghembe kwa upendo, misaada ya kila aina na uvumilivu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkoo na Waziri wa Fedha na Uchumi kwa hotuba zao nzuri ambazo kwa pamoja zilitoa tathmini na mwelekeo wa Bajeti ya Serikali na hali ya uchumi na maendeleo ya nchi yetu kwa ujumla. Aidha, hotuba hizo zimeeleza utendaji wa kazi za Serikali na mwelekeo kwa mwaka 2010/2011. Kwa hali hiyo, hotuba yangu itatoa ufanuzi wa Makadirio na Matumizi yanayohusu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Omar S. Kwaangw' kwa kufanya kazi ya uchambuzi wa kina na kwa ushauri wao katika kuimarisha utekelezaji wa bajeti hii na maendeleo ya elimu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoleza katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka uliopita, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii imekabidhiwa majukumu yanayohusu, Elimu ya Awali na Msingi; Elimu ya Sekondari; Mafunzo ya Ualimu; Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi, Elimu ya Juu, Elimu ya Ufundii na Mafunzo ya Ufundii Stadi na Taasisi na Mabaraza yaliyo chini ya Wizara yanayosimamia ubora wa elimu na mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2009/2010 na matarajio ya Mwaka 2010/2011. Naomba nianze kwa kutoa tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2009/10 na baadaye nitatoa mwelekeo wa Mapato na Matumizi kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu ilipanga kukusanya maduhuli ya Serikali Shilingi 4,510,784,000. Hadi tarehe 30 Juni, 2010; Shilingi 6,325,283,914 zilikuwa zimekusanya. Lengo lilivukwa kutokana na baadhi ya shule za sekondari ambazo zimegatuliwa kuendelea kuwasilisha maduhuli yao katika hesabu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu hadi mwezi Oktoba 2009. Kuanzia mwezi Novemba, 2009 maduhuli hayo yanawasilishwa kwenye Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2009/2010 bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu ilikuwa Shilingi 428,436,913,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya hizo, Shilingi 41,039,652,700 zilikuwa za Mishahara na Shilingi 387,397,260,300 zilikuwa za Matumizi Mengineyo. Hadi tarehe 30 Juni, 2010, matumizi ya kawaida yalikuwa Shilingi 421,204,126,333, ambapo Shilingi 40,536,159,244 zilikuwa za mishahara na Shilingi 380,667,967,089 zilikuwa za matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka 2009/10 ilikuwa Shilingi 129,283,697,000. Kati ya hizo, fedha za ndani zilikuwa Shilingi 65,366,471,999 na za nje zilikuwa Shilingi 63,917,225,001. Hadi kufikia Juni, 2010 ni asilimia 62 ya fedha hizo zilipokelewa, yaani shilingi bilioni 79.6. Hadi tarehe 30 Juni, 2010, matumizi yalikuwa Shilingi 80,453,399,723.05 ambapo Shilingi 50,207,557,2344 zilikuwa fedha za ndani na Shilingi 30,245,842,489 zilikuwa fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya ya jumla ya mapato na matumizi niliyoyatoa, ifuatayo ni taarifa ya Utekelezaji wa majukumu ya Wizara na malengo kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Kamishna wa Elimu ina majukumu ya kuratibu utoaji wa elimu katika ngazi za Awali; Msingi; Sekondari; Mafunzo ya Ualimu; Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi; pamoja na Udhibiti wa ubora wa Elimu, Ukuzaaji Mitaala, Uendeshaji Mitihani, Huduma za Maktaba na Mafunzo ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu. Ofisi ya Kamishna wa Elimu inajumuisha vitengo vya Elimu Maalum, Elimu kwa Mawasiliano, Usajili wa Shule, Ithibati ya Vifaa vya Elimu na Masuala Mtambuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Ofisi ya Kamishna wa Elimu:-

(a) Ilitoa Mafunzo ya Elimu Jumuishi, Stadi za Braille na lugha ya alama (*Sign Language*) kwa wakufunzi 57 wa vyuo vya Ualimu Kasulu na Kabanga;

(b) Ilichambua maombi 354 ya hatua mbalimbali za usajili, ambapo 112 yalikubaliwa na kupewa vibali vya kuendelea na ujenzi na 198 yalithibitishiwa wamiliki na mameneja wa shule. Aidha, maombi 44 yalirudishwa kwa wadau kwa ajili ya marekebisho;

(c) Iliandaa na kutangaza vipindi 580 vya Redio, ambapo vipindi 52 vilikuwa vya ufundishaji kwa kutumia mbinu shirikishi na 528 vilikuwa vya masomo ya redio kwa Shule za Msingi.

(d) Ilipokea maombi 229 ya kusajili shule ambapo shule 112 zilizojengwa kwa nguvu za wananchi na shule 117 (Awali tatu, Awali na Msingi 46, Sekondari 57 na Vyuo vya Ualimu 11) zisizo za Serikali ziliidhinishwa na kusajiliwa;

(e) Ilitoa leseni za kufundisha kwa walimu 293;

(f) Ilikamilisha uandaaji wa ‘Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Masuala ya Kielimu kwa Kuzingatia Usawa wa Kijinsia;

(g) Ilifuatilia utoaji wa Elimu Maalum na Elimu Jumuishi na uanzishwaji wa shule au vitengo vya Elimu Maalum na Elimu Jumuishi katika Halmashauri 16;

(h) Ilisambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia wanafunzi wenyewe mahitaji maalum katika shule 272 za msingi, 29 za Sekondari na Vyuo vya Ualimu sita;

(i) Iliteua vitabu viwili vya kiada kwa kila somo la Elimu ya Awali na msingi kwa ajili ya darasa la 1 – 5;

(j) Ilitoa Waraka Na. 2 wa Mwaka 2010 kuhusu vitabu vya kiada shulenii na kutoa mwongozo wa usambazaji wa vitabu teule;

(k) Ilitoa ithibati kwa vitabu 34 vya kiada kwa shule za Msingi. Aidha, ilitoa ithibati kwa vitabu vya sekondari vya masomo ya Hisabati, Fizikia, Kemia na Biolojia kwa kidato cha I na cha II , kupitia Programu ya msaada wa watu wa Marekani (*USAID*);

(l) Ilipitia Miswada ya vitabu 105 vya elimu ambapo Miswada 34 ilipewa ithibati na 41 ilikataliwa;

(m) Ilipitia upya nyaraka 128 zilizoandaliwa kati ya mwaka 1997 na 2009 na kuzihuisha; na

(n) Iliandika Sura 2 kati ya 8 za rasimu ya taarifa ya matokeo ya utafiti ngazi ya taifa kuhusu ubora wa elimu katika nchi 15 za Kusini na Mashariki ya Afrika (*SACMEQ Project III*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/10, Wizara yangu iliendelea kutekeleza awamu ya pili ya MMEM (2007-2011) ili kuhakikisha kuwa lengo la Serikali la kutoa Elimu ya Awali na Msingi kwa wote linafikiwa. Idara ya Elimu ya Msingi:-

(a) Ilitoa huduma jumuishi za malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto, Wizara yangu ilishiriki katika kuandaa Sera Jumuishi ya Malezi Makuzi na Maendeleo ya Mtoto;

(b) Iliimarisha utoaji wa Elimu ya Awali Wizara, kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mtandao wa Malezi, makuzi na Maendeleo ya Mtoto na *UNICEF* iliratibu uandaaji wa: Mwongozo na Viwango vya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Mtoto; Mwongozo wa Wawezeshaji wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya awali ya Mtoto; Mwongozo wa Vifaa vya Kufundishia na vifaa vya michezo kwa watoto wadogo;

(c) Ilitimiza azma ya Serikali ya kuwa na darasa la awali katika kila shule, Wizara iliratibu uandikishaji wa wanafunzi wa Elimu ya Awali wa shule za Serikali na zisizo za Serikali ambapo idadi ya wanafunzi wa Awali iliongezeka kutoka 638,591 mwaka 2005 (wasichana 319,974) na kufikia 925,465 (wasichana 463,837) mwaka 2010. Kati ya hao, 1,771 ni wanafunzi wenyewe mahitaji maalum. Aidha, idadi ya mikondo ya Elimu ya Awali iliongezeka kutoka 21,607 mwaka 2005 hadi 34,861 mwaka 2010. Walimu wa Elimu ya Awali waliongezeka kutoka 11,148 (wanawake 6,510) mwaka 2005 hadi 16,534 (wanawake 8,884) mwaka 2010;

(d) Idadi ya wanafunzi wa elimu ya msingi iliongezeka kutoka 7,541,208 (wasichana 3,685,496, wavulana 3,855,712) mwaka 2005 hadi 8,419,305 (wasichana 4,216,036) mwaka 2010 wakiwemo wanafunzi 36,585 wenyewe mahitaji maalumu. Walimu wa Elimu ya Msingi waliongezeka kutoka 135,013 (wanawake 64,707) mwaka 2005 hadi 165,856 (wanawake 83,686) mwaka 2010. Aidha, Shule za Msingi ziliongezeka kutoka 14,257 mwaka 2005 hadi 15,816 mwaka 2010. Uwiano wa Mwanafunzi kwa mwalimu uliimariika kutoka 1:56 (mwalimu mmoja kwa wanafunzi 56 ) na kufikia 1:51 (mwalimu mmoja kwa wanafunzi 51);

(e) Ilishirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Monduli kuanza ujenzi wa shule ya Msingi Monduli Jeshini (*Sokoine Cantonment*) na kukarabati shule za mfano ikiwemo Shule ya Arusha (*Arusha School*).

(f) Iliandaan na kutoa machapisho ya miongozo ya ununuzi wa vifaa, ujenzi wa shule, uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza, uimarisaji wa taratibu za kitaasisi, hesabu na usimamizi wa fedha, ununuzi wa vitabu vya kiada na vifaa vingine vya elimu na ufuatiliaji na tathmini kwa ajili ya utekelezaji wa MMEM II. Nakala 2,625 za miongozo hiyo zilisambazwa katika Mikoa na Halmashauri zote Tanzania Bara;

(g) Ilifanya ufuatiliaji, tathmini, utafiti na ukaguzi wa matumizi ya fedha za MMEM kwa kushirikiana na TAMISEMI;

(h) Iliratibu utoaji wa mafunzo kazini kwa walimu 270, ili kuwajengea uwezo wa ufundishaji wa masomo ya Hisabati na Sayansi;

(i) Iligharimia utoaji wa mafunzo katika usimamizi wa elimu kwa viongozi 11, wasimamizi wa elimu 494 wakiwemo Walimu Wakuu, Waratibu Elimu Kata na Maafisa Elimu ngazi ya Halmashauri;

(j) Ilifuatilia matumizi ya ruzuku ya uendeshaji ya shilingi bilioni 80 (shilingi 10,000 kwa kila mwanafunzi kwa mwaka) kwa ajili ya kuinua ubora wa elimu katika

Mikoa ya Mara, Shinyanga, Mbeya, Singida, Rukwa, Dodoma, Lindi Mtwara, Kigoma, Tabora, Manyara na Pwani;

(k) Ilishirikiana na *WFP* katika kuongeza wigo wa ufadhilli wa Mradi wa Lishe Shuleni kutoka Halmashauri 13 (Bahi, Longido, Iramba, Manyoni, Kondoa, Chamwino, Karatu, Simanjiro, Kiteto, Ngorongoro, Mpwapwa, Singida (V) na Monduli) hadi kwenda 16, ikijumuisha Halmashauri za Kishapu, Shinyanga Vijijini na Meatu). Tathmini ya Mradi huu katika shule za Wilaya 16 inaonesha kuongezeka kwa mahudhurio na kupungua kwa mdondoko;

(l) Iliandaa rasimu ya mwongozo wa ufundishaji wa somo la sayansi kwa njia ya majaribio; na

(m) Iliwajengea uwezo wa uendeshaji wa mradi wa *Bridge – IT* walimu 1,000 na Wakaguzi wa shule 17, wawezeshaji 17, kanda za video 417 za kufundishia masomo ya sayansi na Hisabati kwa wanafunzi wa darasa la V na VI ambapo wanafunzi 60,000 wananaufaika na mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Idara ya Elimu ya Sekondari. Elimu ya Sekondari ni kiungo muhimu kati ya Elimu ya Msingi na Elimu ya Juu. Idara ya Elimu ya Sekondari inasimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu katika ngazi hii, kutoa elimu bora kwa usawa kuanzia kidato 1–6 na kufanya ufuatilaji na tathmini ya ubora wa elimu itolewayo. Utekelezaji wa Sera ya elimu katika ngazi hii unalenga katika kuongeza nafasi za elimu ya sekondari na kuhakikisha kuwepo idadi kubwa ya wahitimu wa Kidato cha 6 kwa ajili ya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Idadi ya shule za sekondari imeongezeka kutoka 1,745 mwaka 2005 na kufikia 4,266 mwaka 2010, kwa kujenga shule 3,397 za serikali katika ngazi ya Kata na shule 869 mpya zisizokuwa za Serikali. Aidha, wanafunzi wa elimu ya sekondari kidato 1-6 wa shule za serikali na zisizo za Serikali waliongezeka kutoka 524,325 mwaka 2005 (wasichana 244,571) hadi 1,638,699 mwaka 2010 (wasichana 728,528). Wanafunzi waliojiunga na kidato 1 waliongezeka kutoka 180,239 mwaka 2005 (wasichana 88,559,) na kufikia 438,827 mwaka 2010 (wasichana 198,810). Wanafunzi waliojiunga na Kidato cha tano waliongezeka kutoka 18,893 mwaka 2005 (wasichana 7,147) na kufikia 38,334 mwaka 2010 (wasichana 15,278). Walimu wa shule za sekondari waliongezeka kutoka 23,905 mwaka 2005 kufikia 40,517 (wanawake 12,696) mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upimaji na tathmini ya elimu ya sekondari ulifanyika na mafanikio kadhaa yalijitokeza. Katika kipindi cha mwaka 2005 na 2009, matokeo ya upimaji huo yalijidhihirisha katika ongezeko la kiwango cha ufaulu wa mitihani ya kidato cha nne na sita. Kati ya wanafunzi 85,292 wa Kidato cha nne walifanya mitihani mwaka 2005, wanafunzi 27,298 walifaalu na kupata daraja la IIII. Kati ya hao, wanafunzi 6,322

(23.2%) walitoka shule kongwe za Serikali, 7,933 (29.2%) walitoka 11 shule za sekondari za wananchi za kutwa na 12,953 (47.6%) walitoka shule zisizo za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009, jumla ya wanafunzi 239,434 walifanya mitihani ya Kidato cha nne. Kati ya hao, wanafunzi 41,363 walifaalu kwa kiwango cha daraja la I-III, ambapo wanafunzi 20,742 (50.15%) walitoka shule za wananchi za kutwa, 4,121 (9.96%) walitoka shule kongwe za Serikali na 16,500 (39.89%) walitoka shule zisizo za Serikali. Haya ni mafanikio makubwa sana katika utekelezaji wa mfumo wetu wa Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu hizi zinaonesha kuwa idadi kubwa ya wanafunzi waliofaalu katika kiwango cha daraja la I-III ambao ndiyo wenye sifa za kuchaguliwa kijiungu na masomo ya kidato cha tano ni kutoka shule za sekondari za kutwa zilizojengwa na wananchi. Hali hii ya ufaulu imetokana na ushirikiano mkubwa kati ya serikali na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2009 wanafunzi wa shule zetu za Sekondari walishiriki katika shindano la uandishi wa insha kwa nchi za Jumuiya ya Ushirikiano Kusini mwa Afrika (*SADC*) ambapo Tanzania iliibuka na ushindi wa kwanza na wa pili. Mwanafunzi aliyekuwa mshindi wa kwanza ni Allen Kamnde kutoka Shule ya Sekondari ya Seminari ya Maua na wa pili ni Mary Hingira kutoka Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Machame. Aidha, shule zetu ziliibuka na kuwa na mshindi wa tatu katika shindano la insha la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mwanafunzi aliyepeata ushindi huu ni Peter Emil kutoka katika Shule ya Sekondari ya Tosamaganga. Pamoja na ushindi huu, mwanafunzi Happiness Watimanywa, kutoka *St. Constantine Secondary School* iliyoko Arusha alishika nafasi ya kwanza duniani katika mtihani wa somo la Uhasibu unaoendeshwa na *University of Cambridge, International Examination Syndicate* mwezi Juni 2009. Ushindi huu ni mkubwa na wa kujivunia katika mafanikio katika ngazi hii ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya ongezeko la ufaulu wa wanafunzi yamechangiwa na jitihada za Serikali kuendelea kutoa vifaa vya kujifunzia na kufundishia katika shule; kutoa mafunzo kwa walimu 3,000 wa masomo ya sayansi na hisabati pamoja na kuendesha kambi za sayansi kwa wanafunzi wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha usimamizi wa uendeshaji wa shule za Sekondari, Serikali iligatua uendeshaji wa shule hizo na kuziweka chini ya mamlaka za Halmashauri za Wilaya. Ili kufanikisha utaratibu huu, Wizara iliratibu taratibu za kupeleka usimamizi na uendeshaji wa shule za sekondari katika mamlaka za serikali za mitaa na kutoa Miongozo na mafunzo ya awali kwa maafisaelimu wa Elimu ya Sekondari na maafisaelimu Taaluma kwa kushirikiana na OWM - TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Elimu ya Ualimu ina jukumu la kutoa Elimu ya Ualimu ngazi ya Cheti na Stashahada, kuandaa na kupitia Sera, Miongozo na Viwango vya Elimu ya Ualimu na kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Maendeleo na Menejimenti ya Walimu MMEMWA (*Teacher Development and Management Strategy -TDMS*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo ya elimu ya ualimu ya daraja A na Stashahada hutolewa katika vyuo vya ualimu 34 vya Serikali na 57 visivyo vya Serikali ambavyo vyote kwa pamoja vina uwezo wa kudahili wanachuo 43,098 kwa wakati mmoja. Aidha, baadhi ya vyuo vikuu hutoa Elimu ya ualimu ngazi ya Stashahada. Vyuo vikuu hivyo ni: *Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), State University of Zanzibar (SUZA), Muslim University of Morogoro (MUM), Mwenge University College of Education, St. Augustine University of Tanzania (SAUT), Teofilo Kisanji University (TEKU), Sebastian Kolowa University (SEKUCO), Tumaini University na Mount Meru University*, Chuo Kikuu Mzumbe, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya wahitimu katika vyuo vya Ualimu imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Mwaka 2009/10 wahitimu Daraja A walikuwa 12,305. Mwaka 2010/11, walimu 14,501 wanatarajiwa kuhitimu mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti. Kati ya hao, 7,939 wanatoka Vyuo vya ualimu vya Serikali na 6, 562 wanatoka katika Vyuo vya Ualimu vya watu na Mashirika binafsi. Aidha, katika mwaka 2009/10, wahitimu wa Stashahada walikuwa 5,530. Mwaka 2010/11, Wizara inatarajia walimu 7,084 kuhitimu mafunzo ya ualimu ngazi ya Stashahada. Walimu 6,815 wanatoka katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali na walimu 269 wanatoka katika Vyuo vya Ualimu vya binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la wahitimu katika vyuo vya ualimu limechangiwa na jitihada za serikali na washiriki wa elimu katika kutoa Elimu ya Ualimu ambapo vyuo vya ualimu vimeongezeka kutoka 52 (33 vya Serikali) mwaka 2005 mpaka 77 (34 vya Serikali) mwaka 2010. Katika mwaka 2007, Serikali iliibadilisha Shule ya sekondari Shinyanga (*Shinyanga Commercial Secondary School - SHYCOM*) kuwa Chuo cha Ualimu wa Stashahada kwa masomo ya biashara na mwaka 2008, Serikali ilianzisha Chuo cha Ualimu Dakawa ili kukabiliana na upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2010, walimu 12,464 wa Daraja ‘B’ na ‘C’ walipewa mafunzo na kupandisha kiwango chao kuwa Daraja ‘A’.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Idara ya Elimu ya Ualimu:-

(a) Iliwapatia mafunzo ya ualimu walimu wanafunzi 15,572 wa ngazi ya Cheti A na 12,529 wa Stashahada katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali na kuratibu mafunzo ya ualimu kwa walimu wanafunzi 12,529 wa ngazi ya cheti na 913 wa ngazi ya stashahada katika vyuo binafsi;

(b) Iliwapatia mafunzo ya TEHAMA walimu wanafunzi wa stashahada 5,855 na ambao wamefanya mtihani wa Baraza mwezi Mei 2010;

(c) Iliwapatia wakufunzi 596 Mafunzo Kazini kuhusu ufundishaji kwa vitendo masomo ya Sayansi, TEHAMA na *English*;

(d) Iliendesha mafunzo kazini kwa wakufunzi 300 kuhusu matumizi ya TEHAMA katika kufundisha na kujifunza;

(e) Iliwapatia mafunzo kabilishi (*orientation*) wakufunzi 528 waliopata ajira mpya vyuoni baada ya kuhitimu vyuo vikuu;

(f) Iliwapatia mafunzo ya Elimu kwa Michezo Wakufunzi 30 kutoka vyuo vya Ualimu 12 katika Chuo cha Ualimu Butimba kwa ushirikiano na Shirika lisilo la Kiserikali la Liike kutoka Finland;

(g) Ilitayarisha Vigezo vya Ubora wa Elimu ya Ualimu (*Teacher Competency Framework*) na kutoa mafunzo kazini kwa walimu 154 wa Shule za Msingi kwa ushirikiano na UNESCO na UNICEF;

(h) Ilitoa Mafunzo ya walimu kazini kuhusu Mbinu za ufundishaji Bainifu na Elimu ya Kinga dhidi ya VVU/UKIMWI kwa wakufunzi 154, walimu 50 wa shule za Msingi, walimu 240 wa shule za sekondari na wakaguzi wa shule wa Mkoa wa Kigoma chini ya mpango unaogharimiwa kwa pamoja na mashirika ya Umoja wa Mataifa (*One UN-Joint Programme*);

(i) Iligharimia mafunzo ya Walimu wa leseni 637 wanaosomea ualimu chuo Kikuu Huria cha Tanzania na watumishi wengine 385 wanaosoma vyuo vikuu ndani na nje ya nchi; na

(j) Iliratibu ukarabati na utoaji wa vifaa kwa ajili ya Maabara tatu za lugha katika Vyuo vya Ualimu vya Butimba, Morogoro na Mtwara Ufundii kwa ushirikiano na Shirika la USAID.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi. Moja ya majukumu ya Idara hii ni kuleta msukumo mpya katika juhudhi za Serikali za kukabiliana na ongezeko la watu wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu. Jukumu la idara hii ni kutoa fursa ya kuijendeleza kielimu nje ya mfumo rasmi wa shule mionganoni mwa vijana na watu wazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi:-

(a) Ilianda muswada (*script*) wenye masomo 65 ya redio na televisheni, kitabu cha mwanakisomo, miongozo ya wawezeshaji na wasimamizi kwa ajili ya kufundishia Elimu ya Watu Wazima kuititia programu ya Ndiyo Ninaweza katika Halmashauri za Temeke, Ilala, Kinondoni, Ilemela, Dodoma Mjini, na Songea Manispaa. Mpango mkubwa wa kupanua mafunzo ya kisomo wa Ndiyo Ninaweza nchi nzima umekamilika na utekelezaji utaanza mwezi Septemba 2010;

(b) Ilifanya ufuutiliaji na kuratibu vituo vya Mpango wa Uwiano kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii (MUKEJA) vyenye jumla ya washiriki 987,289 na

vituo vya Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA) vyenye washiriki 82,989 katika Halmashauri zote nchini;

(c) Ilifanya tathmini ya utekelezaji wa Mkakati wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi na kutoa taarifa itakayowezesha kuandaliwa kwa Mpango Mkakati kwa kipindi cha 2010/2011 – 2014/2015; na

(d) Ilifanya ufuutiliaji wa utekelezaji wa Mpango wa Mambo Elimu unaotoa elimu ya msingi kwa watoto wa jamii za wafugaji (Halmashauri za Ngorongoro, Kiteto na Loliondo) na jamii za wavuvi (Halmashauri za Lindi Mjini, Vijijini, Mtwara Mjini na Vijijini).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi: Idara ya Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi ina majukumu ya kubuni, kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Ufundu na Mafunzo. Katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Serikali iliongeza nafasi na ubora wa mafunzo, ambapo Vyuo vya Ufundu Stadi viliongezeka kutoka 819 mwaka 2005 hadi kufikia 889 mwaka 2010. Katika kipindi hicho, idadi ya wanafunzi waliokuwa wakisomea mafunzo ya ufundu stadi iliongezeka kutoka 89,031 (wasichana 31,625) mwaka 2005 hadi 129,468 (wasichana 52,684) mwaka 2010. Katika kuimarisha ubora wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu, Idara iliratibu uanzishwaji wa mafunzo yanayozingatia umahiri (*Competence-Based*) katika vyuo vya ufundu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mwaka 2005/2006 na 2009/2010, Vyuo vya Ufundu Stadi vya Songea, Arusha na Singida vilijengwa. Vyuo 19 vya Oljoro VTC, Mikumi; VTC; Kagera, VTC; Musoma, VTC; Dakawa, VTC; Ulyankulu, VTC; Tabora, RVTSC; Shinyanga, VTC; Mpanda, VTC; Moshi, RVTSC; Dodoma, RVTSC; Tanga, RVTSC; Iringa, RVTSC; Mbeya, RVTSC; Kihonda, RVTSC; Dar es Salaam, RVTSC; Mwanza, RVTSC; Kigoma, RVTSC na Morogoro VTTC vilikarabatiwa na kupewa vifaa, wakati Vyuo vitano (5) vya Ufundu vinaendelea kujengwa katika Mikoa ya Lindi, Manyara, Pwani, Dar es Salaam na Makete. Mfumo wa Tuzo wa Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi (*Technical and Vocational Education and Training Framework*) ulianzishwa na Serikali ambapo utekelezaji wake unasimamiwa kwa pamoja na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu (NACTE) na Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundu Stadi (VETA).

Mfumo huu unaozingatia umahiri unatekelezwa katika ngazi mbili. Ngazi ya kwanza ni kwa wanafunzi wanaosomea cheti ngazi ya ufundu Stadi (*National Vocational Awards Level 1- 3*) na ngazi ya pili ni wanafunzi wanaosomea Cheti, Stashahada, Shahada, na Shahada ya Uzamili (*National Technical Awards Level 4-10*). Hadi sasa, utekelezaji wa mfumo huu umefikia wahitimu wanaomaliza ngazi ya Shahada (NTA 8). Mfumo huu wa mafunzo ni muhimu kwa sababu unawawezesha wahitimu wa Vyuo vya Mafunzo ya Ufundu Stadi kuendelea na mafunzo katika ngazi za juu zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuchangia katika kutoa wataalamu ngazi ya kati, Vituo vinne (4) vya Mafunzo ya Ufundi na Huduma vya Mkoa (*Regional Vocational Training and Services Centres*) vya Dar es Salaam, Tanga, Moshi na Mtwara vimetambuliwa na Bodi ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*NACTE*) ili vianze kutoa mafunzo ngazi ya cheti hadi stashahada (*NTA Level IV – VI*). Katika mwaka wa fedha 2010/2011, vyuo hivi vinatakiwa kukamilisha mipango ya msingi ambayo itakidhi matakwa ya changamoto zilizopo kabla ya kuanza mafunzo rasmi katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/10, Idara ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi:-

(a) Iliongeza udahili katika elimu ya ufundi na iliratibu upanuzi wa Elimu ya Ufundi ngazi ya Cheti na Stashahada kwa kuanzisha programu ya mafunzo ya Stashahada ya Sayansi ya Teknolojia ya Maabara katika Chuo cha Ufundi Arusha na kudhamini wanafunzi 505 wa mafunzo ya Stashahada;

(b) Iliwezesha kila Wilaya kuwa na kituo cha ufundi stadi kwa kufanya uchambuzi wa mahitaji ya stadi katika Wilaya 15 ambazo ni Tandahimba, Nanyumbu, Ruangwa, Liwale, Sumbawanga, Nkasi, Manyoni, Babati, Hanang, Mkuranga, Kyela, Magu, Serengeti, Rarya na Kongwa. Aidha, iliendeleza mashauriano na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto juu ya kuviongezea uwezo wa kutoa mafunzo ya ufundi stadi Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 35;

(c) Ilipanua wigo wa fani za ufundi stadi idara kwa kuratibu uanzishwaji wa Mradi wa '*Education for Employment – (EFE)*' chini ya udhamini wa *CIDA – Canada*, ukiendeshwa na *Association of Canadian Community Colleges (ACCC)* kwa kuhusisha vyuo vya ufundi na ufundi stadi 13 vinavyotoa mafunzo katika fani za Utalii, Kilimo na Madini; na

(d) Iliinua ubora wa mafunzo ya ufundi na ufundi stadi kwa kuhamasisha wanafunzi wa kike kujiunga na elimu na mafunzo ya ufundi. Aidha, iliratibu ushirikiano wa *Italian-Tanzanian Technical Education and Labour Market Support Programme* katika Chuo cha Ufundi Arusha ambapo chuo kimenafaika kwa kupatiwa *Euro 200,000* za kununulia vifaa vya kufundishia, na *Euro 40,000* za kusaidia kuinua ubora wa mafunzo yatolewayo pamoja na kusomesha wanafunzi wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Elimu ya Juu ina majukumu ya kutunga, kusimamia na kutathmini Sera, Sheria, Taratibu na Miongozo ya utoaji wa Elimu ya Juu. Elimu hii hutolewa katika Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki 11 vya Umma na 21 visivyo vya Serikali. Kazi za msingi zinazofanywa na Vyuo Vikuu ni kufundisha, kufanya utafiti unaolenga katika kuinua maisha ya wananchi na kutoa ushauri wa kitaalam kwa Serikali na umma kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti unaofanywa vyuoni una manufaa sana kwa kuvipandisha hadhi vyuo vikuu vyetu kitaaluma, kusaidia wananchi kuondokana na umaskini, pamoja na kuongeza uzalishaji viwandani na mashambani. Baadhi ya maeneo

muhimu yaliyofanyiwa utafiti ni pamoja na chanjo ya UKIMWI, kubaini vijidudu vya malaria kwa haraka, kubaini usugu wa dawa za malaria kwa lengo la kudhibiti malaria nchini, uhifadhi wa ardhi na mazingira kwa ujumla, uzalishaji wa mbegu bora za mazao na kudhibiti wadudu waharibifu wa mimea na wanyama na ufugaji bora wa kuku wa kienyeji na mbuzi wa maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 Wizara yangu imefanikisha ongezeko la udahili katika Elimu ya Juu, ambapo wanafunzi wa vyuo vikuu wameongezeka kutoka 40,993 mwaka 2005/2006 hadi 118,951 mwaka 2009/2010. Jumla ya wanafunzi 10,884 walidahiliwa mwaka wa kwanza katika Taasisi za elimu ya juu zisizo kuwa Vyuo Vikuu zinazotoa shahada (8,824 Shahada ya Kwanza, 249 Uzamili na 1,811 Shahada za Uzamivu) na wanafunzi 9,947 walidahiliwa katika taasisi zinazotoa Stashahada ya Juu (*Angalia Kiambatisho*. Aidha, wanafunzi 130,060 wa Elimu ya Juu walipewa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Sheria ya vyuo vikuu ya mwaka 2005, kila chuo kinatakiwa kuwa na Hati Idhini. Nafurahi kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mpaka sasa vyuo vikuu 17 vimeshapata Hati Idhini na vinaongozwa kwa kutumia Kanuni na Miongozo ya Hati Idhini zao. Vyuo vingine viko katika hatua mbalimbali za kukamilisha zoezi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imechukua juhudzi za makusudi za kulitafutia ufumbuzi wa kudumu, tatizo la uhaba wa walimu katika shule za sekondari kwa kuongeza udahili katika Shahada za Ualimu katika Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki vya Umma na Vyuo Vikuu binafsi. Aidha, kuanzia mwaka 2007/2008 Serikali imekuwa ikitoa mkopo kwa wanachuo wote wanaochukua Shahada za Ualimu, ili kuongeza idadi ya wanachuo wanaojiunga na mafunzo ya ualimu. Nia ya Serikali ni kuondoa kabisa tatizo la uhaba wa walimu shulenii. Ili kuvutia zaidi walimu wa sayansi, kuanzia mwaka 2009/2010 Serikali imekuwa ikiwapatia mikopo ya asilimia 100 wanafunzi wa programu za ualimu na wanaosomea masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha programu za shahada za ualimu katika vyuo vikuu ambapo, vyuo vikuu 10 visivyo vya Serikali (*University College of Education Zanzibar, Tumaini University – Makumira College, Muslim University of Morogoro, Mwenge University College, St. Augustine University of Tanzania, St. John’s University, Sebastian Kolowa University College, Tumaini University – Iringa College, Teofilo Kisanji University na University of Arusha*) vinaendesha programu za ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa vyuo vya Serikali vinavyotoa programu za ualimu, ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa, Chuo Kikuu Huria,

Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na Chuo Kikuu Mzumbe. (Angalia Kiambatisho Na. 18). Kutokana na ongezeko la Idadi ya Vyuo vinyavyotoa mafunzo ya ualimu, Idadi ya wahitimu wa Shahada za Ualimu imeongezeka kutoka walimu 2,760 mwaka 2005 kufikia walimu 5,331 wa mwaka 2009. Idadi hiyo inatarajiwa kuongezeka kufikia walimu 12,120 watakaohitimu kwenye vyuo Vikuu mwaka wa 2010. Aidha, walimu wa shahada watakaohitimu mwaka kesho ni 11,849, na wale wanaotarajiwa kuhitimu mwaka 2012 watakuwa 13,411.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010 Idara ya Elimu ya Juu:-

- (a) Iligharimia Wanafunzi 90 (85 raia wa Uganda na watano wa China) katika mpango wa kubadilishana wanafunzi;
- (b) Iliendelea kuelimisha umma juu ya dhana ya uchangiaji wa gharama za Elimu ya Juu na fursa za Elimu ya Juu kwa kuwatemeblea wadau mbalimbali wa elimu katika mikoa mitano ya Mara, Kigoma, Manyara, Arusha na Singida. Jumla ya shule 50 zilitembelewa na kuwafikia wanafunzi 7,481;
- (c) Ili kupunguza tatizo la wahadhiri, iligharimia mafunzo ya Wanataluma 80 kutoka vyuo vikuu 10 vya umma katika masomo ya shahada za uzamili na uzamivu na kugharimia mafunzo ya wahadhiri 18 wa shahada ya Uzamivu kwa kushirikiana na shirika la DAAD la Ujeruman. Aidha, idara iliratibu skolashipu 193 zinazotolewa na nchi mbalimbali;
- (d) Ilikamilisha na kuzindua Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Juu (MMEJU);
- (e) Iliwezesha wafanyakazi 131 katika vyuo 8 kujiunga na mafunzo ya Shahada za Uzamili na Uzamivu kupitia Mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu (*Science Technology and Higher Education Project*) unaoendeshwa kwa mikopo wa Benki ya Dunia kwa lengo la kuimarisha ufundishaji wa sayansi na teknolojia katika Elimu ya Juu ambapo jumla ya programu tano zimepitwa na kufanyiwa marekebisho; na
- (f) Iiliandaa rasimu ya namna ya kushirikisha Taasisi za fedha katika kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kama njia mbadala ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Ukaguzi wa Shule ina majukumu ya kuhakikisha kuwa Sera, Sheria, Kanuni na Viwango vya utoaji elimu vilivyowekwa vinatekelezwa kwa ufanisi katika shule za awali, msingi, sekondari, vitengo vya elimu maalum, vituo vya ufundidi stadi, Elimu ya Watu Wazima na Elimu nje ya Mfumo Rasmi na vyuo vya ualimu. Mwaka 2005 – 2010, idara iliimarisha Ukaguzi wa shule kwa kuongeza wakaguzi wa shule 365, kukarabati ofisi za Ukaguzi wa shule katika Wilaya 55 na kununua samani za ofisi katika wiliya 53. Aidha, zilinunuliwa kompyuta 120 na magari 91 kwa ajili ya ofisi za kanda na Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Idara ya Ukaguzi wa Shule:-

- (a) Ilikagua jumla ya asasi 9,960 ambayo ni asilimia 49.56 ya asasi 20,094 zilizokuwa zimelempewa. Aidha, ilifanya ukaguzi maalum kwa ajili ya uanzishwaji wa shule mpya za sekondari 147 na msingi 51 na kuchunguza tuhuma na matukio maalum katika shule za sekondari 27 na shule za msingi 627. (Jedwali Na. 1 kinaonesha utekelezaji wa malengo ya ukaguzi wa shule hadi Juni 2010);
- (b) Ilikarabati ofisi za ukaguzi wa shule katika Wilaya 20 na kununua samani za ofisi kwa ajili ya Wilaya 20 na magari 27 kwa ajili ya ofisi za Kanda na Wilaya;
- (c) Ilifanya ufuutiliaji ili kubaini asasi za kielimu zinazoendeshwa kinyume na taratibu katika Mkoa wa Dar es Salaam, ambapo asasi 830 zilipatikana na makosa. Kati ya hizo, 203 zilikutwa na dosari ndogondogo na 627 zilikutwa na dosari kubwa na kuagizwa kusitisha mara moja utoaji elimu;
- (d) Iliendesha Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Pili mwaka 2009 ambapo matokeo ya mtihani yalikuwa kama ifuatavyo: kati ya watahiniwa 394,508 waliojiandikisha kufanya mtihani, 364,957 (92%) walifanya mtihani huo. Watahiniwa 238,267 (65.3%) walifaulu, ambapo wavulana walikuwa 142,691 na wasichana 95,576. Aidha, watahiniwa 126,690 (34.7%) walifeli mtihani huo; na
- (e) Ilizanzisha utaratibu mpya wa kufanya ukaguzi wa shule ambapo shule zilizobainika kuwa chini ya wastani wa ubora wa shule uliowekwa zitakaguliwa zaidi ya mara moja kwa mwaka ili kufuutilia utekelezaji wa ushauri na kutoa msaada wa kitaalam na kitaaluma mpaka kufikia kiwango cha juu cha ubora wa shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Sera na Mipango inahusika na utoaji wa kitaalam na huduma katika utekelezaji, ufuutiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010 Idara ya Sera na Mipango:-

- (a) Ilikusanya na kuchambua maoni ya wadau kuhusu Sera ya Elimu na Mafunzo na kuandaa rasimu ya kwanza ya pendekezo la Sera Mpya. Rasimu hii iliwasilishwa kwenye Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii mwezi Februari 2010 kwa ajili ya kupata maoni;
- (b) Iliendelea kuimarisha mfumo wa takwimu za elimu (*Educational Data Base System*) katika Halmashauri 105 zilizobaki kwa kushirikiana na UNESCO kupitia programu ya *ESMIS*. Mfumo wa takwimu za elimu katika Halmashauri za Wilaya 28 zilizo kwenye majaribio (*Pilot*) ziliendelea kuimarishwa;
- (c) Iliratibu uanzishwaji wa mradi wa *Tanzania beyond Tomorrow* ambao unahusu ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia TEHAMA kwenye shule za sekondari;

(d) Ilikarabati baadhi ya miundombinu kwenye vyuo vya ualimu vya Vikindu, Mhonda na Ilonga;

(e) Ilikarabati maabara tatu (3) za Lugha katika vyuo vya ualimu vya Butimba, Morogoro na Mtwara Ufundu na kuzipatia vifaa husika kwa ushirikiano na Shirika la *USAID*;

(f) Ilianza ujenzi wa shule mpya ya Miono inayojengwa kwa ushirikiano na Kampuni ya *Cushman and Wakefield ya Brussels - Ubelgiji*; na

(g) Ilijenga shule mbili za Msingi kwa msaada wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China huko Msoga – Pwani, na Kiteto - Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Utawala na Rasilimaliwatu inasimamia masuala ya utawala, ajira, maslahi na maendeleo ya watumishi pamoja na sheria, kanuni, taratibu za utumishi na kuratibu masuala ya Programu ya Kuboresha Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara yangu ilikabiliwa na madeni makubwa ya ndani yaliyojumuisha madai ya walimu na watumishi wasio walimu, wazabuni na posho za nyumba kwa wahadhiri wa Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2009/2010 Idara ya Utawala na Rasilimaliwatu:-

(a) Ilishughulikia madai ya watumishi 25,440 yenye thamani ya shilingi 22,779,602,062 yaliyohusu malimbikizo ya mishahara, gharama za matibabu, likizo, safari za kikazi na gharama za masomo. Ilihakiki madeni hayo na kulipa kiasi cha shilingi 5,321,096,409.22 ikiwa ni madai yaliyokubaliwa wakati wa uhakiki kwa kushirikiana na ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Aidha, Wizara bado inaendelea kushughulikia madai yaliyochelewa kuwasilishwa. Mpaka kufikia tarehe 07/06/2010, Wizara yangu imepokea jumla ya madai yenye thamani ya shilingi 6,203,679,120.60;

(b) Iliunda Kikosi Kazi (*Task Force*) kwa ajili ya kushughulikia rufaa za madeni zilizowasilishwa baada ya kukataliwa. Kamati hiyo inahusisha Maafisa toka Tume ya Utumishi wa Umma, Idara ya Utumishi wa Walimu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Chama cha Walimu Tanzania na Maafisa kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu. Hadi kufikia mwezi Mei 2010, jumla ya shilingi 17,703,392,146 zilikuwa zimelipwa kwa wazabuni;

(c) Ilishughulikia malipo ya madai ya wazabuni waliota huduma ya chakula na vifaa vya maabara ambapo, hadi kufikia mwezi Mei 2010, jumla ya shilingi bilioni 17.70 zilikuwa zimelipwa; na

(d) Ilishughulikia malipo ya madai ya wazabuni waliota huduma ya chakula na vifaa vya maabara ambapo, hadi kufikia mwezi Mei 2010, jumla ya shilingi bilioni 17.70 zilikuwa zimelipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo cha Habari Elimu na Mawasiliano kina majukumu ya kuratibu utoaji na upokeaji wa habari za kielimu na kushirikiana na vyombo vya habari na wadau wengine wa sekta ya elimu katika kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/10, Kitengo cha Habari Elimu na Mawasiliano:-

(a) Kiliandaa na kuratibu urushaji wa vipindi 30 vya redio na televisheni ili kuifahamisha na kuhamasisha jamii kuhusu mikakati, mafanikio na changamoto za sekta ya elimu katika kutekeleza mipango ya elimu;

(b) Kiliandaa na kuchapisha nakala 25,000 za Jarida la *EdSDP* na kuzisambaza katika Kanda za elimu, taasisi na Wizara mbalimbali ili kuhamasisha jamii kushiriki katika kutekeleza mipango ya elimu;

(c) Kiliratibu maandalizi ya majibu ya maswali 30 yaliyopokelewa kutoka Tovuti ya Wananchi; na

(d) Kiliandaa Mkakati wa Mawasiliano kuhusu Ugatuaji wa Uendeshaji wa Shule za Sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala, Taasisi na Mabaraza yaliyo chini ya Wizara yangu yanawajibika katika kuchangia usimamizi na hatimaye kufanikisha utoaji wa elimu bora nchini. Mwaka huu, kila Wakala, Taasisi na Baraza lilitekeleza kazi zilizopangwa kwa kuzingatia malengo na mipango ya elimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (*TEWW*) ina jukumu la kutoa mafunzo ya elimu ya Watu Wazima na elimu ya kujiendeleza katika mfumo usio rasmi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima:-

(a) Iliongeza idadi ya wanachuo wa Elimu Masafa na Ana kwa Ana kutoka 30,036 hadi 49,533 ambayo ni asilimia 99.1 ya idadi iliyokuwa imelengwa ya 50,000;

(b) Ilitoa mafunzo ya cheti kwa walengwa 40, stashahada 371, stashahada ya Juu 128 na Shahada ya Elimu ya Watu Wazima (*NTA Level 7-8*) 82;

(c) Iliwajengea uwezo wakufunzi na wahadhiri 56 wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima katika kufundisha kwa kutumia mtaala unaozingatia soko la jira na masharti ya *NACTE* yanayolenga katika kuwapa umahiri (*Competence-Based Education and Training*);

(d) Ilianizisha programu ya *Integrated Post-Primary Education (IPPE)* ambayo inajumuisha Elimu ya Sekondari, ufundi stadi na masuala mtambuka, katika wilaya za Temeke, Bagamoyo, Siha, Mtwara Vijijini, Hai, Magu na Makete;

(e) Iligharimia mafunzo ya watumishi wawili wa shahada ya Uzamivu; tisa shahada ya Uzamili, mmoja wa Stashahada ya Juu, wawili wa cheti, 15 mafunzo ya muda mfupi na watano wa Elimu ya Sekondari;

(f) Ilinunua vifaa vya studio itakayotumika katika kutoa elimu ya masuala mtambuka, haki za binadamu, utunzaji wa mazingira, afya bora, umaskini na elimu ya kujikinga na UKIMWI kwa umma nchini;

(g) Iliunda Kamati ya Kudhibiti Ubora (*Quality Assurance Committee*) ili itengeneze mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya programu za *TEWW*; na

(h) Ilifuatilia na kutathmini utekelezaji wa mpango wa Elimu Masafa (*Open Distance Learning - ODL*) katika vituo vya mikoa 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Elimu Tanzania ina majukumu ya kubuni na kuandaa mitaala na mihtasari ya elimu ya awali, msingi, sekondari, ualimu na elimu maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/10, Taasisi ya Elimu Tanzania:-

(a) Iliendesha mikutano 15 ya paneli za masomo ya mitaala ya shule na Vyuo vya Ualimu ili kupata maoni yatakayochangia katika kufanya mapitio ya mihtasari na hivyo kuinua ubora wa elimu;

(b) Iliandika moduli za masomo 26 kwa ajili ya mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti ambayo inasubiri kuhaririwa, na miongozo ya kufundishia masomo ya Kidato cha 1 – 4 ambayo inasubiri kuhakikiwa na kuchapishwa;

(c) Iliandika miongozo ya walimu ya kufundishia masomo 25 ya mtaala wa masomo ya Kidato cha tano na sita ambayo iko katika hatua ya uhakiki na uhariri;

(d) Illichapa na kusambaza vitabu 24 vya mwaka wa pili wa MEMKWA vya kundi-rika 1 na 2;

(e) Ilikamilisha maandalizi ya vipindi 6 vya redio na televisheni kwa ajili ya masomo ya Hisabati na Kiingereza kwa darasa la III na IV;

(f) Iliandaa chati za somo la sayansi kwa ajili ya darasa la I-VII ambazo zinasubiri kufanyiwa majaribio kabla ya kuchapishwa; na

(g) Ilifanya majaribio ya miongozo ya kufundishia UKIMWI katika shule za awali na msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania ina jukumu la kutoa na kusambaza huduma za maktaba kwa watu wote nchini; kuanzisha, kuendesha, kuongoza, kuimarishe, kutunza na kuendeleza Maktaba za Umma kuanzia ngazi za Mikoa, Wilaya hadi Vijiji na kutoa mafunzo na kuendesha mitihani ya Taaluma ya Ukutubi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania:-

(a) Ilikamilisha mpango mkuu wa kiwanja (*Master Plan*) kwa ajili ya Chuo cha Ukutubi na uhifadhi Nyaraka, Bagamoyo. Aidha, ilinunua viwanja viwili kwa ajili ya kujenga hosteli;

(b) Iliimarisha na kuboresha huduma za Maktaba kwa watu wazima na watoto katika mikoa 19 ikiwa ni pamoja na kuongeza machapisho 63,519 ya vitabu, magazeti na majarida 35,257, kurakai vitabu 135 na kujaridi mabunda 65 ya magazeti;

(c) Ilitoa mafunzo ya Ukutubi na Uhifadhi wa Nyaraka kwa walengwa 113 wa Stashahada, 192 wa Cheti na 151 wa mafunzo ya muda mfupi;

(d) lihamasisha wananchi katika mikoa 21 nchini ili wajenge utamaduni wa kusoma, kwa kuendesha matamasha mawili ya vitabu katika mkoa wa Dar es Salaam na kuongeza idadi ya wasomaji kufikia 886,103; na

(e) Ilitoa ushauri wa kitaalam juu ya uanzishaji, upangaji na uendeshaji wa Maktaba za vyuo na taasisi. Ushauri ultolewa kwa maktaba 89 za shule, moja ya chuo na moja ya taasisi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (*Agency for the Development of Educational Management - ADEM*) una majukumu makuu manne: kuandaa na kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu; kutoa ushauri wa kitaalamu katika mambo yanayohusu Uongozi na Uendeshaji wa Elimu; kufanya utafiti katika masuala yanayohusu Uongozi na Uendeshaji wa Elimu na kuandaa na kusambaza makala na vitabu mbalimbali vya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu. Katika kipindi cha 2005 – 2010, Wakala umeweza kutoa wahitimu 671 wa Stashahada ya Usimamizi wa Elimu (*Diploma in Education Management*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu ulitekeleza yafuatayo:-

(a) Ulitoa mafunzo ya stashahada ya Uongozi wa Elimu kwa wanachuo 289 kati ya 300 waliokuwa wametarajiw;

(b) Ulitoa mafunzo ya Cheti cha Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Walimu Wakuu 100 wa Shule za Msingi kati ya 500 waliokuwa wamelengwa katika Vyuo vya Ualimu vya Tabora na Butimba;

(c) Ulitoa mafunzo ya Uongozi na Uendesahji wa Elimu kwa Waratibu Elimu kata 435 kutoka katika wilaya za Manyoni, Newala, Tandahimba, Bariadi, Meatu, Mpanda, Nkasi, Manispaa ya Morogoro, Kilosa, Ulanga, Ilala, Handeni, Kilindi, Mwanga, Rombo, Siha, Biharamulo, Chato, Muleba na Ngara. Mafunzo haya yanakamilisha lengo la kutoa mafunzo kwa Waratibu Elimu Kata nchi nzima;

(d) Ulitoa mafunzo juu ya utayarishaji wa Mpango wa Jumla wa Maendeleo ya Shule (*Whole School Development Planning*) kwa Maafisa 185 kati ya 194 waliolengwa;

(e) Ulitoa mafunzo ya mwezi mmoja ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa washiriki 92 yaliyoshirikisha Maafisa Elimu Taaluma wa Mikoa. Maafisa Elimu Taaluma na Maafisa Elimu Vifaa na Takwimu wa Wilaya 80 kutoka Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Kilimanjaro, Ruvuma, Singida, Pwani, Shinyanga, Morogoro, Rukwa, Mbeya na Kigoma; na

(f) Ulikamilisha ripoti ya utafiti wa kielimu kuhusu kuinua Ubora wa Uongozi, kwa kuzingatia athari za tabia za Wakuu wa Shule katika kumotisha utendaji wa walimu. Mradi huu uliendeshwa chini ya mtandao wa *LEAD-link (Leadership in Education for African Development)* unaohusisha nchi za Tanzania, Malawi, Uganda, Zambia, Sudan, Swaziland, Msumbiji na Afrika Kusini. Mtandao huu unafadhiliwa na Uholanzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa ya UNESCO ina majukumu ya kulishirikisha Taifa katika utekelezaji wa programu za UNESCO nchini kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nyanja za Elimu, Sayansi Asilia, Sayansi Jamii, Utamaduni, Mawasiliano na Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Tume ya Taifa ya UNESCO:-

(a) Iliratibu ushiriki wa ujumbe wa Serikali na wataalamu mbalimbali katika masuala ya UNESCO kwenye Kikao cha 35 cha Mkutano Mkuu wa UNESCO ambapo mjambe mmoja aliwakilisha vijana;

(b) Iliendelea kusimamia, kuratibu, pamoja na kutathmini utekelezaji wa miradi chini ya *Participation Programme* kwa kipindi cha 2008/2009.

(c) Iliendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya Kuhifadhi Historia ya Ukombozi Barani Afrika;

(d) Iliendelea kuratibu Programu ya Uhuishaji wa Mfumo wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa kushirikiana na *UNESCO*;

(e) Ilisimamia utekelezaji wa miradi chini ya sekta tano za *UNESCO* pamoja na programu ya Mwaka wa Kimataifa wa Astronomia;

(f) Iliendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya Taifa ya Mwaka wa Kimataifa wa Sayari Dunia (*Intenational Year of Planet Earth- IYPE*);

(g) Illichapisha na kusambaza toleo Na. 6 la Jarida la Tanzania na *UNESCO*;

(h) Iliendelea kutoa elimu kuhusu masuala mtambuka ya jinsia, mazingira na Haki za Binadamu chini ya Mtandao wa Shule (*Associated School Project Network*); na

(i) kuimarisha Mtandao wa *UNESCO* wa shule zilizoshirikishwa (*Associated Schools Project Network*) kwa kushirikiana na asasi za Serikali na zisizo za kiserikali Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Mitihani la Tanzania lina majukumu ya kuweka sera ya mitihani kwa kuzingatia Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha, Baraza lina majukumu ya kuendesha Mitihani ya Kumaliza Elimu ya Msingi na Sekondari, Ualimu ngazi ya Cheti na Stashahada, mtihani wa Maarifa na kusimamia uendeshaji wa mitihani itolewayo na bodi za nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/10, Baraza la Mitihani la Tanzania:-

(a) Liliendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi 2009 kwa watahiniwa 1,024,448;

(b) Liliendesha Mitihani ya Kidato cha Nne kwa watahiniwa 351,152 na Mtihani wa Maarifa (*QT*) kwa watahiniwa 25,040;

(c) Liliendesha Mtihani wa Kidato cha Sita 2010 kwa watahiniwa 65,629 na Mitihani ya Ualimu Mei 2010 ambapo jumla ya watahiniwa 22,212 walisajiliwa;

(d) Lilisimamia Mitihani ya Bodi za Nje kwa watahiniwa 832;

(e) Lilinunua printa ya kisasa ya kuchapia vyeti vyenye icha za watahiniwa ili kudhibiti udanganyifu;

(f) likamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa Kituo ha Usahihishaji Mitihani cha Mbezi kilichoanza utumika rasmi Mei 2010; na

(g) Lilifanya uhakiki wa vyeti 54,357 vilivyowasilishwa na asasi mbalimbali ambapo vyeti 1,756 sawa na silimia 3.2 vilibainika kuwa ni vya kughushi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Maendeleo Dakawa chenye eneo la Ekari 7,500 kina jumla ya nyumba 82 na majengo mengine muhimu yanayowezesha uendeshaji wa: Chuo cha Ualimu chenye jumla ya Wanachuo 580 na Wafanyakazi 50; Shule ya Sekondari ya Wasichana yenye kidato cha tano na sita ambayo ina jumla ya wanafunzi 450 na wafanyakazi 20, Chuo cha Ufundı Stadi- VETA chenye jumla ya Wanachuo 160 na wafanyakazi 20, Shule ya Msingi ambayo ina wanafunzi 400 wa Elimu ya Msingi na 50 wa Elimu ya Awali pamoja na walimu 15. Aidha, kituo kina Zahanati inayotoa huduma kwa wanajamii 4,500 walio ndani ya kituo na maeneo ya jirani. Zahanati hii ina Maafisa Tabibu wawili na Wauguzi watatu. 63.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo kina majukumu ya kutunza na kuhifadhi majengo, vifaa na miundombinu iliyokabidhiwa na ANC kwa ajili ya kulinda historia ya ukombozi Kusini mwa Afrika. Baada ya Serikali ya Tanzania kukabidhiwa Kituo cha Maendeleo Dakawa kutoka kwa wapigania Uhuru wa ANC, Wizara yangu imekusudia kukiendeleza na kukitumia katika kutoa Elimu ya Sayansi na Ufundı kupitia Taasisi zilizopo na zitakazoanzishwa hapo Dakawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Kituo cha Maendeleo Dakawa:-

(a) Kilisimamia na kukarabati matanki ya kuhifadhia maji safi na njia kuu ya majisafi kwa umbali wa kilomita 17 kutoka chanzo cha maji (Wami) hadi kituoni;

(b) Kilitoa huduma ya kuondosha majitaka katika makazi ya watu ambayo jumla yao ni zaidi ya 2,000 na kufanya matengenezo ya mifumo ya majisafi na majitaka;

(c) Kiliratibu na kusimamia utunzaji wa mazingira ya kituo yenye eneo la kilometra za mraba 28 kama kiliv yokabidhiwa na ANC; na

(d) Kiliratibu shughuli za kampuni ya ulinzi iliyopewa zabuni ya kulinda eneo zima la kituo na kudhibiti usalama wa vifaa na miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Elimu Tanzania ina majukumu ya kutafuta na kubaini vyanzo mbalimbali vya mapato kwa ajili ya kugharimia maendeleo ya sekta ya elimu nchini ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha wadau wa elimu kuchangia kwa hiari katika miradi ya elimu. Katika kipindi cha 2005 – 2010, mamlaka iliweza kukusanya Shilingi bilioni 4.7 na kutumia shilingi bilioni 34.3 kugharimia maendeleo katika sekta ya elimu. Vyuo Vikuu na Vyuo vya Ufundı 25, Vyuo vya ualimu 16 na shule

za awali na za msingi 61 na za sekondari 724 zimenufaika. Aidha, mamlaka ilitoa ufadhili wa Shilingi 91.8 milioni kwa ajili ya *Pre-entry Programme* kwa wasichana katika vyuo vikuu viwili na na vyuo vya ufundi viwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/10, Mamlaka ya Elimu Tanzania:-

(a) Iliendelea kutafuta rasilimali mbadala kwa ajili ya mfuko wa elimu kwa kuandaa harambee, kuwekeza katika amana za muda mfupi na kutafuta wahisani wa kufadhili au kusaidia baadhi ya miradi. Kufuatia jitihada hizi Shilingi milioni 836 zilipatikana. Kadhalika wahisani wafuatao wameonyesha nia ya kufadhili miradi ya elimu: *Abbott Fund* (Mradi wa maabara za sekondari), *Sightsavers International* (Mradi wa kuwawezesha wanafunzi wenyewe ulemavu wa kuona kujifunza kwa kutumia TEHAMA, Songas, (mradi wa madawati na vitabu);

(b) Iliendelea kupokea maombi na kufadhili miradi mbalimbali ya elimu yenyе kulenga katika kuongeza ubora wa elimu na udahili, na kuleta usawa wa kijinsia. Taasisi 177 zilipata ufadhili wenyе thamani ya shilingi 1.9 bilioni kwa ajili ya miradi ya kuinua ubora wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Aidha, Mamlaka iliendelea kufadhili kozi za awali (*Pre-entry Programmes*) kwa wanafunzi wa kike wanaojiunga na Vyuo Vikuu;

(c) Iliendeleza ushirikiano na Halmashauri katika kuhimiza uanzishwaji wa mifuko ya elimu pamoja na kuhamasisha wadau kuchangia elimu kwenye maeneo yao, kwa kuandaa harambee kwa pamoja. Mamlaka ilishiriki kwenye harambee za Halmashauri 12 kwa lengo la kuzaidia kuchangisha;

(d) Iliandaa rasimu ya marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Elimu No. 8 ya mwaka 2001 ambapo zoezi la kuandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri umeanza;

(e) Iliendelea kutoa elimu kwa umma na kutoa taarifa kupitia vyombo vya habari, vipeperushi na majarida. Aidha, Mamlaka ilishiriki katika vipindi vya radio na televisheni. Tovuti ya TEA [www.tea.or.tz](http://www.tea.or.tz) iliimarishwa kwa kubadili muonekano wake na kurahisisha utafutaji taarifa. Aidha, mamlaka iliandaa jarida la televisheni juu ya mfuko na kampeni ya kuchangia wanafunzi wenyе mahitaji maalum (wenye ulemavu);

(f) Ilifanya tathmini ya miradi 90 kwa lengo la kupima matokeo ya ufadhili; na

(g) Ilikamilisha makubaliano ya kununua majengo yanayomilikiwa na Shirika la Bima yaliyopo Mikocheni B kwa ajili ya matumizi ya ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania ina jukumu la kutoa ithibati, kuratibu uanzishwaji wa Vyuo Vikuu, kuhakiki ubora wa elimu na kuidhinisha programu zifundishwazo ili zikidhi mahitaji ya Taifa na soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania:-

(a) Iilitathmini ubora wa programu 25 za masomo ya Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu vishiriki nchini kwa lengo la kuziidhinisha;

(b) Ilikamilisha rasimu ya andiko la Mfumo wa Tuzo zinazotambuliwa Kitaifa (*National Qualifications Framework*) na kuanza maandalizi ya andiko la kanuni za mfumo wa tuzo;

(c) Iilitathmini vyeti 250 vilivyowasilishwa na wahitimu wa vyuo vikuu toka nje ya nchi kwa lengo la kutambua uhalali wake;

(d) Iliratibu na kutathmini mradi wa majaribio ya kudhibiti ubora wa programu za vyuo vikuu 5 (*St. John's University, University of Dodoma, State University of Zanzibar, Dar es Salaam University College of Education na Muslim University of Morogoro*) vinavyotekeleza mradi huo chini ya *IUCEA*;

(e) Ilikagua na kutathmini mipango ya kuanzisha au kuhuisha vyuo vikuu saba kwa lengo la kutoa hati husika. Vyuo hivyo ni: Chuo Kikuu cha Dodoma, St. John's University, *Nelson Mandela African Institute of Science and Technology*, Chuo Kikuu kitarajiwa cha *Eckenford (proposed Eckenford University)*, *St. Augustine University of Tanzania – Mtwara Centre*, *Kampala International University – DSM Centre* na Chuo Kikuu kitarajiwa cha Mara (*proposed Mara University*); na

(f) Ilian芝ha mfumo mpya wa udahili wa pamoja wa wanafunzi ujulikanao kama *Centralized Admission System (CAS)* ambao unahusisha vyuo vya elimu ya juu 43 (hivi ni pamoja na Vyuo vya Elimu ya Juu visivyokuwa Vyuo Vikuu) ili kuondoa uwezekano wa mwanafunzi mmoja kudahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja na hivyo kuwanyima nafasi Watanzania wengine wenye sifa za kujiunga na Taasisi nyingine za elimu ya juu, kudhibiti uhalali wa vyeti vya waombaji nafasi katika Elimu ya Juu, kuwapunguzia wazazi na wanafunzi gharama za kuomba udahili katika vyuo vikuu na kuongeza nafasi za uteuzi kwa waombaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu linasimamia na kuratibu mitaala, ubora wa mafunzo, mitihani, tuzo, usajili na ithibati za vyuo vya elimu ya ufundu vya umma na binafsi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2009/2010, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu:-

(a) Lilikagua vyuo 28 vya elimu na mafunzo ya ufundu na kuvipa ithibati;

(b) Lilikagua vyuo 24 vyenye uwezo wa kutoa elimu na mafunzo ya ufundu na kuvisajili na kuhakiki utekelezaji wa masharti ya ithibati katika vyuo 18 vyenye ithibati kamili;

(c) Liliratibu uandaaji wa mtaala wa elimu ya ufundi na kuidhinisha programu 46 zenyne kuzingatia umahiri na mahitaji ya soko la ajira;

(d) Lilikagua na kutathimini sifa za wakufunzi 200 na kuwasajili;

(e) Lilisimamia na kuviwezesha vyuo 18 vya elimu ya ufundi kuweka mfumo wa kudhibiti na kuhakiki ubora wa mafunzo yatolewayo;

(f) Liliratibu mitihani ya elimu ya ufundi katika vyuo 28 vinavyotumia mtaala mpya unaozingatia umahiri wa wanafunzi na mahitaji ya soko la ajira;

(g) Liliratibu udahili wa wanafunzi katika vyuo 17 vya elimu ya ufundi vinavyotoa mafunzo ya elimu ya ufundi ngazi ya Shahada na Stashahada ya Juu; na

(h) Liliratibu mafunzo ya ufundishaji katika mfumo wa *Competence Based Education and Training* (CBET) kwa walimu kutoka vyuo 20 vya elimu ya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ina majukumu ya kutoa mikopo kwa wanafunzi raia wa Tanzania wanaosoma katika Taasisi za Elimu ya Juu ndani na nje ya nchi na kukusanya marejesho ya mikopo hiyo. Katika kipindi cha 2005 – 2010, Bodi ilitoa mikopo yenye thamani Shilingi 576.03 bilioni kwa wanafunzi 130,060. Aidha, ilikusanya marejesho ya mikopo yenye thamani ya Shilingi 3.68 bilioni kati ya Shilingi 15.48 bilioni zilizotakiwa kurejeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu:-

(a) Iliwakopesha wanafunzi 74,498 jumla ya Shilingi 197.3 bilioni kwa ajili ya kulipia gharama za chakula na malazi, vitabu na viandikia, ada za mafunzo, utafiti, mafunzo kwa vitendo na mahitaji maalum ya vitivo;

(b) Ilitoa mikopo ya asilimia 100 kwa wanafunzi 7,238 wanaochukua masomo ya sayansi katika vyuo vya elimu ya juu;

(c) Iliongeza madaraja ya mikopo kutoka sita hadi 11 na hivyo kutoa mikopo kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza kama ifuatavyo: daraja ya A (100%), B (90%), C (80%), D (70%), E (60%), F (50%), G (40%), H (30%), I (20%), J (10%), na K (0%); na

(d) Iliendelea kutoa elimu kwa umma kupitia njia mbalimbali zikiwemo vipeperushi, magazeti, redio na televisheni, mikutano, warsha na maonesho yaliyowezesha Bodi kukutana na kuwasiliana ana kwa ana na wadau kuhusu wajibu wa kuchangia elimu ya juu, taratibu za utoaji mikopo na urejeshwaji wake. Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) ina majukumu ya kuratibu, kudhibiti, kugharimia, kutoa na kukuza elimu na mafunzo ya ufundi stadi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/10, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundisti:-

- (a) Ilifanya maandalizi ya ukarabati wa vuo vya ufundisti za Wilaya za Karagwe na Korogwe baada ya Halmashauri za Wilaya hizo kuridhia taratibu za utekelezaji;
- (b) Iliendelea na ujenzi wa chuo cha ufundisti za Wilaya ya Makete;
- (c) Ilifanya upanuzi, ukarabati na ufungaji wa vifaa vya kisasa katika vuo vya ufundisti vya: Mpanda, Shinyanga, Tabora, Ulyankulu, Singida na Njiro – Arusha;
- (d) Iliendelea na ujenzi wa vuo vya Lindi, Pwani, Manyara na Dar es Salaam;
- (e) Ilitoa mafunzo kwa walimu 287 wa elimu na mafunzo ya ufundisti wa ngazi ya Cheti. Aidha, iliwapatia washiriki 542 mafunzo ya muda mfupi katika maeneo mbalimbali (walimu wa ufundisti 25 kutoka vuo binafsi, wakuu wa vuo 70 wa vuo vya Serikali na visivyo vya Serikali) na watumishi 81 kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi na wa Wizara ya Elimu Mafunzo ya kompyuta;
- (f) Ilitoa mafunzo kwa walimu 37 katika ngazi ya Stashahada katika Chuo cha Ualimu wa Ufundisti Stadi Morogoro. Aidha, walimu wengine 40 wanaendelea kuhudhuria mafunzo ya Stashahada katika chuo cha VETA Morogoro;
- (g) Iliwawezesha wanachuo 700 kushiriki katika mafunzo kwa vitendo (*Field Work*) katika hoteli ya *Movenpick* na viwanda vya Tanga Cement na Chemi – *Cotex*. Aidha, ilikamilisha maandalizi ya mafunzo kwa vitendo katika viwanda vya A to Z Arusha, *TPC - Moshi*, Tumbaku - Morogoro, *TANESCO* – Dar es Salaam, *Coca Cola* – Dar es Salaam, na *Aluminium Africa (ALAF)*;
- (h) Iliimarisha ushirikiano kati ya Tanzania na *Chamber of Minerals* ambapo vifaa vyenye thamani ya Dola za Kimarekani 1.3 milioni vilitolewa kwa ajili ya Chuo cha Ufundisti, Moshi na Dola 500,000 za Kimarekani zilizotolewa na Canada kwa ajili ya Chuo cha Ufundisti Mkoa wa Mwanza. Viwanda vya madini vimeanza kufaidika na stadi zinazofundishwa; na
- (i) Ilianiza kufanya majaribio ya mkakati wa kutoa mafunzo katika sekta ya kilimo katika Kanda ya Mashariki na mafunzo ya ufugaji wa kuku wa kienyeji na wa kisasa katika Kanda ya Kati, kwa kushirikiana na shirika la *Swiss Contact*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kina jukumu la kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2009/2010, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam:-

- (a) Kilidahili wanafunzi 6,345 wa mwaka wa kwanza, ambapo 3,686 walikuwa wa shahada ya kwanza (wanawake 1,290) na 2,659 na wa shahada za uzamili na uzamivu (wanawake 764);
- (b) Kiliendeleza ushirikiano na wafadhili mbalimbali katika kugharimia, taaluma, utafiti na kusambaza matokeo yake na ujenzi wa miundombinu;
- (c) Kilitoa machapisho 17 ya vitabu na 275 ya majarida na kusambaza matokeo ya utafiti katika nyanja za demokrasia na utawala bora, biashara na uongozi, lugha, mazingira, sayansi asilia sheria, TEHAMA, uhandisi wa fani mbalimbali na ujasiriamali;
- (d) Kiliajiri wanataaluma 380 ili kukabiliana na ongezeko la wanafunzi na pia kujaza nafasi za kazi zilizoachwa wazi na walioondoka;
- (e) Kiligharimia mafunzo ya wafanyakazi wanataaluma 56 na waendeshaji 22;
- (f) Kiliendeleza awamu ya tatu ya ujenzi wa jengo la Shule Kuu ya Biashara;
- (g) Kiliendeleza upanuzi wa jengo la Chuo cha Sanaa na Sayansi za Jamii kwa ajili ya semina;
- (h) Kiliendeleza ujenzi wa kumbi mbili za miadhara zenyenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kila moja;
- (i) Kilifuatilia utekelezaji wa awamu ya tatu ya mradi wa Mlimani *City*;
- (j) Kilifanya mazungumzo ya kuendeleza ujenzi wa Makao Makuu mapya ya Taasisi ya Sayansi za Bahari (*Institute of Marine Sciences - IMS*) eneo la Buyu – Zanzibar;
- (k) Kiliendeleza mchakato wa ujenzi wa kumbi za miadhara na semina, maabara, ofisi za taaluma na jengo la makumbusho ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kupitia mradi wa Serikali wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia unaogharimiwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia.
- (l) Kilikarabati hosteli sita za wanafunzi, kumbi za semina na miadhara na nyumba 13 za wafanyakazi;
- (m) Kilikamilisha makubaliano na Msajili wa Hazina na Mamlaka ya Bima (*TIRA*) kuhusu kuhamisha majengo ya Chuo cha Bima Mikocheni kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wakati taratibu za kisheria zikichukua mkondo wake;

(n) Kilikamilisha makubaliano na Manispaa ya Kinondoni kuhusu kuhamisha Shule ya Msingi Mlimani kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wakati taratibu za kisheria zikichukua mkondo wake; na

(o) Kilianzisha mchakato wa uchangiaji kutoka kwa wafanyakazi na wadau wa Chuo kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha wanafunzi (*Student Centre*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam kina majukumu ya kufundisha, kutafiti, kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika maeneo ya Elimu na Ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/10, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam kilitekeleza yafuatayo:-

(a) Kilidahili wanafunzi wapya 946 ambapo 120 ni wa masomo ya sayansi na 826 ni wa masomo ya Sanaa na Sayansi ya Jamii., na hivyo kufanya jumla ya wanafunzi wote chuoni hapo kuwa 2,966 ambapo 763 ni wa mwaka wa pili na 1,257 ni wa mwaka wa tatu;

(b) Kilikamilisha ujenzi wa kumbi tatu za miadhara zenyewe uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,000 kwa wakati mmoja. Kumbi hizo zinatarajiwaa kuanza kutumika rasmi katika mwaka wa masomo 2010/2011;

(c) Kiliendelea kugharimia mafunzo ya watumishi 77, ambapo wahadiri 55 wako kwenye mafunzo ya shahada za uzamili na 22 kwenye shahada za uzamivu ndani na nje ya nchi;

(d) Kiliendelea kuimarisha miundo mbinu na matumizi ya TEHAMA; na

(e) Kiliendelea kushirikiana na vyuo na taasisi za ndani na nje ya nchi katika utafiti na mafunzo, hususan kwa shahada za uzamili na uzamivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kina majukumu ya kufundisha, kutafiti, kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika maeneo ya Ualimu na Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/10, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa:-

(a) Kilidahili wanafunzi wapya 750 wa shahada ya kwanza kati ya 800 waliokuwa wamelewanga;

(b) Kiliendelea na mchakato wa upanuzi wa maktaba awamu ya pili kwa kumteua mkandarasi mshauri wa mradi;

- (c) Kiliendelea na mchakato wa kuanza ujenzi wa ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja na kuanza maandalizi ya ujenzi wa hosteli ya wanafunzi;
- (d) Kilikamilisha andiko la mradi wa ujenzi wa jengo la utawala;
- (e) Kilikamilisha ujenzi wa uzio wa Chuo wa awamu ya pili kwa kupanda miti eneo lote la mipaka ya Chuo; na
- (f) Kilikamilisha ukarabati wa barabara za ndani ya Chuo awamu ya kwanza na ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma ilianzishwa mwaka 2003, kufuatia kufutwa kwa Sheria ya mwaka 1981 iliyoanzisha Chuo kilichoitwa *Tanzania School of Journalism (School of Journalism Act No. 8)* na kukifanya kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Chuo hicho kilihamishwa kutoka Wizara ya Habari na kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kupewa hadhi ya kuwa Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma (*School of Journalism and Mass Communication*). Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ina majukumu ya kutoa elimu na mafunzo ya Shahada, Stashahada ya Juu na Cheti katika nyanja mbalimbali, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu na kitaalam katika masuala ya habari, mawasiliano, mahusiano ya umma, matangazo ya biashara, pamoja na utangazaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu iwe sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Shule Kuu hii imekua na kupanua shughuli zake kwa kutoa Shahada za Kwanza ya Uandishi wa Habari (*BA in Journalism*), Shahada ya Kwanza ya Mawasiliano ya Umma (*BA in Mass Communication*), Shahada ya Kwanza ya Uhusiano wa Umma na Matangazo (*BA in Public Relations and Advertising*) na Stashahada ya Juu ya Mawasiliano ya Umma (*Post-Graduate Diploma in Mass Communication*). Ili kuinua ubora wa ufundishaji na kutoa Elimu kwa vitendo, Shule Kuu imeanzisha vituo vya utangazaji vijulikanavyo kama *Radio Mlimani* na *Mlimani Television* pamoja na gazeti la kila wiki la *The Hill Observer*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/10, Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma:-

- (a) Iliongeza idadi ya wanachuo kutoka 40 waliokuwepo kabla ya mwaka 2003 hadi wanafunzi 300 mwaka 2009/10;
- (b) Iliajiri wanataaluma sita;
- (c) Iliandaa mtaala wa Shahada za Uzamili; na

(d) Ilikarabati vyumba 8 vya mihadhara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo: Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kinatekeleza majukumu yake ya kutoa mafunzo ya Shahada za Kwanza, Shahada za Uzamili na Uzamivu, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika nyanja za Kilimo, Misitu, Mifugo, Mazingira, wanyama pori, ufugaji wa samaki na fani nyingine za Sayansi na Teknolojia. Katika kipindi cha mwaka 2005 – 2010, chuo kilitoa wahitimu 4,473. Kati ya hao, 3,969 walikuwa wa shahada za kwanza 811 wa shahada za Uzamili na 65 wa shahada za Uzamivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo:-

(a) Kiliendeleza utafiti sehemu mbalimbali nchini unaolenga katika kuinua ubora wa kilimo, hifadhi za misitu, mifugo na maliasili nyingine, ikiwa ni pamoja na matumizi ya wanyamakazi katika Kilimo (Kisilo Wilaya ya Njombe); Mradi wa mbinu bora za ufugaji wa kuku wa kienyeji (Wilaya ya Handeni); uzalishaji wa matunda na mboga (Wilaya za Morogoro na Mvomero) ambapo wakulima zaidi ya 1,500 hufaidika na mazao kutoka kwenye bustani hiyo kila mwaka;

(b) Kiliendeleza hifadhi na ukarabati wa Chanzo cha Maji cha Mto Mzinga kwa kushirikiana na jamii;

(c) Kiliendelea, chini ya mradi wa *PANTIL*, kutoa elimu kwa wanavijiji juu ya umuhimu wa upandaji miti, ufugaji nyuki na kuongeza matumizi ya pembejeo na ukuzaji wa soko kwa aina za miti isiyojulikana na isiyotumika sana nchini Tanzania. Mikoa ya Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Dar es Salaam na Arusha wamehamasishwa kupanda na kutumia miti hiyo. Mradi huu umetoa machapisho 11 kwenye majarida ya kisayansi;

(d) Kilitoa ushauri wa kitaalam katika: kilimo, mifugo, misitu, wanyamapor, umwagiliaji na tiba ya wanyama ambayo yalikiingizia chuo Sh. 38,009,052.50;

(e) Kiliendelea na mradi wa ‘Uboreshaji wa Zao la Maharage’ ambao umewezesha kutoa aina za maharage za PESA na MSHINDI ambazo hupevuka mapema na kuiva haraka wakati wa kupika; na

(f) Kiliandaa shahada za kwanza sita ambazo ni:- *Bachelor of Science in Human Nutrition, Bachelor of Science in Family and Consumer Sciences, Bachelor of Irrigation and Water Resources, Bachelor of Bioprocess and Post-harvest Engineering, Bachelor in Applied Agricultural Extension na Bachelor of Agricultural Education* zitakazodahili jumla ya wanafunzi 470 katika mwaka wa masomo 2010/2011. Aidha, chuo kiliandaa stashahada 2 ambazo ni: *Diploma in Tropical Animal Health na Diploma in Laboratory Technology Science*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Elimu ya Biashara cha Moshi ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. Majukumu yake ni kufundisha, kufanya utafiti na kutoa ushauri katika nyanja za ushirika, maendeleo ya jamii, biashara, oganaizesheni, ujasiriamali na masuala mtambuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/10 Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Elimu ya Biashara Moshi:-

(a) Kiliongeza udhili wa wanafunzi wa mwaka wa kwanza kutoka wanafunzi 2,186 (wa kike 734) mwaka wa masomo 2008/09 hadi 2,713 (wa kike 980) mwaka 2009/10. Hili ni ongezeko la wanafunzi 527 ambayo ni sawa na asilimia 24 (asilimia 33.5 kwa wasichana). Aidha, chuo kilianzisha programu mpya mbili za Cheti katika Kampasi ya Kizumbi - Shinyanga zenyenye jumla ya wanafunzi 84 ;

(b) Kiligharimia mafunzo ya wanataaluma 24 wanaoendelea na masomo katika ngazi mbalimbali (Shahada za Uzamivu 13 (wanawake wawili, na wanaume 11), Shahada za Uzamili 11 (mwanamke mmoja)) na wafanyakazi waendeshaji wanne (Stashahada ya Uzamivu wanne (wanawake watatu);

(c) Kiliendelea kuimarisha shughuli za utafiti na uchapishaji kupitia mpango wa utafiti mdogo unaogharimiwa na chuo, kwa njia ya ushindani na uendeshaji wa warsha za kuwajengea uwezo wanataaluma katika utafiti na ushauri;

(d) Kiliendelea kuimarisha vituo vya mikoani kwa kuviongezea wafanyakazi, kuainisha mahitaji, kuyaingiza kwenye bajeti ya Chuo. Aidha, kiligharimia ukarabati wa vituo vya Mwanza na Shinyanga;

(e) Kiliendelea kuimarisha ushirikiano na vyuo ikiwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Makerere , Chuo Kikuu cha Malawi, Chuo Kikuu cha Zambia, Chuo cha Ushirika cha Uingereza na Chuo cha Biashara na Teknolojia cha Humber kilichoko Canada;

(f) Kiliimarisha utoaji wa elimu ya ushirika kwa ujumla na ile ya Vyama vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*) kwa kutoa mafunzo katika ujasiriamali na uongozi, utunzaji wa vitabu vya hesabu na uendeshaji wa aina mbalimbali za vyama vya ushirika, ambapo jumla ya wanaushirika na wajasiriamali 18,207 [wanawake 7,112 (39%)] walipata mafunzo haya katika vituo vya mikoani;

(g) Kiliendesha semina na warsha kwa wanafunzi, wafanyakazi na jamii kwa ujumla ili kuimarisha masuala mtambuka na kuyaingiza kwenye mitaala ya chuo katika ngazi mbalimbali;

(h) Kiliendelea kutekeleza masharti yaliyotolewa na Tume ya Vyuo Vikuu ili kujitayarisha kuwa Chuo Kikuu kamili (*Fully Fledged University*) kwa: kugharimia

mafunzo ya wanataaluma katika ngazi mbalimbali, kukarabati majengo ya mihadhara na ofisi za wanataaluma na kuimarisha miundombinu ya maktaba kwa kuifanya iendeshwe kwa kutumia kompyuta (*computarization of library services*), kufunga mtambo wa ulinzi; na

(i) ilikamilisha Mpango Mkakati wa Chuo kwa mwaka 2010/2011 - 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kina majukumu ya kufundisha kwa njia ya masafa na ana kwa ana, kutafiti, kutoa ushauri wa kitaalamu na kueneza maarifa kuititia vituo vya Chuo vilivyopo mikoani. Katika kipindi cha 2005 – 2010, chuo kilitoa wahitimu 1,341 (wanawake 521) wa Vyeti, Shahada ya Kwanza, Uzamili na Uzamivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/10, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania:-

(a) Kilidahili jumla wanafunzi 7,882 wa mwaka wa kwanza (wanawake 2,756) wakiwemo wanafunzi 4,229 wa shahada za kwanza, 1,782 wa shahada za juu na 1,871 wa Cheti na Stashahada na hivyo kufanya idadi ya wanafunzi wote waliopo chuoni kufikia 30,066 (wanawake 7,922). Aidha, kati yao waliodahiliwa katika programu za ualimu walikuwa 1,810 (880 wa Shahada ya Kwanza, 433 wa Stashahada za Uzamili na 497 wa Diploma ya Ualimu);

(b) Kilikamilisha ukarabati wa majengo ya vituo vya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania vya Kilimanjaro, Njombe, Tanga, Dodoma na Mbeya;

(c) Kilifanikiwa kupata umiliki wa majengo ya iliyokuwa *Rukwa Regional Transport Co-operation Limited*;

(d) Kilikamilisha ujenzi wa Jengo la Miliki, ghalaa, vyoo vya nje, jukwaa la muda (*podium*), na uzio kuzunguka eneo lililojengwa, viwanja vya michezo, mfumo wa kuvuna maji, makaravati ya kuzuia mmomonyoko wa ardhi na katika barabara ya eneo lililojengwa katika makao makuu ya chuo; na

(e) Kilianzisha majadiliano kuhusu uanzishaji wa vituo vya Chuo Kikuu Huria nchini Rwanda na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Ardhi kina jukumu la kufundisha, kutafiti na kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika nyanja mbalimbali zikiwemo za maeneo ya ardhi, mazingira na ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/10, Chuo Kikuu Ardhi:-

(a) Kilidahili wanafunzi wa mwaka wa kwanza 807 wa Shahada za Kwanza, wanafunzi 10 wa Stashahada na 68 wa Shahada za Uzamili na Uzamivu. Jumla ya

wanafunzi wote walioko chuoni ni 2,143 ikilinganishwa na wanafunzi 1,701 waliokuwepo chuoni mwaka wa masomo 2008/09. Hili ni ongezeko la asilimia 26. Idadi ya wanafunzi wa kike ni asilimia 24 ya wanafunzi wote;

(b) Kilikamilisha utayarishaji wa maandiko sita (6) ya miongozo na taratibu za uendeshaji wa Chuo. Maandiko mengine 23 yako katika hatua mbalimbali za uandaaji;

(c) Kiliajiri wafanyakazi wapya 108. Kati ya hao, 51 ni wahadhiri na 57 ni waendeshaji;

(d) Kiligharimia mafunzo ya wafanyakazi wanataluma 62 na waendeshaji 45 katika ngazi mbalimbali;

(e) Kiliendelea kufanya utafiti katika maeneo 63, kukamilisha utafiti katika maeneo 11 na kutoa machapisho 19;

(f) Kilianzisha programu mpya tano, ambapo mbili ni za Shahada ya Kwanza, mbili ni za Uzamivu na moja ni ya Stashahada ya Uzamili (*Postgraduate Diploma*);

(g) Kilikamilisha awamu ya pili ya kuweka huduma ya Intaneti katika majengo yasiyo na huduma hii ili kukuza matumizi ya TEHAMA Chuoni;

(h) Kiliendelea na ukarabati wa hosteli za wanafunzi, kumbi za mihadhara, ukumbi wa mikutano, nyumba za wafanyakazi, ofisi za wafanyakazi na ujenzi wa mtaro wa maji ya mvua;

(i) Kilinunua vifaa vya TEHAMA pamoja na kupokea machapisho 512 kupitia miradi ya Benki ya Dunia na *Carnegie Corporation*; na

(j) Kilikamilisha awamu ya tatu ya ujenzi wa jengo jipya la mihadhara na ofisi (*Lands Building*) kwa kutumia fedha kutoka Serikalini na mkopo kutoka Mamalaka ya Elimu Tanzania (*TEA*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kina majukumu ya kufundisha, kutafiti, kutibu na kutoa ushauri na huduma za kitaalam katika maeneo ya tiba na afya. Katika kipindi cha 2005 hadi 2010, chuo kilitoa wahitimu 1,377 wa Shahada ya Kwanza na 238 wa Shahada ya Uzamili na Uzamivu. Kati ya hawa, Madaktari wa Shahada ya Kwanza walikuwa 807, wafamasia 232 na Madaktari wa meno 121.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2009/10 Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili:-

(a) Kilidahili wanafunzi wapya 342 wa shahada ya kwanza katika fani mbalimbali. Hii ni sawa na asilimia 97.7% ya lengo lililowekwa la wanafunzi 350. Pamoja na udahili huu, idadi ya wanafunzi wa shahada ya kwanza Chuoni ilikuwa 1,370;

(b) Kilitoa wahitimu wa shahada ya kwanza 282 katika fani za tiba (177), meno (28), famasia (34), uuguzi (25) na afya ya jamii na mazingira (18) na wahitimu wa uzamili na uzamifu 73;

(c) Kilikamilisha uwekaji wa samani na umeme kwa majengo mapya ya ofisi, maktaba na kumbi za mihadhara;

(d) Kilikamilisha tathmini na kuwalipa fidia jumla ya wakazi 1,919 wa eneo linalotarajiwa kutumika kwa upanuzi wa Chuo la Mloganzila, Kwembe na Kisokwa wanaostahili kulipwa fidia ya mali zao kwa gharama ya Sh. 8,067,904,700;

(e) Kiliajiri watumishi 37 kati ya 67 waliokuwa wamelengwa ambao wanajumuisha idadi ya watumishi Chuoni kufikia 587;

(f) Kiliongeza programu tano za uzamili na uzamivu kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa watu wenye sifa zinazohitajika, pamoja na waalimu wa kufundisha Chuoni na katika vyuo vikuu vyta Afya na Sayansi Shirikishi nchini. Ongezeko hili linafanya jumla ya programu za uzamili na uzamivu Chuoni kuwa 46;

(g) Kimekamilisha ujenzi wa kantini katika eneo la hosteli za Chole ambapo mkandarasi anamalizia kazi ya kufunga majiko ya gesi; baada ya kukamilisha uwekaji wa samani, kantini itakuwa tayari kwa kuanza kuhudumia wanafunzi mia sita (600);

(h) Kilikamilisha ujenzi wa ukuta kuzunguka eneo la hosteli za Chole pamoja na kibanda cha walinzi;

(i) Kilikamilisha utafiti kuhusu upatikanaji wa kipimo cha kugundua vijidudu vyta malaria kwa haraka (*Rapid Malaria Diagnostic Test*) na matokeo yake kutumiwa na Mpango wa Taifa wa kudhibiti Malaria katika kutengeneza sera za kutibu malaria nchini;

(j) Kilianza utafiti wa kuchunguza vinasaba vyta vijidudu vyta malaria kwa lengo la kubaini viashiria vyta usugu kwa dawa mbalimbali za malaria;

(k) Kilijenga uwezo wa ufuatiliaji wa wagonjwa wanaopata dawa bora dhidi ya malaria;

(l) Kiliendelea kutengeneza mfumo wa takwimu (*Data base*) kwa ajili ya akinamama wajawazito uliosaidia kuimarisha utoaji wa huduma na kupunguza vifo vyta kina mama wajawazito. Aidha, utafiti huu uliainisha mikakati ya kupambana na ubakaji wa akina mama na watoto;

(m) Kilitoa mafunzo ya stadi za maisha kuhusu kutambua viashiria hatari kwa maisha ya mama na watoto na kuhusu hatua zinazostahili, umuhimu wa kujifungulia

katika vituo vya afya; kufuata utaratibu wa rufaa na kutafuta huduma endapo athari zinatokea;

(n) Kilikamilisha uchunguzi wa chanjo ya kifua kikuu (*Mycobacteria vaccae vaccine*) kwa watu wenyе virusi vya UKIMWI (VVU) ili kubaini kama inaweza kupunguza uwezekano wa kupata TB kama ugonjwa nyemelezi. Matokeo yalionesha kuwa chanjo hiyo inatoa kinga dhidi ya kifua kikuu kwa asilimia 40 ya wagonjwa wenyе VVU. Matokeo haya yameleta hamasa kubwa sana kwa watafiti duniani kuendeleza utafiti huo zaidi kwa madhumuni ya kupata chanjo dhidi ya TB kwa watu wenyе VVU;

(o) Kiliendeleza utafiti wa chanjo ya UKIMWI kwa awamu ya kwanza na ya pili (*Clinical Trial of HIV Vaccine Phase I & II*), ambapo jumla ya watu sitini kutoka Jeshi la Polisi walijitolea kuchanjwa, na matokeo kuonyesha kuwa chanjo hii ni salama na yenye uwezo mkubwa wa kuchochea utengenezaji wa viashiria vya kinga ya mwili dhidi ya Virusi vya UKIMWI. Aidha, Chuo kilipata ufadhilli wa kuendeleza utafiti wa chanjo hiyo kwa kina zaidi kwa ushirikiano kati ya Tanzania, Msumbiji, Ujerumani, Sweden, Uingereza na Amerika, ukiongozwa na Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili; na

(p) Kilifanikisha machapisho 150 katika majarida ya Kimataifa na ndani ya nchi kutokana na utafiti uliofanywa na chuo katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Mzumbe kina majukumu ya kupata, kukuza, kuhifadhi na kuenzeza maarifa na stadi za menejimenti kwa njia ya mafunzo, utafiti na huduma za kiufundi na kitaalamu. Chuo kimeongeza udahili kutoka wanafunzi 3,210 (wanawake 1,1210) mwaka 2005, hadi 5,172 (wanawake 2,239) mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/10, Chuo Kikuu Mzumbe:-

(a) Kilidahili wanachuo wapya 3,206 (1,362 wanawake), kwa mwaka wa masomo 2009/10, ambapo, 1,577 walikuwa wa shahada ya kwanza, diploma na cheti, na 1,629 walikuwa wa shahada za uzamili, na hivyo kuvuka lengo la 2,310 kwa asilimia 39. Aidha, idadi ya wanachuo wote iliongezeka kutoka 3,537 mwaka 2007/08 hadi 5,210 mwaka 2009/10 Idadi hii ni sawa na asilimia 109 ya lengo la wanafunzi 4,773 waliokuwa wamepangwa kufikiwa mwaka huu wa masomo;

(b) Kilikamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa hosteli ya wanachuo wa kike inayotarajiwa kuwa na uwezo wa kuchukua wanachuo 400 kwa wakati moja, katika Kampasi Kuu Mzumbe, ambapo wanachuo 200 tayari wanaishi humo;

(c) Kilikamilisha asilimia 85 ya ujenzi wa jengo la ghorofa tatu la ofisi, litakalotosheleza wahadhiri 271 na wafanyakazi waendeshaji 127 ambapo tayari limeezekwa na upigaji lipu na uwekaji wa miundombinu ya umeme na mawasiliano unaendelea;

(d) Kilikamilisha michoro ya maktaba na kuendelea na taratibu za kumpata mkandarasi;

(e) Kililipia Sh. Milioni 750 (50%) kati ya Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya vitalu vitatu vilivyopo Upanga Dar es Salaam kwa ajili ya upanuzi wa Shule Kuu ya Biashara Kampasi ya Dar es Salaam;

(f) Kiligharimia mafunzo kwa watumishi 25 ambapo wahadhiri walikuwa 20 (sita Uzamivu na 14 Uzamili) na wafanyakazi waendeshaji 10 (watano shahada za Uzamili, wawili shahada ya kwanza, wawili stashahada, na mmoja cheti);

(g) Kilikamilisha tafiti 20 kati ya 30 na kutoa ushauri katika maeneo 35 ya menejimenti, uongozi na Sayansi ya Jamii kwa ujumla;

(h) Kilichapisha vitabu viwil na makala 26 za kufundishia ambapo makala nane zilichapishwa katika majorida ya kimataifa; na

(i) Kiliajiri wahadhiri 23 kati ya 37 waliolengwa na waendeshaji 10 na kufikisha idadi ya wahadhiri 284 na waendeshaji 315 chuoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Dodoma kinatekeleza majukumu yake ya kutoa mafunzo ya Shahada za Kwanza na za Juu, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalam katika nyanja za Ualimu, Hisabati, Sanaa na Lugha, Sayansi za Jamii, Sayansi za Kompyuta, Tiba na Uuguzi, na Sayansi Asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Chuo Kikuu Dodoma:-

(a) Kilidahili wanafunzi wapya 7,946 na kufanya idadi ya wanafunzi wote chuoni kuwa 15,121;

(b) Kiliongeza nafasi za udahili kwa kuanzisha Shule Kikuu ya Sayansi za Kompyuta na Habari, Sanaa na Sayansi za Jamii, Sayansi ya Tiba na Uuguzi, Sayansi za Ardhi, Hisabati na Sayansi Asili;

(c) Kiliajiri wafanyakazi wapya 676 na kufanya jumla ya wafanyakazi kuwa 978; na

(d) Kilikamilisha ujenzi wa awamu ya kwanza ya Chuo cha Elimu chenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 10,000; awamu ya kwanza ya Chuo cha Sayansi za Kompyuta, Habari na mawasiliano kwa asilimia 50%; jengo la utawala kwa asilimia 90, barabara zinazozunguka na kuunganisha kwa ndani kwa kiwango cha changarawe na lami kwa asilimia 85; awamu ya kwanza ya Chuo cha Sanaa na Sayansi za Jamii kwa wanafunzi 5,000, na awamu ya kwanza ya Chuo cha Sayansi za Afya na Tiba kwa wanafunzi 500. Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kina majukumu ya kuendesha mafunzo katika fani za Sayansi za Jamii kwa kiwango cha

Cheti, Stashahada na Shahada; kutoa Mafunzo ya Uongozi na kufanya Utafiti na kutoa Ushauri wa Kitaalamu kwa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere:-

- (a) Kilidahili wanafunzi wapya 238 wa ngazi ya cheti, 332 wa Stashahada na 313 wa Shahada ya Kwanza;
- (b) Kiliajiri wanataaluma wanne na wafanyakazi waendeshaji watatu;
- (c) Kiligharimia mafunzo ya wanataaluma 15 (10 uzamili na watano Uzamivu) na wafanyakazi waendeshaji watano;
- (d) Kilikarabati Mabweni ya Mwongozo na Azimio;
- (e) Kilijenga uzio kuzunguka eneo lote la Chuo - Kivukoni; na
- (f) Kilianza awamu ya kwanza ya ujenzi wa kumbi tatu za miadhara, ofisi za wahadhiri na wafanyakazi waendeshaji eneo la Bububu, Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Ufundu Arusha kina jukumu la kutoa elimu na mafunzo ya ufundi katika fani za Magari, Ujenzi, Mitambo, Umeme, Barabara, Sayansi na Teknolojia ya Maabara, Eletroniki na Mawasiliano ya Anga kwa kiwango cha Cheti na Stashahada. Aidha, Chuo hufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalam katika maeneo yake ya taaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Chuo cha Ufundu Arusha:-

- (a) Kilidahili wanafunzi wapya 217 (23 wa kike) na kuvuka lengo la udahili la 205 kwa asilimia sita. Aidha, mwezi Januari 2010 chuo kilidahili wanafunzi 150 wa programu za mafunzo ya ufundi mchundo/stadi (*Vocational Education and Training*);
- (b) Kilianzisha programu mpya ya Sayansi na Teknolojia ya Maabara iliyokuwa na wanafunzi 23 (5 wa kike);
- (c) Kilinunua vifaa vya maabara na kuunda Kamati ya Wanataaluma ya kuhakiki ubora pamoja na uwezekano wa kukarabati vifaa na zana za kufundishia na kuandaa mpango mkakati wa kuinua ubora wa mafunzo kwa vitendo na teknolojia chuoni;
- (d) Kilikarabati nyumba mbili za wafanyakazi na kumteua mshauri mwelekezi wa kukarabati bweni na nyumba nyingine za wafanyakazi;
- (e) Kilianza mpango wa kukuza elimu ya kujiendeleza kwa kutoa mafunzo ya stashahada kwa njia ya masomo ya jioni, ambapo jumla ya wanafunzi 21 walidahiliwa (Uhandisi Umeme sita, Uhandisi Elektroniki na Mawasiliano ya Anga 15);

- (f) Kilikamilisha ujenzi wa maabara za Kemia, Fizikia na Biolojia;
- (g) Kiliandaa kozi ya awali kwa ajili ya kuwawezesha wanachuo wa kike kujeungu na Chuo;
- (h) Kiligharimia mafunzo ya wanataaluma na waendeshaji 17 katika Vyuo na Taasisi imbalimbali katika ngazi ya Uzamivu (5), Uzamili (4), Shahada ya Kwanza (6) na Diploma (2). Aidha, chuo kilipeleka wanataaluma watano katika mafunzo ya muda mfupi ya *Automation and Variable Speed Drives* kwa kushirikiana na *Kilimanjaro Institute of Telecommunication and Electronics and Computers (KIITEC)*;
- (i) Kiliandaa mitaala mitatu *NTAs* 4 -6 ya Programu ya Sayansi na Teknolojia ya Maabara ambayo tayari imeanza kutumika;
- (j) Kiliandaa mitaala miwili ya Shahada ya Kwanza ya Uhandisi Ujenzi na Umwagiliaji na kuiwasilisha kwa wadau pamoja na Bodi ya Chuo; na
- (k) Kiliimarisha ushirikiano na nchi wahisani, Mashirika ya Kimataifa, Vyuo vya Elimu ya Juu na vya Ufundu vilivyo nchini na vya Kimataifa kama ifuatavyo:-
- Mpango wa Elimu ya Ajira (*Education for Employment – EFE*) unaofadhiliwa na serikali ya Kanada, Chuo kinashirikiana na Chuo cha *Camosun (Camosun Community College)* cha Canada chini ya uratibu wa *The Association of Canadian Community Colleges (ACCC)* katika kuandaa mitaala ya kozi za *Mining and Mineral Processing, Heavy Duty Equipment Technology* na *Lapidary and Jewellery Technology* ngazi ya cheti na Stashahada ambayo itakamilika katika mwaka wa masomo wa 2010/2011;
- Ushirikiano na Vyuo vya Ufundu barani Afrika chini ya utaratibu wa *Commonwealth Association of Polytechnics in Africa (CAPA)*;
- utafiti wa Mahitaji ya Soko (*Labour Market Survey*) la wahandisi wa Ujenzi na Umwagiliaji, ambao ulikiwezesha Chuo kuandaa mitaala kwa ajili ya kuanzisha Programu ya Shahada ya Kwanza ya Ujenzi na Umwagiliaji;
- Uimarishaji na usajili wa kitengo cha Uzalishaji na Utoaji Ushauri wa Kitaalamu (*ATC – Production and Consultancy Bureau*) kwenyeBodi ya Usajili wa Wahandisi;
- Kilitoa msaada wa Sh. 1,000,000 kwa watoto yatima na watu wenye UKIMWI kupitia Kikundi cha Upendo cha Chuo cha Ufundu Arusha; na
- Ununuzi wa vitabu vyenye thamani ya Sh. 16,000,000 kwa ajili ya programu za Sayansi na Teknolojia ya Maabara, na Elektroniki na Mawasiliano ya Anga, na msaada wa vitabu 610 kutoka *Tanzania National Parks (TANAPA)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Changamoto:-

- (a) Kiwango cha chini cha ufaulu katika masomo ya Hisabati Sayansi na Kiingereza katika ngazi zote za elimu hususan Elimu ya Msingi na Sekondari;
- (b) Kushuka kwa *Net Enrolment Ratio (NER)* katika elimu ya msingi kutoka 97.2 mwaka 2008 hadi 95.9 mwaka 2009;
- (c) Pamoja na kusomesha walimu wengi, bado kuna uhaba wa walimu hususan katika maeneo ya pembezoni kutokana na mazingira magumu ya kufanya kazi;
- (d) Kiwango kidogo cha uandikishaji wa watoto katika elimu ya awali;
- (e) Kushuka kwa uandikishaji wa watoto wenye mahitaji maalumu ya kielimu katika ngazi ya Elimu ya Msingi kutoka 7,241 mwaka 2008 hadi 5,532 mwaka 2009;
- (f) Uhaba wa maabara za masomo ya sayansi katika Elimu ya Sekondari na vyuo vya ualimu;
- (g) Upungufu wa vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia katika Elimu ya Sekondari na Elimu ya Juu;
- (h) Upungufu na uchakavu wa miundombinu katika Elimu ya Juu, Shule Kongwe za sekondari na vyuo vya ualimu;
- (i) Mahitaji makubwa ya rasilimali katika kuviwezesha vyuo vya ualimu kutumia TEHAMA;
- (j) Idadi ndogo ya wanafunzi wa kike wanaosoma masomo ya sayansi katika ngazi zote za elimu na mafunzo;
- (k) Kuongezeka idadi ya wanafunzi wa elimu ya juu wanaohitaji mikopo kutoendana na uwezo wa Serikali wa kutoa mikopo hiyo;
- (l) Uhaba wa walimu, wakufunzi na wahadhiri; na
- (m) Kuongeza udahili wa wanafunzi katika elimu na mafunzo ya ufundi stadi ili kutoa mafundi wa ngazi za kati watakaoinua uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu malengo na bajeti ya mwaka 2010/1. Katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa malengo ya mwaka 2009/2010, Wizara itatekeleza yafuatayo katika mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Kamishna wa Elimu. Katika mwaka 2010/2011, Ofisi ya Kamishna:-

- (a) Kuimarisha utoaji elimu kwa usawa kwa kuandaa mwongozo wa utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Elimu Jumuishi;
- (b) Kutoa elimu kwa umma inayohusu uzuiaji wa mimba za utotoni kwa wanafunzi;
- (c) Kufanya uchaguzi wa wanafunzi wenyewe ulemavu kijiungu na Kidato cha Kwanza mwaka 2011 na kununua na kusambaza vifaa maalum vya kufundishia na kujifunzia na visaidizi kwa wanafunzi wenyewe mahitaji maalum;
- (d) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa utoaji wa Elimu Maalum/Jumuishi katika Halmashauri 16 za Mikoa ya Manyara, Arusha, Lindi na Mtwara;
- (e) Kutayarisha na kutangaza vipindi 580 vya masomo kwa njia ya redio (Sayansi, Kiingereza na Kiswahili Darasa la V – VII; Historia, Jiografia na Uraia kwa Darasa la III – VII), na 52 vya Boresha Elimu na Ufundishaji kwa Kutumia Njia Shirikishi;
- (f) Kufuatilia utekelezaji wa masharti ya usajili wa shule katika mikoa 10 (Arusha, Dodoma, Tabora, Tanga, Mbeya, Mwanza, Iringa, Morogoro, Pwani na Mtwara);
- (g) Kukamilisha uandishi wa taarifa ya matokeo ya Utafiti wa Kimataifa kuhusu Ubora wa Elimu ya Msingi katika Nchi 15 za Kusini na Mashariki ya Afrika (*SACMEQ Research Project III*) na kuisambaza kwa wadau; na
- (h) Kuandaa rasimu ya uanzishwaji wa Bodi ya Weledi ya Walimu (*Teachers Professional Board*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Elimu ya Msingi. Mwaka 2010/11, kazi kubwa za Idara ya Elimu ya Msingi zitakuwa:-

- (a) Kutathmini utekelezaji wa MMEM Awamu ya II kwa ajili ya kuandaa MMEM Awamu ya III;
- (b) Kufuatilia na kutathmini matumizi ya fedha za MMEM II na utekelezaji wa malengo yake ikiwa ni sehemu ya mapitio ya Sekta ya elimu;
- (c) Kufanya utafiti na kuainisha njia mbalimbali za kuongeza uandikishaji na mahudhurio katika shule za awali;
- (d) Kuandikisha watoto 2,043,984 wa Elimu ya Awali na 1,383,752 wa Elimu ya Msingi;

(e) Kuandaa miongozo ya ufuatiliaji na tathmini ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto na upimaji wa utoaji wa elimu ya awali pamoja na kuwajengea uwezo wadau 142 wa malezi/makuzi na maendeleo ya mtoto katika Halmashauri 5;

(f) Kufuatilia uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya awali na wa darasa la kwanza mwaka 2011;

(g) Kuinua ubora wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia na utoaji wa elimu kwa usawa kwa kuendelea kugharimia ujenzi wa Shule ya Msingi Monduli Jeshini (*Sokoine Cantonment*) na kukarabati Shule ya Msingi Arusha;

(h) Kuratibu na kufuatilia Mpango wa Lishe Shuleni katika Halmashauri 16 zinazofadhiliwa na WFP, kukamilisha uandaaji wa Mpango wa Kitaifa wa Lishe shuleni na mradi wa ufundishaji kwa kutumia TEHAMA wa *Bridge IT*;

(i) Kuihamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuwaandikisha watoto katika shule za awali ili wawe tayari kuanza Darasa la Kwanza na kujifunza kusoma, kuandika na kuhesabu;

(j) Kuwajengea uwezo walimu kupitia walimu mahiri 3,000 watakaobainishwa ili kuinua kiwango cha ufundishaji wa masomo ya Hisabati, Sayansi na Lugha; Aidha, katika mwaka 2010/11 majoribio yataanza kutumia vitabu vya *New Oxford English Course for Schools* ili kuimarisha lugha ya Kiingereza shuleni;

(k) Kugharimia mafunzo kwa wasimamizi wa elimu ngazi ya Kata, Wilaya na Mkoa;

(l) Kuimarisha mtaala ili uzingatie umahiri wa mwanafunzi na mahitaji ya soko la ajira (*Competence Based Curriculum*)

(m) Kuwajengea uwezo wasimamizi wa elimu 200 wa ngazi mbalimbali, wakiwemo Maafisa Elimu wapya katika usimamizi na, uendeshaji wa Elimu ya Msingi;

(n) Kuratibu uandaaji na uendeshaji wa mitihani ya Taifa ya Darasa la IV na VII; na

(o) kutafuta wadhamini wa michezo na kuanza kuhamasisha michezo katika Elimu ya Msingi;

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Elimu ya Sekondari katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES), mwaka 2010/2011, Wizara itatekeleza awamu ya pili ya Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES II) kwa kushirikiana na ofisi ya Waziri Mkuu- TAMISEMI. Mradi wa MMES II unafadhiliwa na Benki ya Dunia kwa kipindi cha miaka mitano, kuanzia 2010/2011 – 2014/2015 kwa mkopo wa dola za Marekani 470

milioni. Chini ya mpango huu, shule zitapatiwa ruzuku ya kununulia vifaa vya kufundishia na kujifunzia, kujenga maabara na nyumba za walimu, kuwajengea uwezo walimu wa sayansi, hisabati na lugha ya kiingereza. Katika mwaka huu wa fedha mradi huo umetengewa kiasi cha shilingi 150 bilioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa awamu ya pili ya MMES unategemea kuinua ufaulu katika elimu ya sekondari hususan katika masomo ya Sayansi, Hisabati na lugha za Kiingereza na Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na utekelezaji wa malengo yaliyotajwa awali, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kupunguza uhaba wa walimu kwa kuanza mradi wa *Tanzania Beyond Tomorrow* kwa majaribio (*TestPhase*). Mradi huo unahusu kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji kwa kutumia TEHAMA katika shule 500 za awamu ya kwanza; na

(b) Kufuatilia utekelezaji wa ugatuaji wa uendeshaji wa shule za Sekondari katika Halmashauri za Wilaya, ikiwa ni pamoja na kutoa na kuratibu utekelezaji wa miongozo mbalimbali kwa kushirikiana na OWM-TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Elimu ya Ualimu. Katika mwaka 2010/2011, Idara ya Elimu ya Ualimu itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuwapangia vituo vya kazi walimu 14,501 wa Shule za Msingi wanaohitimu sasa katika vyuo vya ualimu vya umma na vile vya binafsi. Aidha, Idara itawapangia kazi walimu 17,204 (7,084 wa *Diploma* na 12,120 wa *Shahada ya Kwanza*) katika shule za serikali. Mafanikio haya makubwa yataiwezesha Serikali kupeleka angalau walimu watano katika kila Shule ya Sekondari nchini;

(b) Kudahili walimu wanafunzi 4,550 wa ngazi ya Cheti Daraja A, 5,055 wa Stashahada na 320 wa fani maalumu za Michezo, Muziki, Sanaa za Maonesho/Ufundu, Elimu Maalumu ya Sayansi Kimu katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali;

(c) Kuendeleza juhudzi za matumizi ya TEHAMA katika kufundisha na kujifunza, ikiwa ni pamoja na kuendesha mafunzo ya ndani vyuoni (*in-house training*) na kufanya mazunguzo na wahisani wenye nia ya kusaidia juhudzi za matumizi ya TEHAMA;

(d) Kuratibu utoaji wa elimu ya michezo kwa kuanza na vyuo vya ualimu 12 kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali liitwalo Liike la Finland;

(e) Kutayarisha mwongozo wa vigezo vya ubora wa walimu (*Teacher Competency Framework*) pamoja na kuendesha mafunzo ya walimu kazini kwa walimu 700 wa shule za msingi katika Halmashauri saba za majaribio (Mtwara (V), Makete, Bagamoyo, Temeke, Hai, Siha na Magu) kwa kushirikiana na UNICEF;

(f) Kuwajengea uwezo wa wakufunzi 240 kuhusu masuala ya Afya ya Uzazi, Elimu ya UKIMWI, na Stadi za Maisha kwa kushirikiana na *UNESCO* ili kuinua kiwango chao cha kukabiliana na athari zitokanazo na magonjwa hatarishi kama vile UKIMWI, mimba zisizotakiwa, na mahusiano yasiyofaa;

(g) Kuimarisha mafunzo ya ualimu ili kuhakikisha wahitimu wa ualimu katika ngazi ya cheti na Diploma wanafikia viwango stahili katika hisabati na lugha ya Kiingerza ili kuimarisha taaluma;

(h) Kuendesha mafunzo ya mbinu za Ufundishaji Bainifu na Elimu ya UKIMWI kwa Wakufunzi 36, walimu wa Shule za Msingi 190 na walimu wa Shule za Sekondari 40 wa Mkoa wa Kigoma chini ya mpango wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa (*OneUN-Joint Programme North Western Tanzania: Transition from Humanitarian to Sustainable Development*); na

(i) Kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kifaransa kupitia mradi wa mafunzo kazini, kwa walimu wa Kifaransa 160 wa Shule za Sekondari na 240 wa Shule za Msingi, kwa ushirikiano na Ubalozi wa Ufaransa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi itaanza utekelezaji wa Mpango kabambe wa Kisomo kwa wasiojua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Mpango huu ulioanza kwa majaribio katika Wilaya tisa sasa utasambazwa nchi nzima chini ya kauli mbiu ya “Ndiyo Ninaweza”. Pamoja na hayo, Idara itafanya yafuatayo:-

(a) Kuwezesha uandaaji, ununuzi na usambazaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia vya wanakisomo kwa ajili ya programu ya Ndiyo Ninaweza;

(b) Kuratibu mafunzo ya wasimamizi 45 na wawezeshaji 360 wanaofundisha kisomo kwenye Halmashauri tisa za majaribio ya Mpango wa Ndiyo Ninaweza;

(c) Kufanya ufuatiliaji na tathmini katika Halmashauri tisa (9) zinazotekeliza programu ya Ndiyo Ninaweza ili kubainisha mafanikio na changamoto zilizojitekeza;

(d) Kuandaa, kuchapisha na kusambaza vitabu 450 vya wanakisomo (nukta nundu na maandishi makubwa), vitabu 60 vya wawezeshaji na miongozo ya wasimamizi kwa ajili ya programu ya Ndiyo Ninaweza;

(e) Kuandaa Mwongozo wa Uanzishaji na Usimamizi wa Mafunzo ya Elimu Masafa na Ana kwa Ana;

(f) Kuratibu utafiti wa kisomo ili kubaini hali halisi ya kiwango cha kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa kushirikiana na *UNESCO*;

- (g) Kuandaa Mpango Mkakati wa Elimu juu ya Haki za Binadamu; na
- (h) Kuratibu uaandaaji na Uchapishaji wa Magazeti Vijijini na makala nyingine katika vituo vya Kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya katika mwaka 2010/11, Idara ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi *SEADI* itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kukamilisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Ufundi na Ufundi Stadi (MMEU);
- (b) Kuendelea kutangaza na kuhamasisha vijana kijiungu na elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kupitia maonesho na vyombo mbalimbali vya habari, na kutembelea Shule za Sekondari;
- (c) Kuendeleza mpango wa ujenzi wa Vyuo 28 vya VETA vya Wilaya na kukamilisha ujenzi wa Vyuo vya VETA vya Mikoa ya Pwani, Manyara, Lindi na Dar es Salaam;
- (d) Kuendelea kuratibu uandaaji wa *Bridging Course* ya kuwapa sifa wahitimu wa mafunzo ya ufundi stadi kijiungu na mafunzo ya ufundi sanifu;
- (e) Kugharimia mafunzo ya vitendo viwandani kwa wanafunzi 700 wa Chuo cha Ufundi Arusha; na

- (f) Kuimarisha ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa katika masuala ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011 Idara ya Elimu ya Juu itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kukamilisha uandaaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Juu (MMEJU) na kuanza utekelezaji wake;
- (b) Kugharimia mafunzo ya wanafunzi 1,750 wa Shahada ya Kwanza ya Udaktari, Udaktari wa Meno na Tiba ya Mifugo katika vyuo vikuu vya ndani;
- (c) Kugharimia mafunzo kwa wanafunzi 70 raia wa Uganda na watano wa China katika utaratibu wa kubadilishana wanafunzi wa shahada ya kwanza;
- (d) Kuendelea kuelimisha umma kuhusu dhana ya uchangiaji wa gharama za Elimu ya Juu na fursa za Elimu ya Juu ndani na nje ya nchi kupitia vyombo vya habari, maonesho ya taasisi za Elimu ya Juu na kwa kutembelea wadau wa elimu;

(e) Kugharimia mafunzo ya Shahada za Uzamili na Uzamivu kwa wanataaluma 80 wa Vyuo Vikuu vya Umma;

(f) Kuratibu uteuzi wa wanafunzi 270 kwa nafasi zinazotolewa na nchi rafiki ambazo ni Algeria, China, Cuba, Urusi, Uingereza, Korea Kusini, Uturuki, Misri na India na 50 wa wanaokwenda kusoma Msumbiji kwa makubaliano ya kubadilishana wanafunzi;

(g) Kuanza kujenga hospitali ya kufundishia (*University Teaching Hospital*) katika eneo la Mloganzila kwa ajili ya Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili;

(h) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa mradi wa *Science, Technology and Higher Education* unaodhaminiwa na Serikali kuititia mkopo wa Benki ya Dunia, unaolenga kusomesha na kuimarisha ufundishaji wa Sayansi na Teknolojia katika Elimu ya Juu; na

(i) Kushirikiana na Taasisi zingine katika kugharimia ununuzi wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwa wanafunzi wenyewe ulemavu katika vyuo vikuu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Idara ya Ukaguzi wa Shule itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kusimamia ubora wa elimu itolewayo kwa kutumia utaratibu mpya wa ukaguzi wa shule kwa kukagua jumla ya asasi 20,045;

(b) Kuimarisha ukaguzi wa shule kwa kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kuwapatia usafiri, ukarabati wa ofisi, kuwajengea uwezo wakaguzi na kuwapatia stahili zao;

(c) Kuongeza ufanisi katika usimamizi wa elimu kwa kuteua na kutoa mafunzo ya awali kwa wakaguzi wa shule wapya 150;

(d) Kusimamia na kuendesha Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Pili mwaka 2010; na

(e) Kufanya ufuutiliaji wa utekelezaji wa utaratibu mpya wa ukaguzi wa shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Idara ya Sera na Mipango itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kukamilisha na kuchapa nakala 500,000 za Sera ya Elimu na Mafunzo 2011 na kusambaza kwa wadau mbalimbali wa elimu na kuandaa mkakati wa utekelezaji;

(b) Kugharimia utafiti wa kutafuta gharama halisi ya kumsomesha mwanafunzi wa Elimu ya Juu (*Unit Cost Study*);

(c) Kuimarisha Mfumo wa Takwimu (*Database*) ya elimu katika Halmashauri 105 kwa kushirikiana na UNESCO kupitia programu ya *ESMIS*;

(d) Kuratibu shughuli za Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu;

(e) Kuratibu maandalizi ya mpango mkakati wa utekelezaji wa TEHAMA kwa Wizara; na

(f) Kukarabati miundombinu ya vyuo vya ualimu 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Idara ya Utawala na Rasilimaliwatu itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuajiri watumishi wapya 290, kuidhinisha vibali vya ajira za wataalam wa kigeni 1,000, kuthibitisha kazini watumishi 55 na kupandisha vyeo watumishi 906;

(b) Kutekeleza Muundo mpya wa Wizara kwa lengo la kuimarisha utendaji; na

(c) Kuendelea kuratibu ulipaji madeni ya walimu na watumishi wasio walimu na kuweka mikakati ya kupusha malimbikizo ya madeni hayo ili kuondoa usumbufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano kitatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuratibu utoaji wa habari katika vyombo vya habari kuhusu matukio mbalimbali ya kielimu ili kufahamisha wadau wa Elimu kuhusu maendeleo ya sekta ya Elimu na kuweka kumbukumbu za Wizara;

(b) Kuandaa, kutengeneza, kuchapa na kusambaza nakala 300,000 za Jarida la *EdSDP* kwa Kanda nane za elimu ili kuihamasisha jamii kushiriki katika kutekeleza mipango ya Elimu;

(c) Kuandaa machapisho mbalimbali yakiwemo mabango, vipeperushi, vijarida na kalenda kwa ajili ya kuelezea sera na mipango mbalimbali ya maendeleo ya elimu kwa wadau;

(d) Kuratibu upatikanaji wa majibu ya maswali yanayoulizwa na wadau wa elimu kupitia Tovuti ya Wananchi ([www.wananchi.go.tz](http://www.wananchi.go.tz)); na

- (e) Kutayarisha mkakati wa mawasiliano na habari unaohusu shughuli za Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala, Taasisi na Mabaraza yaliyo chini ya Wizara yangu yanafanikisha utoaji wa elimu bora. Wakala, Taasisi na Mabaraza yatakeleza kazi zilizopangwa kwa kuzingatia malengo na mipango ya elimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima. Katika mwaka 2010/2011, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kudahili wanafunzi 420 ambapo, 150 ni wa ngazi ya Cheti, 140 wa Stashahada na 130 wa Shahada;

(b) kuandikisha jumla ya walengwa 75,000 kupitia mpango wa Elimu Masafa na Ana kwa Ana;

(c) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika usimamizi wa taarifa za Elimu ya Watu Wazima na Elimu nje ya Mfumo Rasmi;

(d) Kuratibu utekelezaji wa Programu ya majoribio ya *Integrated Post-primary Education (IPPE)* katika wilaya za Siha, Temeke, Magu, Makete, Mtwara Vijijini, Hai na Bagamoyo na kuandika masomo ya Ufundu na Masuala mtambuka ya programu hii katika mfumo wa moduli;

(e) Kuendelea kuwajengea uwezo wa kufundisha mtaala unaozingatia soko na matakwa ya *NACTE* wakufunzi na wahadhiri wa *TEWW* na Vyuo viliyyo chini ya *NACTE*;

(f) Kufanya tathmini ya kina ya programu zinazoendeshwa na *TEWW* pamoja na mpango wa Elimu Masafa na Ana kwa Ana tangu ulipoanza mwaka 2004 hadi 2009;

(g) Kuandaa mitaala na kuandika moduli za masomo ya kidato cha tano na sita kwa masomo ya *Economics, General Studies, Accounts na Applied Basic Mathematics* kwa mfumo wa Elimu Masafa;

(h) Kuandaa moduli za mafunzo ya Stashahada ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Endelevu kwa njia ya Elimu Masafa; na

(i) Kuendesha mafunzo ya elimu masafa na ana kwa ana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Taasisi ya Elimu Tanzania itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kutoa mafunzo elekezi juu ya mitaala iliyorekebishwa kwa walimu 1,650 wa sekondari;

(b) Kubuni na kuandaa mtaala wa mafunzo ya ualimu unaotumia TEHAMA;

(c) kugharimia mafunzo ya wakuza mitaala 55 juu ya kubuni, kutengeneza na kueneza maandishi ya kielimu yanayotumia TEHAMA;

(d) Kuchapisha moduli za masomo 17 kwa mafunzo ya Ualimu ngazi ya Stashahada na 26 kwa mafunzo ya Ualimu Cheti; na

(e) kuhariri muhtasari wa masomo ya mitaala ya elimu ya awali, msingi na sekondari ili kuingiza maoni ya wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuimarisha na kuinua ubora wa huduma za maktaba kwa watu wazima na watoto katika mikoa 19 ikiwa ni pamoja na kuongeza machapisho 60,000;

(b) Kutoa ushauri wa kitaaluma juu ya uanzishaji, upangaji na uendeshaji wa Maktaba za Shule, Vyuo, Taasisi na Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya nchini;

(c) Kutoa mafunzo ya Ukutubi na Uhifadhi wa Nyaraka kwa walengwa 200 wa cheti; 220 wa stashahada na 180 wa mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi wa maktaba za shule, vyuo na taasisi mbalimbali nchini; na

(d) Kuendeleza ujenzi na kuimarisha Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi wa Nyaraka Bagamoyo ikiwa ni pamoja na kuanza ujenzi wa hosteli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11. Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu utatekeleza yafuatayo:-

(a) Kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa viongozi 300 wa idara mbalimbali za elimu na Mashirika Yasiyo ya Serikali;

(b) Kutoa mafunzo ya mwezi mmoja ya Cheti cha Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi 500;

(c) Kutoa mafunzo ya mbinu za kuandaa Mpango wa Jumla wa Maendeleo ya Shule kwa Maafisa 2,000 katika ngazi ya Wilaya;

(d) Kutoa mafunzo ya mwezi mmoja ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Wakuu wa Shule za Sekondari 240;

(e) Kutoa mafunzo ya awali ya Uongozi na Uendeshaji wa elimu kwa Wakuu Wapya wa Shule za Sekondari 1,000 kutoka katika mikoa yote ya Tanzania Bara;

(f) Kutoa mafunzo ya mwezi mmoja ya Uongozi na Uendeshaji wa elimu kwa Wakaguzi wa Shule 120;

(g) Kutoa mafunzo ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Maafisa Elimu wapya 106 kutoka katika mikoa yote ya Tanzania Bara;

(h) Kugharimia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa wafanyakazi 16 wa Wakala ndani na nje ya nchi juu ya mbini bora za ufundishaji, utafiti na ufuatiliaji wa mafunzo ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu;

(i) Kufanya utafiti wa kielimu kuhusu Uongozi na Uendeshaji wa Elimu katika Afrika Mashariki na Kusini mwa Africa chini ya mtandao wa *Lead-link*; na

(j) Kukamilisha Mpango Kabambe wa Maendeleo wa Wakala (*Master Plan*) na kuanza awamu ya kwanza ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa ya UNESCO. Katika mwaka 2010/11, Tume ya Taifa ya UNESCO itatekeleza yafuatayo:-

(a) Itafanya tathmini ya miradi ya UNESCO inayoendelea chini ya programu inazowashirikisha watekelezaji yaani *Participation Programme* na mingine itakayoidhinishwa na UNESCO;

(b) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa mpango kazi wa progamu ya Mwaka wa Kimataifa wa Sayari Dunia (*International Year of the Planet Earth - IYPE*);

(c) Kuendeleza ushirikiano na Tume za UNESCO za Afrika ya Mashariki chini ya Mpango wa pamoja wa ushirikiano kwa kuanda na kutekeleza mipango ya kujenga uwezo wa wafanyakazi (*capacity building*), kufanya ziara za kielimu (*Study Tours*) na programu ya kubadilishana watumishi (*Staff Exchange Programme*); na

(d) Kuendelea kuratibu mtandao wa Shule za UNESCO (*Associated School Project Network - ASPNET*) na kuendelea kuelimisha wanafunzi katika shule hizo juu ya masuala mtambuka ya jinsia, haki za binadamu, stadi za maisha na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Baraza la Mitihani la Tanzania litatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendesha mitihani ya Kumaliza Elimu ya Msingi, Kidato cha Nne na Sita, Maarifa (*QT*) na Ualimu; na

(b) Kuongeza ufanisi katika usimamizi na uendeshaji wa mitihani kwa kununua *server* yenye uwezo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011 Kituo cha Maendeleo Dakawa kitatekeleza kazi zifuatazo:-

- (a) Kuendelea na mchakato wa kukibadilisha kituo kuwa *Centre of Excellence*; katika kutoa elimu na utaalim wa Sayansi na Ufundu kwa vijana; na
- (b) Kuratibu shughuli za maendeleo ya Taasisi zilizopo kwenye kituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Mamlaka ya Elimu Tanzania itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kutafuta rasilimalifedha kwa ajili ya Mfuko kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwa ni pamoja na kuhamasisha wadau wa ndani na nje ya nchi na kutafuta ufadhilli wa miradi;
- (b) Kutoa ufadhilli wa miradi 250 ya elimu kwa Taasisi za elimu 250 zinazolenga kusaidia kuongeza udahili, ubora na upatikanaji wa elimu kwa usawa;
- (c) kukamilisha uandaaji wa rasimu ya marekebisho ya Sheria Na. 8 ya Mfuko wa Elimu ya mwaka 2001; na
- (b) Kuendelea kuhamasisha Halmashauri za Serikali za Mitaa kuanzisha Mifuko ya elimu na kuimarisha ushirikiano na Jumuiya ya Serikali za Mitaa Tanzania (*ALAT*) na kuhamasisha uchangiaji wa mfuko wa elimu kupitia vipindi vya televisheni na redio, vipeperushi, majarida na vyombo vingine vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania. Katika mwaka 2010/2011, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kukamilisha zoezi la kuandaa kanuni za utekelezaji wa mfumo wa tuzo zinazotambuliwa Kitaifa (*National Qualifications Framework*);
- (b) Kuendelea kuratibu na kutathmini mradi wa majaribio ya udhibiti wa ubora wa programu za vyuo vikuu vitano unaotekelawa na *Inter-University Council for East Africa* (IUCEA); na
- (c) Kuendelea kusimamia udahili wa wanafunzi wapatao 60,000 kwa kupitia mfumo wa udahili wa pamoja (*Centralized Admission System*) ili kuondoa tatizo la mwanafunzi mmoja kudahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja na hivyo kubana nafasi kwa wenyе sifa kudahiliwa katika Taasisi za elimu ya juu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu litatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kukagua vyuo 25 kwa ajili ya kutoa ithibati, kusajili vyuo 20 vya ufundu na kubaini sifa za wakufunzi ili kuwasajili;

(b) Kuratibu na kuandaa mitaala 30 inayozingatia umahiri na mahitaji ya soko la ajira pamoja na kuratibu mitihani katika vyuo vinavyotumia mitaala hiyo;

(c) Kuratibu mitihani katika vyuo 30 vinavyotumia mitaala inayolenga katika kujenga umahiri wa wanafunzi na mahitaji ya soko la ajira;

(d) Kuratibu udahili wa wanafunzi katika vyuo 17 vinavyotoa mafunzo ya elimu ya juu ya ufundi; na

(e) Kuratibu mafunzo kwa wakufunzi katika vyuo 20 juu ya ufundishaji katika mfumo wa elimu unaozingatia kumwezesha wanafunzi kuwa mahiri (*Competence Based Education and Training –CBET*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuongeza udahili kwa kutoa mikopo kwa wanafunzi 89,617 wanaosoma ndani na nje ya nchi katika ngazi mbalimbali za elimu ya juu;

(b) Kuwahamasisha wanafunzi wengi zaidi kuchukua masomo ya sayansi kwa kuendelea kutoa mikopo kwa asilimia 100;

(c) Kuimarisha ukusanyaji wa marejesho ya mikopo kwa kuelimisha na kuhamasisha wadaiwa, waajiri na umma kwa ujumla juu ya umuhimu wa kurejesha mikopo itolewayo na Bodi. Aidha, Bodi inatarajia kukusanya Sh. bilioni tano kama marejesho ya mikopo iliyotolewa;

(d) Kuendelea kutoa elimu kwa umma kwa njia mbalimbali zikiwemo vipeperushi, magazeti, redio, televisheni, warsha na maonesho kuhusu wajibu wao wa kuchangia elimu ya juu na taratibu za utoaji mikopo na urejeshwaji wake;

(e) Kushirikiana na Wizara kujenga mfumo mbadala na endelevu wa utoaji wa mikopo ya Elimu ya Juu kwa kutumia Asasi za fedha ili kupanua wigo wa wanaostahili kupewa mikopo; na

(f) Kuboresha mfumo wa *Means Testing* ili kupunguza malalamiko na rufaa za wanafunzi kwa Waziri. Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kutegemeza awamu ya kwanza ya Programu ya Vituo vya Ufundi Stadi vya Wilaya (*District Vocational Training Centres Programme*) kwa kujenga vituo sita vya ufundi stadi;

- (b) Kujenga uwezo wa wakufunzi 30 na watumishi wa kawaida 315;
- (c) Kuendelea kufanya utafiti katiti (*Tracer Study*) wa nchi nzima ili kubaini soko la elimu ya ufundi stadi;
- (d) Kukarabati karakana za vituo vitatu vya ufundi stadi vya Mwanza, DSM na Kihonda na kujenga Ofisi za Kanda ya Kusini-Mashariki; Mtwara; na
- (e) Kuendeleza ujenzi wa vituo vitano vya Ufundi Stadi - Lindi, Mtwara, Manyara, Pwani na Dar es Salaam na kuimarisha Vituo vya Ufundi Stadi vya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kitatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi wapya 6,785 ambapo 4,125 ni wa shahada ya kwanza na 2,660 Shahada ya Uzamili na Uzamivu na kutoa kipaumbele kwa wanafunzi wa kike na wenyewe mahitaji maalum;
- (b) Kuendeleza ushirikiano na wafadhili mbalimbali katika kugharimia utafiti na mafunzo, hasa katika nyanja za mazingira, ujasiriamali, nishati, utalii, sekta isiyo rasmi, TEHAMA, mabadiliko ya tabianchi, miundo mbinu, lugha, demokrasia, na utawala bora;
- (c) Kutoa machapisho 19 ya vitabu na 280 majarida katika nyanja mbalimbali za utafiti;
- (d) Kuendeleza ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya chuo ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;
- (e) Kuendeleza ujenzi wa Makao Makuu mapya ya Taasisi ya Sayansi za Bahari eneo la Buyu, Zanzibar;
- (f) Kuanzisha shahada nne (4) za kwanza (*B.A. in Kiswahili, B.Sc. in Textile Engineering, B.Sc. in Textile Design and Technology* na *B.Sc. in Actuarial Science*), shahada mbili za Uzamili (*Masters in Intergrated Sanitation Management* na *MSc.in Biodiversity and Conservation*) na shahada moja ya Uzamivu (*PhD. by Coursework and Dissertation in Political Science and Public Administration*);
- (g) Kufanya ukaguzi wa kitaaluma katika Shule Kuu na Idara za kitaaluma (*Academic Audit*); na
- (h) Kuajiri na kusomesha wahadhiri na wafanyakazi waendeshaji kwenye fani mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11 Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam kitatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi wapya 1,000 (150 wa fani ya sayansi);
- (b) Kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ajili ya wanafunzi wenyewe ulemavu;
- (c) Kujenga kituo cha afya ili Chuo kiwe na uwezo wa kutoa huduma za afya ya msingi kwa jamii ya Chuo Kikuu Kishiriki;
- (d) Kuipatia maktaba ya chuo vitabu 1,000, majorida 200 na kuimarisha matumizi ya TEHAMA ili kuinua ubora wa elimu inayotolewa; na
- (e) Kugharimia mafunzo ya wanataaluma 10 katika ngazi ya Uzamili, watano wapya katika ngazi ya Uzamivu na sita wanaoendelea na mafunzo ya Shahada ya Uzamivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kitatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi wapya 800 wa shahada ya kwanza na kufanya idadi ya wanachuo kufikia 2,200;
- (b) Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia; kuanza mchakato wa ujenzi wa jengo la utawala ili kuongeza nafasi za ofisi; na
- (c) Kugharimia mafunzo ya wahadhiri 20 (wanne Uzamivu na 16 Uzamili).  
Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma itatekeleza yafuatayo:-
  - (a) Kudahili wanachuo wapya 195 (Shahada ya Kwanza 150, Stashahada ya Uzamili 15, Shahada ya Uzamili 10 na Cheti 20);
  - (b) Kuanzisha gazeti la wiki la mafunzo kwa wanachuo;
  - (c) Kufanya utafiti katika fani za uandishi wa habari, mawasiliano na utangazaji;
  - (d) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika kufundishia na kujifunzia; na
  - (e) Kujenga na kukarabati miundombinu ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kitatekeleza yafuatayo:-

(a) Kudahili wanachuo 2,304 wa shahada ya kwanza na 300 wa Uzamili na Uzamivu;

(b) Kujenga na kukarabati miundombinu ya chuo ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

(c) Kuanzisha shahada mpya sita za kwanza na sita za Uzamili;

(d) Kuanza mradi wa uvunaji maji ya mvua kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji;

(e) Kuanzisha Taasisi ya Kitaifa ya Bioteknolojia ya Kilimo (*National Agricultural Biotechnology Institute*) ili kukabiliana na changamoto za utekelezaji wa Kilimo Kwanza; na

(f) Kufanya utafiti unaolenga kumwondolea umaskini mkulima, kukuza uchumi na kuboresha mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Elimu za Biashara Moshi cha Chuo Kikuu cha Sokoine kitatekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Kudahili wanafunzi wapya 1,500 wa mwaka wa kwanza ili kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 2,713 mwaka 2009/10 hadi 3,330 kwa Mwaka 2010/11. Ongezeko la udahili wa wanafunzi litatokana na kuanzishwa kwa kozi za cheti katika kampasi ya Kizumbi (Shinyanga);

(b) Kuendelea kugharimia mafunzo ya Wahadhiri 30 katika kiwango cha Shahada za Uzamili na Uzamivu;

(c) Kuimarisha matawi manne ya kanda, Mtwara, Iringa, Mwanza na Tanga ili kuielimisha jamii katika masuala ya Vyama vya Ushirika vya Akiba na mikopo (*SACCOS*), maendeleo ya ushirika, utunzaji mazingira, na mikakati ya kupunguza umaskini;

(d) Kukamilisha utekelezaji wa masharti yaliyotolewa na Tume ya Vyuo Vikuu ili kukiwezesha Chuo kupanda daraja na kuwa Chuo Kikuu kamili ifikapo mwaka 2014;

(e) Kuendelea na ukarabati wa miundombinu ya chuo kwa ajili ya kuinua ubora wa mazingira ya kujifunzia na kufundishia; na

(f) Kufanya utafiti juu ya vyama vya ushirika, *SACCOS* na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/11, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kimejizatiti kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(a) Kudahili wanafunzi wapya 7,306 (wanawake 2,262). Kati ya hao, 2,238 ni wa Vyeti na Stashahada, 2,827 wa Shahada ya Kwanza na 2,241 ni wa Stashahada ya Uzamili na Shahada za Uzamili na Uzamivu. Aidha, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kinatarajia kutoa wahitim 1,697, ambapo 1,257 watakuwa wa Shahada ya Kwanza, 112 Vyeti na Stashahada nyingine, 328 Stashahada ya Uzamili na Shahada za Uzamili na Uzamivu;

(b) Kujenga ofisi za vituo vya Mikoa ya Mtwara na Manyara;

(c) Kukarabati majengo kwa ajili ya kuinua ubora wa elimu na kutengeneza mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunzia katika kituo cha Mkoa wa Rukwa, Kagera, Kilimanjaro, Mara na Ruvuma;

(d) Kununua ardhi kwa ajili ya ujenzi wa ofisi katika vituo vya mikoa; na

(e) Kujenga vituo vya Elimu Masafa (Afrika/ *SADC*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2010/2011, Chuo Kikuu Ardhi kitatekeleza yafuatayo:-

(a) Kudahili wanafunzi wapya 1,350 wa Shahada ya kwanza, 75 wa Shahada za Uzamili na Uzamivu na 20 wa cheti. Jumla ya wanafunzi wote inalengwa kuwa 2,606, ambayo ni ongezeko la asilimia 21 ukilinganisha na mwaka 2009/10. Wanawake wanatarajiwa kuwa asilimia 30 ya wanafunzi wote;

(b) Kuanzisha programu mpya tatu (3) za shahada ya kwanza katika uhandisi-ujenzi (*Civil Engineering*), Fedha na Uhaisibu (*Finance and Accountancy*); na Masoko (*Marketing*);

(c) Kugharimia mafunzo ya wahadiri 25 wapya na wafanyakazi waendeshaji 20 wapya;

(d) Kukamilisha utafiti katika maeneo 15 kati ya 63 yanayoendelea; kutoa machapisho 25 na kutoa huduma za kitaalamu (*Consultancies and Public Service*) katika miradi 100; na

(e) Kujenga na kukarabati miundombinu ya chuo ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2010/11 Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kitakeleza yafuatayo:-

(a) Kudahili wanafunzi wapya wa shahada ya kwanza 350 na wa shahada za uzamili na uzamivu 170;

(b) Kuanza matayarisho ya ujenzi wa majengo ya utawala, kumbi za kufundishia na hosteli ya wanafunzi katika eneo la Mloganzila;

(c) Kujenga miundombinu ya barabara, maji na umeme na kukamilisha makubaliano ya mkopo nafuu kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Korea Kusini na kuanza ujenzi wa Hospitali ya Kufundishia ya Chuo Kikuu (*University Teaching Hospital*) katika eneo la Mloganzila;

(d) Kukarabati na kujenga miundombinu katika kampasi ya Muhimbili ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia; na

(e) Kuendeleza utafiti, katika maeneo mbalimbali kama vile malaria, magonjwa ya akina mama na watoto, chanjo ya UKIMWI na dawa asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Chuo Kikuu Mzumbe kitakeleza kazi zifuatazo:-

(a) udahili wanafunzi wapya 2,600, ambapo 1,400 ni wa cheti, stashahada na Shahada ya Kwanza na 1,200 ni wa Shahada za Uzamili;

(b) Kugharimia mafunzo ya watumishi 20 katika Shahada za Uzamivu na 42 katika Shahada za Uzamili;

(c) Kukamilisha awamu ya pili ya ujenzi wa hosteli ya wanafunzi wa kike yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 400, kukamilisha ujenzi wa ofisi za wahadhiri na wafanyakazi waendeshaji zenye uwezo wa kuhudumia wahadhiri 271 na wafanyakazi waendeshaji 127 katika Kampasi Kuu Mzumbe na kukamilisha ujenzi wa maktaba yenye uwezo wa kuhudumia wasomaji 400 kwa wakati mmoja, kwenye Kampasi ya Mbeya;

(d) Kumalizia malipo ya vitalu vitatu vilivyopo Upanga, kwa ajili ya upanuzi wa Shule Kuu ya Biashara Kampasi ya Dar es Salaam;

(e) Kujenga na kukarabati miundombinu ya chuo ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

- (f) Kukamilisha tafiti 20, kuandaa machapisho na kutoa ushauri katika maeneo ya menejimenti, uongozi na Sayansi ya Jamii; na
- (g) Kuchapisha vitabu sita, makala za kufundishia sita na makala nyingine 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Chuo Kikuu Dodoma kitatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi wapya 5,000 katika shahada ya kwanza na 600 katika Shahada za Uzamili, ambapo asilimia 70 ya wanafunzi hawa wapya watadahiliwa katika shahada za elimu na mafunzo ya sayansi;
- (b) Kuanza ujenzi wa awamu ya pili ya Chuo cha Elimu kwa lengo la kuwa na walimu wanafunzi 10,000, Chuo cha Sayansi Asili na Hisabati wanafunzi 5,000 na Chuo cha Sayansi za Ardhi wanafunzi 3,000;
- (c) Kuanza awamu ya pili ya ujenzi wa Chuo cha Sayansi za Kompyuta, Habari na Mawasiliano ili kiwe na uwezo wa kuchukua wanafunzi 3,500 na kujenga awamu ya pili ya Chuo cha Sayansi za Afya na Tiba ili kiweze kuchukua wanafunzi 4,500;
- (d) Kukamilisha ujenzi wa awamu ya pili ya Chuo cha Sanaa na Sayansi za Jamii ili kiweze kuchukua wanafunzi 15,000. Ujenzi huu wa awamu ya pili ya Chuo Kikuu cha Dodoma utakiwezesha chuo kufikia lengo la kuwa na idadi ya wanafunzi wapatao 40,000 chuoni hapo;
- (e) Kukamilisha ujenzi wa barabara za ndani na za waenda kwa miguu; miundombinu ya kusafirishia maji safi, maji taka na maji ya mvua, umeme na mawasiliano;
- (f) Kukamilisha utafutaji wa maji na uwekaji wa miundombinu ya maji safi, kuinua ubora wa mazingira na upandaji wa miti; na
- (g) Kuinua ubora wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kitatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi wapya 230 wa programu ya Cheti, 300 Stashahada na 300 wa Shahada ya Kwanza;
- (b) Kugharimia mafunzo ya wanataluma 10 (watano Uzamili na watano Uzamivu) na wafanyakazi waendeshaji 10 ikiwa ni pamoja na wanaoendelea na masomo;
- (c) Kutathmini mitaala ya Cheti, Stashahada na Shahada ili iweze kufanyiwa marekebisho;

- (d) Kukamilisha uandaaji wa mitaala ya ualimu kwa programu za Stashahada na Shahada;
- (e) Kuendelea na ujenzi wa awamu ya pili katika Tawi la Chuo eneo la Bububu – Zanzibar;
- (f) Kufuatilia ufumbuzi wa tatizo la mmomonyoko wa ardhi Kivukoni katika ofisi ya makamu wa Rais – Mazingira; na
- (g) Kuanza ujenzi wa hosteli mbili za wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Chuo cha Ufundii Arusha kitatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuanzisha programu mpya ya shahada ya kwanza katika fani ya *Civil and Irrigation Engineering*;
- (b) Kuandaa mitaala ya programu 4 za Stashahada katika fani za *Heavy Duty Equipment Technology, Lapidary & Jewelery Technology, Civil and Irrigation Engineering* na *Computer Engineering*;
- (c) Kutathmini mahitaji na kufanya mapitio ya kozi ya msingi ya ukutubi;
- (d) Kuanzisha kitengo cha uzalishaji wa bidhaa mbalimbali kama mashine za kuchomea na Huduma za Utaalam Elekezi;
- (e) Kugharimia mafunzo ya mbinu za utaalam uelekezi kwa wanataaluma 15;
- (f) Kufanya ukarabati wa jengo la utawala, karakana na nyumba za watumishi; na
- (g) Kuandaa Mpango Mkakati wa chuo kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani za pekee kwa wananchi, viongozi na Wahisani mbalimbali kwa kuchangia utekelezaji wa Mipango ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii. Baadhi ya Wahisani hao ni Serikali za: Algeria, Canada, China, Cuba, Finland, India, Ireland, Jamhuri ya Watu wa Korea, Japan, Marekani, Misri, Norway, Pakistan, Poland, Ubelgiji, Ufaransa, Uhollandi, Uingereza, Ujerumani, Sweden na Uturuki.

Aidha, mashirika yaliyochangia katika kufanikisha programu zetu za Elimu ni pamoja na *Aga Khan Education Foundation, Barclays Bank, Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), CIDA ( Canada), COL, CRDB, DAAD, DANIDA, DFID, EDC, GTZ, ILO, International Reading Association, Irish Aid, JICA, JOVC, KOICA, NBC, NMB, NORAD, OPEC, Oxfam, Peace Corps, Plan International, Sida (Sweden), Umoja wa Nchi za Ulaya (EU), UNAIDS, UNDP, UNESCO, UNFPA, UNICEF, USAID, VSO, WFP, Sight Savers International, UIL, Book Aid International,*

*BP, Care International, CBP, Children International, Winrock International, World Vision na ZAIN.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru viongozi wa matawi ya, *CWT, RAAWU, THTU* na *TUGHE* kwa ushirikiano na ushauri wao katika kushughulikia masuala ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipitishe makadirio ya matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu ya Jumla ya Shilingi 665,572,537,000 kwa mwaka wa fedha 2010/2011 ili kutuwezesha kutekeleza mpango wa mwaka huu wa Wizara, katika maombi haya:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shilingi 72,005,369,000 zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Idara ambapo Shilingi 27,107,197,000 zinaombwa kwa ajili ya mishahara na Shilingi 44,898,172,000 zinaombwa kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shilingi 453,935,161,000 zinaombwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Taasisi ambapo Shilingi 169,745,089,000 zinaombwa kwa ajili yamishahara, na Shilingi 284,190,072,000 zinaombwa kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kati ya hizo, Shilingi 239,900,000,000 zimetengwa kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu.

Shilingi 139,632,007,000 zinaombwa kwa ajili ya Mipango ya Maendeleo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu. Kati ya hizo, Shilingi 56,212,445,000 ni fedha za ndani na Shilingi 83,419,562,000 ni fedha kutoka kwa washiriki wa maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru wewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia kwenye tovuti ya Wizara [www.moe.go.tz](http://www.moe.go.tz). (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe kwa uwasilishaji mzuri sana wa Hotuba yako kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu. Sasa naomba nimwite msomaji wa taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii kwa Niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, namwona Mheshimiwa Martha Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote

ninampongeza Dr Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuteuliwa kuwa mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia tiketi ya Chama Cha Mapinduzi na Dr. Mohamed Gharibu Bilal kuwa Mgombea mwenza na Dr. Ali Mohamed Shein kuwa mgombea Urais wa Zanzibar Mungu wabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha Maoni na Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, kuhusu Utekelezaji wa Malengo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010, na Malengo ya Mwaka wa Fedha 2010/2011, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, Kanuni ya 99(7) na Kanuni ya 114(11).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilipata muda wa kufikiria na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Malengo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 na pia kupitia Malengo na Maombi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2009/2010, Kamati yangu ilitoa maoni na maagizo kwa Serikali katika maeneo mbalimbali yafuatayo:-

- Mazingira ya Elimu ya Juu yaboreshwe kwa kufanyiwa ukarabati ikiwa ni pamoja na ukarabati wa maji safi na taka;
- Serikali iwe na mtazamo mpya wa namna ya kuendelea kutoa mikopo kutokana na kuongezeka kwa waombaji. Aidha, Bodi ya Mikopo iendelee kufuatilia marejesho ya mikopo;
- Serikali iendelee kutoa elimu kwa wadau wote kuhusu Sera ya Uchangiaji wa Gharama za Elimu ya Juu;
- Vibali vyta kusajili shule vitolewe kwa sharti la shule kuwa na maabara zenye vifaa. Aidha, kuimarisha na kukarabati maabara zilizopo; na
- Wizara ifanye utafiti wa Bodi za Shule ili kuona kama sifa za uteuzi wa Wajumbe zimezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı kwa kufanikiwa kukusanya Tsh. 5,930,827,864.34 zaidi ya lengo la ukusanyaji wa maduhuli katika Mwaka wa Fedha 2009/2010, ambapo lengo ilikuwa Tsh. 4,510,784,000. Aidha, inaipongeza kwa utekelezaji wa ushauri wa Kamati kuhusu Malengo ya Bajeti ya Mwaka 2009/2010 unaoishia Juni, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2010/2011, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı imejielekeza kutoa vipaumbele katika maeneo yafuatayo:-

- Kukamilisha mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi;
  
- Kuongeza upatikanaji wa Walimu, Wahadhiri na Wataalam wa Maabara katika ngazi zote husika;
  - Kuongeza nafasi na fursa kwa usawa katika ngazi zote za Elimu na Mafunzo wakiwemo Watu Wenye Ulemavu na wenye mahitaji mengine maalum;
  
- Kuendelea kuimarisha udhibiti na ubora wa elimu kwa kufanya ukaguzi wa shule, ufuatiliaji na tathmini ya Mipango ya Elimu;
  
- Kuanza kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Juu (*HEDP*) na kuandaa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (MMEU);
  - Kuendelea kuimarisha ubora wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za Elimu na Mafunzo kwa wenye mahitaji maalum;
  
- Kutoa mafunzo ya Walimu kazini ili kuinua ubora wa ufundishaji, hususan masomo ya Hisabati, Sayansi na Lugha;
  
- Kuendelea kujenga maabara za sayansi katika shule za sekondari na vyuo ili kuinua ubora wa ufundishaji wa masomo husika;
  
- Kutekeleza mpango wa ufundishaji kwa njia ya TEHAMA na kuhamasisha jamii, asasi na taasisi mbalimbali juu ya umuhimu wa kuchagia gharama za elimu na mafunzo katika ngazi zote; na
  
- Kuendelea kupanua na kukarabati vyuo ili kuweka mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo wa bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi unaonesha kuwa bajeti imeongezeka kuliko ile ya mwaka jana na kufikia jumla ya Tsh. 665,572,538,000. Ongezeko halisi linatokana na Bajeti ya Bodi ya Mikopo kuongezeka kutoka Tsh. 120,345,042,600 (2009/2010) mpaka Tsh.243, 266,608,000 (2010/2011). Vilevile bajeti ya Baraza la Mitihani kuongezeka kutoka Tsh. 14,332,301,900 (2009/2010) hadi Tsh.20, 719,963,900 (2010/2011). Tunaipongeza sana Serikali kuona umuhimu mkubwa kuongeza Bajeti ya Baraza la Mitihani na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kuwa, Wizara isimamie na kudhibiti matumizi ya Fedha zilizoombwba kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011. Aidha, Kamati inatoa angalizo kwa Wizara kuzingatia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (*CAG*) juu ya ukaguzi wa fedha na ukaguzi wa ripoti ya ufanisi kuhusu utendaji na uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maeneo muhimu yaliyozingatiwa na Kamati. Elimu ya Msingi bado inakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo, kushuka kwa ufaulu hasa katika Masomo ya Sayansi, kushuka kwa uandikishaji watoto wenyewe mahitaji maalum, upungufu wa Walimu na Wakaguzi wa Elimu pamoja na mdondoko wa wanafunzi kutokana na utoro na mimba kwa wasichana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa motisha kwa Walimu wanaofundisha katika shule zilizopo pembezoni ili kuvutia Walimu wengi kufanya kazi katika maeneo hayo ni changamoto kubwa sana katika kuinua ubora wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kuendelea kuajiri Walimu wa masomo mbalimbali, bado kuna upungufu mkubwa wa Walimu wa Shule za Sekondari na hasa Walimu wa Masomo ya Sayansi. Hali hii imefanya wanafunzi wengi kusoma masomo ya Sanaa na hivyo kujenga Taifa la baadaye ambalo litakuwa halina Wanasyansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuwa na mpango maalum wa kuwabakiza (*retain*) Walimu, mfano, kuwapa Posho ya Mazingira Magumu na nyumba kutokana na mazingira magumu ya vijiji ambayo hupelekea baadhi ya Walimu kuacha kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ugatuaji wa Elimu ya Sekondari. Itakumbukwa kuwa shule zote za sekondari zilitatuliwa na kupelekwa Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Ugatuaji huu umepata changamoto zifuatazo:-

- (i) Utayari wa Halmashauri kumudu majukumu haya mapya;
- (ii) Gharama za kuanzisha Ofisi za Idara ya Elimu ya Sekondari katika Halmashauri;
- (iii) Mahitaji makubwa ya rasilimali na vitendea kazi;
- (iv) Gharama za uelimishaji wadau;
- (v) Mahitaji ya mafunzo kwa watendaji; na
- (vi) Nafasi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi katika masuala ya utendaji wakati huu wa mpito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuweka mfumo wa wazi na unaoelewaka katika kuhakikisha kuwa Elimu ya Sekondari inasimamiwa vizuri ili lengo lililotarajiwa la ugatuaji lifanikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kushughulikia tatizo la ukosefu wa maabara katika shule na hasa zilizojengwa na wananchi, Serikali kupitia Benki ya (ADB) zimetoa kiasi cha Tshs.6.5 bilioni na kupelekwa katika Halmashauri zote nchini kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa maabara. Ni muhimu wadau wote wajue ni fedha kiasi gani zimepelekwa kwa kila Wilaya na kuwepo na uwazi jinsi fedha hizi zinavyotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ya Ufundu ndio msaada mkubwa hasa ukizingatia ongezeko kubwa la wahitimu wa elimu ya sekondari. Elimu ya ufundu inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ujenzi wa vyuo vinne vya VETA vya Mikoa ya Lindi, Pwani, Manyara na Dar es Salaam mpaka sasa utekelezaji umefikia asilimia 20 tu. Serikali ya Korea ya Kusini wamekubali kufadhili mradi huu kwa kushirikiana na Serikali yetu. Tatizo lililopo ni kwa Serikali kushindwa kutoa mchango wake wa Shilingi bilioni nane na hivyo kusababisha kutopata fedha hizi za wafadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali, kwa kuwa ujenzi wa vyuo hivi vinne umepangwa kukamilika ifikapo Desemba, 2010 na kwa kuwa wahisani wapo tayari kutoa mchango wao kwa sharti la Serikali na yenewe kutoa mchango wake kiasi cha Shilingi bilioni nane, Kamati inaomba Serikali itoe tamko hapa Bungeni la namna gani itatoa mchango wake ili fedha za wahisani za kiasi cha shilingi bilioni nane zisipotee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, VETA inapanuka kutokana na upanuzi wa vyuo vyake ishirini na mbili (22) na pia ujenzi wa vyuo vya Wilaya mia moja thelathini na mbili (132). Fedha iliyopo ya asilimia mbili (2%) ya *Skills Development Levy (SDL)* haitoshi kutekeleza ongezeko hilo la majukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali, ili VETA iweze kufanya kazi zake vizuri na kwa vile wananchi wengi wanategemea sana uwepo wa vyuo hivi, asilimia ya *Skills Development Levy* ipande kutoka asilimia 2% inayotolewa sasa mpaka asilimia 4%. Serikali inasema nini kuhusu ushauri huu katika kuimarisha Vyuo vya Ufundu nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ya Juu ndio chimbuko la wataalam wa fani mbalimbali ambao wanasaidia katika maendeleo ya kiuchumi na kisiasa katika jamii. Pamoja na juhudzi za Serikali za kutatua matatizo ya sekta hii, bado inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Wadau kutoridhika na utaratibu wa Bodi ya Mikopo wa upimaji wa uchumi wa mwombaji (*means testing*);

(ii) Kukosekana kwa maelezo ya kutosha kwamba fedha zinazotolewa ni mikopo na siyo ruzuku na hivyo kuongeza idadi ya waombaji hata wale ambao si wahitaji;

- (iii) Upungufu mkubwa wa Wahadhiri;
  - (iv) Baadhi ya Vyuo kushindwa kutekeleza matakwa ya Ithibati ikiwa ni pamoja na utengenezaji wa mitaala inayozingatia mahitaji ya soko la ajira kutokana na uwezo mdogo wa kifedha;
  - (v) Kuendelea kwa mmomonyoko wa ardhi ufukweni mwa Bahari ya Hindi ambao unatishia kuangusha baadhi ya majengo ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwl. Nyerere;
  - (vi) Mafao duni kwa wastaifu wa Vyuo Vikuu; na
- (vii) Kuendelea kuwa na idadi ndogo ya wanafunzi wa kike wanaochukua Masomo ya Sayansi katika Vyuo vya Elimu ya Juu, licha ya kuwepo na uhamasishaji na uelimishaji wa umuhimu wa masomo hayo. Aidha, bado mazingira ya vyuo hivi si mazuri kuanzia miundombinu chakavu, upungufu wa vitendea kazi, uhaba wa maktaba, vitabu, madarasa na hosteli za wanafunzi.
- Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kushughulikia changamoto hizi ili kuimarisha ubora wa elimu ya juu.
- Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (*TCU*); Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania kupitia Sheria ya Vyuo Vikuu Namba 7 ya mwaka 2005 Kifungu cha 12 (i) imepewa jukumu la kuratibu udahili wa wanafunzi wanaojiunga na Elimu ya Juu. Kifungu hiki kinaipa Tume mamlaka ya kuratibu kwa ufanisi udahili wa wanafunzi ili nafasi za elimu ya juu kwenye vyuo zitumike ipasavyo kwa kila mwanafunzi kudahiliwa katika chuo kimoja.
- Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha ufanisi kwenye udahili, Tume ilibuni taratibu mbalimbali lakini kadri Vyuo vya Elimu ya Juu vilivyoongezeka udahili uligubikwa na changamoto mbalimbali zikiwemo:-
- (i) Wanafunzi kudahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja;
  - (ii) Wanafunzi kutumia vyeti vya kughushi;
  - (iii) Wanafunzi kupokea mkopo zaidi ya mmoja;
  - (iv) Waombaji kutumia gharama kubwa kwa kulipia fomu zaidi ya moja au kufanya safari nyingi kwa chuo zaidi ya kimoja katika kuongeza fursa za kuchaguliwa.

Mfano, katika mwaka wa masomo 2009/2010 zaidi ya wanafunzi 24,622 waliomba kuijunga kwenye vyuo zaidi ya kimoja;

(v) Vyuo kusogeza mbele uanzaji wa mwaka wa masomo kutokana na matatizo ya udahili, mfano, katika miaka miwili iliyopita vyuo vililazimika kufungua baada ya tarehe 12 Oktoba jambo ambalo liliathiri ufundishaji; na

(vi) Vyuo kujiendesha chini ya kiwango chake cha udahili kutokana na wanafunzi waliowachagua kuijunga na vyuo vingine, mfano, katika mwaka wa masomo 2009/2010 kulikuwa na vyuo vilivyo sajili chini ya 45% ya wanafunzi waliowadahili. Hii iliacha wazi nafasi karibu 4000 vyuoni huku kukiwa na vijana wenye sifa za kuijunga na vyuo ambao wameachwa kudahiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya changamoto hizi kuongezeka Tume ilifanya tafiti ya mifumo mbalimbali ya udahili na Mfumo wa Udhili wa Pamoja (*Central Admission System (CAS)*) ulikubaliwa mwezi Machi, 2009 ambapo waombaji hutumia mitandao wa *internet* au ujumbe wa simu za mkononi kutuma maombi yao ya udahili. Mfumo huu mpya wa udahili una manufaa yafuatayo kwa mwombaji:-

(i) Mwombaji anaweza kuomba udahili katika vyuo mbalimbali kwa wakati mmoja;

(ii) Mfumo unapunguza gharama kwa mwombaji na kupunguza usumbufu wa kusafiri kupeleka maombi kwenye vyuo mbalimbali; na

(iii) Mfumo huu utaondoa changamoto zote ambazo zimekuwa zikiukabili mfumo wa udahili uliopita kama waombaji kutumia yeti vyta kughushi, wanafunzi kupokea mkopo zaidi ya mmoja na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri yafuatayo ili kuimarisha utaratibu wa Mfumo wa Udhili wa Pamoja (*Central Admission System*):-

(i) Serikali ihakikishe kuwa utaratibu huu unajulikana kwa watu wote hasa wanafunzi kwa kutoa elimu kwa njia mbalimbali mfano kuanzisha vipindi maalum, kutumia TV, magazeti na semina kwa wadau wote;

(ii) Serikali ifanye utaratibu kuhakikisha masomo ya kompyuta yanafundishwa mashulenii hususan shule zote za Sekondari;

(iii) Serikali ihakikishe utandikaji wa mkongo (*fibre optic cable*) unafanyika nchi nzima ili kufanikisha upatikanaji wa mitandao nchini; na

(iv) Walimu waandaliwe vizuri ili waweze kufundisha na kuongoza wanafunzi jinsi ya kufuata maelezo hasa katika lugha ya Kiingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Sayansi ya Bahari, Zanzibar (*Institute of Marine Science, Zanzibar*); Taasisi hii ni moja ya taasisi zilizo chini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Taasisi hii ilianzishwa tarehe 17/10/1978 chini ya Sheria Na.12 ya 1970 ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa tamko la Serikali Na.34 lililochapishwa tarehe 16/3/1979.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi inakabiliwa na changamoto kubwa na ya muda mrefu ya ufinyu wa eneo. Katika kushughulikia suala hili, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilitoa eneo la ekari karibu 125 huko Buyu, mnamo mwezi Oktoba, 2002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kuhakikisha jambo hili linashughulikiwa, Kamati ilitembelea eneo la Buyu tarehe 16/10/2006 na baada ya kuona kasi ya ujenzi inapungua, ilipendekeza mkataba uangaliwe upya na zitafutwe njia hata za kukopa benki ili ujenzi ukamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 6/4/2010, Kamati ilifanya ziara Zanzibar kwa mara nyingine na ilitembelea Taasisi hii na kuelezwu kuwa ujenzi uko katika awamu tatu, awamu ya kwanza ikiwa ni kujenga jengo la utawala na taaluma, maabara, maktaba na madarasa ambapo itagharimu sh. 6.2 bilioni kwa hesabu za mwaka 2006 na mkandarasi alitakiwa akamilishe kazi kwa muda wa wiki 73.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililojitokeza ni kwamba kiasi cha fedha kinachotolewa na Serikali hakilingani na gharama zinazotakiwa ambapo imekuwa ikitoa Sh. 800 milioni na Sh.1.2 bilioni kwa mwaka na hivyo ujenzi kupungua kasi na hatimaye kusimama kabisa. Aidha, toka ujenzi kusimama, mkandarasi alikuwa amefanya kazi ya Sh.1.8 bilioni na alishalipwa Sh.0.8 bilioni bado Sh.1.0 bilioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari za kusimama kwa ujenzi huu ni:-

- Kuongezeka kwa gharama za mradi ambapo hivi sasa unasemekana unagharimu TShs.18 bilioni kutoka TShs.6 bilioni;

- Chuo kudahili wanafunzi wachache sana mwaka 2009 na mwaka huu huenda wasidahiliwe kutokana na ufinyu wa nafasi; na

- Eneo la Buyu ambapo taasisi itajengwa limevamiwa na wananchi ambapo mipaka imeong'olewa, nyaya za umeme zimeibiwa, uchimbaji wa mawe na ukulima wa vitu mbalimbali, mfano, matunda, mihogo, ndizi na kadhalika, unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri fedha hizo zitafutwe kwa namna yoyote na Serikali ikubali kutoa dhamana ili taasisi hii iweze kukopa kutoka benki au Mifuko ya Hifadhi za Jamii. Aidha, Kamati inamtaka Waziri wa Elimu na Mafunzo ya

Ufundi, atoe ufanuzi wa kukwama kwa ujenzi wa Chuo hiki na hatua zitakazochukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaupongeza uongozi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kwa jinsi unavyofanikisha ujenzi wa Chuo kwa ubunifu mkubwa, mfano, ubunifu wa kuingia mikataba na mitandao ya simu (*VODACOM* na *ZAIN*) ya kuweka taa katika barabara zote za Chuo, kujenga sehemu za wanachuo kusomea (vimbweta) jambo ambalo lingesubiri fedha za Serikali ingechukua muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya Chuo Kikuu cha Dodoma ni mengi lakini ni vema kuanza na yafuatayo:-

(i) Hadi sasa Chuo kimepokea hati za madeni ya TSh. 8.3 bilioni kwa ujenzi wa jengo la utawala, barabara zote, samani za madarasani na mabwenini. Kamati inashauri deni hili litafutiwe ufumbuzi kwa kuangalia ndani au nje ya bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufund; na

(ii) Ujenzi wa Chuo umezorota kwa kuwa Serikali bado hajatoa dhamana kwa wawekezaji wengine. Mfano, *PSPF* wapo tayari kujenga Awamu ya Pili ya Chuo cha Elimu, Hii ingeondoa tatizo la Walimu nchini. *NSSF* wapo tayari kujenga Chuo cha Sayansi za Ardhi, Chuo cha Sayansi Asili na Hisabati, Nyumba za Walimu na mfumo wa kisasa wa maji taka. *LAPF* wapo tayari kukamilisha Awamu ya Pili ya Chuo cha Sayansi za Afya na Tiba. *GEPF* wapo tayari kujenga nyumba za wafanyakazi. Hawa wote, pamoja na kuwa Chuo kimeomba dhamana ya Serikali, bado hajatolewa na hawajaanza kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri suala la dhamana lishughulikiwe mapema ili ujenzi uweze kuendelea na hasa mfumo wa majitaka ili kuepusha madhara yatakayotokea kwa kukosekana mfumo huo hasa ikizingatiwa kuwa Chuo kinatarajia kuongeza wanafunzi msimu huu. Serikali inashauriwa kutoa dhamana haraka kwa *NSSF* ili wajenge kwa haraka mfumo wa maji taka vinginevyo chuo kinaweza kufungwa au kushindwa kudahili wanafunzi zaidi mwaka ujao wa masomo. Chuo mpaka sasa hakina hatimiliki. Aidha, *CDA* wanadai malipo ya TShs.750 milioni kwa mwaka, na chuo hakina uwezo wa kulipa. Kamati inashauri Serikali ishughulikie suala hili ili limalizike kwa vile hakuna sababu ya kuhamisha fedha kutoka mfuko mmoja wa Serikali kwenda mfuko mwingine wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hitimisho; Kwa niaba ya Kamati, ninamshukuru Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu akisaidiwa na Manaibu wake Mheshimiwa Mwantumu B. Mahiza, na Mheshimiwa Gaudentia M. Kabaka, pamoja na Watendaji wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu Profesa Hamis Dihenga na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Selestine Gesimba kwa

jinsi walivyoshirikiana na Kamati kutoa majibu ya hoja za Wabunge kuhusu utekelezaji wa Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010, na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ninamshukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas D. Kashililah na Ofisi yake kwa kutuhudumia vyema kipindi chote Kamati ilipokuwa kazini. Nawapongeza Makatibu wa Kamati hii Ndugu Hosiana John na Asia Paul Ninja, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi Taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kukupongeza wewe kwa jinsi unavyoendesha Vikao vya Bunge kwa umahiri na busara kubwa. Aidha, nampongeza Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa jinsi wanavyokusaidia kuendesha shughuli za Bunge. Vile vile, naomba kuchukua nafasi hii kuwapongeza sana Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge ambao ndio msingi wa mafanikio ya Bunge katika shughuli zake za kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa umuhimu wa kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa ushirikiano wao kwa namna tulivyoongoza shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naomba niwatambue wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Omari S. Kwaangw', Mwenyekiti; Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Dk. Ali Tarab Ali, Mjumbe, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, Mjumbe; Mheshimiwa Profesa Feetham F. Banyikwa, Mjumbe; Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mjumbe; Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mjumbe; Mheshimiwa Hemed M. Hemed, Mjumbe; Mheshimiwa Janet B. Kahama, Mjumbe; Mheshimiwa Dr. Christine Ishengoma, Mjumbe; Mheshimiwa Susan A.J. Lyimo, Mjumbe; Mheshimiwa Martha Mlata, Mjumbe; Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mjumbe; Mheshimiwa Profesa Idris A. Mtulia, Mjumbe; Mheshimiwa Omari A. Mzee, Mjumbe; Mheshimiwa Usi Amme Pandu, Mjumbe; Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mjumbe; Dr. Luka Jelas Siyame, Mjumbe; Mheshimiwa Ali Haroon Suleiman, Mjumbe; Mheshimiwa Fatma Abdulla Tamim, Mjumbe na Mheshimiwa Oscar R. Mukasa, Mjumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuwataenia Wajumbe wa Kamati na Wabunge wote kila la kheri katika mchakato wa Uchaguzi Mkuu ujao. Aidha, tunawashauri wananchi wa Babati Mjini wamrudishe Mheshimiwa Omari Kwaangw' kwa kishindo hapa Bungeni kutokana na umahiri na uwezo wake aliuonyesha katika kuongoza Kamati hii vizuri na kwa ushirikiano mkubwa na bado anahitajika hapa Bungeni. Namtakia kila la kheri Mwenyekiti wangu, Mheshimiwa Omari S. Kwaangw' na naamini Wananchi wa Babati Mjini watamchagua kwa kishindo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba kuwashukuru sana Wananchi wa Mkoa wa Singida hasa wanawake kwa kunichagua kuwa Mbunge wa Viti Maalum ili niweze kuwawakilisha hapa Bungeni. Naamini sikuwaangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kuishukuru familia yangu, watoto wangu, wazazi wangu, ndugu na marafiki wote kwa ushirikiano wao wa hali na mali pamoja na sala ili kufanikisha kazi zangu za Kibunge. Tuendelee kuombeana, pia naomba nimshukuru sana Dereva wangu Isadin Msangi kwa jinsi alivyoweza kufanya kazi yake kwa uaminifu mkubwa. Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, naunga mkono hoja. (*Makofit*)

**MHE. SUSAN A. LYIMO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu hotuba ya bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa fedha 2010/2011, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni ya 99(7), toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na afya njema kwa muda wote huu wa kipindi cha uhai wa Bunge hili na kuweza kusimama hapa leo hii. Kipekee kabisa naishukuru familia yangu hususan mume wangu mpenzi Boney Ngowi na watoto wetu Charlene, Dennis, Arnold na Aidan - Baraka, kwa kuniunga mkono na kunivumilia katika kipindi chote cha utekelezaji wa kazi zangu ndani na nje ya nchi. Naamini wataendelea hivyo hivyo katika Bunge lijalo, *Inshalaah*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Naibu wake Dr. Willibroad Peter Slaa kwa kuendelea kuwa na imani nami kushikilia wadhifa huu wa Msemaji Mkuu wa Wizara hii kwa mwaka wa tano sasa. Vile vile napenda kuwashukuru kwa kunipatia naibu mahiri, Mwalimu Nuru Bafadhili, Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru kambi ya Upinzani, kambi makini kabisa chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Hamad Rashid na Mheshimiwa Dr. Slaa kwa uongozi wao madhubuti unoijenga kambi ya Upinzani na kuifanya kuwa kambi imara na isiyotetereka na hivyo kuweza kufanya kazi yake ya kuikosoa Serikali bila woga wowote. Ninauhakikishia uongozi wa kambi ya Ushindani Bungeni na Watanzania wote Wazalendo kuwa nitafanya kazi hii, kwa uwezo wangu wote kwa lengo la kusaidia maendeleo ya Taifa letu la Tanzania kama msemaji mkuu au kama Waziri CHADEMA ikichukuwa dola katika uchaguzi ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa kuendelea kunipa ushirikiano ndani na nje ya Bunge. Nami naendelea kuwaahidi kuitunza imani ya chama changu na kuendelea kukitangaza kwa Watanzania wote. Mwisho, japo si kwa umuhimu, nawashukuru sana akinamama wa CHADEMA kwa kunichagua kuwa Makamu Mwenyekiti wao Taifa. Nawaomba tuendelee kushirikiana ili tuongeze idadi ya Wabunge wanawake katika uchaguzi ulio mbele yetu. Baada ya kusema hayo, sasa

naomba nitoe maoni ya kambi ya Upinzani katika Wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tokea miaka ya mwanzo ya Uhuru wa nchi yetu, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere alitutaka tushirikiane na tutumie nguvu za pamoja kupigana vita dhidi ya maadui wakubwa watatu yaani; ujinga, maradhi na umaskini. Miaka 49 sasa, tukiwa katika vita hivyo hatujaweza kumshinda angalau adui mmoja kati ya hao watatu na baya zaidi maadui hawa wamezidi kushamiri. Hapana shaka tuna udhaifu mkubwa sana katika mapambano yetu na udhaifu upo zaidi katika sekta ya Elimu nchini. Kwani ni wazi ukifuta ujinga, maradhi na umaskini yatutoweka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama elimu yetu isingekuwa na matatizo mbona tungeushinda ujinga, kwa Elimu tukaushinda umaskini na maradhi; kwa Elimu tukafikia kiwango kizuri cha maendeleo kama tulivyoshuhudia katika nchi za wenzetu (mathalani Singapore, Malaysia, China, Japan na nchi za Scandinavia) waliotumia raslimali watu vizuri, wakawekeza katika elimu na sasa wako mbali sana kimaendeleo. Hivi sisi Tanzania tumerogwa au tuna matatizo gani na elimu yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekosea sana katika elimu kuanzia nini tunachokiamini na tunachokitekeleza kuitia sera zetu na mipango mbalimbali ya elimu. Tumeshindwa kuwathamini askari wa mstari wa mbele katika vita vyetu (Walimu). Tumeendelea kutenga kiasi kidogo sana cha fedha kwa ajili ya sekta hii. Tumechezea mitaala na kuiyumbishayumbisha kana kwamba Taifa hili halina dira wala mwelekeo. Mara kwa mara kumekuwa na mabadiliko ya nadharia za sera na mipango ya elimu isiyo endelevu na sera zisizoendana na ukweli wa kiutafiti ambazo mara zote zimefanya ubora wa elimu uzidi kuporomoka. Kwa mtindo huo Taifa linaangamia kwa kupelekwa hatua moja mbele kisha hatua mbili nyuma ilihali ulimwengu wa utandawazi unasonga mbele kwa kasi, hautungojei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema tujitathmini sisi wenyewe, tutambue madhaifu yetu, tujirekebishe, tukubaliane njia sahihi za kutupeleka mahali sahihi tena kwa haraka. Hakika tunahitaji kwanza kujadiliana kwa pamoja, tuangalie pamoja na mambo mengine, lile ambalo wadau mbalimbali wa elimu wametoa wito tulifanye, yaani Mjadala wa Kitaifa kuhusu elimu, mjadala wetu uangalie ni nini tulipanga kufanya kama nchi, kitu gani kinatikelezwa katika sekta ya elimu na ni kipi kilicho bora zaidi ambacho tungepaswa kufanya. Kwa maana hiyo mjadala huu uwe sehemu ya kutathmini mipango na utekelezaji wake kisha uibue mapendekezo yatakayoliokoa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu taarifa za fedha za Serikali Kuu kwa mwaka ulioishia tarehe 30 juni, 2009; Taarifa za fedha zilionyesha maduhuli yasiyokusanywa ya Sh.1,207,376,154 yanayohitaji jitihada kubwa zaidi za kuyakusanya. Kulikuwa na makusanyo yenye shaka ya maduhuli yatokanayo na kodi ya pango ya nyumba za Serikali yenye thamani ya Sh.64,540,348 kwa kukosekana orodha ya nyumba na majina ya watumishi waliopangishwa nyumba hizo na viwango vya pango kwa mwezi. Maduhuli ya Sh.

45,776,500 hayakupelekwa benki kinyume na Kanuni ya 78(1) ya Kanuni za Fedha za mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004)

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya kiasi cha Sh. 385,350,000 yalifanyika bila kuwa na nyaraka za kutosha kinyume na Kanuni ya 86 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001(zilizorekebishwa 2004). Kwa hali hiyo uhalali wa matumizi hayo haukuweza kuthibitishwa. Posho za Sh. 156,678,954 zililipwa bila idhini ya uhamisho kutolewa kinyume na Kanuni ya 51 ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004). Malipo ya jumla ya Sh. 3,171,388 ya miaka iliyopita yalifanyika katika mwaka wa fedha 2008/2009 kinyume na Kanuni ya 54 (4) ya Kanuni ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha Sh.65,302,000 kilicholipwa kwa wanafunzi kutoka kaya maskini hakikuweza kuthibitishwa kutokana na kukosekana orodha za malipo zilizosainiwa kutoka shule husika. Masurufu ya kiasi cha Sh. 251,307,878 hayakurejeshwa katika muda unaotakiwa kinyume na Kanuni ya 103(1) ya Kanuni za Fedha za Umma za 2001 (zilizorekebishwa 2004).

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya upotevu wa mali kwa mwaka ulioishia 30 Juni, 2009 inaonyesha kuwa upotevu wa fedha na vifaa vyenye thamani ya Sh. 161,149,175 haikushughulikiwa. Wizara ilinunua huduma zenyetamani ya Sh. 291,957,680 ambazo hazikuwa kwenye mpango wa mwaka wa manunuzi mali zenyetamani ya Sh. 138,611,850 zilizoagizwa na kulipiwa hazikingizwa vitabuni na hivyo matumizi yake kutothibitishwa. Wizara ilihamisha kiasi cha Sh. 3,660,828,875 kutoka fungu la matumizi ya kawaida kwenda mradi wa Mipango na ukarabati na Idara nyinginezo kwa ajili ya manunuzi ya vifaa na huduma. Hata hivyo, mpango wa mwaka wa manunuzi na taarifa ya manunuzi vilionyesha kuwa manunuzi hayo hayakufanyika katika mwaka 2008/2009 kutokana na ukosefu wa fedha. ukijumlisha fedha hizi zenyetutata zinifikia sh 6,432,019,802 ambazo zingweza kujenga nyumba 715 za walimu kwa wastani wa shilingi million tisa kwa nyumba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu zimetengwa Sh. 2,045.3 bilioni (kutoka Sh 1,743.9 bilioni mwaka 2009/2010) sawa na ongezeko la asilimia 17.2. Tunaishukuru Serikali kwa kuongeza bajeti walau kukaribiana na ile ya Elimu ya upinzani tuliyopanga ya 22% = Sh bilioni 2,492.689,320. Kwa bajeti hii Serikali imetoka Sh 218 bilioni (2001) kufikia Sh 2.05 trillioni (2011) au ongezeko la mara kumi, ndani ya miaka kumi. Pamoja na shukrani na pongezi hizi na tujiulize tulitumiaje fedha zilizopangwa kwa ajili ya elimu 2009/2010?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kufikia Aprili, 2010 utekelezaji wa Bajeti za Utawala na Kamishna (ambaye ni sehemu ya utawala) ulikwenda vizuri kama ulivyopangwa katika bajeti kwa salio la 6.8% tu huku utekelezaji wa kasma nyingine ukiwa mbaya sana mfano; Habari Elimu na Mawasiliano hawajapata 80%, Sera na Mipango -69%, Elimu ya Msingi ambayo tunaipigania sana walikuwa hawajapata -74% ya bajeti na Elimu ya Watu wazima -58%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyokuwa kwa Matumizi ya Kawaida, utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo hadi Aprili 2010 nao ulioathirika sana katika maeneo ya Sera na Mipango, ukaguzi wa shule, Mafunzo ya Ufundı na zaidi sana katika Elimu ya Juu ambapo karibu 2/3 ilikuwa haijatolewa. Kwa mfano, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilipokea Sh. 1,475,500,000 kati ya Sh. 31,875,863,700 zilizotengwa, hii ina maana kwamba walikuwa (4.7%). Sisi wote tunajua matatizo ya Chuo Kikuu, ni cha zamani sana ambacho miundombinu yake ni mibovu sana. Lakini ukiangalia kwa mlinganisho huu Chuo Kikuu cha Dodoma ambacho wewe mjumbe wao kimeweza kupata 75% yaani Sh. 7,880,503,000 kati ya 10,444,472,000. Kambi inahoji ni kwa nini hakuna uwiano wa ugawaji fedha kati ya vyuo huku vyote vikiwa ni vya Serikali au vya Umma? Wote tunafahamu umuhimu wa fedha za maendeleo kwa miradi. Kama fedha hazitolewi kwa wakati hata zile za ndani tunajiuliza kuna haja gani ya kuitisha bajeti hapa Bungeni na fedha hizo kwa sasa hivi ziko wapi kwa sababu tumemaliza mwaka wa fedha? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya changamoto katika kipindi cha bajeti kinachokwisha ni haya yafuatayo na inapatikana katika ukurasa wa 8 hadi wa 10 wa hotuba yangu. Lakini kubwa ni: Elimu ya Msingi, uhaba mkubwa wa walimu hasa vijijini kwa shule za msingi na sekondari, uhaba mkubwa wa Wahadhiri, ufaulu mdogo wa wanafunzi hasa shule za sekondari zilizoko vijijini, rasilimali watu, miundo mbinu na fedha kutotosheleza katika ngazi zote, *Capitation Grant* kutotekelezwa ipasavyo, kushuka kwa uandikishaji katika elimu ya awali na watoto wenye mahitaji maalum,

mdondoko wa wanafunzi kuongezeka, bajeti kuendelea kushindwa kuweka wazi matumizi yote ya Elimu ya Msingi na elimu ya Sekondari, hamasa ndogo mionganoni mwa Walimu kutokana na mishahara duni, madai mbalimbali na sababu nyinginezo, kushindwa kuelekeza elimu yetu vizuri katika ajira na hasa kujitegemea katika kilimo na nyanja nyinginezo kama vile ufugaji, uvuvi, viwanda vidogo na kadhalika. Pia kushindwa kuelekeza elimu yetu, kujenga tabia njema na utamaduni mzuri ili kupambana na mmomonyoko wa maadili, rushwa, unyanyasaji na mauaji ya wazee, walemavu wa ngozi na kadhalika, Elimu ya Juu, majoribio yasiyo na tija kama vile uandikishaji wa wanachuo unaofanywa na *TCU (Central Admission System)* yenye usumbufu usio wa lazima na mradi wa ufundishaji kwa teknolojia (TEHAMA) ili kufidia uhaba wa walimu katika nchi yenye miundombinu haba na hamasa ndogo ya walimu.

Mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu bado ni kero kubwa. Ni wazi matatizo ya msingi yafuatayo hayakufikiriwa inavyostahili:-

Uhaba mkubwa wa walimu kwa ujumla, uhaba mkubwa wa walimu wa Sekondari na Msingi hasa vijijini, hamasa ya walimu, ikiwa ni pamoja na kiwango cha mishahara na vivutio vingine hasa walimu wa vijijini, suala la unyanyasaji wa wanafunzi ikiwa ni pamoja na mimba na usafiri Dar es Salaam na katika miji mingine na vijijini. Mazingira ya kufundishia hayajapewa kipaumbele; Suala la hamasa kwa walimu halikutazamwa, ufuatiliaji wa kuundwa kwa Bodi za Shule na uwezo wa Bodi hizo kiutendaji haukupewa kipaumbele; Mapungufu ya rasilimali watu na miundombinu na fedha za kuendeshea hayajapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya kujitegemea ili kuwawezesha wanafunzi waweze kujiajiri wamalizapo masomo haikuzingatiwa, Ongezeko la udahili wa wanafunzi katika vyuo bado hauridhishi ukilinganisha na mahitaji, mahitaji muhimu ya uboresho wa ufundishaji yakiwemo *Curriculum, pedagogy* na mbinu za ufundishaji hayajatiliwa mkazo unaostahili, uboreshaji umeendana zaidi na miradi kama vile wa UNESCO wa Afya ya uzazi, elimu ya UKIMWI, *UN programme, Transition from Humanitarian to Sustainable Development in North Western Tanzania* na mradi wa elimu ya Kifaransa; Mafunzo kwa vitendo hayakupewa kipaumbele stahili, vitabu na vifaa vya kufundishia katika vyuo pia, hamasa kwa wakufunzi bado ni ndogo, udahili wa wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali ya nchi na hasa sehemu zenye uhaba mkubwa wa walimu haukutazamwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mafanikio ya Wizara ni uandikishaji wa watoto wa madarasa ya awali kutoka 873,981 mwaka 2008 hadi 896,146 mwaka 2009. Hili ni ongezeko la 2.5% tu, lakini tuijulize watoto hawa wanasomea wapi na je, walimu wanaowafundisha wamesomea kufundisha watoto hawa au ni wale wale wa msingi wanafundisha tena kwa mshahara ule ule? Ni lazima walimu wapate mafunzo ya kufundisha watoto hawa kwani watoto hao wana mahitaji maalum tofauti na watoto wa shule ya msingi. Vile vile kwa watoto wa shule ya msingi, Wizara inasema wameongezeka kutoka 8,410,094 (2008) hadi 8,441,553 (2009) sawa na ongezeko la 0.4%. Hatujui mwaka huu kama wameongezeka au wamepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunafahamu kuwa ubora wa elimu haupimwi kwa wingi wa shule wala idadi ya wanafunzi, la hasha, ingawa mjadala wa Kitaifa kuhusu uboreshaji wa elimu umejikita na kuelekezwa zaidi katika wingi wa vitendea kazi, hii inashangaza ingawaje sote tunatambua kuwa ubora ni tofauti na uwingi. Kambi ya Upinzani inasikitika sana kuona ubora wa elimu Tanzania umeshuka katika shule zetu za msingi kutetereka. Tafiti nyingi zilizofanywa na taasisi tofauti zinadhahirisha hilo. Hii inatisha na kukatisha tamaa. Kwa sababu kama hatujengi msingi mzuri maana yake tunajenga Taifa la wasomi wasio na uwezo kushindana katika ulimwengu huu wa utandawazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulimwengu wote unatambua ukweli kwamba hakuna nchi yoyote iliyօendelea bila wananchi wake kuelimika au kuwekeza katika elimu. Maendeleo yote hutokana na elimu sahihi iliyojaa maarifa, ubunifu, uwezo mkubwa wa kufikiri na kuvumbua dhana mpya. Elimu inayojenga ujuzi na ufundi wa aina mbalimbali, inayojenga kujiamini, kudadisi na kutumia fursa zilizopo kutafuta masuluhihi ya matatizo. Hii ndiyo nguvu ya elimu inayoleta maendeleo katika jamii. Ni mantiki hili suala la kuwekeza katika elimu bora na sahihi haliepukiki hata kidogo na linapaswa kutiliwa mkazo na kila mtu kwa kuzingatia umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inataka maelezo ya kina, ni sababu zipi zilizopelekea kushuka kwa uandikishaji wa watoto wenye mahitaji maalum kutoka 7,241 mwaka 2008 hadi 5,532 mwaka 2009. Hali hii hairidhishi hata kidogo hasa ikizingatiwa kuwa kila mwaka watoto wenye ulemavu wanaongezeka. Kama idadi yao inapungua maana yake tunawapunguzia uwezo wao wa kujitegemea huko baadaye. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani ingependa kujuu nini sababu ya kushuka kwa usfaulu katika masomo ya Sayansi, Hisabati na *English* katika ngazi ya elimu ya msingi na sekondari, wakati tukijua wazi Sayansi ndio msingi wa maendeleo ya nchi yoyote na hivi sasa tuko katika karne ya Sayansi na Teknolojia, wanafunzi wetu bado hawana maabara wala walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hilo, Kambi ya Upinzani inaitaka Wizara husika kutoa majibu katika masuala yafuatayo:-

Ni kwa nini ubora wa elimu umeshuka hata watoto wamalize msingi bila kujuu kusoma na kuandika? Je, Serikali inafanya nini ili kuweza kukabili tatizo hili ambalo limeikumba sekta ambayo inajenga Taifa la kesho? Tatizo la mdondoko na mimba linadhibitiwa vipi na Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpango wa chakula cha mchana kwa watoto. Chakula ni muhimu kwa afya ya binadamu ye yole. Wote tunafahamu kuwa asilimia kubwa ya watoto wa shule wanatoka katika familia maskini ambao kupata mlo mmoja ni tatizo. Uwepo wa chakula shulenii ungekuwa kivutio kwa watoto kupenda kwenda shule kama ilivyokuwa huko nyuma. Tumeshuhudia watoto wakianguka hovyo, hii yote ni kwa ajili ya njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mpango wa chakula duniani unakadiria kuwa chakula cha mchana kwa wanafunzi wa shule za msingi kitagharimu Sh. 33,000/= kwa mwanafunzi kwa mwaka. Kwa wanafunzi 8,441,553 wa shule za msingi mwaka huu 2009 itakuwa Sh. billion 279 kwa mpango wa chakula cha mchana kwa shule zote nchini. Fedha zinazosemekana kupotea kutokana na ujenzi wa majengo pacha ya *BOT* na ghamama za juu ya uchapaji wa noti za *BOT* ya Sh. 35,000,000,000 zingetosha kabisa kumlisha kila mwanafunzi wa shule ya msingi hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti tofauti zinaonesha kuwa, ukosefu wa chakula mashulenii husababisha wanafunzi wengi hasa katika shule za kawaida kuwa na uelewa mdogo darasani kutokana kutokuwa na lishe bora inayomwezesha kutulia darasani hadi mwisho wa masomo. Njaa imekuwa ni tishio kubwa mashulenii kwani ndio kimeonekana chanzo cha kushusha taaluma. Watoto wengi wamekuwa hawahudhurii madarasani kwa kushindwa kupata mlo utakaomwezesha awepo shule hadi mwisho wa vipindi hivyo kuamua kushinda nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa chakula kwa maendeleo ya afya na taaluma watoto wetu, Kambi ya Upinzani inahitaji ufanuzi unojitosheleza ni kwanini Serikali inafanya matembezi ya kutafuta fedha za chakula badala ya kutenga bajeti ya chakula kama ilivyo bajeti nyingine au kama ilivyokuwa huko nyuma? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu ya juu. Naipongeza Serikali kwa ongezeko la ruzuku kwa Bodi ya Mikopo hadi kufikia Sh. bilioni 243, pamoja na ongezeko hilo bado kuna tatizo kubwa la kutolewa fedha hizi kwa wakati kwa wanafunzi hali inayopelekea wanafunzi kukosa fedha na kusababisha malumbano, migomo na wanafunzi kupoteza muda mrefu wa masomo kwa ufuatiliaji fedha kutoka Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na kutupiana lawama kwa kila upande huku bodi ikidai vyuo vinachelewa kupeleka orodha ya wanafunzi wanaostahili mkopo kwa wakati, huku vyuo vikidai kuwa vimekuwa vikipeleka majina hayo kwa wakati ila bado huchelewesha fedha hizi. Hoja inayoungwa mkono na viongozi wa wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashauri, uongozi wa Bodi ya Mikopo, uongozi wa vyuo vya elimu ya juu na uongozi wa wanafunzi wakae pamoja ili kutambua chanzo cha tatizo na kulipatia ufumbuzi. Inatia aibu sana kuona wanafunzi kila mara wakilumbana na bodi, wakisafiri kufuatilia fedha zao na hivyo kupoteza muda mwingi sana wa masomo yao. Ni lazima tuelewe kuwa wanafunzi hawa wanategemea mikopo kwa asilimia mia moja. Hivyo, kutokuwapatia fedha zao kwa wakati ni kutokuwatenda haki. Kibaya zaidi pale wanapodai fedha hizo Serikali imekuwa ikitumia nguvu kubwa ya dola. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi waliokwenda mafunzo kwa vitendo wa *University of Dodoma* kwa mwaka huu hawajapewa fedha zao mpaka leo. Kambi ya Upinzani inahoji ni lini watapata fedha hizo hasa ikizingatiwa wengi wao wanafanya mafunzo haya mbali na wanakoishi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, posho ya chakula na malazi ya Sh. 5000/= kwa siku ni ndogo sana ukilinganisha na hali halisi ya gharama za maisha kupanda na thamani ya shilingi kushuka. Uhaba wa vyumba vya kulala kutokana na ongezeko la wanafunzi kwa mfano *UDSM* asilimia 60 ya wanafunzi wanaishi nje ya chuo (*off campus*). Hali hii imefanya wanafunzi wengi kuishi kinyume cha sheria kubebana au mzungu wa nne kitendo ambacho si tu kinahatarisha afya zao bali pia kuharibu sana vifaa kama vitanda, vyoo, milango na miundombinu kwa ujumla. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho ya kazi -*field work/special faculty allowance* kumekuwa na kiasi tofauti cha posho ya mafunzo (*field work allowance*), kutokana na *Grade* zilizopangwa na Bodi ya Mikopo A-H. Kambi ya Upinzani inapendekeza posho ya mafunzo ingekuwa sawa kwa wote bila kujali makundi yao kwani wanapangwa sehemu mbalimbali. Hii pia inakwenda sambamba na mahitaji muhimu ya vitivo ambayo nayo yanatolewa kiasilimia, kwa kuwa vifaa ni ghali sana mfano, wanafunzi wa *Computer* wanahitaji kununua *laptops*, sasa kiwango cha juu kabisa ni Sh. 80,000/= na *laptop* hata iliyokwishatumika ni Sh. 500,000=/. Je, mwanafunzi huyu atawezu kununua kifaa hiki muhimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wanafunzi wenyе ulemavu. Pamoja na utandawazi na Tanzania kuridhia Mikataba ya Kimataifa kuhusu haki za watu wenyе ulemavu, bado wanafunzi wenyе ulemavu katika vyuo vya elimu ya juu wanaishi kwa tabu, vifaa vyao havifikasi kwa wakati, mfano; *Brailles* kwa ajili ya wasioona zinafika miezi mitano hadi sita baada ya mwaka wa masomo kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ualimu ni taaluma pekee katika jamii inayogusa na kuzaa taaluma nyingine zote. Upekee huu unatokana na kutoa maarifa na kushughulikia binadamu, ana saikolojia ya kuwalea na kuwakuza binadamu wenzie wenyе tabia na sifa tofauti ili wawe watu muhimu katika jamii. Tofauti na Mhandisi anayeshughulika na mitambo au majengo yasiyosema wala kubadili tabia na hisia. Upekee wa mwalimu unakuja katika kazi kubwa ya kutafsiri falsafa na sera ya nchi ili kuzifikisha kwa wanafunzi na jamii. Mwalimu anajishughulisha na mambo makubwa matatu kwa binadamu nayo ni akili, hisia na maadili au mwenendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina upungufu wa walimu 115,000 kati ya hao, walimu wa sekondari wanaohitajika ni 58,000 lakini bajeti imekuwa ni ndogo. Hii ina maana kuwa walimu wa sekondari ni wachache kuliko mahitaji. Upungufu wa walimu nchini ni sawa na 40% ya mahitaji ya walimu nchini. Bila kuwa na mpango mkakati wa kuwalipa walimu mishahara mizuri hakutakuwa na walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa vyuo vinatoa walimu zaidi ya 15,000 kwa mwaka wanaopangwa shulen, lakini walimu hao wako kwenye makaratasu ya Wizara, wengi hawaendi kufundisha katika shule za Serikali na wengine wanafanya kazi kwenye taasisi nyingine kama mabenki na kadhalika. Wengi wa wanaomaliza kozi ya ualimu siyo kigezo cha kuwa kuna walimu. Mishahara ya walimu haikidhi mahitaji halisi, hivyo, Serikali iongeze mishahara. Tanzania inatenga 1.1 % *GDP* kwenye elimu wakati

Kenya wamefikisha 6%, Uganda zaidi ya 4%, Burundi 4.8% na Rwanda 4.5%. Hivyo, hatuwezi kufanikisha masuala ya elimu kwa kutenga fedha kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya elimu ina upungufu kwenye idara ya Mafunzo ya Ualimu. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya idara hiyo ambayo inahusiana na mafunzo ya walimu ili kuboresha elimu ina mapungufu zaidi ya sh.10 bilioni. Chunguza bajeti ya kwenda moja kwa moja kwenye mafunzo ya ualimu. Walimu wengi wamepandishwa madaraja, tunashukuru lakini hawajarekebishiwa mishahara wala kulipwa mapunjo yao wakati fedha zilitengwa kwenye bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Walimu Tanzania kwa kushirikiana na wadau wengine kiliwasilisha Serikalini Muswada wa Kuundwa kwa *Teachers Professional Council*, yaani Chombo cha kusimamia taaluma ya ualimu kama ilivyo kwa Madaktari lakini mwaka umepita Serikali hajatoa maelezo kama Mswada huo umewasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri na lini utawasilishwa Bungeni. Muswada huo ni muhimu hasa wakati huu ambapo kuna uhuru wa kufanya kazi sehemu yoyote kwa wanachama wa Jumuiya ya Afrika mashariki. Posho ya Mazingira magumu hajatolewa na Serikali ili kuwavutia walimu kufanya kazi kwenye maeneo magumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umuhimu wa mafunzo bora ya ualimu. Ni ukweli ulio dhahiri kwamba maendeleo ya jamii yoyote yanahitaji elimu ili wananchi wake waweze kushiriki kikamilifu kutatua matatizo na kupambana na changamoto zinazoikabili jamii. Matarajio ya elimu bora ndani ya jamii yanatokana na mafunzo bora ya walimu ambaa ndio watendaji wakuu katika mchakato wa kujifunza na kufundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo bora ya ualimu ni yale yenyе sifa zina zokubalika kiutaalam, kitaaluma na kijamii. Ni lazima yamjenge mwalimu kufanya anachotarajiwa na wanafunzi na jamii inayomzunguka. Yamjengee mwalimu nidhamu ya kudumu. Katika ulimwengu huu hakuna kitu kinachokwenda kufanikiwa bila kutanguliza nidhamu. Mafunzo ya ualimu yanapaswa kumjengea mwalimu nidhamu ya kiakili, nidhamu ya kiutaalam, nidhamu ya kiujuzi, nidhamu ya kitabia, nidhamu ya weledi na nidhamu ya kijamii na kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa mwalimu ni muhimu sana katika kufanikisha tendo la kujifunza kwa wanafunzi. Uwezo huo unatokana na mafunzo sahihi na ya kutosha ya ualimu. Mwalimu ndiye mtendaji muhimu katika elimu na mafunzo. Mwalimu huwaandaa na kuwaelekeza wanafunzi katika kujifunza na kuhusiana na yaliyomo kwenye mtaala na kukuza, wakati wote fikra za wanafunzi na kuwa tayari kujifunza mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hatari za kukosa mafunzo bora ya ualimu. Kwa watu makini hatari ya kukosa mafunzo bora kwa walimu wetu iko wazi ndani ya jamii. Maeneo yafuatayo yanaweza kuwa ni mionganoni mwa hatari hizo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuuawa kwa vipaji vyatoto na kuvuruga akili zao. Mwalimu asiye na mafunzo ya ualimu kwa kawaada anakwenda darasani kuua vipaji vyatoto na kuvuruga akili zao. Falsafa za makuzi na maendeleo ya watoto zinabainisha kwamba kila mtoto amezaliwa na uwezo wa kufikiri, maarifa na vipaji vyatoto aina mbalimbali. Vipaji hivyo vinapaswa kuendelezwa, kukuzwa na kupaliliwa ili vichanue vizuri na vizae matunda bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kukuza matabaka katika jamii. Mwendelezo wa harakati za kusaka elimu bora nchini sasa zimewatenga watoto wanaotoka familia maskini hasa kutokana na kuwepo kwa walimu duni shulen. Shule za vijijini na hasa za Serikali ndizo zinazoongoza kwa kuwa na walimu duni wasio na mafunzo bora ya ualimu. Kukosa walimu weledi hatimaye huligeuza Taifa kuwa soko la bidhaa za wabunifu na wenye maarifa. Huwafanya watu wa Taifa lile kuwa vibarua wa watu wenye pesa.

Aidha, huwafanya kuwa watumwa wa utamaduni wa Mataifa yanayoelimisha watu wake kupitia uandaaji bora wa walimu wao kufifisha maendeleo ya jamii nzima. Panapokuwepo na walimu duni wanaozaa jamii duni hakuna kasi ya maendeleo katika jamii ile. Hii ni kwa sababu hakutakuwa na wataalam katika sekta nyingine zote, kwani watu wengi hawana maarifa na kwa sababu hiyo, watu wengi hawawezi kushiriki kuleta maendeleo kwa sababu hawana maarifa. Matarajio ya jamii yote ya Watanzania wanaoandikisha watoto wao shule ni kuona watoto wao wanapata maarifa, uwezo wa kufikiri, ubunifu, stadi na ujuzi muhimu, uwezo wa kuwasiliana na uwezo wa kuwasiliana na uwezo wa kutatua matatizo ili wachangie juhud za wazazi wao kutatua changamoto za jamii na hatimaye kujilettea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wenye mafunzo sahihi na ya kutosha ndio pekee tegemeo la kuifikia ndoto hii. Tuliokoe Taifa kwa kuokoa vipaji vyatoto ya maelfu ya Watanzania wanaofundishwa na walimu bandia, kwa kuboresha mafunzo ya ualimu. Tukiweka nia thabiti, tunaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wadau wa elimu Tanzania wamekuwa wakiishauri Serikali uwepo wa bodi ya waalimu itakayoangalia pamoja na mambo mengine kudhibiti nidhamu, ubora wa walimu, maadili na taaluma yao na kadhalika. Ni lini Serikali itakubali ombi hili ili walimu wawe na bodi yao? Kambi ya Upinzani inaungana na walimu wote Tanzania na inapenda kuwatanabaisha kuwa iko nao siku zote. Kwa kutumia nafasi yake itaendelea kuikumbusha Serikali juu ya matatizo yanayowakuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi. Enzi za Mwalimu tulishuhudia Tanzania ikiwa mionganoni mwa nchi zilizokuwa mstari wa mbele kuhakikisha wananchi wake wanajua kusoma na kuandika. Tulikuwa na madarasa ya elimu ya watu wazima. Jambo la kusikitisha pamoja na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, Tanzania imerudi nyuma kwa kiasi cha kutisha na takwimu zilizotolewa hivi majuzi na Waziri mwenye dhamana ya elimu inakatisha tamaa na kujuliza nchi inaelekeea wapi! Kwamba idadi ya wasiojua kusoma na kuandika na kuhesabu imefikia 31% na ameendelea kusema kwamba mikoa inayoongoza ni Dar es Salaam, Kigoma na Mtwara. Sababu zilizotolewa ni mimba za utotonu, umaskini, utoro na jamii kutokupenda kusoma

(Salum Mnjagila- Mkurugenzi wa Elimu ya watu Wazima). Tafiti nyingine zinaonesha kuwa maeneo mengine zaidi ya 60% hawajui kusoma wala kuandika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwaeleza wananchi yafuatayo:-

Kama sababu wanazijua wamechukua hatua gani kurekebisha? Wanaona fahari gani kuwa na theluthi moja ya wajinga? Serikali ina mkakati gani kubadili hali hii hasa tunapoingia katika Soko la Afrika Mashariki tuwe sambamba na wao? Hii ni aibu kubwa kwa Taifa na Serikali na hata Serikali haina mikakati yoyote ya kuonyesha bajeti ya idara kwa sababu ukiangalia bajeti ya Wizara hii utaona kwamba bajeti yake ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizi wa mitihani, Wimbi la kughushi vyeti na udanganyifu kwenye mitihani limezidi kuwa mwiba mkali kwa Serikali. Ingawa ahadi nyingi na mikakati ya kupambana na kudhibiti wizi huu bado tatizo linaendelea tena kwa kasi zaidi. Kila sehemu ya nchi hii jambo linalosikika ni vyeti bandia, kughushi nyaraka udanganyifu kwenye mitihani kuanzia ngazi ya msingi hadi vyuo vikuu. Mbaya zaidi wahusika ni watu wa tabaka zote kuanzia walinzi, maafisa na kadhalika. Kama litaachwa na kutamalaki nchi hii itakuwa ya wasomo bandia hii ni hatari kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inampongeza sana Bwana Msemakweli kwa kuchapisha kijitabu cha mafisadi wa elimu. Tunahitaji watu kama hawa ili wazidi kufichua mafisadi wa elimu na wa aina zote ili wananchi waache tabia za aina hiyo. Tunaitaka Serikali inapopata taarifa kama hizo isifumbe macho bali ishirikiane na watoa taarifa na kuzifanya kazi ili haki itendeke. Ni jambo la kusikitisha kuona mtu amesotea Shahada ya Uzamivu (*PhD*) kwa miaka 4-7 na kuacha familia yake, wengine hata ndoa kuvunjika halafu mwingine anaipata *online* kwa siku tatu au miezi miwili! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya sababu za wizi huu ni Viongozi wengi wanaghushi vyeti, wanatumia majina yasiyo yao au walidanganya wakati wa mitihani. Kiongozi wa aina hii kamwe hawezi kukosoa tabia ya kughushi vyeti. Kama kughushi ni kosa la jinai kwa nini viongozi wanaopatikana na kosa hili hata wale wa kisiasa kama Wabunge wasishtakiwe kwa kosa la jinai? Kughushi vyeti ni sawa na ubakaji wa ajira, ifike mahali sasa kuwe na Mswada wa kisheria dhidi ya wizi wa mitihani na kughushi vyeti. Mtazamo hasi wa viongozi na wananchi wengi ulioifanya elimu kuwa ni cheti na kufaulu mitihani na si uelewa na maarifa. Ni watu wachache sana wanatambua kuwa elimu ni maarifa na uwezo ambao mtu anaupata baada ya kuingiza maarifa kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini baadhi ya viongozi hawana dhamira ya dhati ya kumaliza tatizo hili kwani tatizo hili limeanza zamani na vyombo husika vinawajua wahusika na mbini zitumikazo. Bila utashi wa viongozi na dhamira ya Uzalendo, Taifa hili litaangamia kwa kuwa na wasomi bandia, wasiojua lolote watakaoliangamiza Taifa letu kwa kuuza rasilimali za nchi yetu kwa mikataba mibovu. Kambi ya Upinzani

inataka kujua ni mikakati gani Wizara imepanga ya kumaliza kabisa tatizo hili ikiwa ni pamoja na kuwafikisha Mahakamani wale wote waliogushi yeti hata kama ni wanasiwa kama vile Wabunge na Mawaziri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kwa mtandao wa komputa, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundis, alitangaza kuwa kila mwalimu wa shule ya sekondari ya Serikali atapewa kompyuta kwa ajili ya kufundishia wanafunzi kwa kutumia teknolojia ya habari kama njia ya kukabiliana na uhaba mkubwa wa walimu unaokabili sekta ya elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huo ungeanza kwa majaribio mwezi Oktoba mwaka jana katika baadhi ya maeneo na kuenea nchi nzima baadaye mwakani. Hii ni habari njema sana kama kweli uwezo huo tunao na shule zetu zote zitakuwa na mtandao huo. Lakini ni wazi kuwa Ubora wa elimu kuanzia shule ya msingi hadi Chuo Kikuu umeshuka sana Tanzania. Kushuka huku kwa ubora wa elimu unatokana na kuwa na mitaala isiyoendana na wakati, walimu wasio na sifa za kufundisha, ukosefu wa vifaa vya kufundishia, miundombinu mibovu ya madarasa na kushuka kwa ari Mfumo wetu wa elimu. Hivi ni mwaka umekwisha lakini hatujaona ni maeneo gani tunamtaka Waziri anapohitimisha atuelezee ni maeneo gani ambayo mtandao huu umeanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa kutumia kompyuta kufundishia sio kipaumbele *priority* kwa sasa. Ingefaa tuanze kuboresha elimu katika shule za msingi kwa mfano bado tuna shule zisizo na madawati, watoto wanakaa chini, bado tuna majengo ya udongo, bado hatuna walimu. Vile vile hao walimu watakaopewa hizo kompyuta wamepewa *maandalizi* gani ya *kuzitumia?* Je, tumeandaa mitaala ya kutumika kwenye mfumo wa mawasiliano ya kompyuta? Kambi ina wasiwasni mradi huu mkubwa wa manunuza na tunahoji kwa takriban mwaka mmoja sasa ni wapi mradi huu umetkelezwu? Walimu hawa walipata wapi mafunzo ya utumiaji wa kompyuta? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Wafanyakazi wa Elimu ya Juu (*THTU*), Mishahara ya wafanyakazi waendeshaji, utekelezaji wa maboresho ya mishahara ya wafanyakazi waendeshaji bado haujafanyika kama Serikali ilivyoahidi kupitia mapendekezo ya Kamati ya Rais ya mwaka 2005. Licha ya viongozi wa wafanyakazi wa taasisi za elimu ya juu kulifatilia suala hili kwa makini na licha ya Serikali kutoa maelekezo na ahadi mbalimbali utekelezaji wake haujafanyika kama ilivyopasa tangu mwaka 2006. Ucheleweshwaji huu umejenga taswira mbaya mionganini mwa wafanyakazi wa taasisi husika na unaweza kuathiri imani ya wananchi katika Serikali yao. Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake atueleze sababu za utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Rais ya 2005 kuchukua muda mrefu jinsi hii na hali ikoje sasa. Ni lini basi watatendewa haki kama walivyowafanyika wanataluma, maboresho ya Mafao ya Uzeeni (Mifuko ya Hifadhi Jamii).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafao ya ustaafu yatolewayo kwa wafanyakazi wa taasisi za elimu ya juu ni duni mno. Tunayo taarifa kuwa hoja ya kuboresha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imefikishwa mikononi mwa Serikali na kwamba Serikali imebaini ukweli wa hoja hii na kuahidi kuifanyia kazi. Hata hivyo, kasi ya utekelezaji wa

mchakato wa mabadiliko yake hauridhishi, hasa ukizingatia kuwa kundi kubwa sana la wafanyakazi wa taasisi za elimu ya juu wapo njiani kustaafu katika kipindi kifupi kijacho. Tunaiomba Serikali iongeze kasi ya kufanya marekebisho ya mafao ya Mifuko ya *PPF* na *NSSF* ili tofauti kubwa iliyopo kati ya mafao ya wafanyakazi wa shule za elimu ya sekondari na msingi na zile za taasisi za elimu ya juu ipatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa linalowakumba watumishi wa Vyuo Vikuu vya Umma ni mafao duni wanapostaaafu na ambalo linawagusa watumishi walio wanachama wa *PPF na SSSS*. Idadi kubwa ya watumishi wa Vyuo Vikuu vya Umma wapo kwenye mfuko wa *PPF* ambao unatoa mafao duni sana. Sababu kubwa ya *PPF* kutoa mafao madogo ni matumizi ya kanuni duni ya kukokotoa mafao ikilinganishwa na za mifuko mingine kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali linaloonyesha vikokotoo (*pension factor*) lifuatalo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikokotoo cha 1/960 ambacho *PPF* bado wanakitumia kilifutwa na Sheria ya Bunge ya mwaka 1989 (*Pensions Laws (Miscellaneous Amendment Act) No. 4, Part V section 14 a*). Pamoja na Sheria kuwataka *PPF* wafuatilie michango ya wanachama kwa waajiri, *PPF* walikuwa hawafanyi hivyo na kusababisha kipindi fulani cha mtumishi (haswa miaka ya 70 na 80) kutokuwa na mawasilisho ya mchangano. Kipindi ambacho hakukuwa na mawasilisho ya mchangano *PPF* huwa hakijumlishwi kwenye ukokotoaji wa mafao na hivyo kumwadhibu mstaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu mojawapo iliyokuwa ikielezwa ni mfuko kutokuwa na uwezo wa kulipa mafao bora zaidi, lakini wakati huo huo viongozi wa *PPF* wakijitengenezea mafao (*Group Endowment Fund*) manono kwa kutumia fedha za mfuko ambazo ni fedha za wanachama. Kwa mfano, Wakurugenzi sita wa *PPF* waliomaliza mikataba yao mwaka 2008 walilipwa Sh. bilioni 1.2 (wastani wa shs. milioni 200 kila mmoja; rejea gazeti la Raia Mwema la 7/5/08 na 14/5/2008). Hawa viongozi waliendelea na ajira ya mkataba hapo hapo *PPF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili la mafao duni lilianza kujadiliwa tangu mwaka 1999 na kumbukumbu za kikao rasmi cha Serikali kulizungumzia hili na kuazimia kulitatua ilikuwa Oktoba 19, 2004. Kikao hicho kiliitishwa na aliyejewa Katibu Mkuu, Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu na kilishirikisha wawakilishi kutoka Hazina, Utumishi, *PPF* na Vyuo Vikuu. Hata hivyo hadi leo tatizo hili halijapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukue mfano wa Madaktari wawili walioajiriwa tarehe 1/1/1981; mmoja akiwa Serikalini na mwingine akiwa Chuo Kikuu cha Afya Muhimbili na wote wakifanya kazi Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili hadi walipostaafu Desemba 2009 (miezi 348). Mshahara wa mwaka 2009 wa Daktari wa Chuo ulikuwa kwa mfano, Sh. 19,200,000/= kabla ya kodi, lakini yule wa Serikalini ukiwa Sh.15,000,000/= kabla ya kodi. Wastani wa mshahara wa mwaka kwa miezi 60 ya mwisho ya Daktari wa Chuo, kwa mfano, ni Sh. 16,920,000/= kabla ya kodi.

Kwa kutumia kanuni za ukokotoaji mafao ya *PSPF*, Daktari Serikalini angepata Sh. 74,916,666/= kama pensheni ya mkupuo na yule wa Chuo (*PPF*) angepata Sh. 27,693,281/= kwa kanuni wanazotumia *PPF* yaani 1/960 hadi June 1988 na 1/600 kutoka Julai 1988 ambacho ni kama asilimia 37 ya yule wa Serikalini. Huyu Daktari wa Chuo, pamoa na kutibu wagonjwa alikuwa akifundisha Madaktari wa baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kikitumika kikotoo cha 1/600 kwa kipindi chote huyu mstaafu wa *PPF* angepata Tshs 30,667,500/=. Ni dhahiri kwamba, kwa kutumia vikokotoo viwili, huyu mstaafu wa *PPF* amepunjika takriban Sh. 3,000,000/=. Vivyo hivyo hata mafao yake ya kila mwezi atapunjika. Mbaya zaidi ni kuwa kama kitakuwepo kipindi cha Utumishi ambacho *PPF* itakiondoa kwa kutokuwepo mawasilisho ya michango, hayo malipo yatakuwa madogo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu tulizonazo zinaonyesha Maprofesa waliostaafu kati ya mwaka 2005 na 2008 ambao ni wanachama wa *PPF* wamelipwa kati ya Sh. milioni 15 na 25 kama pensheni (mkupuo) baada ya kufundisha kwa wastani wa miaka 30. Mbaya zaidi wale wa SSSS huwa wanalipwa mafao ya mkupuo tu tena kiasi kidogo (takwimu za 2005-2008 ni kati ya milioni 10 na 42) na hawalipwi pensheni ya kila mwezi ya izeeni ambalo ni kinyume na Mapatano ya Shirika la Kazi la Kimataifa (*ILO C102 Social Security Convention, 1952*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafao ya mkupuo ya mtumishi mwenye cheti Serikalini (*PSPF*) au Serikali za Mitaa (*LAPF*) ni zaidi ya anayolipwa Mhadhiri mwenye cheo cha Profesa mwenye Shahada ya Uzamivu (*PhD*). Mtumishi Serikalini au Serikali za Mitaa mwenye stashahada (*diploma*) anapostaafu mafao yake ya mkupuo ni zaidi ya

mara mbili ya anayolipwa Profesa. Tunaomba umma uelewe kwamba hatusemi kwamba haya mafao Serikalini au Serikali za Mitaa ni makubwa, la hasha. Kimataifa, pensheni ya mtumishi yejote inaendana na mshahara wake, ambao kwa kiwango kikubwa unaendana na elimu na/au majukumu aliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali kubwa ni je, ni haki kumlipa Profesa pensheni ndogo kuliko mwenye ngazi ya cheti na hawa wote wakiwa ni watumishi wa Umma? Je, mtumishi huyu atakapofikia umri wa miaka 50 na kuendelea atakuwa na motisha wa kufanya kazi? Je, waajiriwa wapya wanapoona hali halisi ya Wahadhiri wao wanapostaafu watakuwa na morali ya kufanya kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis Stadi iliunda Kikosi Kazi mwaka 2008 ili kulitazama kwa undani tatizo hilo na kutoa mapendekezo namna ya kuboresha mafao ya watumishi wa Vyuo Vikuu vya Umma. Ripoti kamili ilitolewa Februari 2009 lakini hatima ya pendekezo lililotolewa na Kamati haijulikani, lakini inaashiria likataliwa na bila wadau kujulishwa ni kwa nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pamoja na Wanataaluma kuwasilisha maamuzi ya Vikao Serikalini kuanzia mwezi Aprili 2009, waliwasilisha madai yao Serikalini katika kikao maalum cha Kamati iliyoundwa kushughulikia tatizo hili tarehe 11 Januari 2010. Haya madai yalikuwa kama ifuatavyo:-

Watumishi wa Vyuo Vikuu vya Umma waliostaafu ambao walikuwa wanachama wa Mfuko wa SSSS walipwe pensheni za kila mwezi za uzeeni. Watumishi wa Vyuo Vikuu vya Umma walio kwenye Mfuko wa SSSS wakistaafu walipwe pensheni za kuridhisha za mkipuo na za kila mwezi. PPF waache mara moja kutumia kikokotoo cha 1/960 kwa sababu kilishafutwa kwa mujibu wa Sheria ya 1989. PPF waache vilevile kuondoa kipindi cha utumishi kwa kisingizio kwamba hakukuwa na uwasilishwaji wa makato ya pensheni kwa kipindi husika kwa sababu sheria iliwataka wao kufuutilia kwa mwajiri, hivyo kuwepo kwa kipindi kama hicho si kosa la mtumishi na hivyo hastahili kuadhibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wastaafu wa PPF warejeshewe mapunjo ya mafao yao iliyosababishwa na (3). Watumishi wa Vyuo Vikuu ya Umma ambao ni wanachama wa Mfuko wa PPF wakistaafu walipwe pensheni za kuridhisha; PPF walipe nusu ya mafao, watumie umri wa kuishi baada ya kustaafu wa miaka 15.5 ambao unatambulika Kiserikali na watumie mshahara wa mwaka wa mwisho badala ya wastani wa mishahara ya miaka mitano ya mwisho. Pensheni za kila mwezi zioanishwe na thamani halisi ya fedha kwa kipindi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wa wanataaluma waliamua kusitisha ufundishaji kwa siku chache mwezi wa nne mwishoni kuinga kutopatikana kwa suluhihi la mafao duni ya kustaafu. Lakini kwa kuzingatia ushauri wa Wenyevit wa Mabaraza ya Vyuo

Vikuu vya Umma, wanataaluma waliafiki kuendelea kufundisha. Ahadi tuliyopewa ni kwamba suluhisho lingepatikana ndani ya kipindi cha miezi miwili au mitatu kuanzia mwezi Aprili 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaisihi Serikali ilitatue tatizo hili kwa Taifa lilitumia gharama kubwa kuwaelimisha, nao wawaelimishe wenzao, pia tunawasihi wasiondoke nchini kwani mkimbia nchi si Mzalendo. Aidha, mkiikimbilia wote kwenye siasa kwa sababu yoyote ile nani atawafundisha wanasiasa watarajiwa? Msivunjike moyo kwa sababu tunaamini kwamba haki haipatikani bila kupiganiwa. Mheshimiwa Rais Dr. Jakaya Mrisho Kikwete vilevile alisema “vita vya umma ni vita vya haki na ushindi utapatikana”. Sisi tunaamini Wahadhiri wa Vyuo Vikuu vya Umma kama kundi, hamtendewi haki mnapostaafu na sisi tutaendelea kuwapigania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la ukosefu wa nyumba za walimu, iwe marufuku kufunga shule mpya ambayo haina nyumba za walimu, nyumba zenyé hadhi tena kwa idadi inayoendana na ikama itakiwayo. Aidha, iwe haki ya mwalimu kupewa nyumba ya kuishi na mwajiri (*entitled*) na mwalimu asipelekwe katika shule fulani bila mwajiri kumhakikishia nyumba ya kuishi na familia yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kumwendeleza mwalimu kitaaluma, uwe wajibu wa mwajiri (Serikali au binafsi) ndani ya mkataba wa kazi kumwendeleza mwalimu kila baada ya muda uliotajwa wazi, kuititia njia ya mafunzo kazini na nyinginezo. Ni aibu kwa Serikali kushindwa kufikia lengo walilojipangia wao wenyele la kujenga nyumba 29,639 na kujenga 300 tuu katika bajeti ya maendeleo ya mwaka 2008 huku bajeti ya mwaka huu ikiwa haioneshi fedha za ujenzi huo. Kambi ya Upinzani inahoji nyumba hizi zitajengwa lini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati umekwisha wa kuendelea kuwa mashuhuda wa kudidimia kwa sekta ya elimu nchini bila kufanya jitihada za makusudi tena madhubuti sote kwa pamoja kuliokoa Taifa letu Tanzania. Hatuna budi kutafuta haraka ufumbuzi wa matatizo yote ya elimu kama tunalitakia Taifa letu mema. Tujadiliane kwa nia njema, tuitathmini sera yetu ya elimu kwa kina. Tuangalie wapi tunakosea, wapi tunafanikiwa, nini kinatukwamisha na nini tufanye. Hatimaye tuibuke na dira moja madhubuti itakayotuhakikishia kufika salama kwenye bandari ya maendeleo tunayoyatamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudu mbalimbali zilizosomwa na Waziri za kuboresha mazingira ya elimu hapa nchini kama vile mradi wa komputa yaani e-learning, fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maabara, Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa kama walimu hawatapatiwa mazingira mazuri ya kufanya kazi zao ikiwa ni pamoja na malimbikizo ya madai yao, ujenzi wa nyumba, haya yote ni bure kwani walimu ndio kiungo pekee cha kuendeleza elimu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa hatuna upungufu wa walimu bali walimu wamebadili taaluma zao kutokana na maslahi duni na tasnia hiyo kutothaminiwa kama zamani. Kama mnabisha nendeni katika benki zetu lakini tusiende mbali tujiangalie humu Bungeni. Maslahi yao yasipoboresha tutasomesha walimu maelfu kwa malaki lakini chungu hiki kamwe hakitajaa na asilimia ya wajinga Tanzania itakuwa 50% miaka michache ijayo kama leo tuko 31%. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, na Wenyeviti wenzio, nawaombe afya njema nikiamini mtarudi na kushika nyadhifa zenu ili muendelee kulii marisha Bunge hili lizidi kuwa na viwango kasi na kubadilika zaidi ndani na nje ya nchi. Hayo mavuvuzela yanayonyemelea Majimbo yenu yashindwe na yasambaratike kwani yakilegea yanaweza kuzinduka na kuja kwa kasi kubwa. Kwa Wabunge wenzangu nawapenda wote mbarikiwe sana katika kipindi hiki kigumu kinachotukabili, *Inshallah* tutakutana hapa mwishoni mwa mwaka huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza kwa makini na naomba kuwasilisha. Mungu ibariki Tanzania, Mungu Bariki Uchaguzi Mkuu. Ahsanteni sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo, ahsante sana kwa hotuba yako nzuri na maombiyako kwamba, mavuvuzela wetu wasambaratike, nakushukuru sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, lakini kabla sijawaita wachangiaji, Susan amenichokoza kidogo kwenye Chuo changu cha *UDOM*, amekilinganisha na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakati udahili wa mwaka jana *UDOM* imechukua wanafunzi 8000, Dar es Salaam wanafunzi 6000, *UDOM* ni zaidi.

Waheshimiwa Wabunge katika wachangiaji tunao ambao hawajachangia kabisa tangu Bunge hili lienze na tutaanza na hao wawili. Nilikuwa namtafuta Mheshimiwa Masunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Nimrodi Mkono na wachangiaji ni dakika kumi kumi.

**MHE. JOYCE M. MASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza. Lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuteuliwa kuwa mgombea kwa kura nyingi na kwa kishindo. Lakini vilevile nimshukuru sana Dr. Shein kwa kuteuliwa kuwa Mgombea wa Urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii tena kumpongeza Dr. Bilali kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza. Kwa niaba ya Wanawake wa Mkoa wa Shinyanga tunamhakikishia Mheshimiwa Rais wetu, Dr. Jakaya Mrisho Kikwete na Ndugu yetu Dr.

Bilali Mgombea mwenza kwamba, wanawake wa Shinyanga tutawapa kura nyingi zitakuwa za kutosha na mpaka zitamwagika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii vile vile kumpongeza Mheshimiwa Waziri na wote waliomsaidia kwa hotuba yao nzuri. Nawapongeza sana, tumeielewa na Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwapongeza Walimu wote wa Tanzania kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na matatizo madogo madogo yaliyopo, lakini tunasema Bunge lipo, tutaendelea kuwasaidia na mambo yao yatakuwa poa baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme nafikiri Mheshimiwa Martha Mlata kwa niaba ya Mwenyekiti amezungumzia sana kuhusu walimu. Walimu wapo wa kutosha lakini kwa kweli mazingira wanayopokelewa ndiyo siyo mazuri. Nichukue nafasi hii kuwaomba Wenyeviti wetu wa Vijiji na wa Mitaa kwa kazi yao nzuri wanayoifanya muda wote pamoja na kazi nyingi wanazozifanya, lakini wawapokee walimu hawa, wawatengenezee mazingira mazuri wanapotakiwa kufanyakazi ili walimu wakae, wafanye kazi vizuri na wasilalamike na kurudi kama alivyosema Mheshimiwa Susan Lyimo, kutafuta kazi zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana wananchi wa Shinyanga kwanza kwa kujenga shule na Serikali kutusaidia, sasa tuna shule nyingi lakini shida yetu sisi ni walimu wanapoondoka na kuacha kufundisha na hivyo wanafunzi wanabaki peke yao. Lakini kubwa sana Shinyanga tunaomba nyumba za walimu ili walimu wakae katika nyumba zao kuliko wanavyoendelea kupanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niingie katika hoja ambazo nitakupa, hizi karatasi umpe Mheshimiwa Waziri ili aendelee kutusaidia kwa maana ya Manispaa ya Shinyanga. Manispaa ya Shinyanga wana kero na namwomba Mheshimiwa Waziri anisikilize ili aendelee kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tuna kero ya uhamisho holela, Afisa Elimu anawahamisha walimu kwa jinsi anavyotaka yeye na walimu wanashindwa kufanya kazi vizuri na kupelekea wanafunzi wetu kufeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la likizo. Likizo hizi hakuna *roster* inayotumika, kiwango cha malipo hakieleweki, malipo kutokuwa kamili kwa maana ya kwamba, walimu hawalipwi malipo kamili. Nataka niseme haraka kwa sababu dakika kumi (10) ni chache, lakini kwa vile nitakupa hizi karatasi utaziangalia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Elimu Maalum kule kwetu Shinyanga Manispaa, tuna shule yetu ya Buhangija lakini cha kusikitisha ni kwamba, shule ile hawafundishwi na walimu wenyewe waliofundishwa taaluma hii, Waziri lazima aelewé. Wanafunzi wale wasioona wanafundishwa na walimu wanaona ambao hawakwenda shule zile. Walimu wale waliokuwepo pale, Afisa Elimu huyu amewahamisha, amewapeleka shule zingine, kwa hiyo tunasikitika na tunamwomba Mheshimiwa Waziri alichukulie hili tatizo kwamba, huyu Afisa Elimu hatusaidii ila anatuharibia Manispaa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ninukuu kitu kidogo tu. Kuna fedha ambazo zimerudishwa na hii karatasi nitakupa, kuna Walimu waliohakikiwa madai yao katika uhakiki wa ana kwa ana, malipo yao yakaja lakini hawajalipwa mpaka fedha ikarudishwa Hazina. Kuna Walimu 114 waliostahili malipo ya jumla ya shilingi milioni 38,869,905,000/. Walimu wanasema wanasikitika sana, hii karatasi nitakuletea ili uumpe Mheshimiwa Waziri ili ajue anatusaidiaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la kutolipwa stahili za uhamisho kwa Walimu wa Manispaa na kuna *documents* hizo zitakuja kuonyesha jinsi gani Walimu wanavyojibishana na Afisa Elimu huyo kuomba mafao yao na kutokopewa kabisa. Naomba nitaje Walimu wafuatao, nimeletewa karatasi hizi, kuna Walimu kama 24. Kuna Mwalimu mmoja anaitwa Mwalimu Martha Kilowoka, amehamishwa kutoka Shule ya Msingi Ng'wihando kwenda Mwamapalala terehe 5 Januari, 2010 na mpaka hivi leo bado hajapelekwa ile shule na huyu Mwalimu ana mumewe. Kwa hiyo, Afisa Elimu anaendelea kuwatenganisha mtu na mumewe. Kuna Mwalimu mmoja anaitwa Hosia Elieza, huyu amehamishwa kwenda Shule ya Msingi Mwamapalala kutoka Bugoyi, shule hizi ziko mbali sana lakini anavyodai madai yake hapewi toka tarehe 24 Novemba, 2008, huyu hafanyi kazi yupo tu. Kwa hiyo, kuna Walimu wanahamishwa na wanashindwa kwenda walikopangiwa, wanaomba magari hawapewi, kwa hiyo, kwa kweli sisi tunasikitika na Mheshimiwa Waziri lazima aelewé hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna Walimu ambao wanatoka Shule ya Msingi, wameamua kujiendeleza kwenda sasa Shule za Sekondari nao vilevile hawalipwi chochote. Kwa hiyo, kwa kifupi Walimu wa Manispaa wanasikitika na wananiambia kwamba kama huendi kumwambia Waziri tutakachokifanya sisi huyu Afisa Elimu tutampiga. Mimi nimewaambia watulie kwa sababu niliwaambia Wizara hii ipo leo tarehe 12, Julai, 2010 na sasa hivi wako redioni wanasikiliza Waziri wa Elimu anasema nini kuhusu huyu Afisa Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme, hata na mimi binafsi yananikera. Mwaka jana nilisimama hapa nikamwombea Mwalimu mmoja asiyéona na wewe unajua, Waziri akasema huyo Mwalimu apewe hela zake, Mwalimu huyo amepewa hela, lakini matokeo yake, baada ya kupewa, yafuatayo yametokea. La kwanza, huyo Afisa Elimu amemwambia wewe unajifanya una wakubwa sana, kwa hiyo, utakoma. La pili, amemuhamisha shule ya Bangija ya wasioona amempeleka shule nyininge kiasi kwamba Mwalimu yule akitembea kuna korongo anataka kuanguka, kwa nini? Ina maana Wabunge tukiwasemea watu hapa kule wanateseka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwa uchungu sana nikiwa Mwalimu, Afisa Elimu huyu tunaomba Waziri atuondolee. Kwa sababu Waziri yeye naye ana Wilaya yake ya Mwanga amchukue Afisa Elimu huyu ampeleke Mwanga na wa Mwanga atuletee sisi. Mimi naomba na leo kwa mara ya kwanza nitashika mshahara wake asiponipa majibu haya kwa sababu sasa Walimu hawafanyi kazi, wamemuona yule ni Mungu mtu, akiambiwa hasikii, mpaka wananiambia wanamkumbuka Afisa Elimu wao wa zamani sana, Mwalimu Margaret Mziya huko alipo wanamtakia kila la kheri, tunaomba mtuletee Afisa Elimu ambaye anaweza kufanya kazi na Walimu wa Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri amenisikia, naomba kuunga mkono hoja.  
(*Makofi*)

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya pekee niwe mchangiaji wa pili katika hoja iliyoko mbele yetu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nianze kutoa shukrani zangu za dhati kwa ushindi mkubwa uliopatikana jana kumwezesha Rais wetu mpendwa kupewa kura nyingi kabisa kugombea Urais wa Jamuhuri hii. Pia kuweza kupata mgombea mwenza wake Dr. Bilali, mtu mahiri kabisa. Hii *pair* ya watu wawili, nadhani inahakikisha kwamba uchaguzi Tanzania Bara na Tanzania Visiwani, utakwenda vizuri bila matatizo tena tunaenda kwa kasi ya zaidi kuleta maendeleo kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwa ndugu zangu Wabunge, nichukue nafasi hii kuwatachia kila la kheri tuweze kurudi kama tulivyo bila mmoja kubaki nyuma. Nadhani Watanzania wameona kwa miaka mitano tumefanya nini na lazima tuendelee na kasi hii tulete maendeleo halisi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuja kwenye suala zima la hotuba hii. Nichukue nafasi hii kusema nawapongeza Wizara ya Elimu, imefanya kazi kubwa, nimekisoma kitabu hiki, kinanipa matumaini kiasi fulani, sio yote. Mimi mchango wangu ningeweza kusema hivi, elimu ina dira gani? Elimu yetu ninavyoja, elimu nzuri inaanza na *pre-primary, kindergarten* Wajerumani wanaita, ndio mwanzo wa elimu. Upande wa Waislamu wao, elimu inaanza na Madrasa, hapo ndio mtoto analelewa kabisa, anajua kusalimia baba na mama, anajua dini ni nini, Mungu ni nani, anajifunza mambo mengi *at that stage* kabla hajawekwa shuleni, shule ya kawaida. Ukija kwa madhehebu mengine, haya siyaoni yanafanyika, ningetegemea Wizara ya Elimu ingetoa kipaumbele kwa maadili ya vijana wetu wanaosoma na hii utaianzia kwenye *stage* ya *pre-education, primary* na wakifika sekondari wamekamilila kabisa. *Physical education* pia ni lazima iwekewe mkazo. Kwenye kitabu hiki sioni katika *stage* ya kwanza tumeiwekea kipaumbele kiasi gani? Maeneo ya dini, ya kiroho na elimu ya *physical education* sioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tulikuwa tunaangalia mchezo wa mpira wa dunia. Watanzania wote waliokuwa wanashabikia waliona ni kitu gani, lakini walioshinda bila shaka walikuwa na *foundation* nzuri, walikuwa na msingi mzuri katika shule wanazosoma ndio sababu Watanzania hatukuwa huko na hatutarajii kuwa huko tena

*unless tutafanya a big revolution* katika education system nzima katika foundation level, sioni hii katika kitabu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dira ya elimu ni duni, najua tumejiwekea malengo fulani na tunasema tutafikia huko, lakini sio kweli kama tutafika kama hatuna dira maalum. Kila wakati nasikia fedha ni chache, bajeti finyu, hatuwezi kutekeleza mambo makubwa na mimi nasema kama elimu inaanza na *kindergarten* inakuja na *primary*, inakuja na *secondary*, inakuja na *high school* then unapata chuo kikuu, ni lazima misingi halisi ya kufundisha ipatikane katika hatua zote tano, sioni kama kuna mkazo mkubwa umetekelvezwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa tu mfano pale kwangu, pale Jimboni kwangu kwa kutambua kabisa Serikali haina fedha ya kufundisha watoto sayansi. Nilijaribu kwa makusudi kabisa nijenge shule nzuri na kuwapa kila kifaa pale wafundishwe sayansi. Kwa fedha zangu na za wananchi, nikawapa Serikali kwa *silver plate*. Siku nakabidhi shule hii, sikumwona Waziri pale na mpaka sasa Waziri hajakanyaga pale. Vile vyombo vya sayansi vinaoza, maana Mwalimu aliyejuja pale hajui kuvitumia. Ukiona nyumba za Walimu niliwapa, hata hawana mtu wa *kuzi-maintain* maana *real estate management* katika shule zetu zote ni sifuri, hakuna kitengo hicho. Ndio maana ukiona shule za wakoloni, za zamani ikiwemo *Tabora School* ambayo nilisomea mimi, ukiona Bwiru zilikuwa na makusudi, wamezitengenezea mahali pa kufanya *management* ya kufanya mazingira bora, hizi shule sasa zimetupwa tu, zimetelekezwa. Lakini pia kila siku hapa tunaambiwa bajeti finyu ndio maana shule zimeharibika. Sioni hapa kitengo cha *real estate management program*, hakuna, sifuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule zetu ambazo huwa zinafundisha hawa wataalamu wa kutuungia hivi vitu, *Laboratory Technician*, shule zote zile zilifungwa ama ziligeuzwa kuwa Vyuo Vikuu. Leo tulipofikia, hakuna *Laboratory Technician*, pale kwangu zile shule za sayansi, hakuna *Laboratory Technician* hata mmoja. Sasa hawa wanafunzi tunawafundishaje kwa sayansi ya leo? Haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukilinganisha na wenzetu majirani hapa, Kenya, Uganda, Zambia, Malawi, elimu yao ni tofauti na ya kwetu. Hesabu ambayo ndio msingi kabisa wa elimu, sisi nadhani ukiona matokeo ya Darasa la Saba, *Form Four*, *Form Six*, unapata pengine asilimia 10 - 14 basi, ndio wamefaulu nchi nzima. Sioni katika kitabu hiki tunachukua hatua gani za haraka kuweza ku-retrieve na kuwapa elimu bora vijana wetu ambaeo ndio tegemeo la nchi kesho. Tusipo-reverse hiyo, hii kazi unayoifanya, haina maana kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ushauri wangu twende nyuma, elimu hatukuanza sisi. Wenzetu wanafanya nini *in terms* ya *faculty*. Pale kwangu nasema kama tumeshindwa kufundisha sayansi basi tukabidhi *private individual* watusaidie kufundisha watoto wetu sayansi. Pale kwangu kuna shule mbili, ama mziache, ama mje mziangalie, ama vinginevyo hamtakuwa kweli mmezitendea haki hizo shule mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule ninazozungumzia ni shule ya Oeward Mang'ombe ambayo Waziri hajafika, Chief Wanzagi na Chief Ihunyo ya wasichana tu. Sisi kwetu kule Musoma, wanawake wako hali duni *in terms of education*, ni wasichana wachache sana wanasma, asilimia pengine mbili tu. Nimewajengea *laboratory* pale, nimewajengea mabweni mazuri, lakini Walimu wa kuwfundisha hawapo. Aibu kweli, wale wakubwa wakubwa wanaanza kupendekeza watoto wao wa *Arts* waende pale sio wa *Science*. Inaonekana kabisa ni *deliberate effort* ya upande wa Serikali/Wizara kwamba hawataki watoto wetu wajifunze sayansi, hawataki. Sasa kama hamtaki kufundisha sayansi basi wapeni wanaoweza kufundisha sayansi wawafundishe vijana wetu, vinginevyo hatutafika. Kisingizio cha kwamba eeh, bajeti finyu kwa kweli si kweli hamtutendei haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi yangu ni machache, baada ya kusema haya, napongeza kwa dhati kazi mliyoifanya. Mungu abariki Tanzania, Mungu abariki Wizara ya Elimu na wanafunzi wangu. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nimrod Mkono na hongera sana kwa mchango wako kwa elimu ya Tanzania.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe pungezi kwa Mheshimiwa Waziri na Manaibu Waziri wote, kwa hotuba nzuri waliyowasilisha hapa asubuhi na pia niwapongeze tu kwa kazi zao ambazo zimekuwa nzuri kwa kipindi chote cha miaka mitano. Ni matumaini yangu kwamba wapigakura watarawudisha tena ili waje kuisimamia bajeti waliyoandaa wao wenye na pia niwapongeze watendaji kwani wametoa ushirikiano mzuri ndio maana Waziri na Manaibu Waziri wameweza kuifanya kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nipongeze kwa kazi nzuri ya jana. Mheshimiwa Jakaya Kikwete amefanya kazi nzuri kwa uteuzi wa mgombea mwenza, Mheshimiwa Dr. Mohamed Ghalib Bilali pamoja na mgombea wa Urais Zanzibar, Mheshimiwa Dr. Mohamed Shein. Kwa kweli imetia faraja sana kwa Watanzania. Alijisemea Bwana Mrema, Mheshimiwa Jakaya anatisha na kweli anatisha, ninaamini kampeni imeshamalizika hata wapinzani wengi nimeongea nao nadhani wanaimani na uteuzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pungezi hizo, sasa nijikite katika hoja ambazo nilitarajia kuzichangia kuitia hotuba hii. Ya kwanza, ni mara nydingi nimezungumzia suala la Walimu wastaafu 15 wa Singida ambao walijiriwa kwa mkataba kufundisha Shule za Sekondari. Nimeulizia suala hili kwa uchungu sana kwa mara nne hapa Bungeni. Mheshimiwa Naibu Waziri, rafiki yangu mpenzi, Mwantumu Mahiza amekuwa akinipa majibu mazuri kweli na ninaimani naye sana sana na timu yote, Waziri na pamoja na Mheshimiwa Kabaka, wote ninaimani nao, hata watendaji nawapenda sana.

Nataka nijue hivi kuna shetani gani aliyesimamia suala hili mpaka leo hii pamoja na ahadi nzuri ya mpenzi wangu Mheshimiwa Mwantumu Mahiza kwamba madai haya yatalipwa kabla ya kusoma bajeti. Leo hii bajeti imesomwa na ninasema hivi kwa uchungu mkubwa kwamba hawa wastaafu wanaodai mishahara ya miezi kumi na tano hawajalipwa. Nasubiri majibu ya Mheshimiwa Waziri anieleze, wawili wameshafariki, wamebaki sita sijui na hawa watakuifa wote? Kama hawa wameshindwa kupata madai wakiwa wazima, hivi wakifa hiyo mirathi itapatikana? Tuwaombee Mwenyezi Mungu hawa wasife ili wapate haki zao. Ninaamini kwa kupitia hotuba hii, Mheshimiwa Waziri atanipa majibu ya mwisho katika hili kwa sababu nimeshachoka kuzungumza, hata na kipindi chenyewe ndio hiki kinakwisha, inawezekana naongea hotuba hii ya mwisho hapa Bungeni. Ninaamini kaka yangu Mheshimiwa Prof. Maghembe ama yejote kati yao atanipa majibu ya mwisho katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hoja hiyo, naomba nizungumzie kuhusu upungufu wa Walimu. Nchi nzima ina upungufu wa Walimu pamoja na shule za Mkoa wa Singida. Tukianzia na Shule za Msingi pamoja na Shule za Sekondari. Kitaifa Shule za Msingi, upungufu ni asilimia 40 na kitaifa, Shule za Sekondari ni upungufu wa asilimia 58 ukiwemo Shule za Msingi za Singida pamoja na Shule za Sekondari za Singida. Pamoja na kwamba Serikali imejipanga vizuri katika kuongeza idadi ya Walimu, lakini mbona hata hao wanafunzi wanaomiliza *Form Four* walioomba kujiunga na Ualimu wana alama nzuri za kufaulu lakini hawajapangiwa? Hivi kweli mkakati huu mzuri wa Wizara ya Elimu kuhakikisha kwamba Walimu sasa wanaongezeka, wataongezeka kwa mtindo upi kama hawa tu walioomba kujiunga na Ualimu hawakupangiwa? Ninaomba Serikali itupe majibu, ina mkakati gani wa kuwapata Walimu hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu suala la maabara. Suala la maabara sisi katika Mkoa wa Singida, chini ya Mkuu wa Mkoa wa wetu, Parseko Kone, tumejipanga vizuri kabisa. Tumesema mwaka huu tunahakikisha Shule za Sekondari zote zinakuwa na maabara na kila shule tutahakikisha inakuwa na maabara tatu, maabara ya fizikia, ya baiolojia na ya kemia. Tumejiwekea mikakati mpaka mwezi wa tisa mwaka huu, majengo yote ya maabara yatakuwa yamekamilika. Pamoja na kwamba Serikali imejiwekea mipango yake ya kugawa viwango vya maabara, lakini tuangalie ni wapi watu wanahitaji, ni wapi wamejipanga, hivi kama kweli majengo haya yatakuwa yamekamilika kuna haja ya kumsubiri kumpa vifaa mtu ambaye hajajenga hayo majengo? Mimi naomba Singida tupewe kipaumbele, kwa sababu tumejipanga kabisa, tumechoka kuambiwa sisi Singida ni Mkoa wa mwisho kitaaluma. Tunataka Mkoa wa Singida kitaaluma tuondoke hapa na uwezo upo na nia ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia hilo, naomba niongelee juu ya Posho za Uhamisho na Posho za Usumbufu. Mimi naomba Mheshimiwa Waziri wakati anatoa majumuisho atueleze tofauti kati ya poshi hizi, kati ya Posho za Uhamisho na Posho za Usumbufu kwa sababu Walimu wanapohama, Mwalimu kafunga mizigo, usijali katembea kilomita moja au mbili lakini kahama huyo Mwalimu. Sasa labda tuambiwe wanaostahili kupata Posho za Usumbufu ama Posho ya Uhamisho, ni Mwalimu yupi, aliyeama umbali upi, aliyeenda wapi, tuelewe kwa sababu Walimu wengi wanapata

utata sana katika suala hili. Posho hizi wengi wananyimwa, wanaambibiwa wewe hujafunga mizigo, sijui hujafanya nini na hili naomba litolewe ufanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, naomba niongelee kuhusu Posho ya Mazingira Magumu. Ni kweli katika Mikoa yetu, katika Wilaya zetu, zipo shule ambazo zina mazingira magumu. Ninaomba Serikali pamoja na kwamba viongozi wa Serikali za Vijiji, viongozi wa Serikali za Mitaa, pamoja na Kata, wamejiandaa kuwapokea Walimu hao na kuwapa huduma mbalimbali, lakini bado Serikali inawajibika kutafakari kwa kina kabisa kuhusu hawa Walimu wanaofundisha katika shule zenye mazingira magumu. Wilaya zetu jamani, jiografia yake haifanani. Naomba Posho ya Mazingira Magumu ifikiriwe, Walimu waanze kupata posho hii ili hata hizo shule ambazo Walimu wanashindwa kwenda, ama wanaripoti wanakimbia, taratibu hizo ziishe ili shule nyingi ambazo ziko mbali na maeneo ya mijini ziweze kupata Walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nizungumzie kuhusu malipo ya fedha za mapunjo ya Walimu wanaopanda madaraja. Ni kweli Serikali inapandisha madaraja lakini Walimu hawa wanapopandishwa madaraja, suala la kurekebishiwa mishahara inakuwa ni tatizo kwao na kulipwa mapunjo hayo inakuwa ni tatizo, sijui tatizo hili linatokea wapi? Mwalimu unampa daraja mwenyewe, leo unashindwa kumpandishia mshahara hapo hapo unapompandisha daraja, anapoanza kukudai inakuwa tatizo. Mimi naomba vitu vingine tusilimbikize matatizo, tusiwafifishe Walimu kufanya kazi zao vizuri. Mimi naomba, kama kweli Mwalimu amepandishwa daraja umpandishie na mshahara wake pale pale na siyo hivyo tu na hizi skeli za mishahara mimi naomba ziwe wazi. Pamoja na kwamba mshahara ni siri ya mwajiri na mwajiriwa, basi tupeleke skeli za mishahara ili kila Mwalimu ajue skeli yake anastahili mshahara gani na ongezeko lake ni kiasi gani, ili aelewé.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii, kukushukuru sana kwa kunipa nafasi na nianze kwanza kwa kuunga hoja mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama ili kuishukuru Serikali kwa sababu naamini kama Mbunge unaweza ukalalamika mwaka wa kwanza, wa pili, wa tatu, wa nne na huu ni mwaka wa mwisho, ukaendelea kulalamika, inaweza ikaleta maana kwamba hata wewe hukufanya kazi. Kwa hiyo, nataka nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa yale ambayo tumefanikiwa katika Wilaya yangu ya Makete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza kabisa, nataka kuishukuru Serikali kwa kutoa maamuzi ya upendo kabisa kwa wananchi wa Makete na kuanza kutekeleza ujenzi wa Chuo cha VETA. Wilaya ziko 132 lakini kutokana na ufinyu wa bajeti Serikali ililazimika kuanza kujenga chuo katika zile Wilaya, hii ni Wilaya ya Makete kutokana na

matatizo ya watoto yatima waishio katika mazingira magumu. Kwa hiyo, huu upendo tumeupokea kwa furaha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Profesa Maghembe, Manaibu wake, Katibu Mkuu, vilevile nimshukuru sana Mkurugenzi wa VETA, *Engineer Zebadia Moshi*, Mwenyekiti wa Bodi ya VETA, Profesa Idrisa Mshoro, Mkurugenzi wa Chuo cha VETA Iringa, Mkurugenzi wa Chuo cha VETA, Brigedi ya Mpanda ambao ndiyo waliofika mpaka Makete kuliona eneo na kuunda Kamati kutengeneza *Memorandum of Understanding* na mpaka chuo kimeanza kujengwa. Sisi tunashukuru sana na matokeo ya chuo kujengwa Makete yameshaanza kuleta matunda kwa sababu tayari kuna watu wamepata ajira ya kupeleka vifaa vya ujenzi, kushughulika na shughuli za ujenzi na vilevile kikiisha, vijana wanaomaliza Darasa la Saba, Darasa la Kumi na Mbili, Darasa la Kumi na Nne, watapata fursa za kwenda kusomea mafunzo ya ufundi ambayo yana faida ya kuweza kuajiri na kuweza kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niitumie nafasi hii tuiombe Wizara itusaidie kwa sababu ili shughuli ziharakishwe pale panahitaji umeme. Halmashauri yetu imejipigapiga imefanikiwa kupata shilingi milioni 15 lakini mahitaji ya pale ni zaidi ya shilingi milioni 26. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri kupitia VETA watusaidie kiwango kinachobaki ili tupate umeme na ikiwezekana ule ujenzi uweze kuharakishwa zaidi lakini la msingi tunashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nataka nitumie fursa hii, kuishukuru Serikali yetu ya Awamu ya Nne, wananchi wa Jimbo la Makete, Halmashauri na viongozi mbalimbali kwamba Wilaya ile mwaka 2005 tulikuwa na Shule za Sekondari sita lakini leo hii tuna Shule za Sekondari 16. Maana tulipokuwa na shule sita tuliweza kudahili watoto 960 leo hii tuna uwezo wa kudahili watoto 2,560, hii ni zaidi ya asilimia 166. Ina maana kwamba hawa watoto tusingeweza kujenga zile shule ndiyo hawa wangkuwa mitaani na wengine wangekwenda kwenye ajira ambazo siyo nzuri za kufanya kazi majumbani na baadaye kupata matatizo ya magonjwa haya ya hatari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii vilevile kuishukuru sana Serikali, niliposikia mkakati leo hii wa kupata Walimu kwa sababu tatizo kubwa katika Shule za Sekondari ni Walimu. Mheshimiwa Waziri amesema kwamba wana mpango wa kuona kwamba kila shule itapata Walimu watano. Niiombe Serikali basi huu mkakati uweze kupatikana mapema ili tuzibe tatizo la Walimu katika Shule zetu za Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, nataka niishukuru sana Serikali imetupatia fedha Wilaya ya Makete kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Walimu. Wote tunafahamu kwamba moja ya vitu ambavyo vinasumbua sana Walimu kwenye maeneo kama ya Makete ambayo yapo pembezoni na mazingira yake ni magumu ni nyumba za Walimu. Kwa hiyo, Serikali imetua shilingi milioni 300 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 10 za Walimu na sisi tuliamua kwamba hizo fedha tujenge nyumba za aina ya *two in one* yaani nyumba moja inajengwa ili Walimu wawili waweze kuishi pamoja. Kwa maana hiyo, tumeweza kupata nyumba ya kuchukua Walimu 20. Tunaishukuru sana Serikali kwa upendo huo mkubwa. Niiombe tu kwamba kwa sababu Wilaya ya Makete ina matatizo ya

kuwa pembezoni na Walimu wengi wamekuwa wakiondoka kwa sababu ya ukosefu wa nyumba, basi Mheshimiwa Waziri atufikirie na kutupendelea katika bajeti hii ili tuweze kuongezewa nyumba zingine zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne, naomba sana niishukuru sana Serikali kwa mkakati wake kupitia *TASAF* na kupitia Mfuko wa Halmashauri kwa ujenzi wa mabweni. Tunafahamu sana kwamba vijana wetu wengi hasa wa kike, wanapata mimba kwa sababu wanaishi kwenye nyumba za kupanga. Kwa hiyo, mkakati wa mabweni unasaidia sana kuwaokoa watoto wa kike ili wasipate mimba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, nimshukuru sana sana Mheshimiwa Mama Salma Kikwete ambaye ye ye alipokuja Makete alipata uchungu na akaona hali halisi ya watoto wa Makete, ameamua na akatekeleza na ametujengea bweni la watoto wa kike katika Shule ya Sekondari pale Iwawa. Tunamshukuru sana kwa upendo huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niishukuru sana Serikali, Wilaya yetu ilikuwa haina shule za Kidato cha Tano, leo kwenye Awamu ya Nne yamewezekana. Kwenye shule za Kidato cha Tano na cha Sita katika Shule za Iwawa na Mwakavuta, watoto wameshaanza na hawa vijana wanatoka Mikoa mingine. Hii ina maana kwamba wana Makete wana fursa ya kujifunza na wale wana vijana, wana fursa ya kututangaza sisi wa Makete katika sehemu zingine na vijana wetu pia wanaweza kwenda kwenye Mikoa mingine ambayo hii ndiyo zana aliyoieleza Mheshimiwa Rais ya kujenga Utaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuishukuru Serikali na naomba sana Mheshimiwa Waziri aki-*windup*, aone namna ya kusaidia hizo fedha kwa ajili ya kupeleka umeme pale kwenye Chuo cha *VETA* Makete. Ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. MARGRETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na nitajitahidi kuharakisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naipongeza Wizara na Watendaji wake nikianzia na Waziri, Manaibu Waziri na Watendaji wote, kwa kutuandalia hotuba nzuri na yenyе kuleta matumaini, imechanganuliwa sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimefarijika na Wizara kwamba wataendelea kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika shule zetu na nikiri kabisa nimeshathibitisha kwamba Wizara imejitahidi sana kuwapatia vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia hasa katika shule ambazo zina vitengo vya viziwi. Ninaloomba sasa hizi, pesa za wakati huu muendelee pia kushughulikia kununua vifaa vya wanafunzi wa aina zingine za ulemavu. Viziwi wana vitu *complicated* sana kwa kweli, nashukuru sana kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nimefurahishwa sana kwa kiasi fulani kwamba kumekuwa na ongezeko la wanachuo wenyе ulemavu katika vyuo vyetu vikuu. Lakini bado pamebaki na tatizo, kama mikopo inakuwa adha kwa wale wazima, inakuwa adha

zaidi kwa watu wenyewe ulemavu au wanachuo wenyewe ulemavu kufuutilia Dar es Salaam mara kwa mara na mambo kama hayo na mimi wamenilalamikia mara nyingi kwamba inakuwa tatizo kupata mikopo hiyo. Lakini nashangaa, labda ni jambo dogo hapo katikati linakosekana kwa sababu hata ile Sheria ya Mikopo tulisema kwamba wanafunzi wa Vyuo Vikuu wenyewe ulemavu lazima wapewe kipaumbele katika kukopeshwa. Sasa sijui ni nini kinatoka. Naomba suala hilo lirekebishwe kwa sababu linatusumbua na kutuhuzunisha. Kwanza, wanaoweza kufika huko wala siyo wengi. Kuna wakati niliomba wasomeshwe bure kabisa, ile mikopo wakipewa hakuna haja ya kuwaambia walipe, mbona ni wachache na Serikali ina uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda kulisemea ni ukosefu wa miundombinu muafaka kwa shule zetu, mabweni hasa majengo na vyoo, suala hili nimelisema miaka yote hii mitano. Majibu naambiwa kuna ramani ya majengo na vyoo, sijui iko Wizarani, sijui iko wapi, sasa kwa nini haitolewi kwenye Halmashauri kusudi watu wajenge vitu ambavyo ni stahili kwa watu wenyewe ulemavu? Hawa wanafunzi wanahangaika, vyoo wanatambaa chini, wao wanapaswa kuinuliwa juu, jamani taaluma, Wahandisi wapo, ma-Architecture, wanafanya nini hawa au hapa mtekelezaji anayekosea ni nani? Wanangu hawa wanaendelea kuteseka. Ningombaa hili lirekebishwe wasiendelee kuteseka kama mama yao nilivyokuwa nimeteseka huko nyuma jamani. Sasa kuna wa kuwasemea, dunia inabadilika, dunia nje inasema mambo mazuri, kwa nini haya tusiyachukulie, bado mabweni marefu, madarasa ngazi chungu mbovu, *wheel-chair* ni tatizo mpaka abebwe, wanakataa kubebwa kama mizigo ya sukari, lazima wajitegemee wenyewe kwa viungo vilivyobaki. Kwa hili, naomba sana jamani iwe ya mwisho kwa sababu mambo yenyewe ndiyo lala salama, Mungu atusaidie, nikirudi nitaendelea kuyapiglia kelele. Hata nisiporudi nitawaelekeza wenzangu hawa kwamba mimi niliachia kazi hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi bado naona kuna umuhimu wa kuunda Kurugenzi kamili kabisa ya Elimu Maalum. Wanafunzi wenyewe ulemavu wanaongezeka, majukumu yameongezeka, naomba wawe na Kurugenzi yao badala ya kuwa chini sijui ya Afisa Elimu Kiongozi. Maana ukiwa na Kurugenzi najua mafungu haya yatapangika sawasawa na wataalam wenyewe taaluma hiyo watakuwepo pale. Kuliko hali ilivyo sasa ni wachache na majukumu ni mengi kwa sababu wenyewe ulemavu tunaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Patandi bado kinatoa Diploma mimi nilikuwa nafikiri kwamba ni vema jamani hadhi ya Chuo hiki iinuliwe kisaidiane na Sekuko ili kuweza kuwaendeleza Walimu wa taaluma mbalimbali watakaofundisha watoto wenyewe ulemavu, kama mwenzangu alivyosema Mama Maziwa pale bado ni wachache, kiinuliwe ili kusudi kiweze kutoa Digrii wakisaidiana na Sekuko aliyejitlea jamani Chuo cha *mission* kile mimi ninakishukuru kwani vikiwa viwili vina matatizo gani, kwa sababu wenyewe ulemavu wenyewe tunaongezeka. Hiyo ilikuwa ni rai yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi kwamba katika Vyuo vya Ualimu kutakuwa na kutumia teknolojia, nilitaka kufahamu maeneo yale ambayo umeme haupo, tunafanyaje? Maana kwa kweli maeneo mengine vyuo hivi vilipo hakuna umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani za dhati kabisa kwa wahusika wote wa Wizara hii kwa sababu mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Wizara hii kwa miaka saba iliyopita. Tulishirikiana vizuri, walinisikiliza, maoni yangu mengi waliyachukua. Naomba waendelee hivyo na waendelee kufanya kazi vilevile kwa ari mpya, nguvu zaidi na kasi zaidi kwa sababu Wizara hii kwa kweli mimi nasema ndiyo Wizara Mama ya kumwonyesha mtu macho licha ya hayo aliyonayo lakini dunia nzima inasema hivyo. Mheshimiwa Mkono kasema kwa kweli bila elimu, ujinga ukiwepo, hakuna tutakachokifanya hasa katika dunia hii ya sayansi na teknolojia lakini naomba yazingatiwe haya masuala ya wanangu wenye ulemavu mabwenini na madarasani. Tunafahamu nini kinapaswa kuwepo, hivi tatizo ni nini? Maana vitu vingine havihitaji hata kuongeza bajeti, ni utekelezaji tu na ku-*modify*, basi, mimi nashangaa kwa nini mambo yanakuwa namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia kheri Watendaji wa Wizara hii, nawatakia kheri Waheshimiwa Wabunge wote jamani, tena na hivi tumeshachagua Mheshimiwa Rais wetu atakuwa huyo huyo Kikwete, Mwenza wake atakuwa huyo huyo Bilal na kule atakuwa huyo Shein. Tutakiane kheri ili tuje tuijenge nchi hii hapa tena upya au kuendeleza haya ambayo tunayaachia kuweza kuwashauri wenzetu na nchi ikasonga mbele. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Margareth Mkanga kwa kutumia muda vizuri, ndiyo uzuri wa Walimu.

Waheshimiwa Wabunge, kama alivyosema Mama Mkanga, Wizara hii ni muhimu sana. Nina hakika kama nafasi ingekuwepo hakuna Mbunge ambaye hangesema chochote katika Wizara hii. Kwa hiyo katika wale ambao angalau wameomba waseme leo orodha yetu inaonyesha kwamba kuna Wabunge 32. Mpaka sasa wameongea watano, kwa hiyo, jioni tutaendelea kidogo lakini kwa vyovypate vile wengi hawatafikiwa. Kwa hiyo, jioni tutaanza na Mheshimiwa Mtutura, atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Omar Juma na Mheshimiwa Nuru Bafadhil ajiandaye na wengine watafuata kadri ya muda wetu utakavyokuwa.

Basi baada ya tangazo hilo, naomba sasa nitumie fursa hii kusitisha shughuli za Bunge hili hadi saa 11.00 jioni.

(*Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

**MWENYEKITI:** Majadiliano yanaendelea, simuoni Mheshimiwa Mtutura, namwona Mheshimiwa Riziki Omar Juma na atafuatiwa na Mheshimiwa Nuru Bafadhil, Mheshimiwa Riziki.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi ya mwanzo. Lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ndiye wa kushukuriwa mwanzo kwa kunijalia uwezo na afya njema na

kuweza kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu sana. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu wake kwa kazi nzuri ambayo wanajitahidi kuifanya ili kuiboresha Wizara hii iendane na umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mchango wangu naomba niuelekeze zaidi kwenye ushauri. Wizara hii ya Elimu ndio ambayo inazalisha matunda ambayo yanaongoza Taifa hili na kwa msingi huo, inahitaji kupewa kipaumbele sana. Lakini naomba niseme kwamba katika masomo ambayo tunayafundisha shulenii, kuna somo moja muhimu sana ambalo ninadhani lingepewa umuhimu mkubwa kulifundisha na tukaliingiza katika mitaala yetu, ni somo la dini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania haina dini lakini Watanzania wana dini na inawezekana kwa sababu kutoona umuhimu wa dini ndio maana sasa hivi tunapotea sana katika Tanzania yetu. Kumekuwa na mambo ya ajabu ajabu, kuna mauaji ya kinyama, kuna ukiukwaji wa haki za binadamu kupindukia, wanauliwa watu wasiokuwa na hatia, watu wanabakwa kwa imani za kishirikina, mauaji ya vikongwe, hii inawezekana inatokana na ukosefu wa maadili ya dini zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakristo wana dini yao, Waislamu wana dini yao, wapagani wana dini zao, kila kabilia au kila mtu ana dini yake na kila dini ina maadili yake. Inasemekana kwamba enzi za Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, kulikuwa na Mkoa fulani ambao ulikuwa ukijihuisha sana na mauaji kwa imani za kishirikina. Kwa sababu hiyo, Mzee wetu huyo inasemekana aliunda Tume fulani kuipeleka katika Mkoa huo ili kufanya utafiti. Baada ya kufanya utafiti huo ikagunduliwa kwamba mambo hayo yanatokea kutohana na watu wengi karibu 60% hawana imani ya dini na ndio maana walikuwa wanafanya vitu hivyo vya ajabu ajabu. Nina maana ya kusema kwamba somo hilo la dini liingizwe katika mitaala yetu na lifundishwe shulenii kuanzia *primary* ili watoto wetu waondokane na imani potofu, kwa sababu watajengeka katika maadili mazuri sana ya dini zao kwa sababu dini zote zinakataza uonevu, mauaji yasiyokuwa ya lazima, dini zote zinakataza imani za kishirikina. Hakuna dini ambayo inaelekeza mambo ya kishirikina. Sisi Waislamu kabla ya kuteremshwa *Quran*, kabla ya kuja Mtume wetu Muhammad (S.A.W.), ilikuwa wanawake wakizaliwa wanauliwa kwa imani kwamba wanaleta balaa, wanaleta uchuro, wanaleta umaskini lakini baada ya kuteremshwa *Quran*, dini ikaelekeza, mambo hayo yaliachwa na leo tupo wanawake na wanaume tunazaana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivyo kwa sababu ninaomba sana somo hili liingizwe katika Mitaala yetu na tulifanyie kazi, watoto wetu wakue katika maadili ya kidini ili jamii inayokuja isiendane tena na hizi imani potofu. Leo hebu niambiwe ni tajiri gani ambaye tunamjua Tanzania ametajirika kwa sababu ya kuchukua mkono wa Albino? Ni imani potofu, zinatupeleka kubaya, hatuna imani za kidini vizuri, hatuzingatii, hebu tuwajenge watoto wetu vizuri tangu msingi, kutohana na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nilitaka nilizungumzie ni somo la michezo. Hata Mheshimiwa Rais jana alipokuwa akihutubia mkutano wa CCM, alilagusia sana suala la kukuza michezo. Michezo ni suala muhimu sana na ninakumbuka zamani somo la michezo lilikuweko kabisa katika mitaala na lilikuwa likifundishwa madarasani, lilikuwa na kipindi chake. Pengine utakuta kipindi cha tatu na cha nne ni wakati wa

michezo, wanafunzi wanatoka nje wanakwenda kujipumzisha, wanapumzisha akili zao, wanapumzisha viungo vyao, wanapasha moto viungo vyao. Kwa hiyo, mwanafunzi ambaye anakua na mwili wake unajengeka katika mambo ya michezo, basi anakuwa na akili nzuri zaidi. Mwalimu wangu, *Principal of Education* aliniambia kwamba “*a health mind is in a health body*”. Kwa hiyo, suala la michezo, ni suala la msingi sana na kwa sababu hiyo alituambia kwamba ni lazima mtoto tumjenge katika mambo matatu, *soul, body and mind*. Katika hayo matatu basi utakuta kuna kumjenga mtoto kimwili, kumjenga mtoto kiroho na kumjenga mtoto kiakili. Katika mambo hayo matatu hata lile la mwanzo nililolizungumzia basi litaguswa na hili. Kwa hiyo, pale mtoto anafaidika kimichezo, Taifa letu linafaidika na hata wao wenyewe watoto wanafaidika, wanakuwa vizuri, wanakuwa na afya nzuri, wanakuwa na akili nzuri, wanakuwa na ufahamu wa kusoma. Kwa hivyo, ni suala la msingi sana kufanya kazi hiyo ya kuliboresha somo la michezo ndani ya shule, tukaliwekea hasa mtaala pamoja na somo la kidini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilitaka nilizungumzie, ni suala la malimbikizo ya Walimu. Kuna baadhi ya Walimu hadi hivi leo kwa taarifa tulizonazo, hawajalipwa malimbikizo yao. Kwa hivyo, ninaomba sana tulishughulikie kwa umakini mkubwa ili na wao Walimu wetu waweze kufanya kazi zao ipasavyo. Kila siku ninasema humu ndani, Mwalimu ni mtu muhimu sana na sisi sote tusingekuwemo humu ndani kama si Mwalimu. Tunapaswa Mwalimu tumboreshee mazingira yake, tumuweke vizuri aweze kufanya kazi yake kwa kuipenda sana na kwa uadilifu mkubwa. Mwalimu kama haipendi kazi yake hawezikutoa matunda mazuri. Ili Mwalimu aipende kazi yake ni lazima awe na nafasi nzuri ya kuifanya kazi yake kwa umakini na ule mtindo wa Mwalimu kufanya biashara darasani ili kujipatia chochote, tukimwekea mazingira mazuri, tukawarejeshea *Teaching Allowance* zao, unaweza ukaondoka na masomo yetu yakaenda vizuri, tukajenga Taifa lililo bora kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutake tusitake jamani pamoja na kusema elimu imeboreka, lakini bado tunasema elimu iko katika kiwango cha chini Tanzania. Tusijilinganishe na sisi ambao huko nyuma pengine hatukusoma, sasa hivi ulimwengu ni mwingine, ni ulimwengu wa sayansi na teknolojia. Ni lazima tujipinde kuhakikisha watoto wetu tunawafundisha na tunawapa mazingira bora, Walimu na wanafunzi wenyewe wakiwa katika mazingira mazuri, basi itawasaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa ujenzi wa maabara. Ni muhimu sana kila tunapo jenga shule ya Sekondari tuhakikishe tunajenga maabara kwa vyovyyote iwavyo. Ni afadhali tuwe na darasa moja tu la Sekondari lakini maabara iwepo. Ni jambo la msingi sana, wanafunzi wengi hawalitaki somo la sayansi, wanafunzi wengi hawalitaki somo la hisabati. Mimi ninashangaa sana kwamba wanafunzi hawalipendi somo la hisabati, mimi mwenyewe nilikuwa ni Mwalimu wa hisabati na ninalipenda sana somo la hisabati na niliumia sana nilipoondolewa kazini, kwa sababu ya somo la hisabati na sasa tunapoteza hazina hiyo, sio Walimu wengi wanaopenda kusomesha hisabati, sio wanafunzi wengi wanaolipenda somo la hisabati. Naomba tuwawekee viwango wale Walimu ambao wanapenda masomo ya sayansi na hisabati basi tuwape motisha. Tuweke motisha maalum ili Walimu wanaopenda masomo haya waweze kufanya kazi kwa umakini mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Riziki Omar Juma. Sasa niitaje kidogo orodha ya wanaofuata kwa kadri tulivyowahi humu ndani. Atachangia Nuru Bafadhil, baadaye atakuwa Cynthia Ngoye, atafutatiwa na Susan Lyimo na Janet Mbene ajiandae, akina mama hao, Mheshimiwa Nuru Bafadhil.

**MHE. NURU A. BAFADHIL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuwa hapa kwa siku hii ya leo nikiwa katika hali ya salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kumpongeza Mwenyekiti wangu wa *CUF* Taifa, Profesa Ibrahim Haroun Lipumba, kwa kuchaguliwa kuwa Mgombea wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia napenda kumpongeza Maalim Seif Sharif Hamad, kwa kuchaguliwa kuwa Mgombea wa Urais wa Zanzibar na mwisho ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Juma Duni Haji, kwa kuchaguliwa kuwa Mgombea Mwenza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, napenda sasa kuchangia machache niliyonayo. Kweli nchi yoyote haiwezi kwenda bila ya elimu, leo sisi tupo hapa lakini takribani wote tumekwenda shule, tunesoma kila mtu kwa kiwango cha elimu yake alichofikia. Lakini cha kushangaza kuna baadhi ya wazazi hawataki watoto wao waendelee na masomo na hususan wazazi wenye watoto wa kike. Sasa hivi Serikali inahimiza wasichana waendelee na masomo ili tuweze kupata wasomi wanawake lakini kuna baadhi ya wazazi wanawazuia watoto wao wasiende shulenii baada ya kufaulu mitihani yao ya Darasa la Saba kuingia Kidato cha Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama mzazi, kama mwanamke, kuna jambo lililonigusa. Kuna mwanafunzi, kwa mujibu wa taarifa ya mzazi wake yaani mama yake mzazi, mama yake mzazi anaishi Morogoro anaitwa Elizabeth Dismas. Huyo Elizabeth Dismas ana binti yake ambaye anaitwa Mwajuma Juma, huyu Mwajuma Juma anaishi kijiji cha Mbiti, Kata ya Upuge, Wilaya ya Uyui, Mkoa wa Tabora. Cha kusikitisha, binti huyu mwaka jana alifaalu kuingia Kidato cha Kwanza, alianza Kidato cha Kwanza lakini mwaka huu, baba amemzuia asiende shulenii na amemzuia asiende shulenii kwa kumtafutia mchumba ili aolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu binti kuanzia tarehe 26 Juni, aliwekwa ndani kwa mafunzo na matayarisho ya hiyo ndoa na ametoka tarehe 4 Julai. Msichana huyu, juzi tu mjomba wake ambaye anaishi Ifakara, alimuhoji kwa njia ya simu, mama unataka kuolewa je, mchumba anayekuoanamjua? Akasema simjui. Jina lake unalifahamu? Akasema sifahamu. Je, kazi anayofanya? Akasema pia sifahamu, sasa ona jinsi gani wazazi wengine ambao hawaoni umuhimu wa watoto wao kwenda shule. Yule mama analalamika kwa sababu mtoto wake ni huyo mmoja na wala hategemei kama atapata mwingine, amemzaa huyo msichana ambaye sasa hivi ana miaka 16 lakini cha

kushangaza baba wa mtoto amepokea mahari takribani shilingi laki nne na kutaka kumwozesha mtoto huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoiomba Serikali na inanisikia, ifuatilie suala hili ili binti huyu ikiwezekana kama amezuiwa kwa ajili ya ndoa, arudishwe shule na ikiwezekana asiendelee kusoma huko huko Upuge, atafutiwe shule ya bweni ambapo anaweza akaendelea na masomo. Binti anakubali kuolewa kwa sababu yuko mbali na mama yake na uwezo wa kukataa hana na wakati mwengine anapewa vitisho. Hilo ndio lilikuwa lalamiko au sikitiko langu kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukija kwa upande wa Walimu, kuna baadhi ya Walimu Wakuu wana tabia ya kuwanyanya Walimu wao. Mwalimu anakuwa shulenii pale kila anachokifanya anamnyanya na wakati mwengine inakuwa Mwalimu yule Mkuu ndio chanzo cha matatizo. Kwa sababu Mwalimu Mkuu na Afisa Elimu wanakuwa ni kitu kimoja, kwa hiyo, kila kitu anachokifanya Mwalimu yule, Afisa Elimu anapewa habari. Namna ile inajenga chuki na kumfanya Mwalimu asiweze kuwa katika mazingiora mazuri ya kufundisha shulenii pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna baadhi ya Walimu Wakuu, anapewa uhamisho, anaweza kuambiwa unatoka shule hii uende shule hii, Mwalimu yule anakataa kwenda shule nyengine eti kwa sababu tu pale shule pana mradi mzuri wa mnara wa simu ambaao kwa mwezi unaingiza Sh.2,000,000/=. Sasa ni dhahiri kwamba huenda Mwalimu yule pesa zile zinakuwa ni mali yake, kwa sababu kama ni pesa za shule asingekataa, angeziacha bado zikaendelea kubaki shulenii na ye ye akaenda kwenye sehemu ya uhamisho ambayo amepangiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mitihani. Kuna baadhi ya Walimu wanaskitika wakati wa kusimamia mitihani nya Darasa la Saba. Kila siku wasimamiaji wanakuwa ni wengine na sehemu za Wilaya nyengine ni wale wale, hakuna mabadiliko, hata kama watu wengine hawana uwezo lakini wanabaki ni wale wale tu kwa sababu ya mshiko maana pengine ni shemeji yake au ni rafiki yake au ni jamaa yake wa karibu, kwa hiyo, anabaki ni yule yule kila siku anakwenda kusimamia mitihani. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iliangalie sana suala hili, kuwe na *rotation*, sio kila siku wasimamiaji wawe ni hao hao. Kila mtu ambaye amekwenda shule na kama ataeleweshwa atawenza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani wakati Walimu wanakwenda likizo kulikuwa kunafanya *Refresher Courses*, Walimu wanaweza wakapelekwa chuo fulani, wakaenda wakakaa angalau wiki tatu au mwezi mmoja wakapata mafunzo fulani. Kwa hiyo, utakuta Mwalimu anaweza kumudu kusomesha masomo mbalimbali kutokana na yale mafunzo anayoyapata. Sasa hivi mtu anaweza kupewa semina ya wiki moja tu na Walimu wengine vichwa ni kama hivi, kama mimi nimeshazeeka, kwenda kumchukua Mwalimu ukamfundisha somo kwa semina ya wiki moja, hawezi ku-*gain* chochote. Kwa hiyo, tunachoiomba Serikali, ifikirie tena kurudisha ule utaratibu wa Walimu kwenda *Refresher Courses* ili angalau waweze kupata kitu kitakachowenza kumsaidia ye ye na hali kadhalika kuweza kumsaidia mwanafunzi ambaye ndiye lengo tunalolitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine japokuwa nimeandika kwa maandishi, lakini ninataka nilizungumze hilo. Kuna baadhi ya Shule za Sekondari au za Msingi, kwa kweli madarasa yanajengwa katika hadhi ambayo haikidhi haja. Kuna shule moja iko katika Kata ya Tongoni, Jiji la Tanga, mwaka 2008, tulifanya ziara na Mkuu wa Mkoa, tukakuta ile shule ina nyufa, umeanzia kutoka juu mpaka kwenye ile sakafu. Mkuu wa Mkoa akaagiza akasema, ninaomba darasa hili lirekebishwe. Cha kushangaza mwaka huu mwezi wa tano nilienda kupeleka vitabu kwa ajili nya shule hiyo ya Sekondari, ile hali niliikuta vilevile na wakati wowote ule ukuta unaweza ukaanguka, aidha, ukawaumiza Walimu au ukawaumiza wanafunzi au wakaumia wote kwa pamoja. Kwa hiyo, hii kwa kweli haileti picha nzuri kwa sababu tunachukua Wakandarasi ambao ndio hao hao tunawajua mitaani wanatengeneza vitu ambavyo havina ubora. Kwa hiyo, hii inaweza ikaleta matatizo na hatimaye tukasababisha madhara kwa wale ambao wako katika darasa hilo au katika chumba hicho ambacho wanajifunzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, sasa hivi tuna shule nyingi za Kata ambazo zitatoa wanafunzi kwenda Kidato cha Tano. Basi tunaomba wazazi washirikiane ili kuweza kujenga shule za A – *Level* ili tuweze kuwapeleka watoto wetu kwa sababu wimbi hili la wanafunzi hatutamudu kuwaweka nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundsi. Awali kabisa, naomba nitoe pongezi zangu kwa viongozi wangu wa Chama cha Mapinduzi ambao wameteuliwa kuingia katika mchakato wa kukiongoza Chama cha Mapinduzi, nao ni Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ambaye amepata kwa kura nyingi sana 99.16, Mheshimiwa Dr. Shein, ambaye yeeye pia amechaguliwa kuwa mgombea wa Urais Zanzibar na vilevile Dr. Bilal kuwa mgombea Mwenza. Pongezi zangu dhati kabisa na tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu kwa hakika watapata ushindi wa kishindo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa inawezekana nisipate nafasi baadaye maana leo ni mara yangu ya tatu kuchangia, naomba niwapongeze sana wanawake wa Mkoa wa Mbeya ambao wamekuwa wakiniamini kwa muda wa miaka hii mitano. Wameniamini sana na nimefanya nao kazi kubwa kwa ushirikiano wa pamoja na wamenipenda sana. Ninaomba Mwenyezi Mungu aendelee kutuunganisha na huko mbele basi tuendelee kuwa pamoja katika kuleta maendeleo ya wanawake wa Mkoa wa Mbeya lakini vilevile wanawake wa Tanzania, nawashukuru sana tena sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ni msingi wa maendeleo yote kama tunavyofahamu. Kwa kweli changamoto zake ni nyingi sana na hata leo hapa tukisema tuzungumze watu wote hapa watazungumza na hatutamaliza. Basi nichague maeneo machache ambayo na mimi kama Mwalimu niweze kutoa mawazo yangu hapa na pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hili suala la uhaba wa Walimu katika mashule yetu na hasa katika Shule za Msingi na Shule za Sekondari, tatizo ni kubwa, lakini

jitihada za Serikali ni kubwa vilevile, mimi nazielewa na uhakika kabisa Serikali inafanya juu chini ili katika miaka labda mitano ijayo tusiwe tunazungumzia tena suala la uhaba wa Walimu. Sasa nataka tu nizungumzie namna ya kuwapata Walimu wa Daraja la A. Walimu wa Daraja la A, ni wale waliomaliza Kidato cha Nne, hawa wanatakiwa wawe wamepata si zaidi ya *point* 28 ili waweze kuchaguliwa kuingia katika mafunzo ya Ualimu. Lakini mimi nimeshuhudia vilevile kwamba kuna waombaji wengi ambao wanakuwa na *point* 26 wengine *point* 27, wanaomba kujiunga na mafunzo ya Walimu lakini hawachaguliwi, hivi kuna nini? Basi Serikali itufafanulie ni kwa nini wenye *point* 25 walioomba hawakuchaguliwa, sasa wa 28 mwengine hakuchaguliwa mwengine amechaguliwa, je, Serikali inaweza ikatoa ufafanuzi na wananchi wakaelewa ni kwa nini basi wengi hawa wa *grade* ambazo ni nzuri wanashindwa kuchaguliwa kujiunga na Walimu *Grade A?* (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni lile la ujenzi wa Shule za Sekondari za Kidato cha Tano na Kidato cha Sita, ni mpango mzuri sana huo kwa sababu hivi sasa maana yake tunataka kupata idadi kubwa zaidi ya watoto ambao wanakwenda madarasa hayo baada ya kumaliza Kidato cha Nne ambao ni wengi sana. Shule hizi zinajengwa katika ngazi ya Wilaya na wananchi wenyewe. Mimi napenda nichukue nafasi hii, niwapongeze sana wananchi wa Tanzania hii na hasa wazazi wa Mkoa wa Mbeya ambao wanajitoa kufa na kupona kujenga shule hizi za Kidato cha Tano na Kidato cha Sita, wanajenga kwa bidii lakini kama tunavyofahamu wanaochaguliwa kuingia katika shule hizi hakika ni wa Kitaifa wanatoka katika maeneo mbalimbali na mimi hili sina tatizo nalo kwa sababu ni mbinu za kujenga Utaifa, ni suala nzuri lakini kwa kuwa shule hizi zinajengwa na wananchi, ni kwa namna gani basi ili tujenge Utaifa huu, ushiriki wa Serikali hapa unakuwa wapi? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kabisa Serikali au Wizara inajitahidi kuchangia kuendesha hayo mabweni, lakini mimi ningeshauri Serikali isaidie pia walau hata uwezekaji *for that matter* wa hizo shughuli kwa kuwa shule ni ya Kitaifa, kwa wananchi wa Rungwe peke yake mathalani au wa Mbozi peke yake, Ileje, peke yao, Mbeya Mjini peke yao si haki. Kwa hiyo, Serikali nayo isaidie walau kujenga haya mabweni, kwa sababu mabweni ni sharti mojawapo la kuanzisha hizi shule za *Form Five* na *Form Six*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala linalofuata ni kuhusu suala la maadili, maadili katika Shule zetu za Sekondari, Shule zetu za Msingi na Vyuo, jamani tukubali maadili yameshuka, sio mazuri kwa wanafunzi wetu. Hivi mmeshawahi kusikia wapi wanafunzi wanatoka wanampiga Mwalimu, mmesikia wapi? Katika historia hakuna lakini hivi sasa mambo haya yanafanyika. Juzi pia nilikuwa nasoma tena mambo mengine ya ajabu, mwananchi wa kawaida anaenda shule amewachapa Walimu, kwa nini mmemchapa mwanangu, hivi kweli, hii ni tabia ya kuporomoka kwa maadili kabisa katika taasisi zetu za elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nishauri kabisa kwamba kuna haja ya kuwa na mchakato mkubwa katika kufundisha watoto wetu maadili na jamii kwa ujumla. Ninajua kabisa ni haki ya kila mwananchi, ni haki ya kila mzazi kumuelimisha mtoto

wake, lakini pia hata jamii ina haki kabisa, inawajibu wa kuelimisha wanafunzi au watoto wa shule, anakaa shule zaidi kuliko anavyoishi na mzazi. Kwa hiyo, unahitaji kujenga maadili mazuri sana kule anakoishi kwa muda mrefu zaidi, huko shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tena kwa uzito kabisa kuwe na nafasi kubwa zaidi ya kufundisha watoto maadili hata huko kwenye mabweni yanakojengwa, kila bweni lilipojengwa na waraka utolewa iwe ni lazima katika kila bweni hapo pembeni ijengwe nyumba ya Mwalimu wa Malezi, awepo pale, huyo kazi yake iwe ni kuhakikisha kwamba wanafunzi wanajengwa katika maadili mazuri na anakaa nao, wako pale shule na wanakaa kwa muda mrefu. Ninaomba sana tena sana hili suala ni bayu, tunapoelekeu ni kubaya sana pamoja na mabadiliko hayo tunayoyaona sijui mabadiliko ya sayansi na teknolojia, *fine*, lakini *role* yetu kama Serikali, role kama jamii lazima tuifanyie kazi kwa hali ya juu sana, maadili yanaporomoka sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nataka kuzungumzia suala la Bodi ya Mikopo. Bodi ya Mikopo, ni nzuri na ina madhumuni mazuri ili kumpunguzia mzazi au mwananchi ule mzigo wa kumuelimisha mtoto. Ninaomba yale makundi ya mikopo yapunguzwe, yako makundi tangu A-K ambapo yanaleta *confusion*. Kuna kundi la wale wanaopata asilimia mia, wale mavu, watoto yatima na wale wanaosomea masomo ya sayansi na kadhalika, *fine hundred percent* wanapewa. Halafu kuna kundi la wanafunzi amba wana uwezo na kundi la watu wasio na uwezo basi yapangwe makundi haya matatu yanatosha, makundi mengi namna hiyo yanaleta *confusion* hata kwa wale amba wanafanya mchanganuo. Wengi wanaona kwamba kuna upendeleo na hata mzazi mwenyewe. Mimi ukinifanyia huu mchakato nitaweza kuelewa lakini mzazi mwingine ukimuelimisha kwamba kuna kundi A, B, C,D sijui K sijui kitu gani, haelewi, basi mtoe elimu ya kutosha ili watu waelewe kwamba hii A, maana yake hivi, B, maana yake hivi mpaka huko K, watu waelewe la sivyo malalamiko ya wananchi ni makubwa wanaona Serikali ni kama haiwasaidii na kumbe dhamira ya Serikali ni nzuri katika kuwasaidia wananchi wake wapate elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sipendi kupigiwa kengele na mimi ni Mwalimu mzuri, naomba kuunga mkono hoja hii ya Waziri wa Elimu, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwalimu Cynthia Ngoye na nikuunge mkono, tabia ya wazazi kwenda kupiga Walimu shulen lazima tuilaani wote kabisa, nakushuru sana Mwalimu.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena kwa mara ya pili, kunipa nafasi ili niweze kuzungumza na kuchangia hoja muhimu ya Wizara ambayo ninaamini ni Wizara nyeti sana kwa maendeleo ya Taifa lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwapongeza waliochaguliwa kugombea nafasi za uongozi wa juu katika nchi hii kutoka vyama vya CCM na CUF. Pili napenda kuchukua fursa hii vilevile kuwashukuru sana akinamama wa CHADEMA, kwa kunichagua kuwa Makamu Mwenyekiti wao Taifa na ninaomba tuendelee kushirikiana

na nawasihi sana tufanye kazi kwa pamoja ili tuweze kuongeza idadi ya Wabunge wanawake pamoja na Madiwani wa CHADEMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa nichangie katika hoja hii. Niwashukuru sana Waziri, Manaibu wake pamoja na watendaji wote wa Wizara hii, kwa kuweza kufanikisha kuleta hotuba hii kwani kama wasingefanya kazi hiyo, tusingeweza kuwa hapa tukichangia hoja hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nichangie katika masuala mbalimbali kwa kuwa najua wengi wameshazungumza. Nizungumzie suala ambalo naamini kabisa kama litawekewa mkakati na Serikali na naamini wanaweza kama kweli wanania, ni suala la Walimu. Tunakubaliana kwamba elimu yoyote ile haiwezi kusonga mbele kama hakuna Mwalimu. Mimi pia kama Mwalimu najua vilevile uwiano wa Mwalimu na mwafunzi ni kitu cha msingi sana. Wote tunajua kwamba tuna wanafunzi lakini tatizo kubwa ni Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitofautiane kabisa na wachangiaji wengi kwamba Tanzania tuna tatizo la Walimu, Tanzania hatuna tatizo la Walimu. Tuna Walimu wengi sana ambao wameshapata mafunzo ya Ualimu lakini tatizo kubwa lililopo ni kwamba Walimu hawa hawajaboreshewa maslahi yao na wala hawana mahali pazuri pa kuishi. Wote tunaelewa kwamba huko tulikotoka Walimu walikuwa watu muhimu sana, walikuwa wanathaminiwa sana, lakini sasa hivi Walimu hawathaminiwi hata kidogo. Walimu wamekuwa ni watu wa kuhangaika, Walimu mishahara yao wamekuwa wakilimbikiziwa, Walimu wamekuwa wakifanya kila kazi na wote tunajua katika uchaguzi Walimu ndiyo wanaofanya kazi. Wote tuliomo humu ndani tunajua hatungeweza kufika hapa bila kuititia kwa Walimu lakini Walimu wameachwa solemba, tunaomba Serikali iwaboreshee maslahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaamini kuwa idadi ya Walimu ni kubwa kwa sababu tukipita katika sehemu mbalimbali kwenye sekta binafsi, Serikalini utakuta Walimu ndiyo watumishi. Kwa hiyo, tunaamini kabisa kwamba tatizo la Walimu kwa idadi wapo isipokuwa tu hawajaboreshewa maslahi yao na kwa maana hiyo Serikali itaendelea kuwasomesha Walimu, lakini Walimu hawa kamwe hawatatosheleza kwa sababu hawataenda kule ambako wanastahili kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la Bodi la Mikopo, wote tunatambua kwamba elimu ya juu ni ya msingi sana, lakini wote tunashuhudia ni jinsi gani kila mwaka wanafunzi wakimiminika Bodi ya Mikopo kudai fedha zao. Wote tunatambua kwamba karibia wanafunzi wote kwa asilimia 100 wanategemea fedha hizo, kwa maana hiyo, kutowapa fedha hizi kwa wakati hatuwatendei haki hata kidogo. Wanafunzi wale wamekuwa wakipoteza muda wao mwangi sana wa masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kibaya zaidi, mimi kama mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, tumejaribu kuongea na wahusika, wao wanadai kwamba majina yanacheleweshwa kutoka katika uongozi wa Vyuo Vikuu kupelekwa kule lakini ukiongea

na viongozi wa Vyuo Vikuu wanasema wao wanapeleka kwa wakati na ukiongea na viongozi wa wanafunzi, nao wanakubaliana na viongozi wa vyuo vyao. Kwa maana hiyo, kuna tatizo kubwa sana. Tunaiomba Serikali kupitia Wizara hii, kwa sababu hawa wote ni wao, wahakikishe kwamba wanakuwa na kikao cha pamoja ili kuhakikisha kwamba tatizo hili au kero ya mikopo kwa wanafunzi inakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kuna suala hilo hilo la Bodi ya Mikopo, kama alivyosema Mheshimiwa Ngoye, kwa kweli haya makundi yanachanganya lakini pamoja na kuchanganya kwake, tunaona kwamba hata posho zile za mafunzo bado pia zipo kwa makundi na ile *special faculty requirement* nayo iko kwa makundi. Mimi binafsi naona kwamba fedha hizo zingetolewa za kufanana kwa sababu wote tunajua wanafunzi hawa wanatoka katika maeneo mbalimbali na wanafanya kazi katika maeneo mbalimbali lakini vilevile fedha hizi za mafunzo basi zingekuwa zinafika kwa wakati ili wanafunzi waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nalotaka kuzungumzia ni suala la *OCs* kwa Vyuo vya Elimu ya Juu. Naomba Waziri atakapofanya majumuisho, atuambie *OCs* katika Vyuo Vikuu zinatolewa kwa vigezo gani, kwa sababu utaona chuo kimoja kimepata kiasi fulani, chuo kingine kiasi fulani ambacho ni kidogo, vinatofautiana kwa mbali sana. Kwa hiyo, tunaomba kujua vigezo, ni wingi wa wanafunzi au ni idadi ya wafanyakazi au ni kitu gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo, nilitaka kuzungumzia suala la fedha za maendeleo. Kama nilivyoongea kwenye hotuba yangu lakini hili ni la ziada kwa kweli, tuna tatizo kubwa sana na fedha hizi za maendeleo. Wote tunatambua umuhimu wa fedha za miradi ya maendeleo kwamba hizi ndizo zinazokarabati, zinazojenga na kadhalika. Lakini ni jambo la kusikitisha sana kuona kwamba baadhi ya vyuo, sitaki kuvitaja lakini baadhi ya vyuo, vimekuwa havipati fedha zao kwa wakati. Kama chuo kinaweza kupata fedha asilimia tano tu mpaka mwezi wa nne, hili ni tatizo kubwa sana. Wote tunajua miundombinu ya vyuo vingi hasa vile vya zamani, ni mibovu mno na wanafunzi wanashindwa kuishi katika mabweni, vyoo havifai kabisa, lakini bado fedha za maendeleo hazijafika. Tunaomba Wizara kwa sababu tunapitisha bajeti hapa, wahakikishe kwamba fedha zile zinaenda kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo ninataka kuchangia ni suala la tangazo la Haki Elimu. Kuna tangazo la Haki Elimu ambalo limekuwa likisema kwamba, ni asilimia moja tu ya nyumba zilizokuwa zimepangwa na Serikali mwaka 2008 zimejengwa. Nakumbuka wiki iliyopita Mheshimiwa Waziri alikanusha. Mimi ninataarifa na *records* za Serikali, tena wala sio nyumba 300, katika taarifa hiyo ya Serikali, naomba kunukuu inasema:-

*"The target for 2007/2008 under this component was to construct five thousand seven thirty two pre-primary class room, ten thousand seven hundred fifty three primary class room and twenty one nine thirty six Teachers houses in rural and remote areas. Providing Teachers with houses is a positive incentive and motivation for retaining them in their working areas. In the year under review, a total of one thousand two thousand*

*and sixty three classrooms were built and two seventy seven Teacher houses were constructed”.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atuambie katika mwaka 2008 walisema wangejenga nyumba hizo 21,936 na wao wenye wakajenga nyumba 277, kwa nini Haki Elimu wanavyosema hivyo Waziri anakanusha? Kwa nini anakanusha wakati taarifa hii inatoka kwenye *Annual Performance Report for the year 2000 ya Wizara ya Elimu na Mafunzo na Ufund*i?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabla kengele haijagongwa, nilitaka kuongelea suala zima la TEHAMA. Suala hili ni la msingi na Mheshimiwa Waziri alilitangaza katika Bunge lako Tukufu mwaka jana wakati wa bajeti na akasema kwamba mpango huo ungeanza mwaka jana na ungesambaa nchi nzima mwaka huu. Lakini mpaka sasa hivi kama kuna shule, nimeambiwa labda ni Azania na shule nyingine mbili. Nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni shule ngapi katika nchi yetu wameweza kufanikisha mpango huu wa TEHAMA na je, hicho ni kipaumbele katika Wizara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimalizie kwa kusema kwamba pensheni ya Wastaafu wa Vyuo vya Elimu ya Juu, kwa kweli inasikitisha, inakatisha tama. Wote tunajua kwamba ma-*Professor* hawa au ma-*Doctor*, wanafanya kazi kwa muda mrefu sana lakini inapofikia kwamba *Professor* anastaafu anapata fedha kidogo kuliko mtu mwenye cheti, hii inakatisha tamaa. Pamoja na kwamba wengi wako katika mfuko wa *PPF* na *PPF* wakasema kwamba hawana fedha lakini jambo la kushangaza kule *PPF* kuna wastaafu sita walistaafu mwaka 2008 wakapata pensheni ya shilingi bilioni 1.2.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITU:** Ahsante sana Mheshimiwa Susan Lyimo kwa mchango wako ila siku nyingine itabidi utoe *conflict of interest*, umenielewa.

*(Hapa Mheshimiwa Susan Lyimo hakujibu chochote)*

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Lakini na mimi naomba niungane na wenzangu katika kukipongeza Chama cha Mapinduzi, kwa kumteua mgombea pekee, Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kuwa mgombea wa Urais wa Tanzania Bara. Niipongeze vilevile Halmashauri Kuu ya CCM, kwa kumteua Mheshimiwa Dr. Shein kuwa Mgombea wa Urais Zanzibar na vilevile kupongeza Halmashauri Kuu ya CCM, kwa kumteua Dr. Mohamed Gharib Bilal kuwa Mgombea Mwenza wa Urais kuitia CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kutoa shukrani zangu kwa kunipa nafasi hii na ninapenda kuipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufund, kwa hotuba waliyoiwasilisha leo na kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kuboresha elimu katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo, nina machache ambayo ninapenda kuyatoa kama mapendekezo au ushauri ukizingatia kuwa sasa hivi tumeboresha sana miundombinu ya elimu ya juu kwa maana ya Vyuo Vikuu. Tumeboresha sana miundombinu ya Elimu ya Msingi lakini kuna pengo ambalo mimi naliona kwenye Shule za Sekondari ambalo nafikiri kuna umuhimu wa kuliziba ili wanafunzi watakaokwenda Vyuo Vikuu tulivyovitayarisha wawe na ubora unaokidhi mahitaji ya soko, ushindani na mahitaji ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninapenda kuzungumzia suala la tabaka ambalo linajitokeza sasa hivi kati ya Shule za Serikali na Shule za Binafsi na ninapenda kushauri au kutoa rai kwa Serikali kuhakikisha kuwa bado usimamizi wa mitaala na ubora unabakia mikononi mwao pamoja na kuwa shule nyingine zitakuwa zinaendeshwa kibinafsi. Natoa mfano wa Uganda au hata Kenya na nchi nyingine za Afrika ambako shule za binafsi na shule za Serikali hazina tofauti kubwa sana kiuwezo na kiubora tofauti na kuwa labda kwenye *extra curriculum activities* na vitu vinginevyo. Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo ninapenda tulione kwa umuhimu wake kwa sababu tayari limeanza kujenga matabaka katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile kuzungumzia suala la Walimu, hili ni jambo ambalo limezungumzwa na karibu kila msemaji aliyejita kuwa Walimu ni tatizo. Tunajenga shule nyingi, tunaboresha Vyuo Vikuu lakini tunahitaji Walimu watakaofikisha wanafunzi hao kwenye vyuo hivi na kwa hali hii, suala la uboreshwaji wa mazingira ya ufundishaji wa Walimu ni muhimu, maslahi yao pamoja na masuala mengine ambayo yatawafanya wawe na motisha zaidi katika kufanya kazi hiyo lakini vilevile mafunzo kwa Walimu ili waendane na utandawazi uliopo sasa. Hili ni suala ambalo ninapenda litiliwe mkazo na kwa hali hiyo ningefurahi kuona kwenye bajeti hilo limepewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusiana na ada zinazotozwa katika shule binafsi. Sijui kama kuna uwezekano wa kuziratibu zaidi kwa sababu hizi ada hazina uwiano. Shule ikiitwa tu *academy* basi inaweka *fee* yoyote inayojitakia na wakati mwingine kuleta matatizo kwa jamii. Ninapenda kuona kuwa Serikali inasimamia suala hili pamoja na kuwa na soko huria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ninapenda kulizungumzia ni kuhusiana na Elimu ya Watu Wazima. Zamani wakati sisi tukisoma, nakumbuka suala la Elimu ya Watu Wazima lilikuwa wazi, linaonekana na mtu akipita mahali popote anajua kabisa kuna vituo vya kufundishia watu wazima lakini tunavyoendelea sasa hivi, tunaona watu wazima wengi zaidi ambaao hawakusoma na wengine ni vijana tunawaita watu wazima tu kwa maana kuwa wamepita ule umri wa kwenda shule za *primary* lakini vijana wengi sana hawajasoma kabisa hata lile Darasa la Kwanza lakini tunaambiwa kuwa kuna Elimu ya watu wazima na hatujui inatolewa vipi kwa watu gani na sehemu zippi. Kwa hiyo, ninapenda kuona kwanza bajeti yenyeimeboreshwa kwa sababu naona bajeti iliyotengwa ni ndogo sana ukilinganisha na uzito wa suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninapenda kuzungumzia suala la watoto yatima hasa wanaoingia katika Shule za Sekondari. Watoto yatima wengi sana wanazumbuliwa katika shule hizi hasa inapofikia wakati wa mitihani kwa kurudishwa kwa sababu hawana ada. Sasa sijui Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia yatima hawa ambao tayari wako shule za sekondari na walikuwa wako kwenye njia nzuri ya kujikwamua kimaisha kwa kusoma vizuri zaidi. Sasa kama watakuwa kila mara masomo yao yanakatishwakatishwa kwa sababu ya ukosefu wa ada basi itakuwa inawakwamisha na wakati mwingine inakuwa ni vigumu kupata hizo ada mpaka wengine wanashindwa kufanya mitihani. Sasa sijui kama ni shule fulani fulani tu au ni sera iliyowekwa kwamba wakishindwa kulipa *school fees* warudishwe nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda vilevile kuzungumzia masuala ya michezo. Michezo ni muhimu katika kujenga akili za wanafunzi lakini vilevile miili na taaluma. Ninapenda kujua kama kuna uwezekano wa kuweka shule ambazo zitakuwa zinachukua wanafunzi wenyе vipaji vyа michezo, wakachanganya na masomo ya kawaida ili baadaye tupate wanamichezo ambaо ni wasomi. Wanamichezo wengi wapo tu, wengine wameshindwa kwenda shule wanaingia kwenye mpira na michezo mingine na sisi tufikie mahali ambapo tutakuwa na wanamichezo wasomi ili waweze kutumia taaluma zao za kisomi lakini vilevile watumie vipaji vyа michezo kujajiri na kuajiri wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa kuchukua muda mwingi sana kwa sababu kengele inakaribia kugonga. Lakini vilevile hili suala la ukosefu au upungufu wa Walimu kuna uwezekano wa kuleta Wakufunzi wa Walimu wetu hapa nchini kama *programme* maalum ili kwa muda mfupi sana tupate Walimu waliofuzu ili waweze kuchukua nafasi na kuziba mapengo ambayo yamejitokeza kwa sababu tayari miundombini ipo tunachohitaji sasa ni rasilimali watu kwa ajili ya kuendeleza elimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Janet Z. Mbene kwa kuniokolea muda, Mheshimiwa Manju S.O. Msambya na Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi atakuwa ni mchangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. MANJU S.O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Awali ya yote, niwapongeze Mheshimiwa Waziri na Manaibu Mawaziri wote, Watendaji Wizarani, mashulen na Wataalamu wote kwenye Vyuo Vikuu vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nichukue fursa hii, kuupongeza uongozi wa Chama cha Mapinduzi, kwa kazi nzuri iliyofanywa wiki iliyopita kuanzia uteuzi wa Dr. Shein kuwa Mgombea wa Urais wa Zanzibar na hitimisho la jana la kumpata Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete na Dr. Ghalib Bilal, kuwa Mgombea Urais na Mgombea Mwenza wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza hayo, nimepitia kwa haraka haraka hotuba ya Mheshimiwa Waziri lakini nianze na ukurasa wa 86 - 87 alipokuwa anazungumzia ukaguzi wa shule. Mimi nadhani ukaguzi wa shule unaanza kwenye Kata,

tunao Waratibu wa Elimu wa Kata ndiyo wangekuwa wakaguzi wa awali, lakini sioni kimsingi hasa ukaguzi unaofanywa na hao Waratibu wa Elimu Kata kwa sababu kwa mfano kwenye Jimbo langu wapo Walimu pamoja na uchache wao ambao hawajishughulishi na kazi ya taaluma yao ya Ualimu, wanafanya biashara na wanaingia madarasani kwa hiari, kwa ridhaa yao wala siyo kwa taratibu za ajira yao. Mratibu wa Elimu Kata yuko pale na ndiye mkaguzi wa awali na hotuba ya Mheshimiwa Waziri inazungumzia kuimarisha, mimi nafikiri uimara ungeanzia pale kwa Mratibu Elimu Kata. Kwa hiyo, ninamwomba Waziri na Wizara kwa ujumla waliangalie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni suala la Bodi ya Huduma za Maktaba. Mimi ninavyoolewa, maktaba ni mahali ambapo wengi wetu tunakwenda kupata taaluma na elimu ya ziada kwa kujisomea nyaraka na majarida pamoja na vitabu mbalimbali vilivyopo pale. Sasa ingekuwa vizuri basi tunapozungumzia maktaba ziwe na jina halisi la maktaba na nitoe mfano wa Mkoa wa Kigoma. Tunacho kijichumba tu cha kusomea, ninaiomba Wizara iangalie na si kwa Kigoma tu bali kwa Mikoa yote tuweke maktaba zenye jina halisi la maktaba siyo vijichumba tu vya mtu kwenda kukaa pale kusoma magazeti tu. Vilevile maktaba hizi zisitolewe au zisijengwe kwa upendeleo kwa baadhi ya maeneo na maeneo mengine tukaweka vyumba kama vile watu wanakwenda kupata kahawa tu, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, limezungumzwa na wengi nalo ni hili suala la Walimu. Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo anasema kwamba Walimu wapo wa kutosha, inawezekana kweli wapo lakini nasema vilevile inawezekana hawapo na kama hawapo basi mgawanyo si mzuri. Walimu wengi wamerundikana mijini na vijijini hakuna Walimu tena Walimu wa ngazi zote tangu Shule za Msingi mpaka Shule za Sekondari na sisi tunaamini msingi ndiyo unaojenga mtu kupata elimu hadi kufikia Chuo Kikuu. Inakuwaje baadhi ya shule mijini unakuta shule ina Walimu 30 lakini vijijini unakuta shule ina Walimu wawili na zote ni Shule za Msingi na hawa wote wako tayari kutahiniwa kwenye mtihani wa Darasa la Saba na matokeo yatachukuliwa sawasawa bila kujali shule moja ina Walimu wawili na nyingine ina Walimu 30? Kwa hiyo, nafikiri na ndiyo ninakuja kwenye ile hoja ya ukaguzi, hivi Mratibu Elimu wa Kata, hapeleki taarifa kwa ngazi zote kujua kwamba huku kuna upungufu wa Walimu ili tuwe na uwiano mzuri wa Walimu? Ni vizuri basi Wizara ikajielekeza kuwa na ukaguzi halisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alipokuwa anatoa hotuba yake ya kufunga mkutano wa Chama cha Mapinduzi, alizungumzia juhudhi ambazo zinafanywa na zitaendelea kufanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuzalisha Walimu takribani 5000 na zaidi kila mwaka. Sasa Walimu hawa wanawenza wakazalishwa kwa wingi lakini wakakaa mijini, kwa hiyo, faida ya kuwazalisha itakuwa haipo. Kwa hiyo, naiomba Wizara iangalie namna ya kuwasambaza Walimu hawa kwenda maeneo yote ili elimu inayotolewa iwe elimu halisi kwa Watanzania wote na isiwe elimu kwa baadhi ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine mimi niipongeze Serikali kwa kuanzisha Chuo Kikuu cha Dodoma na Mwenyekiti wewe ni Mjumbe katika uendeshaji wa chuo hicho. Chuo hiki ni uwekezaji mkubwa sana wa Serikali hapa Dodoma na mimi hapa nitangaze

maslahi binafsi. Mimi nimekuwa namsomesha mtoto wangu pale kwa kumlipia ada, amekosa mkopo na ikabidi nilipe ada na nilalamike hapa, kwanza kijana anahimizwa aliye ada, akichelewa, anakumbushwa haraka lakini ada ikishalipwa, kupewa stakabadhi inakuwa tatizo. Eneo kama Chuo Kikuu, mimi nilitegemea katika idara zote kuna wataalamu wenye uzoefu na ujuzi. Idara ya Uhasibu ikishapokea pesa ni lazima itoe stakabadhi haraka sana lakini anaambiwa kesho kesho na mpaka leo hii ziko baadhi ya stakabadhi ambazo mimi nimempa ada kijana wangu kwenda kulipa na amelipa lakini bado hazijapatikana. Kwa hiyo, naomba Chuo Kikuu cha Dodoma kiishi na kufanya kazi kulingana na hadhi ya chuo chenyewe na hadhi yenyewe inakuja kutokana na ufanisi wa watumishi waliopo katika chuo kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na hayo machache ya kueleza na nimalizie kwa kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Msambya, sasa hilo la *receipts*, si tungeongea tu mzee? Mheshimiwa Mpologomyi atamalizia.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii lakini na mimi naomba niungane na wenzangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuteuliwa kwake kuwa mgombea pekee wa Chama cha Mapinduzi, kwa Uchaguzi Mkuu unaokuja wa mwaka 2010 na yeze kwa kumteua Mheshimiwa Dr. Ghalib Bilal kuwa Mgombesa Mwenza kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. Wote nawapongeza sana. Lakini nampongeza pia Dr. Ally Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa kwake kuwa mgombea pekee wa Urais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Naye nampongeza sana kwa kuchaguliwa kwake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri ambayo amekuwa anaifanya katika Wizara hii na kwa kweli inatia moyo. Kazi ni kubwa, inahitaji ujasiri mkubwa, maamuzi makubwa, si haba, watu wengi wanampongeza na mimi naomba niungane nao kwa kumpongeza sana kwa kazi nzuri anayoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niwapongeze wale Walimu na *Ma-Professor* wote wanaofanya kazi katika Wizara hii kwamba kazi wanayofanya. Ni kazi nzuri na kweli itakuwa na matokeo mazuri siku zizazo. Kazi ni nzuri na mimi naomba muendelee na kufanya kazi hiyo kwa moyo mkunjufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ninaomba niseme hivi, hawa Walimu na *Ma-Professor* tunaowapongeza na Wabunge wamezungumza kwamba ni kweli wanahitaji mazingira yao ya kufanya kazi yaboreshwe. Nitazungumzia Walimu wa *Secondary Schools*, wengi wamesema, mazingira yao kwa kweli ni mabaya, ni vizuri yakaboreshwa. Lakini nizungumzie *pension* ya *Ma-Professor* na Wahadhiri waliopo Chuo Kikuu ambao *pension* yao inalipwa katika mifuko miwili maalum. Mmoja ni mfuko wa *NIC* unaoitwa SSSS. Walimu 62 walioajiriwa kabla ya mwaka 1978 ndiyo wanalipwa kwenye mfuko huu lakini *PPF* pia wapo Walimu walijiriwa baada ya mwaka 1978. Mafao ya uezeni na

malipo yao ya pensheni hutolewa kwa awamu mbili. Awamu moja ni ile ya mkupuo wa mafao yote lakini awamu ya pili ni ile ya *pension* ambayo inalipwa kwa *factor* ya moja chini ya mia tisa na sitini. Hii hulinganishwa na mkupuo 50% unaotolewa na *PSPF* na *LAPF*, *pension factor* ya moja kwa mia tano na arobaini kwa wastaafu wa *PSPF* na *LAPF*. Hivyo, *Professor* wakati wa kustaaafu hupata mkupuo wa kati ya shilingi ishirini milioni mpaka shilingi milioni arobaini tu na Makatibu Wakuu wengi hupata shilingi mia moja na ishirini milioni mpaka mia moja na hamsini milioni. Mstaafu wa *SSSS* hapati *pension*, mstaafu wa *PPF* anapata moja ya nne ya *pension* ya *PSPF* na *LAPF*. Ninaomba atakapokuwa akisimama kujibu hoja zetu, azungumzie jambo hili kinagaubaga kwa ajili ya Walimu, Wahadhiri, *Ma-professor* wa Vyuo Vikuu, kwani tunahitaji maelezo sahihi ambayo yanaweza kuonyesha kwamba kweli tunajali kazi nzuri wanayofanya. Tunapanua Vyuo Vikuu, hatuhitaji watu watoroke bali tunahitaji watu wakae hapa na wafanyie kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shule za Sekondari, ni kweli tumepanua lakini naomba mzikague. Kazi wanayofanya ni nzuri, mimi naipongeza sana lakini nafikiri wamejisahau, wakiambiwa mmekosea hapa hawataki kukubali kwamba hapa tumekosea na nitatoa mfano. Kule kwangu kwenye Jimbo la Kasulu Magharibi ambako nawapongeza sana wapigakura wangu katika Jimbo lile kwa ushirikiano mkubwa walionipa kwa miaka yote kumi na tano niliyokuwa nao, kuna shule moja nimekuwa napata matatizo sana na shule ile kwa muda mrefu na Waziri anafahamu, nimeripoti kwake karibu miaka miwili na amelitolea uamuzi. Mheshimiwa Waziri nakupongeza kwa sababu ulilitolea uamuzi, ukaamua kuwahamisha wale watu waliokuwa wanavuruga shule ile, walivuruga namna gani? Mwalimu aliyekuwa kwenye *Secondary School* hii kama *Head Master* ye ye hakutaka kujali *secular* zilizokuwa zinatolewa na Wizara ya Elimu.

Wizara ya Elimu ilitoa *secular*, na *secular* ile ikaonesha kwamba, ada za mitihani za *Form Four*, *Form Six* na *Form Two* zimefutwa. Yule Mwalimu toka Januari aliendelea kukusanya pesa hizi, anakozipeleka sijui, lakini wanafunzi wakihoji huyu Mwalimu anakuwa mkali, anagombana na wanafunzi, anaona hawana maana. Akajikuta haelewani na wanafunzi pale shulenii. Mimi nilipokwenda pale mwezi wa Mei mwanzoni, nilikuwa nimepata malalamiko mengi sana, lakini nilipofika mkoani nikazungumza na *RAS* na Afisa Elimu, Afisa Elimu akaniambia huyu Mwalimu tunamhamisha pamoja na wale walimu wengine wabovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi hela za ada zinavyokusanya hazina mpangilio, anakusanya Mwalimu ye yote, lakini risiti hawapewi. Wanafunzi akifanya fujo ni viboko na adhabu kali kama kuchimba visiki, mpaka mtoto mmoja mimi nina ushahidi alikuwa anakohoa damu kwa kufanya adhabu kali. Nilipokwenda pale mimi nikawaита viongozi wote wa Kata na Wilayani, Afisa Elimu akaniambia mimi ninakuja na barua za Walimu hao na wanahama. Mimi nikaenda pale nikasema ni kweli wanahama.

Kwa hiyo, ninyi msiwe na hofu wala shaka. Kesho yake waliletewa barua za kuhama pale na nikaambwa mimi ndiye nimefukuza Walimu na nimewatukana. Lakini, ile shule ukiangalia *performance* yake ni zero. Mwalimu yule anatembea mara yuko

Tukuyu, yuko Dar es Salaam, yuko wapi, anachofanya hakuna anayejua. Mara yuko Mwanza, sijui ni biashara gani anaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule ile ilikuwa na wanafunzi 200, wanafunzi 80 walipata *Division III*, wanafunzi 133-150 *failure*. Sasa hili lilikuwa sio jambo la kusherehekeea, lakini juu ya hilo wanafunzi 31 waliokuwa hawakubaliani naye na walikuwa wamesingiziwa makosa fulani fulani wakaambiwa hawa wafukuzwe shule, *thirty one!* Nikawaambia kati ya 31 wako akina Mpologomyi wangapi unaowakuta hapa? Wewe unafukuza wanafunzi 31, hao ni darasa zima, hapa akina Mpologomyi 31 wamefukuzwa shule.

Nilishazungumza na Waziri, na yeye alikuwa amesema hawa wanafunzi warudishwe. Huyu Mwalimu, *how important is she?* Yeye kuamua kufukuza wanafunzi 31 bila kueleza makosa yanayolelewka! Bodi yake ilikuwa imekwishamaliza muda, nikasema hii bodi nayo haikutusaidia sana, lakini kwa sababu ilikuwa imemaliza muda wake wacha iondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ooh, niliandikiwa barua kwamba, huyu bwana anakuja kwenye uchaguzi. Kwa hiyo, tumwangalie sana kwa sababu ametutukana matusi. Uchaguzi ikawa ndiyo hoja na iko barua ya Katibu wa CWT, Mheshimiwa Waziri nitakupatia barua hiyo na ninaomba muifanyie kazi. Huyu Katibu hana maadili, maana maneno aliyoaandika kwenye barua yake hiyo ambayo ameisambaza Wilaya nzima, hayana ukweli ndani yake, ninaomba afanyiwe kazi.

**MBUNBE FULANI:** Anataka usirudi Bungeni.

**MHE. KILONSI M. MPOROGOMYI:** Bungeni nitarudi tu, yeye hawezikunizua. Nitarudi tu na mimi ninawaombea wengine wote mrudi Bungeni, tena kwa kujiамии na nguvu kubwa, kwamba mnarudi wote. Ninawapongeza Wabunge wote mlionanyakazi nzuri majimboni kwenu na mwende kwa kujiамии maana hoja mnazo, sababu mnazo na nia mnayo ya kwenda na kutaka kurudi humu ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Secondary Schools* zetu, pale kwenye *diagram* yako ya mwisho kwa sababu sina muda wa kutosha inatia mashaka. Pale inaonesha kwamba *Secondary School Enrolment at O-Level* ni 14.01%. Ukiangalia wale wanaokwenda *A-Level* ni 0.64%, wale ambao wanakwenda *Teacher Education* ni 0.28% sasa hapa tunapata *one* na 13.11 hajulikani wanakwenda wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *this is a time bomb*. Tunakalia bomu! Wanafunzi wengi namna hiyo ambao hawaendi shule wanamaliza *Secondary Schools* tunawaacha hivi hivi, lazima tuwatafutie nafasi. Najua wanapungua, lakini bado *percentage* inakuwa ni kubwa, lazima tuje na mkakati wa kuhakikisha kwamba, hawa wanafunzi wote

wanaopita Secondary School at least iko mipango ya kuhakikisha kwamba wanasomeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikushukuru sana kwa nafasi hii. Nakupongeza kwa kukalia kitihicho, na ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote. Ahsante sana ninaunga mkono hoja. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. LOLESTIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninatoa pongozi kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya ufundi kwa hotuba nzuri. Pongozi pia ziwaendee Naibu Mawaziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufund. Bila kuwasahau Watumishi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kueleza kero zinazokera wananchi katika sekta ya Elimu katika Jimbo la Busanda. Kero ya kwanza ni upungufu wa Walimu katika Shule za Sekondari. Walimu waliopo katika shule za Nyangusu, Nyaluyeye, Kamena, Butobela, Chigunga na Bukondo ni wachache sana ukilinganisha na Idadi ya Wanafunzi waliopo. Hivyo ninaomba katika Bajeti ya mwaka 2010/2011 uwekwe utaratibu mzuri wa kupata walimu wa kutosha katika shule hizi ili kuboresha elimu ya Sekondari katika Jimbo la Busanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero ya pili ni upungufu wa nyumba za walimu. Shule hizi za Kata zina upungufu wa nyumba za walimu. Sambamba na hilo Shule za Msingi pia zina upungufu wa nyumba za walimu. Ninaomba Serikali iangalie namna ya kujenga nyumba za Walimu ili kuboresha mazingira yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero ya tatu ni madai ya Walimu baada ya kutembelea Jimbo, walimu wengi bado wana madai yao. Pamoja na kutengewa fedha katika Bajeti iliyopita, walimu wengi wa Shule za Msingi bado wana madai yao hivyo ninaomba Serikali ifuatilie suala hili ili kupunguza kero za Watumishi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero ya nne ni kuwepo kwa maboma yaliyojengwa kwa nguvu za Wananchi hadi leo hayajaezekwa. Ninaomba katika Bajeti hii tutenge fedha kwa ajili ya kuezeka maboma ili nguvu za Wananchi zisipotee bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero ya tano ni upungufu wa vifaa vya kufundishia katika Shule zetu za Msingi na Sekondari. Ninaomba Serikali iangalie namna ya kuongeza Bajeti kwa ajili ya manunuzi ya vifaa. Hii itaongeza tija na itaboresha elimu katika shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AME PANDU AME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Manaibu Mawaziri kwa hotuba nzuri walioiwasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ni ufunguo wa Maisha pia ni ufunguo wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naishauri Serikali kuboresha zaidi Sekta hii muhimu ya Elimu, kwa kuongeza mafao na maslahi ya Walimu ili wawe na moyo wa kufundisha vizuri mashulenii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali iangalie ujenzi wa Mabanda ya kusomeshea kwa kuzingatia kwamba katika jamii zetu kuna walemavu wa kila aina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia naishauri izingatie ushauri wangu huu, kwani wenzetu wenyewe ulemavu kwa kweli huwa wanapata shida sana kutokana na ile hali Mwenyezi Mungu alivyo wajalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali idumishe michezo mashulenii watoto wawe na stamina ya kimwili na kiakili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitangulie kumpongeza Waziri, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu, na Watendaji wote kwa maandalizi mazuri ya Hotuba hii ya Bajeti. Nikupongeze wewe na Wizara yako yote kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Sekta ya Elimu. Ni mfano wa kuigwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na madeni ya walimu. Naipongeza Wizara kwa kujitahidi kulipa madeni ya Walimu. Mmelipa madeni, yalikuwa mengi na mengine ya hadi miaka 10 nyuma, lakini kwa kiasi kikubwa mmejitahidi kilipa, hongereni sana. Nashauri Wizara/TAMISEMI kuweka mikakati ya kuhakikisha madeni hayarundikani tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni kuhusu upungufu wa Walimu. Niwapongeze kwa jinsi mnavyojitali kuzalisha/kufundisha/kuandaa walimu. Juzi milisema mna uwezo sasa wa kupeleka walimu watano watano kila shule. Angalizo, mijini walimu ni wengi, wanafundisha vipindi vichache. Lakini shule za vijijini zina upungufu mkubwa zaidi, hadi nyingine zina walimu wawili tu. Nashauri ufanyike utafiti ili kuona upungufu uko wapi zaidi na walimu waelekezwe huko zaidi ili kutatua matatizo makubwa yaliyoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nchi yetu iendelee tunahitaji Sayansi na Teknolojia. Hivyo inabidi watoto tuwaandae na kuwafundisha kwa usahihi masomo ya Hisabati, Sayansi na Kompyuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mitaala yetu inawaandaa wanafunzi kuendelea na masomo hadi Vyuo Vikuu. Hivyo wanaoishia darasa la Saba, *Form IV*, *Form VI* wanashindwa kujitegemea. Inabidi tubadilishe mitaala ili wanafunzi wajifunze masomo yatakayowafanya wajali pindi wamalizapo *STD VII*, *Form IV*, *Form VI* wajifunze Kilimo, Kompyuta, Masomo ya Biashara, Sayansikimu na Ujasiriamali. Ili kama hawaendelei na masomo au Vyuo Vikuu, waweze kujiajiri na kujitengemea.

Mwisho, naunga mkono hoja na Waziri na Manaibu Mawaziri wote nawaombea kwa Mwenyezi Mungu wote muweze wote kurudi Bungeni.

**MHE. FREDERICK M. WEREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri na ninampongeza kwa jinsi alivyoiwasilisha. Pamoja na pongezi ninashauri na kuomba yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, yapo mazingira maalum katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu hasa maeneo ya Tarafa ya Kiagata (Musoma Vijijini) katika vijiji vya Baranga, Wegho, Kongoto, Buswahili, Kwisaro, Kiagata na Kyankoma ambapo Wanafunzi wa kike wanaachishwa masomo kwa sababu ya kupata mimba au kuozwa au kupelekwa katika ukeketaji. Ninashauri kwamba Serikali ijenge mabweni ya watoto wa kike ili kuwaepusha na dhahama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, maeneo hayo hayo ni ya pembezoni. Hayavutii Walimu kufanyakazi huko. Walimu ni wachache mno na uwezo wa Wananchi kujenga nyumba za Walimu ni mdogo kutokana na kutokuwepo kwa mazao ya biashara na upungufu wa mifugo kwa sababu inauzwa ili kulipia *School Fees* na chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni kuwepo uwezekano wa kushirikiana na Askofu wa Musoma kwa ajili ya kujenga shule za awali na Msingi katika Parokia ya kiangata ambako kuna Watawa wa kanisa amba wanaweza kusaidia kufundisha elimu ya awali na ya msingi kwa maadili yanayofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara isaidie kupeleka vifaa vya maabara kwa ajili ya masomo ya Sayansi. Shule za Kata zilizojengwa hazina maabara na vifaa vya maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya ni maeneo ambapo mtoto wa kike anahitaji *intervention* ya haraka. Nina hakika unao uwezo wa kufanya *intervention* hizo na ninakualika utembelee maeneo hayo. Utashangaa utaondoka kwa uchungu na masikitiko makubwa sana.

Kwa mara nyingine, naunga mkono hoja yako.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Naomba nianze kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Profesa Jumanne Maghembe, Naibu Waziri Mwantumu Mahiza, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka pamoja na Wataalam wote wa Wizara Hotuba nzuri na ya kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni ombi kwamba Shule ya Sekondari Milambo katika Mkoa wa Tabora. Kwa kuwa shule ya Milambo ina historia kubwa ya Baba wa Taifa kufundisha katika shule hiyo. Kwa kweli shule hiyo iko katika mazingira magumu ambayo wanafunzi na walimu wanafundisha kwa shida.

Tatizo lake kubwa ni uchakavu wa majengo ya Utawala, Bweni, Jiko na *Dinning Hall* yako katika hali mbaya sana.

- Maji tabu, vyoo viko katika hali mbaya.
- Nyumba za Walimu haziridhishi.
- Upungufu wa walimu kwa baadhi ya masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waratibu Kata. Kutokana na Jiografia ya nchi yetu Waratibu hao hawana nyenzo za kutembelea Mashule kwa wakati, hata wakati wa kaguzi. Nashauri maofisa hao wakopeshwe pikipiki ili wafanye kazi yao kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Profesa Jumanne Maghembe, kwa kuwasilisha hoja yake kwa umakini na ufasaha. Nichukue nafasi hii pia kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na Watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri iliyowezesha kutatua changamoto nyingi za elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Bagamoyo, tumejenga shule saba za Sekondari za Kata. Changamoto yetu kubwa sana ni pamoja na uhaba mkubwa wa Walimu na hasa walimu wa Sayansi. Mfano Shule ya Sekondari Matimbwa haikuwa na mwalimu wa Biolojia wa Kidato cha 3 mwaka mzima 2009. Pia hapakuwa na mwalimu wa Kiswahili katika shule hiyo hiyo, pamoja na kuwa na wasichana wa bweni, hapakuwa na mwalimu wa kike. Changamoto nyingine kubwa ni ukosefu wa maabara, maktaba na vitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Wizara katika mwaka mpya wa fedha 2010/2011 itusaidie kutatua matatizo makubwa ya uhaba wa Walimu, maabara, maktaba na vitabu kwa shule zetu Jimboni Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu Shule zote za Sekondari za Kata ziko mbali na makazi ya watu na kwa bahati mbaya, miundombinu ya usafiri katika meneo hayo ni hafifu sana. Wanafunzi wanapata matatizo makubwa sana ya usafiri kwenda na kurudi toka Shule. Serikali ianze kufikiria namna ya kuboresha huduma ya usafiri wa Wanafunzi ili kuwapunguzia adha hiyo na kuwaongeza ari ya kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia 100.

**MHE. KINGUNGE NGOMBALE-MWIRU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naridhika sana na mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya Elimu katika kipindi cha Ilani yetu ya 2005 hadi 2010. Kazi iliyo mbele yetu ni kuimarisha elimu katika nyanja zote hatua kwa hatua. Hili umelifafanua vizuri katika maelezo yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio haya, kuna changamoto nyeti kwa maendeleo ya nchi yetu ambayo inahusu upungufu wa wataalam wanaohitajika kukidhi malengo ya Dira 2025 upungufu huu unadhihirika katika sekta za Uhandisi, Udaktari na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo wa sura za CCM katika miaka ya 2010 hadi 2020 unalizungumzia jambo hili. Je, una la kufafanua?

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu Mawaziri na Watendaji wa Wizara kwa Hotuba nzuri na utekelezaji mahiri wa mipango yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itengete fedha za kutosha ili tuondokane na aibu kubwa ya watoto wa Shule za Msingi kuketi chini kutokana na ukosefu wa Madawati. Wizara ielekeze mafungu maalum kwenye Serikali za Mitaa ili tulitokomeze kabisa tatizo hili ambalo pia linaathiri ubora wa elimu inayotolewa kwa watoto hawa.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa la upungufu wa madawati jambo ambalo linaleta aibu kwa Taifa kwa wale wasioelewa hali halisi ya Uchumi wa Taifa letu kwani wanadhani ni dharau ya Serikali hasa vyombo vyahabari vinapotoa kwenye vyombo vyao na kukejeli Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa tuamue kuweka kwenye makadirio ya fedha ya Wizara hii kama tulivyoamua kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Sekondari za Kata kote nchini. Kwa kategemea Halmashauri zetu za Manispaa kufanya kazi hii itatuchukua muda mrefu kulimaliza.

Naomba tuamue na tuchukue hatua. Ahsante sana.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri. Kwanza, nashauri uteuzi wa *Form One* ufanyike Wilayani chini ya usimamizi wa *DC*. Pili, Wizara itusaidie kukamilisha Sekondari za Mlongwema, Malibwi na Ubiri ziwe na kidato cha tano kuanzia 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu Wizara itekeleze ahadi yake ijenge Chuo cha Ufundji Lushoto. Jambo la nne, Wilaya ya Lushoto yenye Shule za Msingi 260 na Sekondari za Wananchi 80 inahitaji sana kuwa na Chuo cha Ualimu ngazi ya Cheti na Diploma. Tupate tamko la Mheshimiwa Waziri kuhusu maombi haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa kazi nzito ya kuondoa adui ujinga nchini. Pia nawapongeza kwa Walimu kufanya kazi katika mazingira magumu.

Naomba kutoa ushauri kwa Wizara iweke kipaumbele kwa Sekondari zote kuwa na Maabara pamoja na vifaa vyake. Pili, naomba Wizara izingatie kuondoa tatizo la upungufu wa Walimu katika Shule za Msingi na Shule za Sekondari. Tatu ni kitengo cha Ukaguzi wa Elimu na Waratibu Elimu Kata wapewe nnyenzo (usafiri) wa uhakika.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo langu la Siha naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Profesa Jumanne A. Maghembe, kwa hotuba nzuri ambayo imekuwa na uchambuzi wa kina na kwa hiyo kuwapa Watanzania matumaini ya hali ya juu. Aidha nawapongeza Manaibu Mawaziri wote wawili Mheshimiwa Mahiza na Mheshimiwa Kabaka, kwa kazi nzuri ya kumsaidia Waziri mwenye dhamana na hivyo kuleta ufanisi wa hali ya juu. Ninaomba nikumbushie tatizo la Walimu katika Wilaya ya Siha pamoja na mradi wa maabara katika shule 14 ambazo zimejengwa kwa nguvu za Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hongereni sana naunga mkono hoja.

**MHE. RAJAB HAMAD JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundis kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya ufundis katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Migomo ya Vyuo Vikuu. Serikali ifanye mapitio ya Sheria zake ili iziimarishe ziweze kudhibiti wimbi la migomo ya ovyo ya Wanafunzi wa Vyuo Vikuu. Isifike pahala Serikali ikawa inawaogopa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umakini wa matokeo ya Mitihani. Matokeo ya mitihani ya Kidato cha Sita na Nne mara nyingi huwa na utata na huonyesha upungufu mkubwa. Kuna Wanafunzi hupasi vizuri lakini hupewa pasi za chini na kulazimika kukata rufani. Wanapokata rufaa hushinda na hivyo huonyesha wazi kuwa wameonewa. Kwa nini iwe hivyo?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MASOUD A. SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Nyumba za Walimu Vijijini. Upungufu wa Walimu katika Shule za Vijijini unatokana na kutokuweko kwa nyumba za Walimu. Mazingira ya kazi, hivyo Walimu wanaishi nyumba zisizokidhi hadhi na heshima ya kazi ya Ualimu. Ushari wangu ni kuwa Serikali iandae mazingira ya lazima kujenga nyumba za Walimu mazingira ya kazi na kuepuwa Walimu wanaonyanyaswa na jamii kwa kuibiwa au kupigwa katika mazingira yasio salama kwa kazi ya Ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni ya Walimu. Walimu bado wanadai fedha nyingi zikiwemo za kupandishwa madaraja fedha za likizo na marupurupu mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mishahara ya Walimu ni midogo sana na Mwalimu anaeanza kazi ukishamkata *Income Tax* anabakiwa na fedha chache sana. Ushauri kupandisha mishahara ya Walimu na kutenga fedha maalum kwa Walimu wa mazingira magumu ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mimba za Wanafunzi. Bado tatizo linaongezeka na elimu imekuwa ni ndogo. Serikali ni vyema itoe ufanuzi ni watu wangapi wanaohusika na kuwapa Wanafunzi mimba, wamechukuliwa hatua za kinidhamu kwa kipindi cha mwaka 2006/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inasemaje juu ya tabia ya wazazi wanaopokea kitu kidogo baada ya watoto wao kupewa mimba na kuridhika na rushwa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni kuhusu mafunzo kazini. Uelewa wa Walimu ni vyema ukaendelezwa kwa Walimu kupewa mafunzo yanayoendana na mabadiliko ya mitaala, ili walimu watoe elimu itayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizi wa Mitihani unatia doa Taifa letu, kwani inaonekana nchi yetu baadhi ya watu walio na vyeti vyenye sifa mbali mbali vya viwango vya ufaulu si halali kutokana na baadhi ya Watendaji kutokuwa waaminifu hivyo kulisababishia Taifa kuingia katika tatizo la kushuka kwa kiwango cha elimu kisichoendana na hali halisi ya vyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali kuwa makini sana na udhibiti wa kero hii ambayo imekuwa ikiendelea mara nyingi.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii adimu ya kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Manaibu maziri wa Elimu kwa kazi nzuri ya kusimamia Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuamua Sekta yote ya Elimu kuwekwa Wizara moja ili iwe rahisi ufuatiliji wa Elimu sehemu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya CCM 2010 imetekelzeza vizuri asilimia 99.9%, Shule za Msingi zipo kila kijiji, Sekondari kila Kata, Vyuo Vikuu sasa ni vingi sana, naipongeza sana Serikali ya CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na kejeli kuwa Sekondari za Kata ni Yeboyebo, wote wanaotamka maneno haya walaaniwe na kila mpenda maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujenga shule tayari nina uhakika, walimu wengi watapelekwa katika Sekondari hizi, nawatakia kheri hili jambo litekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ombi moja tu katika Wizara hii, Vijana wengi sasa wanatosoma lakini wanahangaika sana kupata Ajira, naomba wapatiwe Mikopo ili wajitegemee. Ombi langu kwa vijana hao ni Wizara ikishirikiana na Wizara ya Utumishi Kazi na Ajira, iwasaidie Vijana wetu Watanzania kuwawezesha elimu wanayoipata

waitumie Tanzania au hata nchi za nje wakismamiwa na Serikali. Nalisema hili kwa sababu vijana wanapomaliza Vyuo vikuu na vyuo vya Ufundu, wanahangaika sana kupata ajira na mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Wizara ya Elimu ni kusomesha na kutoa Ufundu, lakini Serikali ikijipanga vizuri kuhakikisha vijana hawazagai mitaani bila kuwa na vitu vya kufanya, waanzishiwe vikundi na *Saccos*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaombea Mheshimiwa Waziri Profesa Maghembe, Naibu Waziri Mheshimiwa Gaudentia Kabaka na Naibu Waziri Mheshimiwa Mwantum Mahiza wachaguliwe tena 2010.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kutoa mchango wangu katika hoja ya Bajeti hii iliyopo mbele yetu. Hoja hii ni muhimu na ni usfunguo wa maisha ya Watu duniani kote. Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Maghembe pamoja na Manaibu wake Mheshimiwa Mahiza na Mheshimiwa Kabaka, kwa kazi nzuri wanazozifanya. Kwa kuwa Wizara hii ni muhimu, ni imani yangu kuwa kazi ya kuiongoza ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuchangia upande wa Walimu. Ndugu zetu hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana pamoja na vitendea kazi makazi na maeneo wanayofanya kazi, mabaya na manyanyaso pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa hali ya kusikitisha sana pale tunapoona walimu wananyanyasika na kama kupigwa na Mkuu wa Wilaya, kule Mkoani Kagera. Kama hiyo haitoshi ni hivi karibuni tu katika Mkoa wa Shinyanga Walimu wamepigwa na Sungusungu tena hadharani na kwa taarifa baadhi wakiwa hawajavaa. Hii si busara kabisa huu ni udhalilishaji kwani mukutano wa kijiji, vinauhusiano gani na taaluma. Naomba Serikali idhibiti hali hii, na nitumie nafasi hii kuwataka Wananchi wajue wazi, kama adhabu ya viboko kwa wanafunzi watu au wazazi wanapiga kelele. Je, iweje kwa walimu inaonekana kushamiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi walimu hao mishahara haikidhi haja, makazi yao sio mazuri hata baada ya walimu hao kuwa wachache, na wanafundisha masomo mengi ambayo mengine hawajayasomea, hasa katika Shule za Kata. Mwalimu mmoja kwa vidato vinne. Hii ni hatari sana pia wanahitaji motisha ili kuwatia moyo. Naiomba Serikali iwafikirie zaidi walimu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuongelea suala la walimu ambao wanakwenda kuongeza elimu. Imekua ni jambo ambalo halina tija, kwa baadhi ya Wakurugenzi wa baadhi ya Halmashauri, ambao wanawazuia walimu ambao wametimiza masharti ya waraka wa Serikali, Mwalimu anapomaliza masomo na akapangiwa kazi anatakiwa afundishe kwa miaka miwili ndio aende kusoma tena. Lakini baadhi ya Wakurugenzi huwazuia japo hawatumii mfuko wa Halmashauri, mbaya zaidi Walimu wenyewe wanujuana nani kaja leo na nani alikuja jana. Kuna baadhi ya waliokuja jana

hawana ruhusa ya kwenda kusoma na waliokuja leo wanasomeshwa na Halmashauri. Hii inawafamya baadhi ya walimu kuona kuwa wengine wanapendelewa au kufikiria ni ukabila. Ningependa kujua kama waraka ule wa mwalimu afundishe miaka miwili kama umetenguliwa. Kama umetenguliwa, basi ni bora ukawa ni moja ya ufahamisho kwa walimu wote. Tuwaruhusu walimu waongeze elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kufahamu kuwa ni kwanini baadhi walimu ambao wanapata uhamisho hawalipwi fedha ya usumbufu wakati wa kuhama hii inachangia pia kuwavunja moyo walimu wetu, ambao pia ndio tegemeo la watoto wetu hasa wale wazazi wasiweza kuwapeleka watoto wao shule za kulipia. Walimu ni mwanga wa jamii. Tuwapende walimu na tuwajali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaombea Mungu awafanikishie, na kuwatakieni kheri katika Uchaguzi Mkuu ujao ili mje muiongoze tena Wizara hii ambayo ndiyo tegemeo la Watanzania wote. Mungu awajalie awape wepesi katika Uchaguzi ujao *Inshallah* mtashinda.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuipongeza Wizara hii kwa jitihada kubwa zinazofanywa za kuinua sekta ya elimu hapa nchini, pamoja na hayo pongezi pia kwa kazi nzito iliyofanyika ya kuandaa Bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza sekta hii ya elimu Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekuwa ikitilia mkazo elimu kwa walemvu, pamoja na mpango huu wa kuwaendeleza walemvu kielimu bado maandalizi mazuri hayajafanyika kwa walemvu kwa maeneo ya kujifunzia na vifaa ambavyo vingeweza kuwawezesha kujifunza kwa urahisi wa kuleta ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao mfano wa shule ya watoto wenye mtindio wa akili Wilayani Masasi, Kata ya Lukuledi. Tatizo kubwa sana katika Shule hii ni kwamba majengo yanayotumika ni majengo ambayo yalikuwa ya Wamisionari yakiwa Shule ya Kata kwa miaka mingi sana. Majengo haya ni machakavu sana, yapo katika eneo dogo sana, hakuna eneo ambalo wanaweza kuwa na viwanja vya michezo kwa ujumla ni kama wapo kifungoni kwani shule hii ipo ndani ya shule ya Sekondari Lukuledi ambayo pia ina eneo dogo sana. Ni kwa nini Serikali isiwe na mpango wa haraka wa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule hii ya watoto katika eneo la Shule ya Msingi Lukuledi ambako kuna eneo la kutosha na kitengo hiki cha shule ya watoto wenye mtindio wa akili ipo chini ya shule ya Msingi Lukuledi, hivyo majengo ya shule hii yakijengwa huko itatoa na nafasi kwa shule ya Sekondari Lukuledi kuwa na eneo na majengo ya kutosha, hivyo kuwezesha upanuzi wa majengo ya Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri alione tatizo kubwa na zito wanaloopata watoto hawa na Walimu wao kwa ujumla kwa kuishi katika eneo finyu na katika magofu. Naomba sana ombi langu hili la kujenga majengo mapya ya shule hii yatiliwe mkazo na kupewa kipaumbele ili kuleta ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ujenzi huo naomba uambatane na kuboresha huduma bora na vifaa vya kisasa na vya kutosha kuwawezesha walimu kutenda kazi zao vizuri ili watoe huduma bora zitakazowanufaisha watoto hao kuendelea kupata elimu ya Sekondari na hatimaye Vyuo Vikuu, ili kuwajengea maisha yao ya baadaye yaliyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia Serikali ione umuhimu wa kuwaendeleza Walimu hawa wa vitengo maalum na kuwasomesha walimu wapya ili kuwa na uwiano kati ya watoto na walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nazidi kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri Mheshimiwa Mahiza kwa umahiri mkubwa wa kujibu maswali kwa umakini na ufanisi mkubwa sana, Mwenyezi Mungu awabariki na awajalie katika Uchaguzi Mkuu ujao 2010 waweze kurudi katika nafasi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu unahusu walimu walioajiriwa kwa mkataba kutolipwa. Wameajiriwa Wanafanya kazi lakini hawalipwi kwa kuwa mikataba yao haijarudi toka Wizara ya Utumishi lakini mishahara inaingia Halmashauri.

Naomba ufanuzi Mheshimiwa Waziri. Jimbo la Vunjo wapo.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa hotuba nzuri. Napenda kuchangia mambo mawili yafuatayo:-

Elimu ya Kilimo Shuleni ili kujenga misingi imara ya kuwandaan wanafunzi wetu kutekeleza Dhana nzima ya Kilimo Kwanza, ni vema masomo ya kilimo yafundishwe katika shule za msingi na Sekondari. Utaratibu huu utawaandaa wanafunzi kukipenda kilimo (hasa kilimo cha umwagiliaji) ili hata wanapomaliza masomo yao ya Elimu ya msingi au Sekondari wawe tayari kuitumia elimu waliopata katika kujiajiri mashambani.

Aidha, elimu ya kilimo itawapa mawazo na uelewa mzuri wanapopata maelekezo ya maafisa kilimo katika "mashamba – darasa" wakulima walio na elimu wanafundishika vizuri. Ikiwezekana tuanzishe mitaala ya ufundishaji wa elimu ya umwagiliaji shuleni. Nashauri masomo hayo ya kilimo cha umwagiliaji upimaji ardhi (*Land surveying*) ambayo naamini yanafundishwa kama sehemu ya somo la Jiografia.

Maabara, TANAPA, katika mwaka 2009/2010 waliahidi kupitia KINAPA kusaidia ujenzi wa maabara ya Sayansi na *Pasua High School*. Fedha hizo hazikupatikana shule ikaahidiwa kupata msaada huo mwaka 2010/2011. Naomba KINAPA watekeleze ahadi hiyo kwa kuzingatia umuhimu wa Sayansi katika Elimu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja .

**MHE.DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilikwisha ahidi kwamba muda siyo mrefu itaanza kutoa posho maalum kwa walimu wanaofanya kazi kwenye mazingira magumu. Je! Utaratibu huu utaanza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je! ni walimu wangapi waliokataa kwenda kufundisha au kutoroka toka maeneo yenye mazingira magumu walichukuliwa kisheria hatua zipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je! Mpango wa kuendeleza elimu ya watu wazima mbona haiendelei kama ilivyoanza. Ndiyo kusema hivi sasa hakuna watu wazima wanaotaka kujifunza elimu ya watu wazima?

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri pamoja na Naibu wake wote wawili kwa kazi nzuri wanazozifanya katika maendeleo ya Elimu hapa Tanzania. Baada ya pongezi hizo naomba kuunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia yafuatayo:- Ujengaji wa Bweni kwa wanafunzi wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kuwa maadili ya wanafunzi yanaendelea kuporomoka kutokana na utandawazi uliopo na hauwezi kuzuilita jambo ambalo linaathiri vijana wengi hasa wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo inapelekea wanafunzi wengi waishio nje ya Bweni (Uraiani) wanakumbwa na tatizo la kushawishika na hali iliyopo nje ya shule zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wa kike wanapoishi katika Bweni wanaepukana kwa kiwango kikubwa na hali hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iendelee kwa kasi zaidi ari zaidi na nguvu zaidi kujenga bweni za wanafunzi wa kike ili waepukane na athari zinazowanyemelea wawapo nje ya maeneo ya shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema mabweni ya wanafunzi wa kike yasiwe karibu na mabweni ya watoto wa kiume kwa kuzuia mimba za utotoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wanasaifiri umbali mrefu kufuatilia shule zilizopo mbali njiani wanakumbana na vikwazo vingi hasa vya wanaume waharibifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaondosha kabisa athari hizo kama itaendelea kujenga mabweni ya wanafunzi wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongeza nyingi kwa Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu. Pongezi ziwafikie Mheshimiwa Waziri Prof Jumanne Maghembe na Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote. Hatua kubwa imeonekana katika maendeleo ya mipango yote iliyopangwa kama vile MMES na kadhalika. Shule za msingi nyingi na Sekondari pamoja na vyuo vingi vimejengwa katika Kata, Wilaya, Mikoa mbalimbali. Ninaamini kuwa nguvu uwezo huu utaendelea zaidi baada ya Budget hii kupita. Aidha bado kuna changamoto nyingi zinazokabili Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya kwanza ni kuhusu nyumba za walimu katika maeneo mengi hasa vijijini. Bado ni muhimu nyumba imara zikawepo kwa kujengwa ili kuwawezesha waalimu kutaka kufundisha katika maeneo hayo. Ujenzi wa vyoo bado ni muhimu. Pia somo la usafi lizingatiwe kwa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni Wizara kuhakikisha kuwa Watanzania sasa tuwe na uelewa na utaratibu wa kupenda kutumia *Libraries* (Maktaba). Aidha katika vyuo na shule zote ingefaa kama kungekuwa na Maktaba na kuwepo na vitabu vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni kwamba ufikie wakati sasa wa kupanua mafunzo ya Sayansi zaidi katika eneo la masomo ya Sayansi, katika vyuo vingine ulimwenguni hivi sasa vimeanzisha mafunzo ya *Natural Health Science* hata hapa jirani Afrika Kusini, Taaluma hii ni muhimu sana hasa katika kinga ya tiba ya maradhi na hivyo kupelekeea kupunguza maradhi yanayoweza kuepukwa kama *BP, DIABETES* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni mimba za utotoni, jambo hili limekuwa tishio kubwa sana katika Taifa letu. Pamoja na jitihada za kutafuta mbinu mbali mbali za kukabiliana na hili jambo kubwa sana ni kutoa elimu ya uelewa wa mafunzo na maradhi kwa wanafunzi wote wa kike na wa kiume. Ni muhimu sana kwa Serikali kufikiria kuwa ni mpango kabambe wa kujenga *Hostels* katika kila shule ya Sekondari, mpango huu utasaidia sana katika kupunguza mahusiano ya wasichana na wavulana na wanaume kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa *PASHA* umesaidia sana ingefaa iwapo mradi huu utasambazwa nchini kote. Nashukuru kupata nafasi ya kuwa mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii na Kushirikiana na wafanyakazi wa ngazi mbalimbali wa Wizara hii kila la kheri na kazi njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante sana.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia siku ya leo kuamka nikiwa mzima. Pia, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Jumanne Maghembe na Manaibu wake pamoja na wataalam wake wa Wizara kwa hotuba yao iliyoandikwa kisayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu ni mwanga wa Watanzania kwani ni eneo linalozalisha wataalamu hivyo ni wazi Bajeti ya Wizara ni ndogo jambo ambalo litapelekea Wizara kushindwa kutekeleza majukumu yake, na kusababisha migogoro kwa wafanyakazi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya majengo ya kusomea katika nchi yetu ni ukweli Wizara wakishirikiana na wananchi imejenga shule nyingi. Tatizo sugu ni uhaba wa walimu. Shule za Kata zina upungufu mkubwa wa walimu, jambo ambalo linaonekana ni tatizo lililoshindikana kutatuliwa. Je, Wizara kupitia Bajeti hii ya mwaka 2010 – 2011 itaweza kutatua suala hili? Ukosefu wa maabara mashulenii mwetu, majengo (nyumba za walimu) madarasa ya kusomea pia maslahi ya walimu. Mambo haya ni changamoto kubwa katika Wizara. Naiomba Serikali itueleze hali ya kutatua mambo haya. Uvujaji wa mitihani ni muda mrefu sasa kila ifikapo wakati wa mitihani Wizara hukabiliwa na tatizo hili ambalo linadhoofisha wanafunzi. Nadhani kuna mapungufu katika kitengo cha Baraza la Mitihani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikopo ya Wanafunzi wa Vyuo Vikuu, ongezeko la wanafunzi linaongezeka siku hadi siku kwa vile ongezeko hili ni lazima na ongezeko la mahitaji litaongezeka. Bajeti ya Wizara ni kama hiyo. Je! Wizara imejiandaa vipi kutatua tatizo hili ili wanafunzi wapate haki yao ya kusoma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu inakabiliwa na matatizo mengi. Hivi sasa kuna upungufu mkubwa wa mabweni, vifaa vya sayansi, walimu kwa baadhi ya masomo mashulenii, athari kubwa ni pale Baraza la Mitihani huandaa mtihani kwa kila somo, lakini Mwanafunzi ambaye anategemewa kufanya mtihani huo hajawahi kusomeshwa somo hilo. Je! tunamhukumu mwanafunzi huyu bila ya kumsomesha?

Hata hivyo upungufu wa vitabu mashulenii ni utaratibu gani Wizara imejiwekea katika Baraza la Mitihani na Wizara ili kumtendea haki mwanafunzi huyu ambaye anapewa mtihani bila kusomeshwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo napenda tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake kwa imani yao ya kumpiga vita adui ujinga. Ahsanteni sana.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Nashukuru kwa kunipa nafasi kuchangia kwenye hotuba hii, pili napenda kumpongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo, Manaibu Waziri kwa hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ndiyo msingi mkubwa kwa Taifa lolote lile kwa ustawi wa maendeleo ya uchumi wa nchi mara zote mimi kwangu. Elimu kwanza ingawaje Serikali imesema kilimo kwanza. Tunahitaji kuwa na wananchi wenyewe elimu ili kulima kilimo cha kisasa na elimu hii inapatikana shulenii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Napenda kuwashukuru walimu wote hapa nchini kwa juhudii kubwa licha ya mazingira magumu ya kufundishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba wananchi pamoja na Serikali tumejenga shule nyingi za Sekondari za kata (*Community Secondary School*) tatizo kubwa ambalo linakabili hizi shule ni tatizo la walimu. Shule zetu hazina walimu wa kutosha, shule nyingi zina walimu kati ya wawili hadi watano ni vigumu sana walimu hao kuweza kumudu kuwafundisha wanafunzi.

Kimsingi mwalimu wa *Secondary* ana uwezo wa kufundisha masomo mawili ni ukweli kwamba wanafunzi huwa hawapati elimu ya kutosha. Naishauri Serikali kuajiri walimu wa kutosha ili wanafunzi waweze kupata elimu stahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi zetu za Afrika ya Mashariki zimeanza utaratibu mzuri wa kuwalipia karo wanafunzi napenda kuishukuru Serikali kuwalipia ada wanafunzi wa kidato cha pili, nne na sita. Pamoja na shukrani hizo kuna haja ya Serikali kuchukua jukumu la kuwalipia karo wanafunzi wote Tanzania kama vile Kenya, Uganda, Burundi, wanavyogharimia kulipia karo wanafunzi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu ina Raslimali za kutosha na kama zikitumika vizuri hakuna sababu ya msingi ya Mtanzania kukosa elimu ya *secondary* kwa sababu ya karo, naishauri Serikali kuwalipia karo wanafunzi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masomo ya Sayansi, *MEJ*, hisabati, kiingereza, yatiliwe mkazo zaidi ili tuweze kuingia kwenye ushindani wa soko hasa kwa sasa tulivyoingia soko la pamoja wanafunzi wanapata shida sana kuiongea lugha ya kiingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho kwa ajili ya wanafunzi wa vyuo vikuu haitoshi shilingi 5000/= ni kima cha chini sana na gharama ya maisha imepanda sana. Naishauri Serikali kuwaongeza posho wanafunzi angalau ifikie shilingi elfu kumi kwa siku. Naishauri Serikali kutoa mkopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Vyuo Vikuu wote kila wanafunzi aweze kupata mkopo na kuwa tayari kulipa pale anapopata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema Serikali iwachukue wanafunzi waliofaulu vizuri kuijunga na vyuo vya ualimu ili waweze kupata kutoa elimu stahiki kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya walimu na wananchi wenye umri mkubwa wanarubuni wanafunzi wa kike na kuwapa mimba. Tatizo hili limekuwa kubwa sana, naishauri Serikali kuhakikisha kuwa wanachukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ndio msingi mkubwa wa maendeleo ya jamii yoyote ile hapa duniani na zaidi ya elimu ya Sayansi ndio dunia yetu ya leo imekuwa ni miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kuona elimu ya Sayansi hapa nchini bado ina changamoto nyingi ikiwemo kukosa walimu wa Sayansi wanaotosheleza, ukosefu wa maabara na vijana wengi kutopendelea kusoma masomo ya Sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja Serikali iliangular sana suala hili, kwani bila ya elimu ya Sayansi taifa letu halitakwamuka kutoka hapa lilipo. Ni vizuri kuwepo motisha maalum kwa wanafunzi wale watakaoamua kusoma masomo ya Sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni juhudzi zimejengwa shule nyingi za Sekondari katika Kata, tatizo lililopo ni kuwa shule hizo zina upungufu mkubwa wa waalimu na maabara. Bila ya kuwa na waalimu wa kutosha kwenye shule hizo itafikia wakati wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne katika shule hizo wawe kwenye kiwango kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja Wizara hii sasa kuziimarisha hizi shule ziliopo badala ya kuziongeza nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabili tatizo la walimu katika maeneo ya pembezoni ipo haja Serikali kuangalia uwezekano wa kuweka motisha maalum kwa waalimu watakaosomesha katika maeneo hayo, motisha ya nyumba za walimu kuweko katika maeneo hayo itasaidia sana kuwafanya waalimu wavutiwe kufanya kazi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu iliyoko ni ile inayomfanya msomi aweze kujitegemea anapomaliza masomo yake kuliko kutegemea kuajiriwa. Leo duniani mpira wa miguu ni ajira pia. Je! Wizara ya Elimu imejipanga vipi kwa vijana walioko mashuleneni kuwemo katika michezo hususan mpira wa miguu, Vijana hawa watakaoendelezwa kuanzia shuleneni. Ni dhahiri watakuwa wanamichezo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ni ufunguo wa maisha, msingi wa maendeleo hivyo basi ipo haja kuendeleza elimu kwa ngazi zote ili kupata Taifa lililo bora kwa maslahi ya wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inafanya kazi yake vizuri kuendeleza elimu pamoa na changamoto zinazoikabili katika utendaji wa kazi zake kwa ngazi zote, kuanzia elimu ya Awali, Msingi, Secondary na Vyuo vya Elimu ya Juu (Chuo Vikuu na kadhalika).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoa na changamoto zilizopo lakini bado tatizo la waalimu bado inaikabili Wizara hii, maslahi madogo kwa waalimu bado ni mzigo mzito hivyo ipo haja kuwaendeleza walimu kuwapatia maslahi yaliyo bora kwa lengo la kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado walimu wanakabiliwa na upungufu wa nyumba za kuishi pamoja na mpango wa MMEM na MMES. Lakini lengo la kuwa na nyumba halijafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule nyingi za Kata zimejengwa kwa nguvu za wananchi, lakini bado kuna changamoto za vikalio (madawati) na maabara hivyo kuwafanya watoto wetu wasisome vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukosefu wa maabara kunalipunguzia Taifa kukosa wanasayansi, hivyo ipo haja ya shule zetu kupatiwa maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili watoto wetu wasome katika mazingira mazuri ipo haja ya kuwapatia chakula na mahitaji mengine ili kuwaondolea uchovu watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vya VETA ni msingi mkubwa wa maendeleo kwa watoto wetu. Lazima tuviendeleze vyuo hivyo kwa kuvipatia nyenzo zote zinazohitajika, ili kutoa wahitimu walio bora katika fani hizo mbali mbali zinazofundishwa katika Vyuo vya VETA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vingi nchini vimechakaa hivyo ipo haja sasa kukarabarti miundo mbinu, majengo kwa wakati kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza sana Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara walioshiriki katika maandalizi ya Bajeti hii na kuiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu. Hata hivyo nina mambo machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Ufundi (VETA) katika Bajeti ya wizara hii ya mwaka 2007/2008, Serikali kuititia Wizara hii iliahidi kujenga Chuo cha Ufundi VETA Wilayani Mbozi. Hata nilipofuatilia suala hilo niliambiwa kwamba mipango bado ipo. Sasa nataka kujua kwa hakika. Je! Chuo hicho ambacho Serikali kuititia Wizara hii iliahidi kuwajengea wananchi wa Wilaya ya Mbozi, kitajengwa lini? Na ni sababu gani ambazo zimechelewesha utekelezaji wa ahadi hiyo kwa karibu miaka mitatu sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa shule za Kidato cha Tano, jimbo la Mbozi Mashariki ambalo kwa mujibu wa maeneo mapya ya utawala sasa ni wilaya kamili badala ya jimbo la Mbozi Magharibi ambalo sasa lina jumla ya Shule za Sekondari 39. Kati ya Sekondari hizo shule ya kidato cha tano ni moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na wingi huo wa sekondari za kidato cha kwanza hadi cha nne, zinazokisiwa kuwa na wanafunzi zaidi ya 15000, bado jimbo hili lenye Tarafa nne ni kubwa sana. Hivyo jimbo hili kuwa na Sekondari moja ya Kidato cha Tano ni jambo ambalo haliendi na hali halisi. Sasa nataka kujua ni vigezo gani vinavyotakiwa ili shule ya Kidato cha Tano iweze kujengwa?

Je, Wizara itakubali ombi la wananchi wa Wilaya ya Mbozi ili kila Tarafa (Igamba, Iyula, na Itaka) ijenge shule yake ya Kidato cha Tano? Izingatiwe kwamba katika Tarafa ina wastani wa sekondari kumi, hivyo kuwa na umuhimu wa Sekondari ya Kidato cha Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maabara katika shule za Sekondari, Wilaya ya Mbozi (jimbo la Mashariki) lenye Sekondari 39 lina shule za maabara zisizo zidi tatu, nataka kujua nini mpango wa Serikali wa kujenga maabara katika Sekondai zote Wilayani Mbozi na nchini kote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya shule za Sekondari, ili shule za Sekondari ziweze kufanya kazi zake vizuri zinahitaji kuwa na Bodi na Bodi zilizo imara zaidi na mchanganyiko mzuri wa wajumbe wa Bodi. Hata hivyo hadi leo hii kuna Sekondari nyingi za kata bado hazina Bodi. Je, ni kitu gani kinachelewesha uundwaji wa Bodi za Sekondari hizo.

Je, Serikali haioni kwamba kuchelewesha kuunda Bodi hizo kuna sababisha wakuu wa shule za sekondari wasiwe waaminifu kutumia madaraka yao vibaya kwa sababu hakuna chombo cha kuwasimamia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Bodi ambazo zipo nyingi siyo nzuri, baadhi yake zinaongozwa na watu ambao kiwango chao cha elimu ni cha darasa la saba! Hii inashangaza sana Bodi inayosimamia maendeleo ya Sekondari kuongozwa na mtu wa darasa la saba! Tunategemea nini katika mazingira haya ambayo wakati mwingine hata wajumbe wa Bodi hizi zaidi ya nusu ni wahitimu wa darasa la saba?

Nashauri hali hii irekebishwe maana leo hii wasomi huko vijijini wako wengi sasa. Aidha nashauri wajumbe wa Bodi wateuliwe kutoka Wilaya husika ili kuzipunguzia shule hizo mzigo wa kulipa posho kwa wajumbe kutoka nje ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme katika shule za Sekondari. Zipo shule za Sekondari nyingi (zaidi ya 10) katika jimbo la Mbozi Mashariki ambazo zimejengwa jirani sana (chini ya robo /nusu km) na njia kuu ya umeme (*National Grid*) lakini shule hizo hazina umeme! Sasa nataka kujua.

Je, Serikali kuitisha Umeme bile kuzijali hizo shule ina maana gain. Wizara hii inampoango gain sasa wa kuzipatia shule hizo umeme? Je, pale ambapo wananchi wapo tayari kuchangia gharama za kuingiza umeme shulen i wizara itakuwa tayari kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo, pamoja na ukweli kwamba Bodi inafanya kazi zake vizuri lakini bado kuna kasoro kadha zinazojitokeza sana, nazo ni kama ifuatavyo, moja ucheleweshaji wa mikopo kwa wanafunzi na hivyo kuwafanya wanafunzi kuishi kwa dhiki wakati wakisubiri mikopo yao; naomba hili lirekebishwe , pili bado vijana wanaotoka familia maskini wanapata asilimia ndogo ya mikopo ukilinganisha na baadhi ya watoto wanaotoka familia tajiri na zile za uwezeo wa kati; naomba bodi ifuutilie kwa karibu suala hili, tatu bodi inategemea zaidi taarifa za kwenye

makaratasi taarifa ambazo nyingine zinaweza zisiwe sahihi sana. Naomba bodi pale ambapo waombaji wanakata rufaa ya mikopo yao kwamba ni midogo ukilinganisha na hali za uchumi wa ndugu zao basi bodi ifuatilie ili watanzania hao watendewe haki.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Prof. Jumanne Maghembe, nichukue fursa hii kumpongeza kwa kazi nzuri na kubwa sana ambayo amekuwa akifanya katika sekta hii nyeti ya Elimu. Aidha niwapongeze Manaibu Waziri, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza na Mheshimiwa Gaudensia Kabaka, pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara yake, kwa kazi ambayo kila mtu anaiona. Aidha, nikupongeze kwa hotuba yako nzuri iliyosheheni utekelezaji na mipango endelevu inayokusudiwa katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru kwa niaba ya wananchi wa Kilindi, Wizara yako kwa misaada tuliyopata kutoka Serikalini hususan ukamilishaji wa Ujenzi wa Shule za Sekondari na msingi, ujenzi wa maabara na ujenzi wa mabweni. Aidha msukumo wa kuanzisha Kidato cha Tano na Sita katika shule mbili za Sekondari ambazo ziko katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nia njema ya kuendeleza elimu ya ufundi katika wilaya ya Kilindi tayari eneo limetengwa na tathimini kufanyika. Kwa vile wanafunzi wetu wengi wanapomaliza kidato cha IV wangenufaika na elimu hiyo na kwa vile Halmashauri imekwishafanya maandalizi ya awali basi niombe sana Serikali kupitia Wizara yako mtupe kipaumbele kwani wachache wakipata elimu ya ufundi huweza kuelimisha nguvu kazi iliyopo. Naomba sana mtuangalie kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile mkombozi wa Kilindi ni Elimu na kwa kuzingatia kuwa watumishi wengi hawaripoti kutokana na miundombinu hafifu tuna upungufu mkubwa wa Waalimu na zaidi waalimu wenye sifa. Halmashauri tumetenga eneo, michakato ya awali inaendelea. Naomba sana Wizara yako iweze kutoa ushirikiano ili tukitumia nguvu za wananchi ili kukamilisha chuo hicho. Kwani tukianza kutoa mafunzo ya ualimu hakika maisha bora kwa wananchi wa Kilindi yatakuwa ni hakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimba mashulenii pia zimeshika kasi katika miaka mitatu iliyopita baada ya kusaidiwa ujenzi wa hosteli katika baadhi ya shule, mabadiliko yamekuwa ni makubwa sana, pamoja na jitihada za kutafuta wafadhili na nguvu za wananchi ili tujenge *Hostel* katika shule zilizo nyingi kama si zote. Nichukue fursa hii kuwapongeza kiwanda cha Saruji Tanga, (*Tanga Cement*) kwa kutusaidia ujenzi wa Bweni la wavulana baada ya Halmashauri kujenga bweni la wasichana, bwalo na vyoo, kwa jamii ya wafuagaji ili endapo kiangazi kitatokea na jamii kulazimika kuhama kutafuta malisho basi wanafunzi wasiadhirike. Aidha wafadhili wote nawapongeza hasa wa mafunzo kwa Radio na wengine wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mnyimi wa fadhila endapo sitawapongeza viongozi wa vyuo vikuu vyote kwa kazi ngumu na nzuri wanayofanya. Kipekee niwapongeze viongozi walimu na wafanyakazi wote wa Chuo Kikuu Huria (*OUT*) Prof.

Mbwete, amedhihirisha umahiri wake wa kiutawala na kitaaluma kwa ubunifu wake na ujasiri wakusimamia chuo hiki ambacho kipo nchi nzima na kupanuka siku hadi siku. Nimethibitisha hayo kwa kuwa Mjumbe wa Baraza la *OUT*, na kushiriki katika maamuzi mbalimbali ya chuo hicho.

Aidha, nimpongeze Prof. Mbilinyi kwa uenyekiti wa Baraza hilo na hivi sasa Prof. Wangwe pamoja na wajumbe wote wa Baraza bila kusahau Seneti. Mheshimiwa Waziri niombe chuo hiki kwa vile ni mkombozi wa wananchi walio wengi suala la fedha zinazoombwa lipewe kipaumbele hasa pale ambapo zilishapitishwa kwani linachelewesha utekelezaji wa masuala muhimu ambayo mwisho hupoteza dhana halisi ya chuo hiki. Aidha, malipo ya wanafunzi yatolewe kwa wakati. Ni muhimu pia vituo vya mitihani kuanzishwa katika wilaya mbalimbali ambapo itapunguza adha ya watumishi kuondoka katika vituo vyao vya kazi, kwenda kufanya mitihani. Wilaya ya Kilindi ipo katika ukamilishaji wa kituo hicho, niombe Wizara itupe ushirikiano ili ikamilike mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upungufu wa waalimu kweli ni suala mtambuka ila niombe Wilaya kama Kilindi yenye miundombini inayoanza kujengwa ili kuwapa motisha waalimu hao kwenda kwenye vituo vya kazi. Motisha ndogo utawawezesha kuripoti kama ilivyo katika mikoa ya pembezoni ambapo shule ina wanafunzi 320 mwalimu mmoja. Je, kweli tutatoa hao wa *Division I and II* wanaostahili mikopo? Naomba msaada wenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Dr. Mcharazo wa Maktaba Kuu pamoja na Mama Kizingi na wengine wote wa hapo. Wametupatia sisi Kilindi vitabu zaidi ya elfu mbili, ambavyo vimesambazwa katika shule zetu za Msingi na Sekondari BURE. Naomba wapatiwe fedha wanafanya kazi katika mazingira magumu kinachosaidia ni ubunifu alionao, msaidieni.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto zilizopo, ninapenda kupata maelezo, inawezekana kweli kwamba tunatoa elimu bora, elimu ya Sekondari kwa watoto wetu kama vile Shule ya Sekondari Mwangaza, shule kongwe pale Mpanda yenye wanafunzi zaidi ya 600 kwa Walimu tisa (9) tu, lakini pia shule nyingine nyingi zina uhaba wa Walimu, kama Wizara inaweza kusaidia kupunguza uhaba tulionao wa Walimu wa Sekondari katika Halmashauri ya Mji wa Mpanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Sekondari ya Wasichana Mpanda haina uzio. Zipo jitahada zinazofanywa na uongozi wa Shule, je, sasa Serikali itakuwa tayari kwa kiasi gani kusaidia juhudhi hizo ili Shule ya Wasichana Mpanda ipate hifadhi kwa kuwa na uzio?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kupata mpango na mkakati wa kupanua elimu ya Kidato cha Tano na Sita kwa kuwa tunayo mafanikio makubwa ya ujenzi wa Shule nyingi za Kidato cha Kwanza hadi cha Nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na tatizo la Walimu wapya katika Wilaya ya Nkasi kucheleweshewa malipo yao hadi sasa. Je, kuna mpango gani wa dharura

kunusuru hali hiyo ili Walimu wanaoletwa katika maeneo yenyе mazingira magumu, wasivunjike moyo na ari ya kufanya kazi na hasa mazingira wanayofanyia kazi hawapaswi kukatishwa tamaa kwa kutowalipa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kwa kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa elimu ni ufunguo wa maisha na ni muhimu, kila mtu anahitaji apate elimu ikiwa ni mtoto au mtu mzima, elimu ni lazima wala elimu haina mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu majengo ya shule, ni lazima panapojengwa majengo hayo pajengwe na nyumba za Walimu za kutosha. Ikiwa Mwalimu hana nyumba ya kuishi mahali anapofanya kazi, Mwalimu huyo hawezi kufanya kazi yake vizuri. Mwalimu ni mtu wa kuheshimiwa kwa sababu ndiye anayemwongoa mtu katika maisha yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima Serikali ijenge nyumba za Walimu, mabweni na maabara ili wanafunzi waweze kusoma masomo ya sayansi, kwa sababu tuna upungufu wa wanafunzi wa masomo hayo. Serikali kila siku inatia mkazo kuhusu masomo hayo lakini vifaa hakuna mashulenii na kupelekea wanafunzi kufeli na kuyachukia masomo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana mabweni ya wanafunzi wa kike, inasababisha wanafunzi kukodi na kupanga nyumba na kupelekea wanafunzi kupata mimba bila kutarajia kutokana na matatizo ya kimaisha wanayoyapata wakiwa mitaani na vishawishi vingi wanavyovipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule nyingi zina upungufu wa Walimu hasa vijijini hili ni tatizo. Wanafunzi wengi wanafeli wakiwa wadogo hasa wa Darasa la Saba na watoto hao husafiri kuelekea mijini kufanya kazi za majumbani hasa watoto wa kike na wale watoto wa kiume baadhi yao hujiunga na vikundi vya wavuta unga, vibaka, wezi na wengine hufanya kazi za ajira mbaya na kuhatarisha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wanaofundisha elimu ya sekondari, wanalamika kuwa mishahara yao ni midogo na kushindwa kufundisha vizuri kwa sababu ni lazima ajiunge na ajira ya kujitegemea kama vile kilimo, uvuvi, mifugo na kadhalika ili kukidhi mahitaji yake katika maisha yake. Hivyo, tunaomba mishahara yao iboreshwe ili waweze kuwajibika inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara ya Elimu kwa kazi kubwa wanayofanyia, hasa hasa pongezi hizi kwako Waziri wa Elimu pamoja na Manaibu wako wote wawili, Katibu Mkuu na watendaji wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huu, nawatachia kila kheri. Amina.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kule Jimboni kwangu Musoma Vijijini, wananchi waishio maeneo mbalimbali kama vile Butuguri, Busegwe, wamejenga shule za kisasa kwa nguvu zao wakishirikiana na mimi Mbunge wao na kwa kuwa shule hizo zikiwemo *Chief Ihunyo Girls High School*, Oswald Mang'ombe High School for Boys zilikabidhiwa Serikalini. Kwa kuwa lengo la kuzikabidhi shule hizo Serikalini ilikuwa kuziendeleza kama shule za kufundisha sayansi tu na kwa kuwa baada ya kuzikabidhi shule hizo Serikalini, hakuna chochote kinachofanyika kuzitunza, je, isingekuwa jambo la busara kwa Serikali sasa kuwaambia wananchi na mimi mwenyewe kwamba Serikali haina uwezo kuziendeleza shule hizo ili zikafadhiliwe na madhehebu ya dini ili wazitumie kama ilivyokusudiwa na wahisani walizozijenga na kuzikabidhi Serikalini? Ni jambo la aibu kwa Watanzania na mimi mwenyewe kuona kwamba Serikali imeshindwa hata kuwapa majisafi wasichana wa Chief Ihunyo au kuwajengea uzio (*fence*) kuwalinda wasivamiwe usiku na mafataki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Oswald Mang'ombe, ilikusudiwa iwe *exclusively for science*, nashangaa kuona tayari ufisadi unafanywa na Wizara ya Elimu kupeleka wanafunzi wa Arts ambao hawakutakiwa kwenda pale. Je, kwa nini Waziri wa Elimu, hajaenda kuangalia kulikoni kwenye shule hizo mbili ijapokuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ye ye amezitembelea mara kwa mara? Ni lini Serikali itazipatia shule hizo mbili Walimu wazuri wa Sayansi ili wawaunge mkono wananchi wa maeneo hayo na mimi binafsi. Tulijitolea kwa hali na mali kuzijenga kwa kiwango hicho cha juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Oswald Mang'ombe ina maabara ya kisasa. Cha kushangaza ni kwamba hata '*chemicals*' zinaanza kuharibika kwa kuwa Walimu waliopelekwa kufundisha hapo hawajui kuvitumia vyombo vilivyowekwa kwenye maabara hizo. Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu Shule hizo ambazo ni zawadi kubwa iliyowahi kutolewa na Mtanzania kwa Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ahadi ya Serikali kujenga nyumba za Walimu kwenye shule hizo mbili, hakuna hata nyumba moja iliyojengwa. Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi zake kuhusu shule hizo mbili? Je, ni lini Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi atafika kwenye shule hizo na kujionea mwenyewe hali halisi? Je, ni nini hatma ya shule hizo mbili? Mimi naona Serikali imezitelekeza shule hizo.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Prof. Maghembe pamoja na Manaibu Mawaziri wote wawili na Katibu Mkuu na watendaji/wakurugenzi wote. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakipongeza Chama cha Mapinduzi, kwa kutoa maelekezo ya kujenga Shule ya Sekondari katika kila Kata. Maelekezo hayo yametuokoa sisi watu wa Singida kwani tumeweza kujenga shule mbili kila Kata na katika Jimbo

tumetoka Sekondari nne hadi sasa tuna Sekondari 33. Tunashukuru Serikali hasa Mkuu wa Mkoa wa Singida na wananchi wenyewe waliochangia ujenzi wa shule hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo, kwanza, ni uhaba wa Walimu na hasa Walimu wa Sayansi. Pili, uhaba wa maabara jambo ambalo linaathiri masomo ya Sayansi. Ukosefu wa maabara unachangia sana wanafunzi kutofanya vizuri katika mtihani na tatu upungufu mkubwa wa nyumba za Walimu. Naomba upungufu huu ufanyiwe kazi ili sisi wananchi wa Singida tupige hatua ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri katika awamu ijayo ya Serikali mpya baada ya uchaguzi, elimu ya lazima iwe hadi Darasa la 12 na ada ya Shs.20,000/= ionndolewe kwani bado ni kikwazo kwa baadhi ya wazazi ambaa hawana uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Sekondari ya Mgungila iwe Sekondari ya *boarding* hasa kwa wasichana. Naomba Wizara ishirikiane na Mkuu wa Mkoa ili kufanikisha suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu tumefungua shule mbili za sekondari kwa Kidato cha Tano na sita, yaani Sekondari ya Ikungi na Iliongero. Tuna nia ya kila Tarafa iwe na *High School*. Hivyo, naomba Wizara itusaidie kufanikisha hilo hasa wataalam wa maabara na nyumba za Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu na watendaji, kwa hotuba hii. Mchango wangu katika bajeti hii uko katika maeneo yafuatayo. Kwanza, upungufu wa Walimu. Wilaya ya Bukombe inao upungufu mkubwa sana wa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari. Hata hivyo, wanaopangwa kuja Bukombe hawaji kuripoti. Kupitia Wizara, imetusaidia nafasi za vijana kuijunga na Vyuo vya Ualimu hasa Daraja la IIIA.

Naomba Serikali itusaidie vijana wanaotoka Bukombe waliohitimu May, 2010 Daraja la IIIA warejeshwe Bukombe. Orodha ya vijana hao wapato 101 tayari nilishamwandikia Mheshimiwa Naibu Waziri kuomba warejeshwe. Naamini mkiwareejesha pamoja na mgawo mwingine, tutapunguza tatizo la upungufu wa Walimu. Kuhusu Walimu wa Sekondari, upungufu nao ni mkubwa sana, naomba Serikali iendelee kuwakumbuka Bukombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, VETA, naomba Serikali iharakishwe ujenzi wa Chuo cha Ufundı kwani Wilaya inalo hitaji kubwa sana kutokana na Sekondari nyingi zilizojengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, maabara. Wananchi wa Bukombe, Halmashauri kwa kushirikiana na Serikali Kuu, tumefanikiwa kujenga maabara nyumba 69 katika sekondari 23 na tayari nyumba 32 vya maabara vimekamilika. Naomba Serikali ipeleke vifaa vya maabara katika vyumba hivyo ili kuwatia moyo wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, nyumba za Walimu. Pamoja na juhudhi ambazo Serikali imefanya, naomba tuongezewe bajeti ili Walimu wapate makazi bora na kuwashawishi wakubali kuja Bukombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, *generator*. Serikali ilitupatia jenerata mwaka 2006 ambayo tuliikabidhi Sekondari ya Runzewe. Kwa kipindi chote hiki Sekondari hawajaweza kuitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Serikali imejitahidi sana kuboresha elimu katika Wilaya ya Bukombe, naomba msonge mbele. Hata hivyo, Mheshimiwa Waziri anapohitimisha, naomba awahakikishie wananchi wa Bukombe masuala yafuatayo:-

- (a) Wanavyuo waliomaliza Daraja la IIIA 2010 wanaotoka Bukombe mtawarejesha kama nilivyoomba?
- (b) Maabara za Bukombe ambazo Mheshimiwa Waziri aliahidi kutupatia vifaa na Mheshimiwa Rais anajua suala hili, ni lini mtatupatia vifaa?
- (c) Jenereta iliyoko Runzewe kwa kuwa ni kubwa kwa nini Wizara isitoe kibali ili washirikiane na Kituo cha Afya, Polisi na Sekondari kuiendesha kuliko inavyokaa hivyo muda wote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana hotuba ya bajeti ya Wizara hii. Ni hotuba nzuri inayoonesha matumaini ya kutatua baadhi ya kero zinazoikabili Wizara hii. Naipa pole Wizara hii katika kipindi cha mpito cha kuhamisha Kurugenzi ya Sekondari kutoka Serikali Kuu kwenda TAMISEMI. Nafahamu hakikuwa kipindi rahisi na chenye changamoto nyingi. Ninaamini kipindi hicho kimepita na watumishi wa Wizara ya Elimu kuanza kuizoea hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninatumaini kuwa Walimu na watendaji wote wa Kurugenzi ya Sekondari, wamepokelewa vyema TAMISEMI na kuwa wamekwishaanza kupazoea. Ombi langu ni kuwa kipindi kile kimepita, muda hautusibiri na nchi yetu ni moja tu, hatuna mahali pengine pa kwenda. Sasa tuangalie mbele, tufanye kazi tena kwa nguvu zetu zote. Ninaunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, napenda nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dr. J. M. Kikwete, kwa kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi kuwa mgombea wa Urais kwa Chama hicho katika uchaguzi ujao. Ninamtakia kheri na ushindi wa kishindo katika uchaguzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kumteua Dr. Bilal, kuwa Mgombea Mwenza. Timu hiyo ni nzuri na ni ya ushindi. Hongera sana. Kuchaguliwa na Mheshimiwa Dr. Shein kugombea nafasi ya Urais Zanzibar, ni hatua nyingine ya kupongezwa. Uteuzi huo ni wa afya njema kwa Pemba na Unguja na ni wa faraja kubwa kwa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hotuba hii, sina marefu, nina maombi matatu yanayohusu Jimbo langu. Kwanza, ni mafao ya watumishi waliostaafu muda mrefu na hajapata mafao yao. Mmoja ni Mstaafu Charles P. Mamoni, alistaafu tarehe 30.6.2009, check number 5508567, EDPF.622. Alikuwa Mkuu wa Shule ya Sekondari Ngudu. Hajapata mafao yake kwa kuwa kuna mgogoro wa kiwango kilichokuwa kikiwasilishwa na Wizara *PSPF*, Wizara ina taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni ombi la gari. Mwamashimba ni Shule ya Wasichana “A” Level na “O” Level. Iko Kilomita 80 kutoka Makao Mkuu ya Wilaya na Kilomita 100 kutoka Mkoani. Nimefikisha maombi ya gari mara kadhaa Wizarani. Nimekuwa nikiahidiwa mara nyingi, je, shule hiyo itapata gari lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, naomba kupatiwa taarifa ya maendeleo ya ujenzi wa Chuo cha Ufundı Kwimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yanayofanywa na Wizara hii ni mazuri, ninashauri ufuatao:-

(i) Wizara iongeze juhudzi za kuandaa Walimu. Fedha nyingi ziende kwenye mafunzo ya Walimu. Lengo liwe ni kuwa na Walimu wa kutosha katika shule zetu kwa muda mfupi izekanavyo.

(ii) Maslahi na mazingira ya Walimu na shule zetu ziendelee kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la mwisho, ni Shule ya Sekondari Nyamilama ikubaliwe kuwa ya Kidato cha Tano na Sita. Inakidhi vigezo vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali pitia maelezo ya vijana wa *UDOM* niliyoyaambatanisha wanateseka sana, wanahitaji msaada wa Wizara haraka.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya na kushiriki katika kikao cha leo cha Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ni ufunguo wa maisha. Elimu ndiyo inayomwezesha mwanadamu kupambana na mazingira yake kiuchumi, kisiasa na kijamii. Serikali inahakikisha vipi kwamba elimu inayotolewa nchini inamwezesha Mtanzania katika kukabiliana na sekta za kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo kwa madarasa ya kutosha katika mashule mengi hapa nchini, ni hatua moja muhimu lakini kuwapo kwa Walimu wa kutosha ni hatua nyingine muhimu zaidi. Serikali inatoa tamko gani kuhusu kujitosheleza kwa Walimu wenye sifa zinazotakiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wanajifunza na kufahamu zaidi pale wanaposhirki katika masomo kwa vitendo hususan masomo ya sayansi. Serikali

imejiandaa vipi ili kuhakikisha mashule yote ya sekondari yanapata maabara yenge vifaa kamili vinavyohitajika kwa masomo hayo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mipango gani itakayohakikisha kwamba wanafunzi wanapata vifaa vya kusomea na kujifunza kuanzia ngazi ya Msingi, Sekondari hadi Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Mwalimu aweze kufanya kazi yake vizuri na kwa ufanisi, anahitaji maslahi bora pamoja na makazi bora. Serikali inasema nini kuhusu uboreshaji wa maslahi pamoja na maakazi ya Walimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi walemvu wanasoma katika mazingira magumu. Serikali ina mpango gani wa kuboresha mazingira ili wanafunzi walemvu walio wengi waweze kufikia Sekondari na Vyuo Vikuu badala ya kuishia Elimu ya Msingi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho ya chakula na malazi kwa wanafunzi wa elimu ya juu, ni ndogo mno kiasi kwamba hailingani na gharama za maisha. Baadhi ya wanafunzi wanazimika kulala nje ya vyuo vyao kutokana na uchache wa vyumba vya kulala jambo ambalo linaleta usumbufu kwa wanafunzi hao, Serikali inaiboreshaje hali hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani maalum wa kukomesha tatizo la vyeti vingi vya kughushi pamoja na udanganyifu katika mitihani kuanzia Msingi hadi Vyuo Vikuu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani wa kuzipatia umeme shule za sekondari?

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Prof. Jumanne A. Maghembe, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wao wote ambao kwa namna moja ama nyingine wametoa mchango wao katika kufanikisha utayarishaji wa bajeti hii. Hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kupitia kijitabu hiki cha Ofisi ya Waziri Mkuu kinachonesha mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Nne kwa kipindi cha Desemba, 2005 – Mei, 2010, kwa Mawizara mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sehemu ya Elimu, inasema, nanukuu:-

*“Madai ya Walimu 19,861 yenye thamani ya Shs. Bilioni 25.1 yalihakikiwa ambapo jumla ya madeni yenye thamani ya Shs. Bilioni 12.6 yamelipwa”.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri ile bakaa ya Shs. Bilioni 13.5 zilizosalia zitalipwa lini au hazistahili kulipwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye Baraza la Mitihani. Kuna utaratibu unaotumika na wanafunzi kulalamika baada ya kusahihishwa mitihani yao na kufeli kukata rufaa na kulpia Shs.20,000/= kwa kila somo moja ili asahihishiwe upya na bahati wanafunzi wengine wanabahatika kufaulu. Sasa inakuwaje hali hii inatokea wakati watu waliochaguliwa kusahihisha mitihani ni wasomi au wataalamu? Je, inakuwaje kwa mwanafunzi aliyefelishwa na hana uwezo wa kukata rufaa? Kwa wale Walimu waliofanya makosa ya kuwafelisha wanafunzi na wao wanachukuliwa hatua gani baada ya wanafunzi kufaulu kwa kusahihishiwa na mtu mwingine na kufaulu?

**MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu pamoja na watendaji wote, kwa hotuba nzuri yenyewe kueleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mazuri yote yaliyofanywa, pamoja na maendeleo yaliyopatikana katika Wizara hii lakini kuna mengine ambayo yanatakiwa kufanywa ili tupige hatua. Kama vile kumalizwa majengo ya Shule za Sekondari za Kata, kupatikana nyenzo, kama vile madawati, vitabu, vifaa vya maabara, Walimu na kadhalika. Pia elimu kwa watu wenye ulemavu iboreshwe zaidi, Walimu waongezwe, wataalamu waongezwe, vifaa vya kujimudu na kusomea viongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Patandi ambacho kinatoa mafunzo ya Walimu kwa ajili ya watu wenye ulemavu, nacho kiimarishe zaidi, nacho kimetupwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kama tunavyojua ulemavu upo wa aina nyingi, kama vile viziwi, wasioona bado Wizara hawajawatambua na kuwashughulikia, kwa hiyo, naomba iwatambue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Vyuo vya VETA vijengwe kwa haraka kwenye Mikoa ambayo havipo, kwani vinasaidia vijana wetu na watu wenye ulemavu na wao wapelekwe kwenye vyuo hivyo, navyo vitawasaidia ili waweze kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majengo yaimarishe ili walemau na wao waweze kuyatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia kila la kheri.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Prof. Maghembe (Mb), Waziri mwenye dhamana, niwapongeze pia Mheshimiwa Mwantumu Mahiza (Mb), Naibu Waziri na Mheshimiwa Gaudentia Kabaka (Mb), Naibu Waziri. Nimpongeze pia Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudzi za Serikali za kuongeza bajeti ya Wizara hii mwaka hadi mwaka, ni nzuri sana, ni juhudzi ambazo zina lengo la kujenga Taifa imara lenye uelewa wa wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule za Msingi, Serikali ione umuhimu wa kupandisha kiwango cha kumhudumia mwanafunzi mmoja kwa gharama ya vifaa na kadhalika. Viwango vya sasa ni vidogo na mara nyingi hucheleweshwa kufika mashulenii na hivyo kulazimu Walimu Wakuu kutumia fedha zao mifukoni na hivyo kuleta usumbu wakati wa kudai marejesho yao waliyokopeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua hii, naomba Serikali kuharakisha kupeleka fedha kwa ajili ya kuunga mkono juhudi za wananchi juu ya ujenzi pale wanapoanzisha ujenzi wa maboma. Mara nyingi maboma haya hubaki yamesimama kwa muda mrefu bila kukamilishwa kusubiri fedha kutoka mfuko wa Serikali Kuu kuunga mkono juhudi hiso.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwalimu Mwantumu Mahiza (Mb), aliyetembelea Jimbo la Iramba Magharibi mwaka 2007 na kutembelea Shule ya Msingi Ndurumo iliyopo Kata ya Kidaru. Mheshimiwa Naibu Waziri alitoa ahadi kusaidia ujenzi wa madarasa mawili ahadi hiyo hadi sasa haijatekelezwa. Pamoja na juhudi zangu za kumfuta Mheshimiwa Naibu Waziri mara kwa mara hakuna kilichotekelizwa. Naomba Mheshimiwa Prof. Maghembe, anipe majibu juu ya ahadi hiyo maana napata usumbu wa Kijiji cha Ndurumo, vinginevyo naomba nielezwe kama ahadi hiyo ilikuwa ni kiini macho? Naomba majibu ya kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Walimu Shule za Msingi na Sekondari, naomba mgawo wa kutosha Jimbo la Iramba Magharibi ambayo sasa ni Wilaya inayojitegemea baada ya kuanzishwa Wilaya mpya ya Mkalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika, udhibiti uwekiwe kudhibiti Walimu watoro ambao mara nyingi hawatekelezi wajibu wao ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara pia itoe msukomo juu ya uanzishwaji wa Shule Kidato cha Tano na Sita (*High Schools*) kwa Shule za Lulumba, Shelui, Kizaga na Urughu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ikubali kuendelea kuwatumia Walimu Wataafu kwa mkataba maalumu hasa kwa nyakati hizi ambapo tunazo Shule nyingi mpya za Sekondari za Kata na zile za Msingi.

Kadhalika katika suala la Walimu Wastaafu, ni vema pale wanapokaribia kustaa fu nyaraka zao ziandaliwe mapema na kuwasilishwa Utumishi na Hazina ili wapate mafao yao kwa muda mwafaka. Mara nyingi Walimu wamekutwa na matatizo ya usumbu kufuutilia mafao yao mara wanapostaafu kwa uzembe unaosababishwa na watumishi wa Wizara ya Elimu katika Halmashauri nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Ufundu cha Songela kilichoanzishwa maeneo ya Kizaga, Kata ya Ulemo, Jimbo la Iramba Magharibi, Wizara inatoa misukumo gani katika kukiendezea Chuo hiki ili kitoe mafunzo kwa ufanisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuomba Mheshimiwa Waziri, Prof. Maghembe ahakikishe ahadi ya Ndurumo Shule ya Msingi, inakamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono hoja hii baada ya majibu.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake, kwa hotuba nzuri ya bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuongelea suala moja tu la maktaba. Waingereza wana msemo “*A good leader is a good reader*”, yaani kiongozi mzuri ni msomaji mzuri. Kwa Tanzania, msemo huu haujashika kasi kwani utamaduni wa kusoma vitabu hakuna. Nasisitiza kuhusu vitabu kwa kuwa Watanzania wengi ni wasomaji wazuri wa magazeti, hasa ya udaku. Hivyo fikra zetu kwa kiasi kikubwa zinajengwa “kiudaku-udaku” tu. Tuna safari ndefu kujenga utamaduni wa kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kuwa bila kujenga utamaduni wa kusoma, hatuwezi kushindana vema kiuchumi, kisiasa na kijamii na wenzetu ndani ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na Umoja wa Afrika. Utamaduni wa kusoma hauji tu hivi hivi, unajengwa, unalelewa vizuri na kuwezeshwa. Nyenzo kuu ya kwanza katika kujenga utamaduni huu ni maktaba. Bila maktaba za kutosha nchini na zenye vitabu muafaka si rahisi kujenga utamaduni huu. Tumeweza kujenga shule za sekondari za kutosha lakini karibu zote hazina maktaba. Tuna Wilaya zaidi ya 132 sasa lakini karibu zote hazina maktaba za umma. Hii ni dosari kubwa katika maendeleo ya Taifa letu. Upo umuhimu kwa Wizara kutenga fedha mahsus kwa ajili ya ujenzi wa maktaba katika kila Shule ya Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo upo umuhimu mkubwa kwa Serikali kuiongezea fedha Maktaba Kuu ya Taifa ambayo pamoja na ufinyu wa bajeti yake, imechangia sana kuboresha usomaji wa vitabu vyta kiada na ziada katika shule zetu changa za sekondari. Nachukua fursa hii kumpongeza sana, Dr. Ali Mcharazo, kwa kazi nzuri anayoifanya na taasisi yake (Maktaba ya Taifa) kuzipatia vitabu shule mpya za sekondari bila ubaguzi. Taasisi hii ikiwezeshwa, itafanya makubwa zaidi.

Mheshimia Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Naipongeza Serikali ya CCM kwa utekelezaji mzuri na bora katika uwanja wa elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu imekuwa ikiongezewa bajeti mwaka hadi mwaka hasa katika bajeti hizi mbili mfululizo zimeipendelea sana. Kwa kuwa fedha hizi zilizo nyingi zinateremshwa ngazi za Serikali za Mitaa kwenye Shule za Msingi na Sekondari, nashauri ufuutiliaji uwepo ili zitumike vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira magumu kati ya Wizara zenyenye mtandao mkubwa ni pamoja na Wizara hii. Kuna maeneo ambayo yako nyuma kimaendeleo au mazingira yake ni hatarishi kama vile karibu na mbuga za wanyama na visiwani. Watumishi hawa wanajitao zaidi ya wenza. Kwa kuwa Serikali kupitia TAMISEMI imetusaidia kwa kuwajengea nyumba, ninaloomba, kuwepo na *special fund* wanayolipwa moja kwa moja watumishi hawa, hata kama si sehemu ya mshahara lakini walipwe maana wanaoathirika ni mtu na mtu si wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali sasa ione uwezekano wa kutenga fungu maalum na la kipekee kwa ajili ya Vyuo Vikuu mfano Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho mimi ni mjambe wa Baraza la Chuo. Tumekuwa tukipokea matatizo inayopata menejimenti ya Chuo hicho kutokana na fedha zao kuwekwa pamoja na fedha za Wizara kiujumla. Ninashauri, kwa kuwa sasa, mikopo ya wanafunzi ya Vyuo Vikuu itakuwa na fungu lake, basi pia Vyuo Vikuu viwe na fungu lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali katika zoezi zima la ujenzi na urekebishaji wa Elimu ya Sekondari, iwe ni pamoja na kuzingatia Serikali Kuu kutokwepa watoto wetu kupata walau mlo mmoja wa kutwa wanapokuwa shule. Suala zima la watoto kushinda na njaa, ni tatizo kubwa la kiafya na kitaaluma maana mtoto mwenye njaa hawezo kufuatilia vizuri masomo. Pia njaa ni chanzo cha ukosefu wa maadili kwa watoto kuwa omboomba na wakati mwingine kukutana na vishawishi vyta kuijingiza kwenye ngono wakiwa watoto na hivyo kukabiliwa na mimba za utotoni, magonjwa ya ngono na kupoteza mwelekeo wa maisha yao kama wangelihitimu mafunzo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga tena mkono hoja.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nakutakia kila la kheri Waziri na Manaibu Waziri, kwa kazi nzuri mnayoifanya katika kufanikisha shughuli za Wizara pamoja na matatizo lukuki yanayoizingira Wizara yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza sana na ninakushukuru sana kwa kuipatia gari Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Sumve. Kwa niaba ya Walimu na wanafunzi, tunaishukuru sana Wizara kwa kutekeleza ahadi yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa nchini kote kila Kata ina Shule ya Sekondari zinazoanzishwa/zilizoanzishwa na wananchi. Katika Wilaya ya Kwimba, nayo inazo sekondari ambapo wapo vijana wanaofaulu kuendelea na Kidato cha Tano na kadhalika. Kwa wale wanaoshindwa kuendelea na masomo, Serikali iliweka utaratibu wa kila Wilaya angalau kuwe na Chuo cha Ufundji (VETA).

Wilaya ya Kwimba katika bajeti zilizopita ilipangwa kujengwa kwa Chuo cha VETA ambapo eneo tayari lilishatengwa, wataalamu toka VETA walishafika na kuangalia eneo na waliridhika. Je, ni lini kazi ya ujenzi wa Chuo cha VETA Kwimba itaanza ili vijana wetu wanaomaliza Elimu ya Msingi, Sekondari na kadhalika waweze kuijunga na mafunzo ya ufundi ili wamalizapo hapo waende kujiajiri? Vyuo vyta VETA nchini ni vyta

muhimu sana hasa kwa kipindi hiki cha mapinduzi ya uchumi. Tunavihitaji vyuo hivyo ili kuongeza ujuzi kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na upungufu mkubwa wa Walimu uliopo, naomba Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari katika Wilaya ya Kwimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia. Napenda kumpongeza Msemaji Mkuu wa Upinzani kwa hotuba yake ambayo imefanyiwa utafiti wa kina, ni mategemeo yangu Serikali itayachukua na kuyatumia maoni hayo ili kuboresha changamoto zinazozikabili Wizara hii. Aidha, napenda kuipongeza Wizara kwa kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya nchi yoyote ni lazima yaendane na Serikali kuhakikisha wananchi wake wanapata elimu ili kuwaondoa ujinga. Njia mojawapo ya kupata elimu ni kuwepo na walimu wa kutosha, vitendea kazi, vitabu, maabara na kadhalika. Naishukuru Serikali kwa kupitia hotuba ya Waziri, Serikali itaongeza walimu wa kutosha katika mashule. Pamoja na hilo walimu bila kupata nyumba nzuri za kuishi hawawezi kufundisha vizuri na hata wakipangiwa huko kwa kutokuwepo nyumba za wakuu hao na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, Serikali ihakikishe kabla ya kuwapangia walimu kwenda haswa vijijini wahakikishiwe kuwa nyumba za walimu zipo kwao pamoja na familia zao. Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha kuwa nyumba za walimu za kutosha kutokana na idadi ya walimu watakaohitimu na mahitaji ya kila mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha, inaonekana kama Serikali inakurupuka kujenga shule za sekondari wakati kukiwepo na mipango mizuri kila mkoa ingetakiwa kujua ni watoto wangapi waliozaliwa mwaka fulani na baada ya miaka saba wataingia shule ya msingi wangapi, baada ya miaka saba wataingia sekondari wangapi. Hii ingerahisisha kutayarisha walimu, majengo na kadhalika. La sivyo tatizo la upungufu wa walimu litazidi kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Serikali ni kujenga Vyuo vya VETA kila Wilaya kama hili likifanikiwa ingeongeza ajira nyangi kwa vijana wetu. Lakini naona hili ni suala la kisiasa tu, vyuo vilivyopo bado havijatekelezwa kwa kisingizio cha Serikali kukosa kushindwa kutoa mchango wake wa shilingi bilioni nane. Ni jambo la aibu ukizingatia kuwa vyanzo vingi tu vya kupata fedha zetu za ndani. Naishauri Serikali ipitie hotuba ya Msemaji Mkuu wa Upinzani kwa Wizara ya Fedha waone ni wapi wangeweza kupata fedha za ndani bila kusubiri wafadhili. Tukisimamia tu vizuri na kuongeza mishahara au kuhakikisha madini yanapewa au yanaongezewa thamani hapa nchini. Zipo fedha nyangi tu za kutosha kujenga vyuo vya VETA kila Wilaya nchi nzima. Tatizo ni mpangilio wa vipaumbele vya Serikali.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Ushauri wangu kwa Wizara hii muhimu ni:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Ualimu, Kabanga ni cha siku nyingi takriban miaka 28 sasa, bado kufanyiwa upanuzi na ukarabati, ni ajabu kabisa Wizara au Serikali kusahau taasisi hii muhimu. Aidha, chuo hakina gari la chuo kwa miaka mingi. Ni lini Wizara itapeleka gari Chuo cha Kabanga na ni lini chuo hiki kitapanuliwa na kufanyiwa ukarabati mkubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, usaizidi kwa mikoa iliyobaki nyuma kielimu siku nyingi, mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara ya Elimu ilitoa pesa kwa mikoa minne ilioachwa nyuma kielimu kwa sababu mbalimbali, sababu nyingi ni za kihistoria na utawala. Mikoa hiyo ni pamoja na Kigoma.

(a) Kwa nini utaratibu huu ulisitishwa ni dhahili utaratibu huu ulisaidia angalau kuweka usawa (*Equalization*) kwa mikoa hiyo iliyokuwa imeachwa nyuma?

(b) Kwa nini mikoa sasa isiongezewe fedha hasa katika ujenzi wa maabara ya sayansi, nyumba za walimu na vifaa vya kufundishia. (*Slitly over and above the allocated funds*).

(c) Kwa Mkoa wa Kigoma kwa nini Chuo cha Elimu kilichopo Kasulu kisifanywe chuo kikuu kishiriki kama ilivyo Mkwawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba mkubwa wa walimu wa shule za msingi na sekondari, Mkoa wa Kigoma na hususan Wilaya ya Kasulu, tunalo tatizo la uhaba wa walimu. Baadhi ya walimu wakipangwa kuja Kigoma na Kasulu wanashindwa kufika kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na miundombinu duni katika shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini shule au mikoa iliyopo pembezoni kama Kigoma, Rukwa, Lindi na Mtwara isipewe *special preference* ili kusaidia walimu kubaki katika mikoa hiyo! Ushauri kwa Wizara au Serikali ni kwamba, itoe motisha maalum kwa walimu wanapangiwa katika maeneo hayo ya Mikoa ya pembezoni na hasa Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Elimu Sekondari katika Halmashauri ya Wilaya zote, Wizara kuleta au kuteua maafisa hawa ni hatua nzuri. Hata hivyo, *SEC DEO* wapewe vitendea kazi kama vile magari madogo aina ya Suzuki kama ilivyo kwa maofisa wa TAKUKURU Wilayani. Haiwezekani kabisa maafisa hawa kuachwa hivi walivyo. Aidha, ofisi hizi za Maafisa Elimu hawa ziboreshwani ziongezwe, rasilimali watu ikiwa ni pamoja na *computers*. Gharama za Suzuki ni ndogo na Wizara inaweza pamoja na *TAMISEMI*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika Moshi, (*MUCCOBS*). Kwa kuwa, chuo hiki kinajipanga kuwa chuo kikuu kamili, nashauri *strongly* fedha zake zote zilizotengwa kwa 2010/2011 zipelekwe bila ucheleweshaji na bila upungufu. Hii itasaidia sana azma ya chuo hiki kuwa kamili ifikapo 2014, zaidi ya

hayo *OC* inayopangwa ifike kwa wakati na fedha za maendeleo zipelekwe kwa wakati muafaka ili majengo yaliyopangwwa yatekelezwe kikamilifu.

Wizara pamoja na *SUA* wasimamie kwa karibu mchakato huu wa chuo hiki kuwa *University* kamili kwa kipindi tajwa. Azma hii ipewe kipaumbele na Wizara yako na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MATHIAS M. CHIKAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natamka kwanza kuwa naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya elimu ni moja ya sekta muhimu sana hapa nchini, hakuna nchi yoyote duniani ambayo imeendelea bila kuzingatia elimu. Elimu ni msingi wa maendeleo, nasi tumezingatia hili na kuwekeza vizuri katika sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nachingwea kama zilivyo Wilaya nyingi katika Mikoa inayoitwa ya Pembezoni ina tatizo na shida ya uhaba mkubwa wa walimu. Shule tunazo za kutosheleza za msingi na za sekondari, lakini kuna uhaba mkubwa wa walimu kama ilivyo kwa wataalam wengine ambao ndiyo hasa *agents of change!* Pamoja na uhaba wa walimu, upo pia uhaba wa vitabu maabara na vifaa muhimu vya kufundishia. Naomba Wizara itoe kipaumbele kwa Wilaya ya Nachingwea na sehemu zingine za pembezoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Elimu ya Juu. *UDOM* ni mfano wa kuigwa nchini na katika ukanda huu wa Afrika, lakini pamoja na mafanikio haya, ipo changamoto ya walimu katika Elimu ya Juu. Umri wa kustaafu wa maprofesa inafaa uongezwe na kufikia miaka 70. Profesa wa umri huo anakuwa amebobeaa na ni *authority* katika fani yake, wazo hili lifikiriwe na kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na kuweza kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake ukurasa wa 23, Mheshimiwa Waziri ameelleza kuwa kazi za msingi zinazofanywa na Vyuo Vikuu ni kufanya utafiti unaolenga katika kuinua maisha ya wananchi, nataka kuelewa ni kwa vipi tafiti hizo zinasaidia maisha ya Watanzania na ilihali maisha ya wananchi wengi ni duni sana hasa huko vijijini. Je, Serikali inao mpango gani ya kuzitumia tafiti hizo kuinua hali ya uchumi wa wakulima wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania sote tunajua umuhimu wa vyuo vya *VETA* kwani ni tegemeo la kuzalisha ajira za vijana wetu. Kwa hivyo, ni jambo la busara kama

Serikali itakuwa na mikakati madhubuti ya kunyanya hali ya vyuo vya VETA kwa kuvipatia mahitaji yake zikiwemo fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hadi sasa bado idadi ya wanafunzi wa kike wanaochukua masomo ya sayansi ni ndogo sana. Je, Serikali inao mpango gani wa muda mfupi na mrefu wa kuhakikisha kwamba idadi ya wanafunzi wa kike wanaochukua masomo ya sayansi inaongezeka maradufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la walimu nchini bado halifuatiliwi hasa katika kupatiwa maslahi yao kwa ujumla. Hili limebainika kuwa kero kubwa hapa nchini, malalamiko yamekuwa mengi mwaka hadi mwaka. Serikali ituambie hivi ni jinsi gani itakabiliana na kero za walimu na hivyo kutoweka kabisa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine katika Wizara hii ya Elimu ni lile la mimba za wanafunzi wakiwepo masomoni, kwa kuwa tatizo hili limekuwepo kwa muda mrefu, sasa natambua kwamba zipo taratibu na mipango ya kukabiliana na hili lakini naomba kufahamu, je, Serikali inayo mipango na mikakati gani madhubuti na inayotekelzeza ya kupambana na kero hii na hivyo kuondoka kabisa hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kupata nafasi hii kabla ya yote, nimpongeze Mheshimiwa Spika kwa jinsi anavyoliongoza Bunge. Kwa niaba ya wananchi wa Misungwi tunakuombea kwa Mungu uendelee na moyo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nimpongeze Waziri, Manaibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na wasaidizi wake wote, wamekuwa mstari wa mbele kusikiliza shida za Wabunge pamoja na kukumbwa na matatizo mengi ambayo yanakuwa na ugumu wa ufumbuzi kwa sababu ya bajeti kuwa ndogo. Hata hivyo, bado usimamizi wao ni wa kupongezwa. Nawapongenza hongereni sana, nyinyi na watendaji wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi nzuri, ninayo matatizo ambayo ni vyema nikapata ufanuzi, Idara ya Ukaguzi wa Shule, imesahaulika kwa muda mrefu japo Serikali imeliona hilo na kuanza kuwapatia vitendea kazi. Mfano, Wilaya ya Misungwi imepata gari nzuri sana. Tatizo ni mafuta ya kuendeshea shughuli za ukaguzi, OC hawajapata inayoendana na kazi, je, Waziri umejipanga vipi kwa kero hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la madeni ya walimu bado ni tatizo. Baada ya uhakiki wapo walimu hawakulipwa wakati walishiriki katika zoezi la uhakiki wa madeni yao, wengine wamelipwa na baadhi bado. Jambo hili bado ni tatizo, nini suluhisho la kero hiyo? Taarifa ziko Wizarani, tunaomba majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Elimu ya Sekondari ni muhimu sana, utekelezaji wa sera, lakini tatizo ni walimu, nini mkakati wa upungufu wa walimu katika

shule za sekondari ngazi zote form I na IV na V na VI? Tatizo ni kubwa, hii ni pamoja na maabara, maktaba, nyumba za walimu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Elimu ya Ualimu ni muhimu sana katika kuwapata walimu na ili uwapate ni vyema uwe na vyuo vya kutosha vyenye vitendea kazi vinavyotakiwa. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza vyuo vya ualimu ukiondoa vilivyopo ambavyo kwa sasa vimezidiwa na wingi wa wanachuo wanaotaka kujiunga? Utakubaliana nami kuwa kusomesha mwalimu katika chuo cha mtu binafsi ni gharama kubwa ambayo mwananchi wa kawaida hataweza. Au ni kiasi gani cha ruzuku ambayo Serikali huchangia katika vyuo vya ualimu vya binafsi na wanatakiwa watoze shilingi ngapi maana kwa sasa ni kati ya 800,000 na 1,200,000.

Bodi ya Mikopo ni mkombozi, cha msingi ongezeni bajeti ili Mfuko uwafikie wengi. Naupongeza kwa jinsi unavyowahudumia Watanzania, nina mfano wa watoto wa wananchi wa kawaida wa Misungwi wamesaidiwa na Mfuko huu. Wito wangu, tuzingatie masharti yaliyowekwa na bodi. Pia bodi iendelee kukusanya madeni ili wengine wafaidi mkopo na mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja mia kwa mia. Naomba bajeti hii ipite.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu za uteuzi wa wajumbe wa Bodi za Shule za Sekondari zinawapa wakuu wa shule uwezo wa kuteua wajumbe wa bodi hizo wanavyotaka wao. Nashauri majina ya wapendekezwa kwa shule za sekondari yapitishwe na Kamati ya Elimu ya Halmashauri na kabla ya hapo yapitiwe na *WDC* ndipo yaende mkoani, tatizo hili ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wanaomalaiza *form IV* wenye *Point 26, 27 na 28* sasa hawachukuliwi na vyuo vya ualimu vya sekondari kwa kukosa sifa. Kwa kuwa upungufu wa walimu wa shule za msingi ni mkubwa mno na baadhi ya vijana hawa wanajitolea kufundisha katika shule zetu na wanafaa, Serikali inasema nini kuhusu jambo hili? Je, kwa nini Serikali isiwasadie vijana hao kuwapeleka katika vyuo binafsi kwa vile viro vingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Je, Vigezo vinavyotumiwa sasa kuchagua wadahili ni vipi? Naomba Mheshimiwa Waziri afafanue jambo hili kwa kuwa litasaidia wengi kujua kama wana sifa ama la.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya mtihani wa darasa la saba yanaonesha kuwa shule zenye walimu wachache (3 -5) zinafelisha zaidi ya zile zenye waalimu wa kutosha. Je, Serikali hajagundua kuwa pamoja na upungufu wa walimu kuna tatizo la kupanga zaidi walimu katika baadhi ya shule hasa za mijini. Kutokana na upungufu wa walimu kwa kustaafuli, vifo na kuacha kazi, Serikali iliwatangazia walimu wastaafu na wakaomba kufundisha kwa mkatuba. Je, ni kwa nini Wizara ya Elimu hajashughulikia maombi hayo hadi leo? Je, watajibowi lini barua zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo, je, ni kwanini *UDOM*, hawajapta *title deed* hadi leo?, fedha za *OC* wanazopewa ndogo sana ikilinganishwa na ukubwa wa chuo hicho? Deni la Bilioni nane kwa nini Serikali hailipi? Lengo la Serikali ni *UDOM* kudahili wanafunzi 40,000 by 2012. lengo hili halitafikiwa hata ifikapo 2015. Je, Serikali inalijua hilo? Tunajipangaje kutekeleza lengo hilo kwa haraka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za sekondari hazina vitabu hasa za Kata, kuna mpango gani wa kupeleka vitabu vya kujifunzia na kufundishia mashulenii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *UDOM*, lipo tatizo la kupatikana *lecturers* wa kiwango kinachohitajika kwa vyuo vikuu katika soko la ajira hapa nchini. Serikali imejipangaje kwa vile upungufu huo unazuia malengo ya kuongeza udahili katika vyuo vyetu vya umma. Lipo tatizo *UDOM* la namna ya kushughulikia maji safi na hasa majitaka, kwa jamii ya *UDOM* inayotarajiwa kuwa laki moja (walimu, familia zao, watumishi chuoni, wafanyabiashara na kadhalika) panahitajika mabwawa makubwa ya majitaka na mifereji ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mpango wa kujenga *teaching hospital* katika shule ya tiba ya *UDOM*. Jukumu la kufundisha Waganga na Manesi kutafiti, kutibu na kutoa ushauri wa kitaalam panahitajika hospital ya kiwango cha rufaa. Je, Serikali imejipangaje kujenga hospital ya Rufaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mkataba ya dhamana ya Serikali liishe ili mashirika yanayojenga *UDOM* yaendelee kufanya hivyo. Je, kuna mpango gani wa kuwapandisha madaraja na kuwalipa mishahara walimu waliokwenda kujiedeleza na kusoma Digrii ya ualimu ambao walajiriwa wakiwa na Diploma? Mbona malalamiko ya kada hii ni makubwa sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. SALIM YUSUF MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha katika Bunge hili leo tukiwa katika hali uzima na Usalama. NaKUshukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa kuliongoza Bunge letu kwa viwango vya aina yake. Nawashukuru Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri, pamoja bna wataalam wao na wafanyakazi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu ni mionganii mwa Wizara mama na ni Wizara ambayo siku zote inahitaji msaada wa nguvu za Serikali kwani inazalisha matunda ambayo kwa macho hayaonekani kwani ni fedha taslimu lakini ni rasilimali ambayo ni kichocheo pekee kwa maendeleo ya nchi. Hivyo, pamoja na kuwa inaendelea kuongezewa bajeti yake lakini bado haijatosha kulingana na changamoto nyingi zinazoikabili Wizara kwa mfano, nchi inao upungufu wa walimu karibu asilimia arobaini, hii ni hatari kwani kutookana na ongezeko la wanafunzi kila mwaka lisilolingana na upatikanaji wa walimu litazidi kuwa changamoto kubwa kwa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto hiyo Wizara haina budi kuandaa mikakati madhubuti kuhakikisha tatizo hilo linatakiwa kwa haraka ili ilingane na idadi ya walimu kwa wanafunzi, katika kukabiliana na hili ni vyema Wizara ijinipange upya na kuhakikisha matumizi mazuri ya fedha zinazopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wanafunzi wengi kulala nje ya vyuo ni tatizo kubwa, mazingira ya maeneo ya vyuo ni tofauti sana na yale ya nje ya vyuo hivyo. Matokeo ni kuwa kwa kiasi Fulani wanavyuo hao hupata vishawishi vya kila aina na kwa hivyo husababisha hata chanzo cha migomo kwani huenda wakapata watu wa wakatia fitina kwao na kutokana na maslahi duni waliyonayo wakafuata mkondo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilione hilo na kulitafakari vyema na kuweza kulipatia ufumbuzi.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundsi kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri pamoja na Katibu Mkuu. Kazi hii imejidhihirisha katika uboreshaji wa elimu kuanzia ngazi za awali, msingi, sekondari, vyuo vya elimu na vyuo vikuu. Jambo hili limethibitisha matumizi mazuri ya bajeti ambayo imekuwa ikitolewa kwa kuzingatia kipaumbele cha elimu katika nchi yetu, kimsingi ongezeko la wahitimu wa mafunzo ya ualimu ambalo limepelekea Serikali kupanga kupeleka walimu watano katika kila shule ya sekondari litatoa matumizi makubwa kwa wananchi wa Tanzania katika mafanikio ya elimu.

Nalo ongezeko la vyuo vikuu kikiwemo Chuo Kikuu cha Dodoma ni dalili kwamba nchi yetu iko mbioni katika kujitosheleza na wataalam wa fani mbalimbali ambao watatoa mchango mkubwa katika kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania endapo watatumika vizuri, hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri na timu yake yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mazuri mengi yaliyofanyika ningeiomba Wizara izingatie sana changamoto zilizojitokeza za watoto wale mavu na wale ambao wako katika mazingira hararishi kukosa elimu katika ngazi mbalimbali. Ushauri wangu ni kwamba, Serikali iwatumie watendaji wa Mitaa na Kata pamoja na Maafisa Maendeleo ya jamii ili kupata takwimu sahihi za watoto wa aina hii walikosa elimu, sababu zilizosababisha pia kujua mahitaji yao ya lazima katika kuhakikisha wanawezeshwa kupata elimu ya ngazi husika.

Baada ya kupata takwimu hizi Serikali iwatengee bajeti kwa kuzingatia mahitaji yao. Pendekezo la pili ambalo pia nadhani lingeweza kusaidia ni kuongeza shule za watoto wenye ulemavu hasa wasioona, *albino* na viziwi ili walimu kwa ajili ya makundi haya pamoja na vifaa viweze kutumika kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la uhaba wa walimu katika Mikoa ya Pembezoni, napenda kuishauri Serikali ipitie mikakati iliyowekwa na hiyo mikoa kisha iwasaidie kutatua vikwazo vianvyokwamisha mikakati hiyo. Pale ambapo tatizo ni ukosefu wa huduma katika maeneo husika ni vyema Serikali (Wizara) ishirikiane na Wizara husika kwa mfano, Maji, Afya, Nishati na Miundombinu ili maeneo haya yawekewe umuhimu katika vipaumbele vya Wizara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kumwomba Waziri wa Elimu afuatilie suala la mgogoro wa ardhı ambao umesababisha kusitishwa ujenzi wa shule za sekondari katika Kata ya reli mkoani Mtwara. Mgogoro huu kati ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara na TBA. Madhara ya mgogoro huu kwanza ni kusitishwa ujenzi wa shule.

Pili, kukosa eneo la kujenga maabara na kusababisha fedha za kujenga maabara zikae katika akaunti kwa zaidi ya miezi sita sasa. Tatu, kuwakatisha tamaa wananchi. Nne, kubomoa majengo yaliyopo ili kujenga maghorofa ambapo matokeo yake ni hasara ya fedha za TASAF ambazo zilitumika kujenga majengo yaliyopo na tano ni kuchelewesha maendeleo ya elimu kwani Halmashauri haina uwezo wa kujenga maghorofa kwa sasa kwa ajili ya madarasa na maabara. Hivyo basi, namwomba Mheshimiwa Waziri afanye kikao na viongozi wa Manispaa ya Mtwara viongozi wa Wizara ya Miundombinu pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Mtwara ili kushauriana zaidi na kupata ufumbuzi wa haraka, hili linawezekana kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. KHADIJA S. AL-QASSMY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kumshukuru *Subhana Wataala* kwa ukarimu wake wa kunipa afya na nguvu za kuweza kushika kalamu kuchangia hoja hii iliyokuwa mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri, Manaibu na watendaji wote wa Wizara walioandaa hotuba hii na leo hii inawasilishwa mbele ya Bunge lako. Vile vile naipongeza sana hotuba ya msomaji wa Kambi ya Upinzani jinsi ilivyopangwa kwa ufasaha mzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nitakuwa sikuwatendea haki kama sijawapongeza kwa kazi zenu nzuri na jinsi mnavyoliongoza Bunge hili kwa umahiri mkubwa na viwango vya uhakika. Mwenyezi Mungu akuongozeni ili mzidishe uadilifu. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa mchango wangu naiomba Serikali iongeze bajeti ya Wizara hii kwani nchi hii ni kubwa na changamoto zake ni nyingi. Pamoja na mkazo wa Serikali kwa kuipa kipaumbele Wizara hii lakini bado haijakidhi mahitaji. Bado walimu ni kidogo sana katika shule na kusababisha wanafunzi wengi kupata elimu ambayo haina kiwango cha kutosha, kwani wanafunzi wanaomaliza elimu

ya msingi, hata ya juu, basi ni aibu kama ukilinganisha na wanafunzi wa Afrika Mashariki ambao elimu zao zina kiwango kizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijue kama tumeingia katika ushirikiano wa nchi za Afrika Mashariki na kitu ambacho kitatupa maendeleo na ushindani mkubwa ni elimu. Sasa hali hii iliyokuwapo sasa, itatufanya sisi tusiendelee kwenye soko hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ukosefu wa walimu na ukosefu wa walimu, watoto au wanafunzi wengi wanakuwa mapocco na kusababisha watu wasiopendelea nchi kuiba mitihani na kuiiza na kuwasababishia wanafunzi wengi kufutiwa mitihani. Nadhani kama kweli Wizara hii itakuwa *serious* basi mambo yatakuwa mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na upungufu wa walimu vile vile vitendea kazi kama maabara, madawati, vitabu, vyote hivi ni muhimu sana kiasi kwamba wanafunzi wanasoma kinadharia zaidi kiasi kwamba wanakosa masomo ambayo ni muhimu sana. Walimu wanashindwa kupenda kazi zao kutokana na kutokupata mafao yao kwa uhakika na kupata nyumba nzuri za kuishi na kuifanya fani kudharauliwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mimba mashulen. Naiomba Serikali iwachukulie hatua kali ili mwingine aogope kufanya kitendo kibaya hicho na kuwakosesha masomo watoto wa kike na kuwafanya wanawake wengi wakose elimu ya juu na kubakia nyuma na maisha yao kuwa duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nawapongeza Waziri na Manaibu Waziri kwa hotuba nzuri. Pia nawapongeza Katibu Mkuu na watendaji wote kwa ujumla wao. Mchango wangu leo utagusa zaidi kwa upande wa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuongelea upungufu wa walimu wa elimu maalum. Ili kuondoa hili tatizo ni vema somo hili lisomwe na kila mwali muhimo anayesomea ualimu, hii itasadia sana kuondoa tatizo hili, naomba wakati Waziri anajibu anieleweshe endapo hili linawezekana.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kuhusu mazingira ya shule za bweni zenyé watoto wenye ulemavu. Tatizo kubwa ni kwamba mabweni yapanuliwe na pia zijengwe *hostel* kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Miundombinu iboreshwe kwa ajili yao kwani majengo mengi ya shule hawazingatii miundombinu kwa ajili ya walefavu, vyoo vipewe kipaumbele. Uzio kwenye shule hizo ni muhimu sana kwa ajili ya usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia kuhusu huduma muhimu kwa watu wenye ulemavu. Je, kwenye mipango ya Halmashauri mbona hawaingizwi, mara nyingi wamekuwa wakitegemea wahisani zaidi. Halmashauri zishirikiane na Wizara ya Elimu kuhusu hizo huduma muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu inahusika zaidi na *Quality Control* ambapo wakaguzi wanaoshughulikia elimu iwe na viwango. Mitihani, sera na mafunzo wakati ambapo TAMISEMI ni *Management* na *Administration*. Ombi langu ni kwamba, ruzuku ya Serikali iongezwe kwenye Halmashauri ili huduma muhimu za watu wenye ulemavu ziweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia mchango wangu kwa kuunga mkono hoja.

**MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu kwa kusema naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sekondari za Kata. Ngara tumejenga sekondari 18 tangu hoja ya kujenga sekondari za Kata ianze. Ilikuwa siyo rahisi kujenga hizi sekondari lakini baada ya majadiliano marefu tumeweza kujenga hizi sekondari. Niishukuru Halmashauri ya Wilaya ya Ngara kwa kujenga na kusimamia hizi sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na sekondari za kidato cha tano na sita, naishukuru Serikali kwa kutoa vibali Ngara tuanzishe sekondari za kidato cha tano na sita. Shule hizo ni Kabanga *high School*, Lukole *high School*, Muyenzi *high School*, Ngara Mjini *high School* na Murusayamba *high School*. Hapa twatoa shukrani sana kwa Serikali kwa kuruhusu kuanzisha *High School* tano katika miaka mitano ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Dr. Jakaya Mrisho Kikwete. Hii ni sifa kubwa sana kwa Serikali ya Mheshimiwa Rais Dr. Kikwete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, VETA katika maelezo ya Serikali tuliahidiwa kuwa tutapata kituo cha VETA Ngara, mpaka sasa hivi haijatokea na wananchi wa Ngara wanaomba Serikali ijenge shule au kituo cha VETA katika Wilaya ya Ngara,

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalı langu ni kwamba, tunaomba kujua lini Serikali itajenga hiyo shule ya ufundı ?

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Napongeza sana shule za Kata, naomba kushauri tuwe na *phase II* ya elimu ambayo ni *A level* kila Kata, sababu uwezo na nia ipo. Sambamba na hilo ni muhimu ramani za shule ziwe na eneo la hostel, Miundombinu ya umeme na maji ya kunywa ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la elimu ya juu. Mfuko huu wa elimu ya juu ni muhimu ukawekewa mikakati ili mfuko uwe *revolving fund*. Ushauri wangu, yeti vyta wahitimu viwe na alama kuwa mhitimu ni *loans board beneficiary*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Loans board beneficiary grade A or B or C or D* ili anapoajiriwa mwajiri aweze kumkata na hela irudi Serikalini ili wengine wapate kunufaika. Aidha, nipongeze sana mchango wa Wizara kwa chuo cha Muhimbili Mlonganzila shilingi bilioni nane na nipongeze vyuo vyta ualimu vilivyopo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lini ujenzi wa chuo cha VETA Ludewa Iringa utaanza?

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa dhati kabisa kutoa hongera na pungezi nzuri na mafanikio ya kimapinduzi katika utendaji wa Wizara. Ukitazama shule za sekondari toka 1,745 (2005) hadi shule 4,266(2010) na ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, ni alama tosha ya utendaji kazi uliotukuka. Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara na wale waliomo katika vyuo vyetu tembeeni kifua mbele, mmeefanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zangu, Serikali itusaidie sisi toka Wilaya ya Rufiji ili tufungue (tuanzishe) *high school*, tafadhali msituachie peke yetu yaani bila Serikali Kuu kusimamia, tutazidi kudidimia kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ichukue hatua za dharura kupeleka walimu wengi katika shule zetu hususan katika shule za sekondari, kwa vile Rufiji iko nyuma kielimu, bado mgao wa walimu Rufiji iwe zaidi ya walimu watano walioahidiwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Rufiji itazamwe kwa jicho la huruma, msitutupe ndugu zenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali ifungue shule ya ufundi ya VETA katika Jimbo langu la Rufiji (Wilaya) Naomba Serikali ikubali kuwa kwa kweli hakuna chuo chochote cha ufundi (*VETA*). Tuanze kujenga chuo cha ufundi Wilayani Rufiji upya kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza tena Serikali kwa mpango wa *MMES* kwa kupanga fedha za kutosheleza kununua vifaa vya shule, ukamilishaji wa majenzi ya madarasa, maabara, nyumba za walimu, na maktaba. Aidha, suala kuwapatia wanafunzi wa elimu ya msingi kupata chakula cha mchana wakati wakiwa shuleni, ni jambo kubwa na litaongeza ufanisi shuleni na kupunguza kabisa utoro shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Manaibu Waziri, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza na Mheshimiwa Gaudensia Kabaka, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri sana ambayo imejikita sana katika kuboresha suala zima la elimu kwa sekta zote kuanzia shule za awali, shule za msingi, shule za sekondari na vyuo vikuu kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa natambua uwezo wa Waziri, Mheshimiwa Profesa Maghembe ; Naibu Waziri, Mheshimiwa Mahiza na Mheshimiwa Kabaka, nawaombea Mwenyezi Mungu waweze kushinda katika uchaguzi ujao kwa kura za kishindo ili warudi kuendeleza kazi nzuri waliyofanya kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli usiofichika kuwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa aliyofanya kwa ujenzi wa madarasa ya shule za msingi kupitia mpango wa MMEM, madarasa ya shule za sekondari kupitia mpango wa MMEM na hasa ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Mungu aendelee kumpa afya, nguvu na ushindi wa kishindo kwa uchaguzi ujao, uwe wenyе kura za kishindo kama ilivyopata kura za kishindo kwenye kura za maoni jana tarehe 11 Julai, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya walimu wastaafu, nasikitika sana kuona Serikali imeshindwa kutekeleza ahadi yake kuwalipa walimu wastaafu walioajiriwa kwa mkataba, mishahara ya miezi kumi na tano kupitia maswali yangu hapa Bungeni mara nne. Nasubiri majibu ya mwisho ambayo yatamaliza tatizo hili ukizingatia walimu wawili sasa ni marehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kurekebishiwa mishahara na kulipwa mapunjo walimu waliopandishwa madaraja. Naipongeza Serikali kwani huwajaliwa walimu kwa kuwapandisha madaraja kila muda ukifika wa kila mwalimu kupitia utaratibu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kwamba, bado kuna tatizo la kucheleta kuwabertilishia viwango vya mishahara yao, tatizo ni nini? Vile vile hujitokeza tatizo la kucheleta kulipwa mapunjo yao pia nipatiwe maelezo.

Mheshimiwa Spika, Walimu kuundiwa chombo cha kuangalia taaluma zao, pamoa na walimu kuwa na vyombo mbalimbali vya kuwapa huduma ama kuwasimamia lakini bado hawana chombo kusimamia hii hasa kwa upande wa taaluma kama ilivyo kwenye kada ya Madaktari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali, ni lini Walimu wataundiwa chombo chao cha kuangalia taaluma zao ili watu wasio na taaluma wasivamie fani ya Walimu kama ilivyo kwa Madaktari na kada zingine mfano Wahandisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie tatizo la upungufu wa walimu wa shule za msingi na sekondari pia. Pamoja na juhudhi kubwa za Serikali bado tatizo la walimu ni kubwa kwani kwa shule za msingi upungufu ni asilimia 40 na shule za sekondari upungufu ni asilimia 58. Upungufu huu ni pamoja na Wilaya zote kwa Mikoa 26 kwa kuwa hata wanafunzi waliomaliza kidato cha nne wengi waliotaka kujiunga na mafunzo ya elimu waliochagua, hawakuchaguliwa, tatizo ni nini kutokuchukua wanafunzi wakati upungufu bado ni mkubwa sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije katika suala la kupandisha mishahara ya walimu. Naipongeza Serikali kwani imekuwa tayari kukaa kwenye meza ya majadiliano na walimu ili kuzungumzia suala la mishahara ya walimu. Pia naipongeza Serikali kwa kuwapandisha watumishi mishahara wakiwemo walimu, vile vile naungana na Serikali kuwa kima cha mshahara ni siri ya mwajiri na mwajiriwa, hakuna sababu ya kutangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ipeleke skeli za mishahara ya walimu kufuata madaraja yao ili wajue Serikali imewaongezea mishahara kwa kiwango gani. Hii itasaidia kupunguza mizozo pia kuwapa walimu moyo wa kufanya kazi. Vile vile itasaidia walimu kuacha tabia ya kukimbilia shule zisizokuwa za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makato ya asilimia 15 ya PSPF, bado kuna tatizo la makato ya asilimia kumi na tano ya mishahara ya walimu kutokupelekwa mapema kwenye mfuko wa PSPF au kutokupelekwa kabisa wakati fedha hukatwa, napenda kujua tatizo ni nini na lini tatizo hili litaondoka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiomba Serikali kutafakari tena tatizo la walimu wanaopangiwa kufundisha wilaya ambazo zina mazingira magumu au jiografia ngumu kiasi cha kukatisha tamaa, walimu kuwa tayari kwenda kufundisha huko na kusababisha shule nyingi za Wilaya hizo utoaji wa taaluma kuwa mgumu. Nategemea majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichangie kuhusu posho ya uhamisho na posho ya usumbu. Napenda kuiomba Serikali kutoa maelezo tofauti ya hizi posho mbili nilizotaja hapa juu. Hii itasaidia walimu kufahamu hasa posho ya usumbu pale mwalimu anapofunga mizigo kutoka mahali kwenda sehemu nyingine wengi wao wanakosa haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao upendo mkubwa wa Mheshimiwa Profesa Maghembe na Manaibu Waziri wote wawili hivyo sina lengo la kutoa shilingi kwenye mshahara wa Mheshimiwa Waziri Maghembe, bali nataka maelezo yenye kukidhi haja kwenye hoja zote nilizozitoa hususan madai ya walimu wastaafulu, watakuwa kwa maisha magumu. Hivyo naunga mkono hoja hii kwa moyo mkunjufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya vifaa vyta maabara, napenda kuitaarifu Serikali kuwa Mkoa wa Singida chini ya Mkuu wetu wa Mkoa, Mheshimiwa Dr. Parseko Kone imejiwekea malengo ya kujenga maabara kwa kila sekondari ya Kata pamoja na shule za kidato cha tano na cha sita, mpaka mwezi Septemba 2010 majengo haya yote yatakuwa yameisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuptia bajeti hii Serikali kutenga fedha kwa ajili ya maabara za Mkoa wa Singida ambazo hadi Septemba, 2010 majengo yake yatakuwa tayari, nategemea majibu ya Serikali yenye matumaini na wana Singida amba ni wa mwisho kielimu kwa nchi nzima.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja, ila ninayo haya machache ya kuiambia na kuishauri Wizara kutafiti na kutupia haya machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie uhaba wa Waalimu. Napenda kuishauri Wizara ione umuhimu wa kutatua tatizo la waalimu. Ni kweli kuwa Taifa tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa kujenga tangu Shule za Msingi takriban kila Kijiji na Shule za

Sekondari takriban kila Kata. Shule hizi ndio kichocheo cha maendeleo ya Taifa letu. Shule hizi ndio jiko la kupikia watalaan wa sasa na miaka ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, napenda Serikali itambue kuwa kuwepo Shule ni suala moja na kuwa na walimu katika shule hizi kwa upande mwininge ni muhimu sana. Ni kweli kwamba zipo juhudzi zinazofanywa za kuondoa tatizo la uhaba wa walimu. Hata hivyo, mchakato unakwenda taratibu. Haileti faraja hata chembe kuwepo walimu wawili au watatu katika shule za misingi amba wanazimika kufundisha tangu darasa la kwanza hadi la saba zenye mikondo miwili miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri ahadi aliyotoa Mheshimiwa Rais Kikwete jana Jumapili tarehe 22 Julai, 2010 wakati wa kufunga mkutano mkuu maalum wa CCM kuwa tatizo la walimu litakwisha hivi punde kwani vyuo vinavyofundisha walimu nchini kuanzia mwaka huu vitazalisha zaidi ya walimu 5,000 kila mwaka. Hili lifanyike haraka ili shule zikiwemo zile za Jimbo la Kigoma Kusini ziondokane na uhaba wa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni vivyo hivyo kwa upande wa shule za sekondari za Kata. Nashauri sekondari hizi za Kata zipate walimu wa kutosha na wenye weledi wa kazi zao ili waweze kuwaandaa wanafunzi kufaulu vizuri mitihani ya Taifa na hivyo kuwezesha wanafunzi wengi kwenda sekondari za juu (*High Schools*) na hatimaye elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara itueleze Idara ya ukaguzi inakagua nini na wapi? Katika Jimbo la Kigoma Kusini katika Kata za Mwambao wa Ziwa Tanganyika za Ilagala, Sumuka, Sigunga, Igalula, Buhingu na Kahya. Kata hizi hazina ukaguzi japo hotuba ya Mheshimiwa Waziri imezungumzia ukaguzi. Nashauri tujitahidi kupanga Wakaguzi ili kuweza kubaini upungufu na hatimaye kuimarisha elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya Juu – Chuo Kikuu Dodoma. Naendelea kuipongeza Serikali na uongozi wa Chuo kwa hatua iliyofikiwa.

Hata hivyo, napenda kushauri ama uongozi wa Chuo au Serikali itazame upya namna ya kulaza watoto shulenii. Imekuwaje ngazi ya Chuo Kikuu wanazalawa wanne kwenye chumba kimoja. Wanafunzi hawa ni watu wazima wanahitaji usiri. Wawili wa kike chumba kimoja ni sawa. Lakini wanne ni hakika Serikali iangalie kwa haraka uwezekano wa kujenga mabweni ili wanafunzi wakae wawili wawili kila chumba.

Hapa *UDOM* kuna tatizo la pili la kutunza kumbukumbu za mahesabu ya malipo ya ada. Inekuwaje wanafunzi wanaojilipia wanahimizwa kulipa ada kwa wakati lakini wakishalipa hawapewi stakabadhi. Wanazungushwa kupewa stakabadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kauli hii natangaza maslahi. Nimekuwa namlipia kijana wangu pale *UDOM* lakini kupewa stakabadhi yaelekeea ni mpaka pengine mfanye juhudzi za pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona wakati kijana anapodaiwa ada haambiwi apeleke kwa muda wake?

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wa Idara mbalimbali kwa hotuba na mpango mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya sekondari – Kiteto, madai bado walimu kwani kuna watoto waliokosa masomo *form one and two*. Hawa wanahitaji program maalum ili wafidie vipindi walivyokosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za msingi zina uhaba mkubwa wa walimu na watoto hawafundishwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna walimu wengi Wilayani Kiteto ambao hawajalipwa bado madai yao. Hawa walipwe kama uhakika umeshakamilka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itoe uamuzi juu ya suala la vitabu vyta kiada na ziada na pia ibainike vitabu vyta kufundishia darasa la VI hadi VII.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya ujenzi wa Chuo cha VETA, Kiteto isukumwe ili ujenzi uanze.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakupongeza kwa hotuba yako nzuri yenye ufanuzi wa kina kuhusu Wizara yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwanza, je, ni fedha kiasi gani zimetengwa kwa ajili ya kujenga nyumba za walimu, maabara kwa Shule za Sekondari za Kata.

Pili, je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza udahili wa wanafunzi wanaojiunga na vyuo vyta ualimu Shule za Sekondari.

Tatu, je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia usafiri Chuo cha Ualimu Mpwapwa na Shule ya Sekondari ya Mpwapwa?

**MHE. NURU A. BAFADHIL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kunipa uhai. Pili, napenda kumpongeza Waziri, Manaibu Waziri na watendaji wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya na ushirikiano wanaotupa wakati wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia kuhusu mimba za wanafunzi. Wanafunzi wengi wanapata mimba kwa vile ufuatiliaji ni mdogo ukizingatia mwalimu ndiye ana muda mrefu wa kukaa na mwanafunzi kuliko mzazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya 60 shule nyingi zilikuwa na utaratibu wa kuwapima wasichana wote kila baada ya miezi mitatu. Halmashauri ziliandaa utaratibu

wa kuleta *mobile clinics* mashulenii. Kwa hiyo, wanafunzi wa kike walikuwa waangalifu kwa kuwa walifahamu hilo wakati baada ya muda fulani tutakuja kuchunguzwa afya zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha utaratibu wa kupima afya za wasichana ili kubaini wenyewe mimba na kudhibiti pia kutokuwa na ufuatiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko sana bado hadi leo kuna shule za sekondari zina mabango yanayoonesha Wizara ya Elimu na Utamaduni. Hivi hawa walimu wenyewe shule hizo hawajui kama Wizara ya Utamaduni haimo katika elimu au ni kukosa fedha au ni dharau. Tunawafunza nini wanafunzi wetu, watamke Wizara ya Elimu na Utamaduni au Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali iwalazimishe wale walimu wakuu ambaao mabango yao bado yanaonesha Wizara ya Elimu na Utamaduni yabadilishwe yawe Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba kuelezea kuhusu makandarasi ambaao wanajenga madarasa yetu ya Shule za Sekondari. Kwa kweli madarasa hayapo katika kiwango mfano, katika Jiji la Tanga tulifanya ziara 2008 na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga Mheshimiwa Mohamed Abdulazizi, Mbunge ambaye sasa ni Mkuu wa Mkoa wa Iringa. Katika Kata ya Tongoni tulikuta darasa lina ufa kuanzia juu ukutani hadi chini sakafuni. Alitoa agizo la kufanya chumba hicho marekebisho. Cha kushangaza nilifika pale mwezi Mei, 2010 nilikuta chumba kile hadi leo hakijaguswa kabisa na kimeongezewa tofali kwenda juu zaidi. Hii ni hatari wakati wowote jengo la darasa hilo linaweza likaanguka na kujeruhi walimu na wanafunzi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaombe wana kamati au Bodi za Shule zisiidhinishe kazi kwa kujuana ili kuepuka ujenzi ambaao hauna ubora.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake pamoja na watendaji wote Wizarani na taasisi zake zote kwa kazi nzuri wanayofanya katika hali ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mji wa Tabora kuna shule tatu za Kitaifa (*Tabora Boys School, Tabora Girls School* na *Milambo Secondary School*). Shule hizi ni za wanafunzi wenyewe vipaji maalum pia, zinakabiliwa na upungufu mkubwa wa walimu na maabara. Ili kulinda kuendeleza watoto wetu wenyewe vipaji maalum katika shule hizi, Serikali haina budi kuyapatia ufumbuzi wa haraka matatizo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kulipongeza Shirika la *UNHCR* kwa uamuzi wake wa kujenga madarasa mapya, mabweni na nyumba nzuri za walimu katika Shule ya Wasichana Tabora. Vile vile Shirika hili limechimba visima vya maji kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iwasiliane na Shirika hili la *UNHCR* kwa madhumuni ya kuomba msaada wa ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu, maabara, visima vya maji katika Shule za Tabora *Boys* na Milambo pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule za Tabora *Girls* na Milambo zinakabiliwa na tatizo kubwa sana la kukosa uzio kwa ajili ya usalama wa wanafunzi na mali zao. Wezi na vibaka wamekuwa wakiingia na kutoka katika maeneo ya shule hizi bila hofu na kuiba watakavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa nyumba za walimu ni tatizo kubwa sana katika shule zote hapa nchini lakini Shule ya Milambo, Tabora ina tatizo maalum kutokana na ukweli kwamba wakati Serikali ilipochukua shule hii toka kwa Wamisionari, haikuzichukua nyumba za walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu Chuo cha Ufundı Tabora. Napenda kuipongeza Serikali kwa kukamilisha ujenzi wa majengo mapya ya Chuo cha Ufundı Tabora. Majengo ambayo yalizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais Dr. Jakaya M. Kikwete tarehe 10.08.2010. Nafahamu kuwa ufunguzi wa mashine (mitambo) mbalimbali katika Chuo hiki uko mbioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawahimiza wananchi wa Tabora Mjini waitumie fursa hii kupata Chuo cha ufundı kwa kuwapeleka watoto wao wenye sifa stahili kupata mafunzo ya stadi mbalimbali zitakazowawezesha kujajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia Chuo Kikuu cha *St. Augustine*, Tawi la Tabora. Kanisa la *Roman Catholic* bado linaendelea kuwasiliana na Wizara ya Elimu ili kupata ruhusa au kibali cha kuanzisha Chuo hiki Mjini Tabora. Ni matarajio yangu kwamba mawasiliano yanayoendelea yatazaa matunda mazuri mapema ili kukiwezesha Chuo hiki kianze mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, natanguliza shukrani zangu Wizarani kwa kukiwezesha Chuo cha *St. Augustine* kuanzisha Tawi la Tabora. Chuo hiki kitakapoanza Mjini Tabora, kitaamsha vuguvugu la maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika Mji wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee pia suala la Shule za Kata. Tabora imefanikiwa kujenga Shule 19 za Sekondari katika kipindi cha 2006 – 2010. Shule hizi zinakabiliwa na matatizo mengi kama vile upungufu wa walimu, madawati, nyumba za walimu, matundu ya vyoo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa hatua inazochukua kukabiliana na matatizo haya. Aidha, naishauri Serikali iangalie uwezekano wa kuuweka wazi zaidi mpango wake wa kutatua matatizo haya ili kila Mkoa, Wilaya na Kata zifahamu nafasi yake katika program hiyo ya maboresho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Elimu Tanzania. Tatizo kubwa la mamlaka hii ni ufinyu wa bajeti. Napendekeza namna ya kukabiliana na ufinyu wa bajeti yamekwishawasilishwa Wizarani kwa uamuzi. Naishauri Wizara iharakishe uamuzi kuhusu suala hili ili ufumbuzi upatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, moja ya mapendekezo ni Serikali kuangalia uwezekano wa Serikali kuitengea mamlaka hii sehemu ya *SDL* isiyopungua angalau asilimia moja. Yaani kwa sasa *SDL* ni asilimia sita, sehemu yake kati ya asilimia mbili hadi asilimia tatu, inakwenda *VETA*. Je, kwa nini sehemu inayosalia isipewe Mamlaka ya Elimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MWENYEKITI:** Sasa tunarudi kwa Waheshimiwa Manaibu Mawaziri kwa ajili ya kuendelea na uchangiaji. Anaanza Mheshimiwa Naibu Waziri, Mwantumu Mahiza.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninakuomba fursa kidogo ili nimshukuru Mwenyezi Mungu mwenye wingi wa rehema kwa kuniwezesha kumudu majukumu aliyonijalia. Ninamshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kunitfea mara mbili kuwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Nampongeza yeye binafsi na mwenza wake kwa kuteuliwa kuwa Wagombea wa urais kupitia CCM. Ninampongeza sana Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein kwa kuteuliwa kuwa mgombea wa Urais wa Zanzibar, inshallah, Mwenyezi Mungu awafanyie wepesi katika azma yao na awajalie ushindi mkubwa na wa heshima kwa chama chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana Mheshimiwa Prof. Maghembe na Mheshimiwa Mama Kabaka, Mwalimu wangu kwa ushauri na miongozo ambayo imenijengea uwezo kitaaluma na kitaalam. Shukrani pia ziwaendee Makatibu Wakuu, Wakurugenzi wote, Wakuu wa Vyuo, Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya, Wakaguzi Wakuu wa Kanda na Wilaya, Walimu wote wa Shule za Msingi na Sekondari kwa ushirikiano wao mkubwa na wa karibu ambao kwa hakika umewezesha utendaji wangu kuwa mwepesi.

Shukrani maalum zimfikie Mheshimiwa Bi. Salma Kikwete kwa kuanzisha Shule Maalum ya Sayansi kwa Wasichana yatima Nakayama iliyopo Rufiji. Shule hii ni ya aina yake na ninawataki heri wote waliojaliwa kupata fursa ya kusoma shule hiyo. Hongera sana Mheshimiwa Bi. Salma. Usikate tamaa kwa maneno na kejeli za wasiojua unachokifanya kwani mabinti hawa wanahitaji sana msaada wako, wetu na wa jamii kwa ujumla ili nao waweze kupata elimu bora kwa mustakabali mwema wa nchi yetu na maisha yao ya baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru wanawake wa Mkoa wa Tanga kwa heshima kubwa walionipa kwa kuniwezesha kuwawakilisha Bungeni kwa miaka

mitano. Ninaomba Mwenyezi Mungu awajalie hekima na busara ili waweze kuchagua viongozi wengine, na wanipe ushirikiano mkubwa hasa katika kipindi hiki ambacho nimeitikia wito wa 50% - 50% kwani ninakwenda jimbo la Mkinga. Naomba Mwenyezi Mungu pamoja nao awape uwezo mkubwa ili tuweze kushinda. Kwa namna ya pekee ninamshukuru bwana Bakari Mahiza, mume wangu na wanawe kwa kuwa karibu nami wakati wote katika harakati zangu za medani za kisiasa. Mungu awajalie afya njema na umri mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja za Waheshimiwa Wabunge ni kubwa, ni nyingi na ni muhimu. Nitaanza kuzijibu kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyoniwezesha. Naanza na madai ya Walimu wastaafu Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya Walimu wastaafu yameletwa mara kadhaa na kila mara tulikuwa tunapata jibu kwa kadri ambavyo na sisi tulikuwa tunashirikiana na wenzetu wa Hazina. Jibu la sasa ambalo tunampa Mheshimiwa Mbunge aliyelileta hapa, tunamwomba radhi kwamba tulichelewa kuwapa majibu sahihi, lakini hivi sasa watalipwa mwezi Julai na kama itashindikana naomba tuwasiliane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwaarifu Walimu wote ambao walajiriwa mwaka 2008 au baada ya mwaka 2008 ambao bado hawajapata mishahara yao, wajaze fomu maalum ili madai hayo yaweze kufikishwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii kwani bado tunayo baadhi ya mishahara ambayo ni *unclaimed salaries* katika Akaunti ya Amana na bado haijapata wanaodai. Madai mengine ya Walimu baada ya uhakiki rufaa zao zimepokelewa na Kamati Maalum kutoka TAMISEMI, CWT-WEM, Wizara ya Utumishi na CAG na zinafanyiwa kazi. Madai hayo yatalipwa mara baada uthibitisho kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhamisho holela wa Walimu wa Wilaya ya Shinyanga, Tume Maalum itaundwa ikiongozwa na Mkaguzi wa Kanda ili kuweza kupata ukweli wa madai wa mgogoro huo uliojitekeza kati ya uhamisho holela uliofanywa na Afisa Elimu huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninapenda kuzungumzia ujenzi wa Shule za Sekondari Kidato cha Tano. Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya elimu ameeleza bayana kwamba Mpango wa Elimu MMES-II utazingatia sana ujenzi wa Sekondari za Kata kwa ajili ya Kidato cha Tano na Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi imeletwa hoja juu ya elimu maalum kuwa Idara. Naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, mazungumzo bado yanaendelea kati ya Wizara ya Elimu, Wizara ya Utumishi na Hazina ili kuweza kupata kibali cha kuanzisha Idara hiyo. Aidha, fedha kiasi cha shilingi bilioni tatu kimetengwa kwa ajili ya kuboresha miundombinu kwa ajili ya kuweka mazingira na maeneo ambayo wanafunzi walemvu watakuwa wanaishi au kusomea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuzungumzia juu ya Walimu Wakuu kutokuelewana na watumishi wengine katika Idara zao. Sio jambo la kawaida Wakuu wa

Shule na Walimu wengine kutofautiana, lakini kama hali hizi zipo, naomba Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo zifuatwe ili kuwe na maelewano na hivyo kuleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi kwenye mchango kumezungumziwa pia kutokuwepo na Walimu wa sayansi katika Shule za Sekondari za Chifu Mang'ombe na Chifu Osward. Suala la Walimu wa Sayansi ni kubwa, mara kadhaa tumekuwa tukilizungumzia. Ninamwomba Mbunge wa eneo hilo kwamba tutalifanya kazi. Uhaba wa Walimu nao umekuwa ukizungumziwa kwa mapana na marefu na mikakati mbalimbali imeoneshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa maabara ni kipaumbele cha kwanza katika Mpango wa Elimu wa mwaka 2010 - 2020 nyumba za Walimu nazo zimepewa kipaumbele cha pili ili kuhakikisha kupatikana kwa nyumba za walimu kutakakoweka utulivu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa mitihani ni suala ambalo linazingatia mambo mengi, kwanza uadilifu wa mwalimu, uwezo wa mwalimu kutunza siri na mambo mengine. Kwa hiyo, kuendelea kuwa na wale wale inawezekana kwamba bado hatujapata wengine lakini naomba Maafisa Elimu wapokee hili na waone kwamba wapo walimu wengine vijana wenye ari na wenye sifa wanaoweza kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na hoja mbalimbali za kuboresha taaluma ya msingi na sekondari. Naomba niseme kwamba mwanzoni mwa mwaka huu tuliweza kuwa na m Kutano mkubwa kabisa wa watalaa na kwa kina tuliweza kujadili na tuliweza kutoa taarifa kadhaa ambazo zilionesha ni namna gani tunaweza kuondoka mahali hapo ambapo tumefika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa madarasa kuwa chini ya viwango ni dhahiri kwamba hakukuwa na usimamizi wa karibu. Hivyo niwaombe ndugu zetu wa Halmashauri wote ambapo kutakuwa na ujenzi huu wawe karibu zaidi kufuutilia siku hadi siku kwani madarasa haya na baadhi ya majengo hujengwa na wananchi wenyewe kwa kujitolea na hivyo wanahitaji sana msaada wa kitalaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka miwili sasa idara hii ya vyombo vyaya usafiri kwa wakaguzi imekuwa ikipata bajeti ndogo. Lakini kuanzia mwaka wa fedha 2009/2010 Idara hii imekuwa ikipatiwa fedha na kwamba tumeweza kununua magari kadhaa ambayo yameshasambazwa kwenye Halmashauri mbalimbali na hivi sasa tunatarajia kupokea magari mengine nane na kwa kadri hali ya bajeti itakavyoruhusu tutaendelea kununua magari haya ili tuweze kuwapatia wakaguzi waweze kutimiza wajibu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu udhalilishaji wa walimu katika Mikoa mbalimbali, ni jambo la kusikitisha sana katika kipindi hiki ambacho kila Mbunge anayesimama analalamikia uhaba wa walimu. Vitendo vyaya kuwadhalilisha walimu kwa kuwachapa na kuwafanya matendo mengine ambayo hata hayapaswi kuzungumzwa, kinarudisha nyuma juhudi za Serikali za kutoa taaluma ya walimu na kuwapangia vituo. Mambo haya hayaleti sifa wala hayapendezi. Haifurahishi kuona kwamba Mikoa hiyo

hiyo ambako walimu ndiko wanakodhalilishwa wanasimama na kudai tena walimu wapelekwe. Kwa bahati mbaya sana naomba kutoa wito kwamba ni vizuri sisi Wabunge kwa sababu ni sehemu ya Madiwani na sehemu ya wakazi na wawakilishi wa wananchi tukatoa elimu namna Serikali inavyopata taabu kuwafundisha walimu hawa na kuwapangia kazi.

Ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba tunawapatia makazi na tunawalinda. Pale mwalimu anapoonekana kukosea au kukosea taratibu, basi hatua za kinidhamu zichukuliwe na siyo kuwadhalilisha walimu kwa kuwachapa kama vile ni wanyama na kadhalika, haipendezi. Mimi naungana na Wabunge wote walioleta hoja hii kwamba nisingependa kusikia tena walimu wanachapwa hata kama ana kosa, ndio maana kuna Mahakama zimejengwa za Mwanzo na kuendelea mpaka Mahakama za Rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu somo la michezo, somo la michezo linaendelea kufundishwa, limebadilishwa jina linaitwa haiba na michezo na ninaomba niseme tumezingatia na mashindano ya michezo kwa Shule za Msingi na Sekondari yote yamerudishwa na hivi karibuni tulikuwa na mashindano ya Shule za Sekondari ambayo yamefanyika kwenye kituo cha Kibaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, somo la dini vile vile linafundishwa na masomo haya yanatolewa mara mbili kwa wiki kwenye Shule za Msingi, mara moja kwenye Shule za Sekondari pamoja na Vyuo vya Ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamezungumzia juu ya kuporomoka kwa maadili. Hili ni jambo kubwa ambalo sote kwa pamoja tunapaswa tulizungumze, kwani hali imeharibika. Hivyo, sio vyema tukamwachia mtu mmoja. Mwalimu kumwacha afanye kazi za taaluma na yeye akafundisha maadili tutakuwa tunawapa mzigo. Watoto hawa tumewaleta wenyewe duniani, hivyo ni jukumu la wazazi kuhakikisha tunachukua nafasi ya kwanza. Mwalimu atasaidia kwa mujibu wa kanuni na sheria na taratibu anazozitumikia. Kwa hiyo, mimi naomba niseme suala la kuporomoka kwa maadili bado liko mikononi mwa Waheshimiwa wananchi na Wabunge wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nitumie nafasi hii kuwapongeza wananchi wote wa nchi hii kwa namna ya kipekee walivyoweza kushiriki katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi hususan katika sekta ya elimu. Shule nydingi za Sekondari na Msingi zimejengwa na matokeo tunayoyaona ya uhaba wa walimu ni mafanikio ya kuwepo kwa hizo shule na uandikishwaji wa wanafunzi. Hivyo, naomba niseme kwamba changamoto zote zilizojitokeza tunazitambua, tumeziwekea mikakati na Ilani mpya iliyotoka hivi sasa inaonesha mwelekeo wa namna gani wa kukabiliana na hoja mbalimbali ambazo zimejitokeza baada ya mafaniko haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kuunga mkono hoja na tunatakiana heri wote, Mwenyezi Mungu atupeleke kwenye mchakato tukachakachue na turudi tena kwa kadri atakavyotuwezesha. Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, umesikika mpaka kule Tanga. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote naomba nianze pia kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Naomba niungane na wasemaji wenzangu waliopita katika kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kura za kishindo alizozipata kutoka kwa Wajumbe wa Mkutano Mkuu Maalum ili kumteua aweze kuwa mgombea pekee wa Urais kwa Chama cha Mapinduzi. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa uteuzi wake wa kuwa mgombea wa Urais katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Dr. Bilali kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kuwa mgombea mwenza katika duru la Urais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa heshima na imani aliyoonesha kwangu na kuendelea kuniweka katika nafasi hii ya Naibu Waziri kwa kipindi chote cha miaka mitano. Aidha, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa kunishirikisha vyema katika kumsaidia kazi za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Ninamshukuru pia Naibu Waziri mwenzangu na mwanafunzi wangu, Mheshimiwa Mwantum Mahiza, kwa ushirikiano mkubwa ambao amenipatia wakati wote tulipokuwa naye katika Wizara hii. Naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, chini ya uongozi shupavu wa Katibu Mkuu Prof. Hamis Omar Dihenga na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Selestine Gesimba kwa ushirikiano wao na kunishikirisha vyema katika shughuli ambazo zilhusu Wizara yetu.

Nawashukuru pia Watendaji pamoja na viongozi wote wa Taasisi zilizoko chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi zikiwemo Taasisi za Elimu ya Juu na Taasisi nyingine kwa ushirikiano mkubwa walionipatia na kuifanya kazi yangu isiwe na suluba kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa namna ya pekee niishukuru sana familia yangu nikianzia na mume wangu Bwana John Kabaka kwa ushauri, upendo na uvumilivu katika kipindi chote wakati sipo nyumbani ili kutekeleza kazi za Wizara. Lakini pia nimshukuru sana binti yetu Patricia Robi, mume wake Joel Kamonjo, wajukuu zetu Tina, Patrick na Michael Angelo kwa upendo na faraja kubwa ninaiyopata wakati wote nikiwa nao. Nawashukuru wadogo zangu kwa kuendelea kumlea mama yetu mpendwa aliye

kitandani sasa kwa muda wa miaka mitano na wamemlea kwa umakini na upendo mkubwa na hivyo kuniwezesha kufanya kazi yangu kwa utulivu.

Mwisho, napenda nichukue fursa hii kuwashukuru sana wanawake wa Mkao wa Mara kwa kura zao walizonipatia kwanza mwaka 2005, lakini pia niendelee kuwashukuru kwa kuendelea kunipa ushirikiano na upendo mkubwa katika kutimiza majukumu yangu. Naamini kabisa kuwa sikuwaangusha na hivyo niwaombe tena kwa mwaka huu 2010 wiki chache zijazo kura watakazonipa zisipungue kabisa na hata yule mtu mmoja ambaye hakunipa kura, basi sasa hivi aone sababu ya kunipatia kura hiyo na hivyo nipate asilimia mia moja ya kura zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuwashukuru Wabunge wenzangu kwa ushirikiano mkubwa mlionipa katika kunisaidia kutimiza majukumu yangu. Naomba niwashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo naomba sasa nijibu baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Naomba nianze na hili suala la uchaguzi wa wanafunzi wa Vyuo vya Ualimu hasa mwaka huu. Suala hili limezungumziwa na Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, lakini pia na Mheshimiwa Diana Chilolo na madai ni kwamba wanafunzi wameomba wengi na wengi walikuwa na sifa lakini hawakuweza kuchaguliwa. Naomba niseme kwamba kulikuwa na ushindani mkubwa sana katika uchaguzi huu wa wale walioomba kujiunga na mafunzo ya Ualimu daraja la IIIA.

Walioomba kujiunga na mafunzo na waliokuwa na sifa walikuwa zaidi ya wanafunzi 43,000. Waliochaguliwa walikuwa wanafunzi 4,500. Hii ni kulingana na nafasi zilizopo na kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya Idara hii. Lakini vigezo vilivyotumia ni ufaulu usiozidi pointi 28 na pia waliofaulu Hisabati, Sayansi na Kiingereza ukizingatia kwamba haya masomo ndiyo yana upungufu katika shule zetu za msingi. Pia kigezo kingine ilikuwa ni kuzingatia uwakilishi wa kila Mkao. Wanafunzi 37,000 amba wana sifa hawakuweza kuchaguliwa na wengine walikuwa wa *Division Three*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni changamoto ambazo zimeonyeshwa na Mheshimiwa Susan Lyimo wakati wa kutoa hotuba yake hasa changamoto za Vyuo Vikuu ikiwemo uhaba wa Wahadhiri, uchakavu wa miundombinu, ufinyu wa bajeti, idadi ndogo ya wanafunzi, pia Wahadhiri wa kike na mazingira kwa wafanyakazi. Hili suala la uhaba wa Wahadhiri wa Vyuo Vikuu Serikali inaendelea kulifanya kazi kwa mambo mbalimbali kwa mfano kutoa vibali vya ajira kwa Vyuo Vikuu ili waweze kuajiri Wahadhiri kila mwaka, lakini Wizara kwa kushirikiana na vyuo huwapeleka masomoni Wahadhiri Wakufunzi na Wahadhiri Wasaidizi katika masomo ya uzamili na uzamifu.

Vyuo vimeingia mkataba na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ili kukopeshwa fedha kwa ajili ya programu ya uzamili na uzamifu, Serikali kwa kutambua uhaba wa Wahadhiri inatoa kibali kwa kuajiri kutoka nje ya nchi kama India na Russia. Vile vile Vyuo vinaajiri Wahadhiri, Maprofesa wa muda mfupi toka nchi mbalimbali,

yaani *visiting professors*. Pia Vyuo vinaingia mkataba na makubaliano ya kubadilishana wanataaluma na watafiti vile vile na wanafunzi.

Suala la uchakavu wa miundombinu, Wizara pamoja na vyuo vyenyewe vimeandaa programu ya miaka 10 juu ya ukarabati na ujenzi wa majengo mapya katika Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki. Serikali inashughulikia tatizo hilo na kwa kupitia mpango huo kwenye mpango wake wa *MMEJU* na Programu ya Sayansi na Teknolojia inayofadhiliwa na Benki ya Dunia ukarabati huu utafanyika.

Kuhusu ufinyu wa bajeti, Vyuo vimeandaa mikakati kamambe ya kuingiza mapato kwa mfano kutoa huduma kwa kitaalamu kwa viwanda na Mashirika na wanapata fedha kwa huduma hizo, lakini pia kutoa kozi fupi kama za ujasiriamali na teknolojia mpya. Idadi ndogo ya wanafunzi na Wahadhiri wa kike inashughulikiwa kwa kuendesha programu ya *pre-entry* kwa wasichana ambao hawakufikia kiwango cha kuingia Chuo Kikuu.

Mazingira duni ya kuvutia na kuwaweka watumishi, suala la kuboresha mafao ya izeeni litazungumziwa na Mheshimiwa Waziri kwa kirefu, lakini kwa Vyuo Vikuu tunajitahidi sasa hivi kutoa mishahara mizuri na kuongeza na kuboresha vitendea kazi. Najua muda unaendelea kwisha, lakini naomba nijibu swali linalohusu *VETA*. Wazungumzaji ni wengi, kuna Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge na Mheshimiwa Bakar Khamis. Wote wamezungumzia suala la *VETA*. Kwa kifupi Serikali imechukua hatua kubwa sana ya kupanua na kuboresha miundombinu ya vyuo vyetu vya *VETA* kuanzia mwaka 2005/2010. Katika kipindi hiki miundombinu ya Vyuo vifuatavyo vimeboreshwa ambavyo ni Songea, Singida, Shinyanga, Tabora, Ulyankhulu, Mpanda, Dakawa, Mara, Kagera, Moshi na Mikumi. Wizara yangu itaendelea kuboresha miundombinu ya Vyuo vilivyobakia.

Kuhusiana na Chuo cha Songela ambacho amezungumzia Mheshimiwa Killimbah, Chuo hiki kiko katika majengo ya mkandarasi wa barabara yaliyokabidhiwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba. Halmashauri ilishaingia mkataba na mtu binafsi ili akiendeshe. Aidha, Wizara yangu kupitia Ofisi ya *VETA* Kanda ya Kati ilikifanyia tathmini ya kitaalamu na kutoa mapendekezo yake kwa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba namna ya kukiboresha na kukiendeleza Chuo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Janeth Massaburi ameuliza: Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kujenga vyuo vya ufundi *VETA* ili kuweza kunusuru hali ya kikazi na ili kuweza kunusuru kizazi hiki ambacho kikipatiwa ujuzi na stadi za kutengeneza bidhaa za mafunzo mengine itasaidia kupunguza wimbi la vijana kukaa vijiweni. Hii ni kweli maandalizi yako tayari kama tulivyokwishesha ni kwamba tathmini ya kubaini stadi zinazohitajika katika kila Wilaya imeshafanya na fedha ndio tatizo letu.

Lakini kama mnavyofahamu na kama alivyosema asubuhi Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge tumeshaanza kwa Wilaya ya Makete na hivi Vyuo vya VETA vitajengwa kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana. Swali hili pia limeulizwa na Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, lakini yeze anashauri Serikali itafute vyanzo vingine vya fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa Vyuo vya Wilaya badala ya kutegemea ufadhili. Mheshimiwa Owenya tunashukuru sana kwa ushauri wako na Serikali inaahidi kuufanya kazi ushauri wako.

Mheshimiwa Bakar Khamis anasema, VETA ni tegemeo la kuzalisha. Yuko pale pale! Kuhusiana na umuhimu wa VETA na sisi tunasema ni kweli tutaendelea kujenga Vyuo hivi kadri fedha itakavyokuwa inaruhusu. Mheshimiwa Prof. Idris anasema Serikali ifungue Shule ya Ufundu ya VETA katika jimbo lake la Rufiji. Tunakubali, tutafanya hivyo pindi fedha itakapokuwa imepatikana. Prof. Feetham Banyikwa anaomba Serikali itimize ahadi yake ya kujengewa Chuo cha Ufundu. Kama nilivyosema, haya yatafanyika katika Wilaya zote 28, tatizo ni fedha na kama alivyotushauri Mheshimiwa Owenya, basi tutajaribu kuangalia vyanzo vingine vitakavyosaidia kupata fedha ili tuweze kujenga Vyuo hivi. Masuala mengine tutajibu katika ile *matrix's* kusudi kila mmoja aweze kusoma, lakini naomba sasa nimwachie Mheshimiwa Waziri aendelee na mimi niendelee kuwashukuru wote nirudie na kuungana na wenzangu kuwaombea kila la heri na kwamba *inshallah* Mungu akitujalia, basi tukutane tena mwaka huu huu Novembra.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mjadala wa hoja niliyoitao leo asubuhi tumefaidika sana na michango mizuri sana. Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kutoa hotuba hapa Bungeni wametueleza mambo ya msingi sana ambayo napenda kuwahakikishia kwamba tutayazingatia na pale fedha zitakapokuwa zinapatikana tutayatekeleza japo mengine magumu sana lakini palipo na nia kuna njia.

Aidha, tumepeata michango mingi sana ya Waheshimiwa Wabunge ambayo imetolewa kwa maandishi, nimeisoma michango hiyo michache kwa sababu ya muda ulivyo mdogo na michango ilivyo mingi. Lakini michango ambayo nimeisoma na wenzangu ambayo wameisoma na wataalamu wetu wameisoma na kuitolea majibu ni michango mizuri sana. Ninawaombea *Mwenyezi Mungu Subhanah-wa-taala* awarudisheni wote kwenye Bunge kwa jinsi ambavyo mmetoa mawazo mazuri na ambayo yakitekelezwa yatatuletea maendeleo makubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliotoa michango yao kwa kutoa hotuba nikianza na Msemaji wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii - Mheshimiwa Martha Mlata na Msemaji wa Upinzani katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu - Mheshimiwa Susan Lyimo. Wengine ni Mheshimiwa Joyce Masunga, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye,

Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Janet Mbene, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza na Mheshimiwa Gaudentia Kabaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, walioleta michango yao mizuri sana kwa maandishi walikuwa Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kiwanga, Mheshimiwa Lucas L. Selelili, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Rajab Hemed Juma, Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Senator Paul Kimiti, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Janet B. Kahama, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Charles Mwera na Mheshimiwa Said Arfi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mheshimiwa Mathias Chikawe, Mheshimiwa Bakar Khamis Faki, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa Salim Yusuf Mohamed, Mheshimiwa Khadija Al-Qassmy, Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mheshimiwa Lucas Siyame, Mheshimiwa Prof. Feetham Banyikwa na Mheshimiwa Pindi Chana. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Manju Salum Msambya, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Haji Juma Haji, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Mwinchoum Abdallah Msomi, Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimiwa Lolesia Bukimbwa, Mheshimiwa Jacob Dalali Shibili, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu na Mheshimiwa Mwanne Mchemba. Nawashukuru sana kwa michango yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango iliyoletwa ni mingi na muda wa kujibu michango hii ni kidogo, lakini nitajitahidi kwa nguvu zote kujibu kwa jinsi ambavyo nitaweza na napenda kwanza niwashukuru Manaibu Waziri kwa kutoa majibu mazuri. Nianze mwenyewe kwa kumshukuru Rais - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuniamini na kunitfea kuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu tangu Februari, 2008 hadi leo.

Napenda pia niwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Mwanga kwa mara nyingine kwa kuniamini na kunichagua na kushirikiana na mimi kwa hali na mali kuleta maendeleo katika Wilaya yetu na kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kiwango cha asilimia 95 tangu mwaka 2005 mpaka hivi leo. Ninawaomba tuungane

katika uchaguzi unaokuja ili tuweze kupata maendeleo makubwa zaidi katika mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa sana niishukuru Kamati ya Huduma za Jamii kwa hotuba nzuri na kwa kuibua mawazo mazuri sana ambayo tumeyapokea kwa mikono miwili na tutayafanya kazi kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyotuwezesha kwa sababu imelenga sana katika kuendeleza elimu hapa nchini kwetu. Matatizo ambayo yameibuliwa katika hotuba ile tutayashughulikia kwa kadri ambavyo Mwenyezi Mungu atakavyotujalia na kadri ambavyo tutapata fedha za utekelezaji wa malengo ambayo wameyaweka pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tu kusema juu ya machache yaliyomo mle la kwanza likiwa ni *Institute of Marine Sciences in Zanzibar*. Taasisi hii iko chini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na inaendelea kujengwa katika eneo la Buyu. Katika miaka mitatu mfululizo ujenzi huu umetengewa shilingi bilioni 1.2 na mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2010 fedha zote ambazo zilitengwa katika bajeti hizi za miaka mitatu zimetolewa. Tatizo ambalo liko pale ni ufinyu wa fedha zenyewe na mahitaji ya ujenzi wa Chuo kile. Nimezungumza katika Kamati juu ya tatizo hili na kuhakikisha Kamati kwamba Serikali itatafuta fedha kwa kadri itakavyoweza ili kuhakikisha inaongeza kasi ya ujenzi wa Taasisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetolewa hoja juu ya ubora wa elimu ya Tanzania. Ni kweli kwamba katika shule zetu kuna matatizo au changamoto za aina mbalimbali, lakini sio vizuri kuchukua kwa ujumla na kusema kwamba kiwango chetu cha elimu kimeshuka. Yapo maeneo na masomo ambayo tuna changamoto kubwa. Katika Elimu ya Msingi na Sekondari tuna changamoto kubwa ya ufaulu na uelewa duni katika Hesabu, lugha ya Kiingereza na katika masomo ya Sayansi. Tumechukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha kwamba tunaanza mchakato wa kubadilisha hali hii mbaya katika hesabu. Hatua ya kwanza ni kuongeza mafunzo ya Walimu walioko kazini ambao wanafundisha Hesabu, Kiingereza na Sayansi ili kuhakikisha kwamba wanakuwa na stadi mpya za kuweza kufundisha masomo haya na kuleta mabadiliko yanayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine ni kuongeza msisitizo katika kufundisha Kiingereza na Hesabu katika Vyuo vya Ualimu ambapo kila Mwalimu wa cheti daraja la IIIA atatakiwa kufaulu mtihani maalum wa Kiingereza na mtihani maalum wa Hesabu kabla hajapewa cheti kwenda kufundisha ili kuhakikisha kwamba wana stadi za kutosha za masomo haya. Wale Walimu ambao wanachukua Diploma ya Ualimu watatakiwa kufaulu mtihani wa Kiingereza ili kuwa na uhakika kwamba wanawenza kufundisha kwa Kiingereza kwa sababu Walimu wa Diploma wanapelekwa kufundisha katika Shule za Sekondari ambazo lugha ya kufundishia ni lugha ya Kiingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika ufaulu kumekuwa na kuboreka kwa ufaulu kwa wanafunzi katika ngazi za sekondari ambapo kwa kweli ni kuzuri ukilinganisha mwaka 2005 na mwaka 2010 utaona kwa kweli kumekuwa na kuboreka sana katika kufaulu kwa wanafunzi wetu.

Ukichukua daraja la kwanza mpaka la tatu kama ndiyo msingi wa kupima. Yaani *division one to division three*, utaona kuwa wanafunzi wengi walioko kwenye daraja hili katika mwaka 2009 walikuwa wanatoka kwenye Shule za Sekondari za Kata asilimia 50.15. Ukienda kwenye Shule za Sekondari hizi ambazo ni za zamani na kongwe za Serikali utaona ufaulu katika daraja hizo la kwanza mpaka la tatu ni asilimia 9.96 na ukienda kwenye shule hizi za binafsi utakuta ufaulu ni asilimia 39.96.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukilinganisha kwa namna hii utaona kwamba kumekuwa na kuboreka kwa shule zetu. Utekelezaji wa mradi wa MMES II mwaka huu utakaolenga katika kukamilisha madarasa kupeleka vifaa vya maabara shulenii, kupeleka vitabu shulenii, kuongeza walimu shulenii. Ningependa Waheshimiwa Wabunge mtuamini katika kazi hii ambayo tunaifanya hatua kwa hatua, lakini kwa uhakika mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande mwingine ambaao unaongeza ubora ni upande wa walimu shulenii. Ninajua kuna wale wanaodhani kwamba tunao walimu wa kutosha shulenii. Hatuna walimu wa kutosha humu nchini na ndiyo maana Serikali imeweka msisitizo mkubwa sana katika kufundisha walimu. Mwaka 2005 Walimu wenyewe shahada waliotoka kwenye Vyuo Vikuu, walitoka Chuo cha Dar es Salaam pekee na walikuwa walimu 610. Hao ndiyo Walimu wenyewe Shahada waliokwenda shulenii. Mwaka huu Walimu wenyewe Shahada watakaokwenda shulenii wanafikia 12,124. Watu lazima waone hatua hii kubwa ya Serikali ya kuongeza kuanzia Walimu 610 kufikia 12,124.

Tutaendelea kuboresha hali ya Walimu, mazingira yao ya kufanyia kazi kwa kujenga nyumba zaidi za Walimu kama ambavyo imewekwa katika mpango wa MMES II kuangalia na kuweka mazingira ya kufanyia kazi katika madaraja ili wale ambaao wanafanya kazi katika madaraja magumu waweze kupewa mafao zaidi ya kuweza kumudu hali zile. Lakini napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba hatua zote zinazohitajika kuchukuliwa zimechukuliwa ili kuhakikisha kwamba tunatatua tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubora wa wanafunzi wetu pia unaweza pia kupimwa wakishindana na wanafunzi wengine. Kwa mwaka 2009 kulikuwa na mashindano ya Insha katika Shule za Sekondari za nchi za *SADC*.

Katika mashindano hayo, wanafunzi wa Tanzania wawili walishinda mashindano yao katika nafasi ya kwanza na nafasi ya pili. Mwanafunzi wa kwanza alikuwa Allen Kamnde kutoka *Maua Seminary* na Mwanafunzi wa pili anaitwa Hilda Hingira kutoka Shule ya Wasichana ya Machame. Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kulikuwa na mashindano ya Insha kwa wanafunzi wa Sekondari pia na mwanafunzi wa tatu kwa ushindi katika mashindano haya ni mwanafunzi Peter Emil anatoka kwenye shule yangu mwenyewe niliposoma mimi ya *Tosamaganga Secondary School*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, mwanafunzi Happiness Watimanywa kutoka *St. Constantine Secondary School* wa Arusha amekuwa mwanafunzi wa kwanza katika nchi za *Commonwealth* katika mtihani wa *Accountancy* uliofanywa Juni, 2009 ambaao umetolewa na *University of Cambridge Examination Syndicate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la mafao ya pensheni ya Walimu wa Vyuo Vikuu. Napenda kuungana na wasemaji wote. Mheshimiwa Kilonsti Mporogomyi, Mheshimiwa Susan Lyimo na Waheshimiwa Wabunge wengine wamelisemea suala kwa hisia na uchungu sana.

Napenda kulieleza suala hili kidogo kwamba wachangiaji katika Vyuo Vikuu, wachangiaji wa mafao ya uzeeni wote wanachangia asilimia tano ya mishahara na Serikali inachangia asilimia 15. Uchangiaji huu ni sawa na ule wa wanaochangia wafanyakazi wa Serikali za Mitaa na Wafanyakazi wa Serikali Kuu ambao mafao yao yanatolewa na *LAPF* na *PSPF*.

Pili, napenda nieleze kwamba mafao ya SSSS ni asilimia 25 ya mkusanyiko wa mafao yote ambayo yamechangiwa kwa mfanyakazi anapostaafu. Asilimia 25, na hawapati pensheni. Hivyo hivyo kule *PPF* mafao pia yalikuwa ni asilimia 25 kwa mkupuo wakati mtu anaondoka kwenye kazi.

Sasa haya unalinganisha na asilimia 50 kwa wafanyakazi wanaochangia *PSPF* na *LAPF* na *pension factor* zile fedha za kila mwezi wanachukua mafao yote wanatoa mkupuo halafu wanagawanya kwa moja ya 500. Kwa SSSS hakuna pensheni kwa *PPF* wanagawanya kwa 100 ya 960.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mshahara wa kuweza kukokotoa pensheni ni mshahara wa mwisho wa mfanyakazi wa *LAPF* na *PSPF*. Lakini kwa *PPF* ni wastani wa mishahara wa miezi wa miaka mitano. Kwa hiyo, utaona kwamba wafanyakazi wa Vyuo Vikuu walikuwa wanapunjwa sana katika mafao ya pensheni na mimi nakubaliana na wote mliese maamuzi kama ifuatavyo:-

Kwanza mkupuo kwa ajili ya wafanyakazi wa SSSS na *PPF* itakuwa ni asilimia 50 kama ilivyo kwa *LAPF* na *PSPF*.

Pili, wafanyakazi wa SSSS ambao ni kama mimi na mimi nilikuwa chini ya utaratibu huu watapata pensheni kupitia *PSPF*. Halafu *pension factor* ya *PPF* itarekebishwa iwe moja ya 600 kama ambavyo Sheria ya Pensheni ilivyorekebishwa na *commutation factor* itakuwa ni miaka 15 kama ilivyo kwenye *LAPF*.

Kwa hiyo, tatizo hili limetatuliwa na Serikali yamebaki mambo madogo madogo ambayo ni ya kufanya ili kuhakikisha kwamba Shirika la *PPF* lenyewe linaweza kutekeleza maagizo haya ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Bodi ya Mikopo na madaraja mengi, mtakumbuka kwamba Bodi ya Mikopo imekuwepo kwa miaka mitano. Hili ni Shirika

ambalo ni jipya kabisa na ambalo limeingia katika kuwapa wanafunzi mikopo na katika kipindi cha miaka mitano kwa kweli limefanya kazi kubwa na nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho, Serikali pia imetoa fedha nyingi sana za kugharamia mikopo. Fedha za mikopo zimeongezeka kutoka shilingi bilioni 56 miaka mitano iliyopita na katika Bajeti hii fedha hizo zimefikia shilingi bilioni 239.

Kwa hiyo, ni hatua kubwa sana. Madaraja yale yaliyokuwepo yaliongezwa kwa sababu ya mapendekezo yaliyofanya na wadau wanafunzi wenye wakiwemo na Waheshimiwa Wabunge, kama mtakumbuka katika Bajeti ya mwaka 2008/2009. Hii inafanya ile *means testing* kuwa *accurate* zaidi kuliko ambavyo imekuwa huko nyuma. Sasa kumekuwa na matatizo ya mikopo kufika kwenye Vyuo Vikuu kwa wakati.

Mheshimiwa Rais alipokuwa anazungumza na wanafunzi wa Vyuo Vikuu hivi juzi alituagiza kwamba fedha za mikopo zitatengwa. Zitakuwa *right from the very beginning*, kuanzia mwanzo kabisa wa mwaka wa fedha. Kwa hiyo, tatizo hili kuanzia mwaka huu wa fedha litaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na michango mingi sana na ile ambayo kwa kweli mtu unajisikia kuitolea majibu kwa sababu michango yenye inaangalia sana mbele na jinsi ambavyo tutaondoka hapa kwenda huko. Moja ya michango hiyo ni suala la kuingiza sayansi na teknolojia katika mafunzo yetu ya Vyuo Vikuu na namna ya kurekebisha hali mbaya ya Vyuo Vikuu tuliyonayo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuwaambia wananchi wote wa Tanzania kupitia kwenye Bunge lako Tukufu kwamba Serikali iko katikati ya mchakato wa kuandaa mpango wa miaka kumi wa Maendeleo ya Elimu ya Juu. Mpango huu utaangalia ukarabati wa miundombinu ya Vyuo Vikuu, kujenga maabara katika Vyuo Vikuu, kujenga karakana mpya, kujenga kumbi za miadhara, kujenga *hostel* na kupanua elimu ya juu.

Katika kazi hii, Serikali imejipanga vizuri na itaanza kujenga hospitali ya kufundishia ya Chuo cha Afya Muhimbili na Sayansi Shirikishi katika eneo la Mlonganzira. Chuo Kikuu cha Dodoma kinaendelea kupanuliwa na ukamilishaji wa Chuo cha Afya utafanyika katika mwaka huu wa fedha na ukamilishaji wa ujenzi wa Chuo cha Sayansi za Ardhi utaendelea kufanywa na kukamilishwa jinsi tunavyokwenda.

Lakini kama ambavyo mnajua katika kipindi cha mwaka 2010/2015 tumeanzisha Chuo cha Sayansi ya Kilimo katika Mji wa Songea karibu na Uwanja wa Ndege pale Songea Mjini na tutaanzisha Chuo Kikuu cha Mwl. Nyerere cha Sayansi za Kilimo ambacho kitajengwa kule Musoma na Vyuo Vikuu vingine kama Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia kule Mbeya kitajengwa ili kuhakikisha kwamba tunapambana na changamoto za maendeleo ya Taifa na kujenga Taifa lenye uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewashukuru sana Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi ambaye alileta taarifa ya matatizo katika Shule ya Sekondari kule Kasulu

Magharibi inaitwa Mharuro na ambayo tulipelekea timu ya wataalam wakaenda kuangalia hali ilivyo na walipokuwa kule wakatuletea taarifa na napenda kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba matatizo yale yalitatuliwa na kuwekwa kando.

Pili, tumemsikia Mheshimiwa Joyce Masunga na maelezo yake kuhusu Afisa wa Elimu katika eneo lile na matatizo ya Walimu kuhamishwa. Tutapeleka timu ya wataalam na nitumie fursa hii kumwagiza Mkurugenzi wa Ukaguzi aunde timu hiyo iweze kwenda Shinyanga mara moja ili iweze kuangalia tatizo hilo kwa undani na kutupa mapendekezo ya hatua za kuchukua ili tuweze kurekebisha hali aliyoitaja alipokuwa anazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilizungumzwa pia kuhusu vigezo gani ambavyo vinatumika kutoa *OC* na fedha za maendeleo katika Vyuo Vikuu. Vigezo ni pamoja na wingi wa wanafunzi, wingi wa watumishi, miundombinu ilivyo na hali yake. Fedha inayotolewa kama *OC* kwa Vyuo na hali ya fedha ambayo imepatikana kutoka kwenye Bajeti. Hali ya Vyuo Vikuu vyetu vile vya zamani ni mbaya sana na ndiyo maana tumechukua hatua ya kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Juu.

Ninategemea mpaka ikifika tarehe 20 Mei, 2011 karibu na mwisho wa *financial year* hii ambayo tunakwenda nayo sasa, mpango huo utakuwa umekamilika na mchango wa Serikali utakuwa umepatikana au umetengwa pamoja na mchango wa washirika wetu wa maendeleo ili tuwe na Mpango wa Elimu ya Juu ambao ni sawa na huu Mpango wa Elimu ya Sekondari ambao tumeutangaza hapa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, yako mambo mengi ambayo yamechangiwa katika kabrasha hili na napenda niwaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba michango yote ni muhimu sana kwetu, tutaiweka katika bango zuri ambalo kila mmoja wetu anaweza kuona mwenzie alikuwa amechangia nini na kutoa majibu ambayo yanalingana na michango hiyo.

Hata hivyo, kwa kuwa muda bado ninao, napenda nitoe maelezo machache mpaka hapo nitakapofikia ili yale ambayo yatakayobaki tuendelee kuyaleta majibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Madeje aliuliza kama Wizara ya Elimu itenge fedha ya kutosha ili kuondoa tatizo la wanafunzi wa Shule za Msingi kukosa madawati. Majibu ni kwamba katika mwaka wa fedha 2009/2010 jumla ya Sh. 3,955,000,000/= zimetengwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo zikiwemo za ununuzi wa madawati kwa Halmashauri zenye upungufu. Aidha, kati ya fedha hizi, matumizi halisi yatakuwa shilingi bilioni 2.028.

Mheshimiwa Mwinchoum Msomi alitoa mawazo kwamba kuna upungufu wa madawati katika shule za msingi hususan Jimboni kwake kule Kigamboni na napenda kueleza kwamba jibu lake ni sawa na Mheshimiwa Madeje wa Dodoma Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani ilieleza juu ya uhaba mkubwa wa Walimu hasa vijiji. Uhaba wa Walimu na Walimu wanaofundishwa katika Vyuo vyetu mbalimbali tumeutoa na kueleza wazi kwamba tutaendelea kuboresha mazingira ya vijini

kwa kujenga nyumba za Walimu na kupeleka Walimu wengi zaidi katika Elimu ya Msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha hatutawapangia walimu wa shule za msingi katika maeneo ya mijini kwa sababu maeneo ya mijini yana walimu wengi na walimu wote 14,501 ambao watahitimu mwaka huu tutawapanga katika maeneo ya vijiji na hasa yale ambayo yana uhaba mkubwa wa walimu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Ruth Msafiri wa Muleba Kaskazini na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee wa Kiwani Zanzibar na Mheshimiwa Profesa Idris Ali Mtulia, wameomba Serikali itoe angalau mlo mmoja kwa kutwa kwa wanafunzi wanapokuwa shulenii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa ni Halmashauri kumi na sita ambazo zinahudumiwa na mpango wa *World Food Programme* wa kulisha watoto katika shule zetu. Mpango huu umekuwa na matokeo mazuri sana ya kuongeza mahudhurio shulenii kupunguza mdondoko na kuboresha taaluma. Kwa hiyo, tumeona kwamba mpango huu ni mzuri na usambazwe nchi nzima. (*Makofî*)

Kwa hiyo, Wizara yangu inaandaa mpango kabambe ambao utatuwezesha kusambaza mpango huu katika shule zote za msingi na sekondari katika nchi yetu; na mpango huu unaandalialiwa na tunategemea kwamba Baraza la Mawaziri litaukubali ili uweze kutekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Paul Kimiti alisema Wizara idhibiti uhamisho wa walimu bila sababu za msingi hasa pale ambapo hakuna fedha. Serikali imetoa maagizo ambayo yako moja kwa moja, yanaeleweka moja kwa moja kwamba Afisa Elimu wa Wilaya haruhusiwi kumhamisha mwalimu pale ambapo hana fedha ya kumtoa kwenye kituo chake na kumpeleka kituo kingine kwa hiyo Maafisa Elimu ambao wanafanya hivyo tungependa mtueleze ili tuweze kuchukua hatua ambazo zinastahiki. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepewa hoja kwamba uboreshaji wa ufundishaji haujatiliwa mkazo unaostahili. Ningependa nirudie rai yangu hapa kwamba mwaka huu tulifanya Mkutano Mkuu wa Elimu wa dharula hapa Mjini Dodoma mwezi Februari mwaka huu, tukawekeana malengo ya kupandisha taaluma katika elimu ya msingi na elimu ya sekondari na tukawekeana malengo ya ukaguzi unaofanywa kuanzia Mwalimu Mkuu katika shule, Waratibu wa Kata na Maafisa Elimu wa Wilaya pamoja na Idara ya Ukaguzi. Kwa hiyo, tunategemea kwamba katika kipindi hiki cha mwaka 2010/2011 matokeo ya haya maazimio na usimamizi huu ulioongezwa utaonekana katika matokeo ya mitihani ambayo inakuja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo ya vitendo hayakupewa kipaumbele stahili. Katika elimu ya sekondari mafunzo ya vitendo yako hasa katika mafunzo ya sayansi na haya hutolewa katika maabara. Aidha, mafunzo ya vitendo pia hutolewa kwa wanafunzi kufanya safari katika mazingira yao walipo na kuangalia ni vitu gani vilivyopo kule. Kwa

hiyo, hilo la pili linatekelezwa kikamilifu, lakini la kwanza litatekelezwa kwa kuongeza maabara chini ya mpango huu wa MMES ambao tumeutangaza leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda umekwisha, ningependa kwanza niwashukuru wachangajia ambao bahati mbaya hatukuwataja ambao ni Mheshimiwa Riziki Omar Juma na Mheshimiwa Bakari Shamis Faki ambao tulikosea jina lako tukasema Bakari Hamis Faki, ni Bakari Shamis Faki, ndilo nimeletewa hapa. Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, tunakuomba radhi kama kuna makosa katika hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yote ambayo yamebaki, tutayajibu kwa maandishi. Naomba sana kupitia kwako kuwa Waheshimiwa Wabunge watupitishie Bajeti hii ya Elimu kama ambavyo tumeomba ili twende kazini na kuboresha elimu kama ambavyo ni ndoto ya Watanzania wote. Naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki! (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa Iamuliwe*)

## **KAMATI YA MATUMIZI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **Fungu 46 – Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı**

Kifungu - 1001 *Administration and General* .....Sh. 28,822,235,300

**MHE. DR. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu ananihujumu, kila nikisimama inakataa! (*Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Mavuvuzela hayo! (*Kicheko*)

**MHE. DR. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mavuvuzela hao!

Nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kuuliza swali. Sina nia ya kuchukua mshahara wa Waziri moja kwa moja, najua Waziri atalijibu vizuri na atalijibu kwa kuzingatia kuwa mimi ni mwalimu mzoefu, mwalimu wa walimu.

Swali langu ni kuwa kwa kuwa kwa muda mrefu nimekuwa nikizungumza na Waziri na Naibu Waziri kuhusu hali halisi ya walimu katika Wilaya ya Ukerewe na nikatoa mapendekezo bila kudai malipo ya *consultancy*. Nikatoa mapendekezo ya kwamba Chuo cha Mrutunguru kiongeze idadi ya wanafunzi wanaotoka katika Wilaya ile wakizingatia kwamba walimu wengi wanaogopa kuvuka yale maji na hivi karibuni tulipata ajali ambayo tulimpoteza mwalimu mmoja. Kwa hiyo, wengi wanaogopa kuja

katika Wilayaile. Je, kwa nini hawa ndugu zangu, walimu wenzangu wamedharau kabisa mapendekezo ambayo niliwapa bila kudai malipo?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii.

Kwanza, ningependa nisahihishe kuhusu suala la *pension* ya walimu wa Vyuo Vikuu ambayo nilisema walimu wa SSS kuwa *pension* yao italipwa na PSPF. Nilikuwa na maana ya kusema italipwa na PPF. Kwa ajili ya *Hansard* nilikuwa naomba masahihisho hayo yafanywe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mheshimiwa na Dada yangu Dr. Getrude Mongella tumepata kuzungumzia juu ya kuongeza wanafunzi pale Mrutunguru wanaotoka katika Visiwa vya Ukerewe. Sasa kwanza niseme tu kwamba nia yetu ya kuchanganya wanafunzi kutoka nchi nzima ni katika kujenga Utaifa na tulikuwa tunapenda Watanzania wengi iwezekanavyo waweze kwenda na kujua mazingira ya kule Ukerewe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hatuna tatizo la kuongeza wanafunzi wanaotoka katika Visiwa vya Ukerewe na visiwa vingine katika chuo kile ili wawe wenyeji wa wale wengine wageni ambao watakuja. Kwa hiyo, suala hili nilikuwa ninamuomba Mheshimiwa Mbunge tulizungumze na tuone ni jinsi gani tunaweza kulitekeleza. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana! Sasa kwa vile mliosimama mlikuwa wengi, mtakuwa mkiuliza wawili wawili. Nianze na upande huu, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi halafu utafatiwa na Mheshimiwa Suraju Kaboyonga, halafu Mheshimiwa Waziri atatoa ufanuzi.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mnwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ni rafiki yangu sana huyu, alitoa ahadi kwamba Wilaya ya Makete na Ludewa zingepewa kipaumbele katika ujenzi wa VETA (Vyuo vya Ufundi). Nashukuru kwa sababu mwenzangu wa Makete mwana Njoloma mwenzangu ameanza kujengewa. Mimi imekuwa matataizo kweli lakini *at last* tarehe 3 mwezi uliopita viongozi wa VETA Makao Makuu na VETA Kanda ya Nyanda za Juu walikuwa Ludewa tarehe 3 ku-sign, kuzungumza na Halmashauri kuhusu kuanza ujenzi huo na tulikubaliana kwamba mkataba wa kukubaliana uwe *signed* katikati ya mwezi uja na ujenzi uweze kuanza mwezi Oktoba mwaka huu. Sasa kwa vile lugha niliyoisikia hapa Waziri hasa Naibu Waziri anazungumza kwamba kama fedha zinapatikana, tutaendelea na ujenzi. Nilitaka tu Waziri baada ya kuchelewa kwa muda mrefu wote huu anithibitishie kwamba hayatakuwa maneno matupu, sasa kweli mwezi Oktoba Chuo cha Ufundi VETA Ludewa kinaanza kujengwa kwa sababu maandalizi yote yako tayari. Ahsante sana.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nilitaka kufahamu ni lini Serikali itaanza kuwalipia wanafunzi wa sekondari karo au shule za sekondari wanafunzi waweze kusoma bure. Ukiangalia katika nchi zetu za Afrika Mashariki, ukiangalia Kenya, Uganda, Burundi,

wanafunzi wamekuwa wakilipiwa karo na Serikali, na nchi yetu ina rasilimali ya kutosha na sioni sababu ya wanafunzi kushindwa kusoma kwa sababu ya karo. Mheshimiwa Waziri, naomba ufanuzi.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge hawa wawili kwa maswali yao mazuri. Kuhusu *VETA* kule Ludewa, hakuna shaka juu ya hatua za ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Ludewa. Hatua ya *ku-sign* mkataba katikati ya mwezi Agosti itafanywa na ujenzi utaanza kama ulivyopangwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya CCM inapenda sana wananchi wachangie katika huduma za jamii ambazo na wenyeze zinawafaidisha ikiwa ni pamoja na elimu. Lakini kama unavyojuua Serikali imetuwa inaondoa mzigo huu wa ada kwa wananchi hatua kwa hatua. Hatua ya kwanza, mwaka 2004 Serikali ilipunguza ada ya elimu ya sekondari kutoka shilingi 40,000 kwa mwaka kufikia shilingi 20,000 na mwaka huu wa 2010 Serikali imewapunguzia wananchi mzigo wa wa ada ya mitihani katika shule zote za Serikali za Sekondari katika kidato cha pili, cha nne na kidato cha sita. Kwa hiyo, kwa jinsi ambavyo uwezo wa Serikali utaongezeka itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuwapunguzia wananchi mzigo na kuhakikisha kuwa watoto wengi iwezekenavyo wa Tanzania wanapata elimu hiyo ambayo kwa kweli ndiyo msingi. (*Makofi*)

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo furaha kumpongeza sana Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya ambaye alikuwa anatunukiwa *Ph.D* yake ya Uzamivu katika masuala ya Biashara na suala hilo kwetu tumeliona ni suala zuri na tumeshangaa kuona kwamba ametunukiwa na Chuo cha Califonia wakati Tanzania tuna vyuo kama hivyo na havijawahi kutambua michango mizito kama hiyo ya Wabunge. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kufuatalilia michango mikubwa iliyofanywa na Waheshimiwa Wabunge ambayo haijatambuliwa na kuweza kupewa sifa kama hizo kwa manufaa ya nchi?

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa na hoja mbili. Kwanza ni shule ya sekondari ya Mpwapwa ambayo ina matatizo makubwa ya usafiri ni miaka mingi sana. Nimelalamika hapa Bungeni na Serikali ilikuwa imeniahidi kwamba Shule ya Sekondari Mpwapwa ingepata usafiri, gari ambalo liko pale liko juu ya mawe. Lakini la pili Chuo cha Ualimu Mpwapwa kuna wanafunzi zaidi ya 1,000. Tumeletewa lori ambalo ni bovu, lilikuwa linatumika Chuo cha Ualimu Chang'ombe zamani tukaletewa pale Mpwapwa. Kwa hiyo, gharama za matengenezo ni kubwa. Kwa hiyo, naiomba Serikali isaidie usafiri Shule ya Sekondari Mpwapwa pamoja na Chuo cha Ualimu Mpwapwa.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana kwa maswali haya mawili. Swali la kwanza nitalijibu na swali la pili atalijibu Mheshimiwa Mwantumu Mahiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niungane na Mheshimiwa *Engineer Stella Manyanya* kumpongeza Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya kwa kutunukiwa Shahada

ya Heshima ya Udaktari wa Falsafa. Shahada hizi zinatolewa kwa ridhaa za Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu hivi vimeundwa na vimepewa hati, idhini au *charter* pamoja na idhini ya kutoa shahada aina mbalimbali. Shahada ya kwanza, Shahada ya pili ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu, nje ya hapo zimepewa pia mamlaka ya kutoa Shahada za Uzamivu ambazo zinaendana na fani ambayo mwanazuoni amesomea na kuzamia huko. Aidha, zinatoa pia Shahada za Uzamivu kwa watafiti ambao utafiti wao umeleta maendeleo ambayo ni ya kipekee katika fani hiyo *to make a significant contribution to knowledge*.

Sasa hizo ni shahada ambazo una-*earn* kwa kufanya kazi, sasa ziko shahada ambazo watu mashuhuri waliochangia katika maendeleo ya binadamu labda mtu amechangia katika kuhakikisha kwamba anaondoa Malaria kwa mfano Shahada ya Heshima ya Udaktari wa Falsafa aliopewa Dr. Amani Abeid Karume, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar alipewa Shahada ya Heshima ya Udaktari wa Falsafa na Chuo cha Kumbukumbu za Hurbert Kairuki amepewa Shahada ya Heshima ya Udaktari wa Falsafa kwa sababu ya juhudhi zake za kutokomeza Malaria katika Visiwa vya Zanzibar na Pemba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile ni kazi kubwa ambayo imeleta mabadiliko makubwa sana katika eneo lile na amepewa Shahada ya Heshima ya Udaktari wa Falsafa Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, ni mtu *special* sana, kwanza amefanya kazi sana hapa Bungeni amekaa hapa zaidi ya kila mmoja wetu na Vyuo Vikuu vyote duniani vinaweza kumfikiria kwa kumpa Shahada ya Heshima sasa chuo hiki cha Marekani kimemuona. (*Makofi*)

Kwanza tumpongeze kwanza tumpongeze kwamba ameonekana na Chuo hicho na tuvihusie Vyuo Vikuu vyetu viangalie watu wetu wengine ambao wamepata shahada hizo, lakini tusivilazimishe kutoa Shahada ya Heshima ya Udaktari wa Falsafa kama wanasiisa, sisi tuwaachie wataalamu wetu watumie *charter* zao, watumie sheria iliyopo wakati wa kutathimini ni nani apewe Shahada ya Heshima ya Udaktari wa Falsafa. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Lubeleje kama ifuatavyo, ingekuwa ni jambo jema sana endapo Bajeti yetu ingekuwa kubwa na pana, kwani tungependa kila shule ya sekondari ipate usafiri. Kutokana na ufinyu wa Bajeti nasikitika kusema kwamba kwa sasa haiko kwenye kipaumbele, hata hivyo Chuo cha Ualimu kina gari aina ya *Toyota Hardtop*, mimi namuomba tu Mheshimiwa Mbunge avute subira ili tuangalie hivi vipaumbele vyetu tulivyonyavyo, tukivuka hapo tukakwenda kwenye usafiri. (*Makofi*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Naibu Waziri Mheshimiwa Mwantumu Mahiza kwa imani aliyoonyesha kwa hawa wastaafu na kuamua kufunga mjadala katika hoja hiyo. Lakini pia katika mchango wangu

wa maandishi nilikuwa nimeomba Serikali angalu itoe tamko tu kwa sababu walimu mpaka sasa hivi hawajui mishahara yao angalau zipelekwe *scale* za mishahara ya zamani, na ya sasa walimu wajijue wana mishahara kiasi gani lakini pia niliwaomba kwamba ni usumbufu mwalimu anapohamishwa wananyimwa pesa za uhamisho na Maafisa Elimu wanaambiwa kuwa wewe umeenda hatua chache wangetoa ufanuzi hapa wanatakiwa walimu wahamishwe kwa umbali gani ndipo walipwe hela ya usumbufu.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Wizara kwa kulipa shilingi bilioni 12 katika ya shilingi bilioni 26 ambazo walimu wanadai na shilingi bilioni 13 ambazo ni zaidi ya nusu ya madai yanayoonekana kama vile ni *fake*, sasa labda Waziri anaweza kutueleza ni jinsi gani amejiandaa ku-solve hilo tatizo, ninachotaka kuuliza hii inanitia wasiwasi hii Bajeti ya *Higher Education*. Ukiangalia Mheshimiwa Waziri anatuambia ame-ring face shilingi bilioni 236 ambayo ni karibu nusu ya Bajeti yake, nilikuwa nachungulia hivi vitabu sioni mahali popote ambapo nitaona shilingi bilioni 236 kwa mkopo sasa hii hiki kitu uwazi wake uko wapi na anaweza kutuonyesha ni wapi katika vitabu hivi hiyo pesa inaonekana ya shilingi bilioni 236?

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari ya kutokuwa wazi inatuletea baadaye hoja za ukaguzi lakini pia kwa sababu hili ni jambo la kudumu unapoona kuwa karibu shilingi bilioni 576 ndiyo zimekopeshwa katika miaka mitano na marejesho ni shilingi bilioni tatu tu, kwa hiyo, inaonyesha wazi kuwa hii bodi itaendelea kula kasma kubwa sana ya Bajeti ya elimu, nilikuwa nashangaa labda baadaye kama itafaa kuwa tuwe na *vote* yake maalum ili tuende tuone kuwa *movement* ya zinazoingia na zile zinazotoka kwa ajili ya ufanisi na kuhakikisha kuwa kuna fedha ya kutosha kwa ajili jambo hili muhimu la kuweza kuwapa vijana mkopo waweze wakasoma elimu ya juu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Diana Chilolo kuwa mtumishi yeote anapoajiriwa anapaswa katika barua yake ile ya awali tunaita *first appointment* inapaswa kumuonyesha mshahara wake atakaolipwa na daraja lake, kwa hiyo hivyo hivyo Maafisa Utumishi wote nchini wanalo jedwali linaloonyesha kiwango cha kuanzia cha mshahara na kile cha mwisho cha daraja hilo au kwa taaluma hiyo aliyonayo sasa inasikitisha kidogo kama maafisa wetu hawafanyi hivyo, lakini pia kulikuwa na kitu kingine kwamba walimu wanapata mishahara, hawafahamu hiyo maana yake ni *salary slip* basi mimi nitoe wito nikishirikiana na wenzetu utumishi pamoja na TAMISEMI kwamba *salary slip* ni haki ya mtumishi, tunaomba wapatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umbali unaostahili mtumishi kulipwa anapohamishwa kama tunavyozifahamu taratibu zinasema endapo mtumishi atahamishwa siyo zaidi ya kilomita na nane malipo hakuna. Sasa kama kilomita nane hizi kwa baadhi ya maeneo zinaweza zikawa na *impact* tofauti mimi hapa naomba niseme hekima zitumike. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ufanuzi kuhusu suala la Mheshimiwa Cheyo?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru kaka yangu Mheshimiwa John Cheyo. Suala lake hili liko kwenye *sub vote 7001* eneo la 270900 pale shilingi 243,266,608,000 liko pale sasa hiyo ya kwanza lakini la pili, ni hii ya marejesho, ni kweli kabisa kuwa urejeshaji wa mikopo umekuwa ni tatizo na kwamba Sheria ile ambayo imetungwa kwa ajili ya kuanzisha *Higher Education Student Loans Board* ina *loop holes* ambayo inawafanya wakopaji wapotee bila kuzingatia ulipaji wa mikopo yao kwa hiyo tumechukua hatua mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaangalia uwezekano wa kutoa mikopo hivi sasa kupitia kwenye vyombo vya fedha kwa sababu mzigo kwa Serikali unaendelea kuwa mkubwa sana. Mwaka kesho yaani 2011/2012 mahitaji yatakuwa zaidi ya shilingi bilioni 350 ambayo kwa kweli haibebeki kwa hiyo tumetengeneza rasimu mpya ya utoaji wa mikopo na inajadiliwa na wadau itafikisha kwenye Baraza la Mawaziri na ikishapitishwa mazungumzo ya kina yatafanywa ili kuanzia wakati huo tuweze kutoa mikopo kupitia kwenye vyombo vya fedha, la pili, tutabdalisha sheria ile ili sasa iwe kama Sheria ya *TRA* ambayo inakuwa na *access* na mishahara na maelezo mengi kuhusu *individuals* ambao wamekopa ili waweze kulipa hata wale ambao hawajalipa mpaka sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningesema nimeelezwa kuwa kama kuna walio humu ndani ambao wanadaiwa basi wajihimu ili waweze na wenywewe kurejesha na wale ambao wako katika ajira mbalimbali sasa wajitokeze ili waweze kulipa. Tulitoa orodha yao huko nyuma kwenye magazeti, tutaendelea kuitoa ili muweze kuwajua watu ambao wanakwepa majukumu yao na waweze kujisikia vibaya waanze kulipa, lakini mwaka kesho wale ambao mtarudi hapa tutatengeneza Sheria ili kuweza kuwabana wale wote wanaokwepa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Profesa. Mheshimiwa anachoongelea ni wale wadaiwa wote waliomaliza vyuo tangu mwaka 1994. Wengine tuliwahi kidogo Mheshimiwa Fatma Mikidadi atafuataiwa na Mheshimiwa Godfrey Zambi.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilisema kuwa ujenzi wa mabweni katika shule za sekondari kwamba watoto wengi wanapokuwa wamefika katika shule za sekondari wamekuwa tayari ni watu wazima sasa, shule zenyewe ziko mbali kidogo kwa hiyo, kutembea kutoka shule hadi shule pale ndipo wanapata matatizo ya kupata wanaume na kutembea mitaani na hivyo hupambana na mimba.

Sasa je, Serikali itatusaidiaje kwa sababu mpaka sasa ni taasisi, watu binafsi ndiyo wanaosaidia kujenga shule za sekondari kwa mfano kwetu Ngongo, Lindi mjini, mama Salma Kikwete ameweza kutusaidia sana kujenga mabweni ambayo yanaingiza wanafunzi zaidi ya mia moja, kwa kweli tunamshukuru, sasa tunaomba Serikali iweze kutusaidia kwa suala hilo vinginevyo nashukuru kwa kutujengea *VETA* na vilevile nashukuru kwa shule ya sekondari Mbekenyera, Ruangwa. Ahsante sana.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Bajeti ya mwaka 2007/2008 aliyejekuwa Waziri wa Elimu wakati huo Mama Margaret Sitta alitangaza kuwa Mbozi itakuwa moja ya Wilaya 28 ambayo ingejengewa Chuo cha VETA. Nimesikiliza majibu ya Serikali hapa hayajatoa matumaini yoyote lakini pia namuomba Mheshimiwa Waziri ajue kwamba Mbozi ni moja ya Wilaya kubwa katika Mkoa wa Mbeya ambayo inapeleka vijana wengi sana sekondari na wengi wanamaliza darasa la kumi na mbili na wanashindwa kupata nafasi za kuendelea mbele kwa hiyo, tungekuwa na Chuo cha Ufundı VETA kingeweza kutusaidia sana maana vijana wangeweza kupata mafunzo katika nyanja mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu Mheshimiwa Waziri aliahidi naomba leo awaeleze wananchi wa Wilaya ya Mbozi kwamba kile chuo ambacho tayari walishatueleza mwaka 2007 maendeleo yake ni nini? Naomba ufanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Serikali kwa kushirikiana na wananchi ndiyo iliyojenga shule za Sekondari za Kata. Hivyo hivyo ujenzi wa hosteli hupaswa kufanywa kwa kushirikiana kwa taarifa tulizonazo wenzetu wa TAMISEMI mbao sasa ndiyo walezi wa hizi shule, wameupelekea Mkoa wa Lindi na hususani Wilaya anayoizungumzia kiasi cha shilingi milioni 250 ambazo wanapaswa kupangana wao wenye wapi wajenge hosteli. Lakini tu naomba nitoe rai fedha hizi hazitoshi kukidhi ujenzi wa bweni kwa kumpa mkandarasi kosa ambalo linafanya na Halmashauri nyingi, fedha zote zinazokwenda zinapaswa zichangiwe na nguvu za wananchi ukimpa mkandarasi kazi haiishi.

**MWENYEKITI:** Kabla ya kuendelea na ufanuzi wa swali la Mheshimiwa Godfrey Zambi niseme tu kuwa muda wetu ni dakika kumi kabla kufikia muda wa kumaliza muda wa mambo yetu hapa. Kanuni yetu ya 104 inasema iwapo imesalia dakika kumi kabla kufika muda wa kuahirisha Kikao cha Bunge na Kamati ya Matumizi na iwapo Mwenyekiti hajamaliza kupitisha mafungu, Mwenyekiti anaweza kuongeza muda usiozidi dakika 30 bila kuihoji Kamati ili kumaliza shughuli ya kupitisha mafungu yaliyobakia kwa hiyo, naongeza dakika 30 maana yake ni mpaka saa mbili na robo bila kuwahoji. Mheshimiwa Naibu Waziri tuendelee na ufanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi kuhusiana na suala alilouliza Mheshimiwa Zambi kuhusiana na ujenzi wa Chuo cha VETA Mbozi kama ifuatavyo:-

Kwanza niseme kwamba Wilaya ambazo zinajengewa Vyuo vya VETA ni zile ambazo hazina aina yoyote ya Chuo cha Serikali au cha Mashirika ya dini. Kwa hiyo, kama Mbozi ni mojawapo ya Wilaya za aina hiyo basi Mbozi iko kwenye utaratibu huo na Wilaya hizi ziko 28 na kama Mbozi ndiyo hivyo na kwa kuwa taratibu za awali zimeshaanza ambazo ni pamoja na kukamilisha kubaini ujuzi unaohitajika, uchoraji wa ramani na kwa hali hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa chuo hicho kitajengwa, dhamira ipo, tunachosubiri ni kupata fedha na tumepewa ushauri pia kuwa

tujaribu kutafuta vyanzo vingine vya fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyuo hivyo. Kwa hiyo, wananchi wa Mbozi watuamini kwa hilo.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kwimba ni moja ya Wilaya ambayo haina Chuo cha VETA na kwa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuwa kama labda kuna chuo lakini kwa bahati nzuri hatuna Chuo cha VETA cha Serikali na hatuna chuo cha aina yoyote ile. Serikali kwa kuwa tayari imeshafanya utafiti kiwanja kipo kwa maana ya eneo, walishakuja wakapima na kila kitu kimeshakamilika ni lini sasa Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga Chuo cha VETA katika Wilaya ya Kwimba. Naomba maelezo na ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri jibu la Mheshimiwa Richard Ndassa, linafanana na jibu nililompa Mheshimiwa Godfrey Zambi wa Mbozi kwamba kama Wilaya ya Kwimba ni moja kati ya Wilaya zile 28 ambazo hazina aina yoyote ya Chuo cha Ufundi ukweli ni kwamba kama alivyosema eneo lipi basi Chuo hicho mimi ninaamini kuwa kitajengwa.

Naomba tuendelee kwa sababu tunajua kuwa awamu hii pesa ya kujenga vyuo itapatikana baada ya awamu hii kwa sababu bado tunaendelea na mwaka wa fedha ambao ungetupatia fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyuo kwa hiyo, bado hatujakata tamaa kuhusiana na ujenzi wa vyuo hivi ikiwemo Wilaya ya Kongwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutawapatia orodha ya Wilaya hizi 28 ambazo zinahusika na ujenzi huo wa vyuo vya VETA.

**MHE DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kwa kuongea hapa ndani nilikuwa nimeishukuru sana Serikali kwa maamuzi yake ya kujenga Chuo cha VETA, Wilayani Makete, lakini nikaomba msaada kwamba Halmashauri imepeleka maji kwenye *site* na Halmashauri imepeleka barabara kwenye *site* ili kuharakisha ule ujenzi inatakiwa umeme uende pale, Halmashauri katika vyanzo vyake ilionekana kama inapwaya kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaomba msaada kwamba ili kuharakisha ule ujenzi na kutimiza azma ya Mkurugenzi kwamba kile chuo kianze mwezi wa kumi na mbili Wizara ione namna ya kutupelekea umeme ili kuharakisha ujenzi wa Chuo cha VETA. Naomba ufanuzi.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge kwamba matayarisho ya awali yamefanyika kwa ajili Wilaya 28 ambapo eneo la ujenzi limeshatambuliwa katika kila Wilaya, ardhi imepimwa na michoro kwa ajili ya VETA ambazo zitajengwa katika maeneo hayo yote imekamilika, tumetengeneza *proposal* kubwa kwa ajili ya kuomba fedha kwa ajili ya VETA, hizi Wilaya 28 na tupo mbioni kabisa kupata fedha hizo. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba hizi zote 28 zitajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la msingi alilouliza Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge napenda kumhakikisha kwamba umeme utawekwa punde, majengo yatakapofikia kiwango ambacho kinahitaji umeme na gharama hizo zitachukuliwa na VETA.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mimi nimechangia kwa maandishi, katika mchango wangu nilikuwa naongelea juu ya walimu ambao wameshastaafu lakini kwa bahati mbaya mahesabu yao walipokuwa wanaandaliwa mafao yao ikashindikana katika Mfuko wa Utumishi wa Umma, kwa sababu michango iliyokuwa inatolewa na Serikali ambayo ni Wizara hii ilikuwa pungufu na kiwango kilichokuwa kinatakiwa na nikatoa mfano wa Mwalimu Charles Manoni ambaye alikuwa Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Ngudu, ambaye kwa bahati mbaya sana tangu mwaka jana mwezi wa sita amestaafu na hajapata chochote mpaka leo kwa sababu ya matatizo hayo. Je, walimu hao pamoja na huyu Charles Manoni mafao yao yatapatikana lini?

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza niwashukuru Waziri na Naibu Mawaziri wake kwa kuwa waungwana sana leo na kujibu kwa ufasaha. Aidha, naishukuru sana Serikali kwa kuvalia njuga suala la pensheni ya Wahadhiri wa Vyuo Vikuu hali iliyokuwa inawafanya Maprofesa wanapostaafu kuhemea *contracts* ambazo zilikuwa zinachukua muda mrefu sana kwa sababu pensheni waliyokuwa wanaipata kwa kweli ilikuwa ndogo sana kiasi kwamba wasingewenza kufanya jambo lolote zaidi ya kurudi kuomba *contracts* za kuendelea kufundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la msingi nilikuwa naomba kujua kwamba takwimu zinaonesha wazi kwamba Watanzania sasa hivi wamefikia asilimia 31 ya wajinga kwa kuwa hawajui kusoma, kuandika wala kuhesabu. Jambo hili ni baya sana na ni aibu kwa Taifa hasa ukizingatia kwamba tunaingia kwenye soko la Afrika Mashariki na ninaamini kabisa kama hali hii halitadhibitiwa tutakuwa na matatizo kama ilivyokuwa Afrika Kusini ambapo tuliona kabisa watu walivyouana kwa sababu ya kuona kwamba mataifa mengine yanakuja wanapata ajira na hili linaweza kuja kujitokeza kwa sababu Watanzania watakuwa nyuma kielimu na kwa maana hiyo hata ajira hawatapata na hawa wenzetu ndiyo watapata ajira hapa nchini.

Je, Serikali ina mikakati gani ya dhati ya kuhakikisha kwamba suala hili linapewa kipaumbele na vilevile tuone kwamba watoto wanaomaliza darasa la saba sasa wanajua kusoma na kuandika kwa sababu naamini kabisa hao ndiyo wanaoongeza idadi ya wasiojua kusoma na kuandika. Waziri anatoa tamko gani?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, mimi naomba kutoa ufanuzi kwenye swali la Mheshimiwa Bujiku Sakila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la walimu wastaaafu ambao wanapata mapunjo au kuchelewa kupata mafao yao kutokana na kutokupelekwa kwa michango yao tumelipata katika miaka miwili iliyopita. Naomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu mimi mwenyewe ndiye ninayesimamia suala hilo, na tumefuatilia kwa kushirikiana na Mhasibu Mkuu wa Wizara na tumeweza kugundua matatizo yalipo. Naomba nimhakikishie kwamba juhudzi zimefanyika na kwamba tunaamini baada ya Bunge hili wale wastaaafu wapatao 72 wenye tatizo hili watakuwa tayari kupata stahili zao. (*Makofit*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa pongezi alizotupa Mheshimiwa Susan Lyimo, juu ya pensheni za walimu na wawezeshaji na waendeshaji wa Vyuo Vikuu. Kuhusu Elimu ya Watu Wazima na elimu nje ya mfumo rasmi katika hotuba yetu hapa leo, tumeeleza hatua ambazo Serikali imechukua katika kupambana na changamoto hii ya Watanzania wengi kutokujua kusoma, kuhesabu na kuandika, tukishirikiana na Serikali ya Cuba, tumetengeneza mpango wa Elimu ya Watu Wazima, mpango wa kisomo unaojulikana kama ndiyo ninaweza (*Yes I can*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu ni mpango wenye masomo sitini na tano ambao umetumika Cuba na kuondoa kutokujua kusoma, kuandika na kuhesabu kabisa. Utaratibu huo utaanza mwezi Oktoba mwaka huu na utatumia redio na *television* na tunategemea kabisa kwa sababu baada ya Bajeti hii tutakuwa na fedha za kuanza kuhamasisha watu waweze kujiunga na kisomo tunategemea kabisa kwamba tutarudi pale tulipokuwa katika kiwango chetu cha kujuu kusoma kuandika na kuhesabu.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Wakati nachangia kwa maandishi nilieleza suala la walimu wa daraja la tatu A. Kwanza niipongeze Serikali wamekuwa wakitusaidia sana vijana wanaotoka Wilayani Bukombe kupata nafasi za kwenda Vyuo vya Ualimu.

Katika mwaka huu mwezi Mei kuna vijana 101 wanaotoka Wilaya ya Bukombe wamemaliza Chuo cha Ualimu, nilikuwa nimeomba vijana hawa warejeshwe katika Wilaya Bukombe kwa ajili ya kusaidia kupunguza tatizo la upungufu wa walimu. Lakini zaidi sana tukisema hali ya Utaifa tusingweza kuififikiria sana kwa sababu tunapokuwa na upungufu mkubwa Wilayani Bukombe na sehemu zingine hazina upungufu, bado pia hali ya Utaifa haipo. Kwa hiyo, naomba mtusaidie hawa vijana warudi Bukombe na baadaye uwiano utakapo-*balance* mtaanza kuwahamisha kwenda Wilaya zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na pale kuna vymba vya maabara 36 vimekamilika hatujapata vifaa mpaka leo na Waziri analifahamu hili mezani kwake naomba ufanuzi.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi pamoja na mambo mengine niliyozungumzia lakini lipo jambo ambalo nimepewa ufanuzi, naishukuru sana Serikali na Waziri kwa kupewa ufanuzi huo hasa wa suala la Ndurumo na Kinandeu, lakini nina swali moja ambalo nahitaji Waziri anipe ufanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule ya Sekondari Tumaini ni shule ya muda mrefu, ipo Kata ya Kinampanda na ni shule kongwe, lakini kwa mwaka huu shule hii imepokea wanafunzi wa kidato cha kwanza ambao wapo kumi na moja wasioona na kwa bahati mbaya sana shule hiyo siyo shule ya walemovu na hakuna vifaa vya kufundishia walemovu wala hakuna walimu wa walemovu. Je, Waziri unayo taarifa hiyo? Na kama taarifa hiyo mnayo ni kwa nini sasa mlipeleka wanafunzi walemovu wasioona mahali ambapo si shule ya walemovu? Kama mliwapeleka pale sasa mnautaratibu gani kupeleka facilities katika shule hiyo ili waweze kuapta elimu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Bukombe utaratibu ni kwamba wanachuo wanapokaribia kumaliza kozi ya ualimu wanapewa nafasi ya wao wenye kuchagua wanataka kwenda kufundisha wapi. Baada ya kumaliza kwa wanachuo wanaochukua *Diploma* na wale wanaochukua daraja la tatu A. Wizara ya Elimu inachukua yale mapendekezo yao, mara nyingi unakuta ni kweli wanawenza wakapelekwa katika ile Mikoa, tunaomba wachague Mikoa. Lakini wakati mwininge unakuta Mikoa ile labda ina walimu wa kutosha kwa hiyo, inabidi Wizara iangalie ni mahali gani ambapo pana upungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa suala analozungumzia Mheshimiwa Luhahula, ameshatupatia *list* na ile *list* tumeshaipeleka Wizarani katika Idara husika ili kusudi waweze kuangalia kama inawezekana wote kuwapeleka Bukombe au wengine wapelekwe katika Mikoa yao. Pia niseme tu kwamba vijana hawa tunaweza kuwa tunawalazimisha waende katika maeneo hayo lakini wao wanapenda kwenda katika maeneo waliyochagua na sisi tungependa kuwapeleka kadri walivyochagua. Lakini suala la Mheshimiwa Mbunge tunalifuatilia. (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufanuzi juu ya suala la vifaa vya maabara huko Bukombe pamoja na wanafunzi wenye ulemavu kupelekwa katika shule ya sekondari ya Tumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vifaa vya maabara vinavyopelekwa fedha hupitia kwenye Halmashauri na wanapaswa kutangaza ili apatikane mzabuni wa kupeleka hivyo vifaa, huu ndiyo utaratibu wa kanuni za manunuzi. Naomba kuagiza kwamba Afisa Elimu anayeshughulika na shule ya sekondari ahakikishe kwamba anafuatilia kazi hiyo inafanyika na vifaa vya maabara vinapatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wanafunzi wenye ulemavu kupelekwa kwenye shule ya sekondari ya Tumaini hivi sasa tunafanya juhudhi ya kuchanganya hawa wanafunzi, tukisema tuwe na shule ya peke yao nako pia ni kuwanyanyapaa, ndiyo maana awali nilipokuwa najibu hoja za kiujumla tulisema kwamba Wizara imetenga takribani shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kuboresha miundombinu. Kwa hiyo, naomba niseme kwamba wenzetu wa Halmashauri watakapopelekewa fedha hizi wahakikishe wanarekebisha miundombinu kwa haraka ili wanafunzi hawa waweze kupata haki yao. Hata hivyo fedha kwa ajili ya vifaa vyao pia Wizara imetenga shilingi milioni 950 kwa

ajili ya kuwanunulia vifaa mbalimbali vikiwemo vyta walemavu wasioona, viziwi na kadhalika. (*Makofit*)

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niombe ufanuzi juu ya masuala niliyoyaandika, lakini kwa kuwa tumepewa nafasi moja tu na mambo yenewe ni mengi kuna suala la Chuo Kikuu Tabora, Shule ya Wanawake Tabora na kadhalika, naomba ufanuzi kuhusu ufinyu wa Bajeti katika Mfuko wa Mamlaka ya Elimu Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii iliidhinisha utaratibu unaojulikana kama *skills development levy* ambayo ni asilimia sita inalipwa na waajiri wengi. Pesa hizi zikikusanywa zinapaswa kutengwa kama ifuatavyo; asilimia fulani isiyopungua tatu inakwenda *VETA*, asilimia inayobaki sijui inakwenda wapi. *Tanzania Education Authority (TEA)* ni chombo cha Serikali kinacho-*develop skills* na sasa hivi Wizara inazungumza kuwa haina pesa. Naomba ufanuzi hii *skills development levy* sehemu ambayo haiendi *VETA* na huko *VETA* kwanza wanapeleka sehemu ndogo kama sikosei ni asilimia mbili kati ya asilimia sita, hizi nne zinakwenda wapi? Naomba ufanuzi.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani swali la msingi hapa siyo kwamba *skills development levy* inakwenda wapi, nadhani swali la msingi hapa ni namna gani tutapata nyongeza ya Bajeti katika *Tanzania Education Authority* ambayo kwa kweli imefanya kazi nzuri sana ya kuvipa mikopo Vyuo Vikuu, kujenga miundombinu, kujenga *hostels* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaangalia Sheria ya *TEA* na uwezekano wa kuona ni jinsi gani Serikali inaweza kuongeza fedha katika Bajeti ya Taasisi hii ili kuongeza uwezo wake wa kuhudumia elimu ya juu, elimu ya sekondari na elimu ya msingi. Hiki ndiyo kitu kikubwa na tunategemea kwamba ikifika mwaka unaokuja tutakuwa tumeipitia Sheria ile na kuileta hapa Bungeni ili kuweza kuleta afueni katika Taasisi hii muhimu.

**MWENYEKITI:** Tatizo nililonalo hapa ni kwamba Profesa amejibu vizuri sana, lakini katika yale makubwa, katika lile ambalo limeulizwa na Mheshimiwa Siraju Kaboyonga bado hatujapata maelezo, Waziri wa Fedha upo? Swali lake ni kwamba asilimia sita inatakiwa iende *TEA* inaenda asilimia mbili, je, asilimia nne inaenda wapi? Kama nimekupata sawa sawa au unaweza kufafanua vizuri?

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweka rekodi sawasawa ni kwamba asilimia sita ndiyo inayokusanywa, asilimia mbili inakwenda *VETA*, mimi nilitarajia asilimia fulani ingekwenda *TEA* ya ile inayobaki. Lakini ile inayobaki asilimia nne yote inayeyuka huko ndani ya Serikali sijui inakwenda wapi, kwa nini isipelekwe *TEA* angalau asilimia tatu? Wakati mpango anaousema Waziri unaendelea kufanyiwa kazi, maana yake hivi vitu siyo *mutually exclusive*. Unaweza ukatumia hizi *skills development levy* wakati mpango ambao Waziri unausema na wenywewe unaendelea kufanyiwa kazi kwa sababu *skills development levy* ipo.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongezea majibu mazuri ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu kwamba si kweli asilimia nne ya pesa za *TEA* zinayeyuka. Majibu aliyojibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Elimu ndiyo sahihi kwamba pesa hizi sehemu inakwenda *VETA* asilimia zaidi ya 90 ya Bajeti ya *TEA* inatokana na pesa hizi. Sina hakika wanachopata ni asilimia ngapi inakwenda *TEA*, sitaki nikatoa kitu ambacho si sahihi katika *Hansard*. Lakini ukweli ni kwamba *TEA* inapata pesa zake kutoptaka na ile asilimia sita.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia nilieza mambo mawili kuhusu ile shule ambayo Waziri ameielezea vizuri sana, nami namshukuru sana, lakini pia namshukuru kwa majibu mengine ambayo ameyatoa.

Suala la shule ile katika Jimbo la Kasulu Magharibi hivi sasa ni siasa kali. Mimi nahitaji tamko la Waziri, kuna wanafunzi 31 wamefukuzwa shule. Waziri aliagiza warudishwe shuleni. Nilipokwenda kule wakati ule walikuwa hawajarudishwa shuleni, watu wanageuza maneno wanasingizia hili, wanasingizia lile.

Mimi naomba tamko la Waziri watoto wale warudi shuleni, tunawaharibia maisha. Wale ni watoto sawasawa na mtoto wangu akifukuzwa shule mimi nitaumia na wale wazazi wanaumia. Nikionyesha barua ambazo nilikuwa napata zingine zinasikitisha na mtu yejote hapa mtoto wake akifukuzwa shule hatafurahi. Naomba tamko la Mheshimiwa Waziri.

Lakini la pili yule mfanyakazi wa CWT anaandika uongo na anapeleka kwa walimu wote baada ya kupeleka kwa walimu wote yale aliyopeleka hayahusiani na yale niliyozungumza wala tuliyoyafanyia kazi. Kwa taarifa Mheshimiwa Waziri tuliposema kwamba yule mwalimu tayari anaondoka wananchi wa sehemu ile na wanafunzi walilala wanacheza mpaka asubuhi. Tafadhali naomba Mheshimiwa Waziri ultolee tamko. Ninakushukuru sana rafiki yangu Waziri. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba suala hili lilikuwa limeletwa Wizarani juu ya wanafunzi ambao waliachishwa shule na nilikuwa nimetoa maagizo kwa *REO* alioko kule Kigoma ili waweze kusimamia kwamba wanafunzi wale amba kwa kweli hawana makosa ya kuachishwa shule warudishwe shuleni. Ningependa nitoe maagizo na kusisitiza sana kwamba Kamishina wa Elimu asimamie kurudishwa shule kwa watoto hawa na kusisitiza kwa kweli walimu wasichukue watoto kufukuzwa shule kama ndio adhabu ya kwanza kwamba walimu wafukuze shule watoto kama ndio adhabu ya mwisho baada ya kuchukua hatua mbalimbali za kuweza kuwarekebisha watoto wetu. *Of course* ni muhimu sana watumie bodi ya shule na pale ambapo bodi ya shule imefanya maamuzi ambayo labda yangetaji rufaa kuna bodi pia ya mkoa na bodi ikishindwa pia kuna *appeal* chini ya Waziri wa Elimu kwa Waziri wa Elimu. Ninachopenda kusema sasa ni kwamba uongozi wa elimu usimamie watoto wale warudishwe shuleni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyama vyta Wafanyakazi haviwajibika kwa Waziri kwa hiyo, tutaangalia ni taarifa gani ambayo imetolewa na kushirikiana na uongozi wa

CWT kuhakikisha kwamba kama kuna upotoshaji unaondoka kwa sababu maamuzi yale yalifanywa na Wizara na wala hayakufanywa na Mbunge. Mheshimiwa Mbunge, tunakuomba sana wananchi wa Kasulu Magharibi waweze kukurudisha tena Bungeni kwa sababu ya michango yako ambayo wote tunai-*appreciate*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nililetewa pia hapa ombi moja la Mheshimiwa Seneta Paul Kimiti kuhusu *VETA* ya Mkoa wa Rukwa, nilikuwa nakuomba nitoe jibu kwamba mwanzoni ujenzi wa *VETA* ya Mkoa ulilengwa ukajengwa pale Mpanda na *VETA* ya pale Mpanda ikiwekewa vizuri kwamba inaweza kuwa na *function* ile ile ya *VETA* ya Mkoa. Lakini Kamati ya Maendeleo ya Mkoa wa Rukwa, ikatuletea taarifa kwamba wangependa *VETA* ya Mkoa ijengwe Mkoani Sumbawanga na Serikali imekubali kufanya hivyo na tunawashukuru kwamba wametafuta eneo na sisi tutashughulika na kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi huo. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa kujibu hoja zote hizi. Sasa kwa kweli kwa muda ambao uko mbele yetu tutakwenda kwa utaratibu wa *gillotine* sasa.

#### **Fungu 46 – Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı**

Kifungu 1001 – <i>Administration and General</i> .. . . . .	Sh. 28,822,235,300
Kifungu 1002 – <i>Finance and Accounts</i> . . . . .	Sh. 629,187,000
Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning</i> .. . . . .	Sh. 4,154,031,000
Kifungu 1004 – <i>Internal Audit Unit</i> .. . . . .	Sh. 296,215,000
Kifungu 1005 – <i>Procurement management Unit</i> .. . . .	Sh. 402,230,600
Kifungu 1006 – <i>Information, Education and Communication</i> .. . . . .	Sh. 441,652,700
Kifungu 2001 – <i>Commissioner for Education</i> .. . . . .	Sh. 8,642,283,800
Kifungu 2002 – <i>Inspectorate</i> .. . . . .	Sh. 11,369,319,500
Kifungu 2003 – <i>UNESCO Commission</i> .. . . . .	Sh. 0
Kifungu 3001 – <i>Basic Education</i> .. . . . .	Sh. 2,839,250,700
Kifungu 3002 – <i>Adult Education and Non Formal Education</i> .. . . . .	Sh. 983,112,500
Kifungu 4001 – <i>Secondary Education</i> . .. . . . .	Sh. 1,731,712,000
Kifungu 5001 – <i>Teacher Education</i> .. . . . .	Sh. 28,361,809,600
Kifungu 7001 – <i>Higher Education</i> .. . . . .	Sh. 426,263,209,800
Kifungu 7002 – <i>Techn. and Vocation Training Division</i> .. . . . .	Sh. 11,004,280,500

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

#### **MIPANGO YA MAENDELEO**

## **Fungu 46 – Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufund**

Kifungu 1001 - <i>Administration and General</i> ... .. . . .	Sh. 346,789,000
Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning</i> ... .. . . . .	Sh. 13,776,833,000
Kifungu 2001 – <i>Commissioner for Education</i> ... .. . . .	Sh. 1,073,295,000
Kifungu 2002 – <i>Inspectorate</i> ... .. . . . .	Sh. 600,000,000
Kifungu 3001 – <i>Basic Education</i> ... .. . . . .	Sh. 3,115,375,000
Kifungu 4001 – <i>Secondary</i> ... .. . . . .	Sh. 14,679,990,000
Kifungu 5001 – <i>Teacher Education</i> ... .. . . . .	Sh. 533,368,000
Kifungu 7001 – <i>High Education</i> ... .. . . . .	Sh. 99,201,684,000
Kifungu 7002 – <i>Techn. and Vocation Training Division</i> ... .. . . . .	Sh. 6,304,673,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufund kwa mwaka 2010/2011 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufund kwa mwaka 2010/2011 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufund, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Naibu Waziri Mheshimiwa Mwantumu Mahiza na Gaudentia Kabaka, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii kubwa na nzito ambayo ndiyo msingi wa maendeleo ya Taifa letu, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufund. Tunawatakia kila la kheri kwa Bajeti ambayo Bunge limewapitishia kwa ajili ya kufanya kazi kwa mwaka mzima ujao, matumaini ya Watanzania ni makubwa sana kwenu, tunawaamini, tunajua kabisa kwamba mtafanyakazi nzuri na Waheshimiwa Wabunge hawa wanaenda kwenye majimbo yao wakiamini kabisa kwa kazi nzuri mliyofanya katika elimu ndiyo itakayotuvusha sote kurudi hapa. (*Makofi*)

Mimi niwapongeze sana, yamefanyika maajabu katika nchi yetu. Lakini pamoja na maajabu yote, ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dodoma, kama mjumbe wa huko ni lazima niseme kidogo kwa heshima ambayo nilipewa na Bunge hili kuwawakilisheni maajabu yale mmeyaona. (*Makofit*)

Mheshimiwa Waziri, niseme tu kwamba wale Maprofesa pale, Profesa Idris Kikula, Profesa Mlacha na Profesa Kinabo ambao ni ma- *deputy vice chancellors* hebu tuwatazame kipekee. Hawa ni Watanzania, wamefanya jambo ambalo si la kawaida hata kidogo. Kwa hiyo, tutafute kitu fulani hivi tuwatambue. Kwa kweli menejementi waliyoiongoza pale ya ku-*handle* pesa zile na ujenzi mkubwa namna ile ni jambo la kujivunia kabisa. (*Makofit*)

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umeisha na shughuli zote zilizokuwa zimepangwa katika *Order Paper* ya leo zimekamilka, kwa hiyo, kwa fursa hii naomba sasa kuahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 2.10 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumanne, Tarehe 13 Julai, 2010 saa tatu asubuhi*)